

‘...Hili ni bomu au niite shambulio la kibaiolojia. Na bado kuna mabomu mengi yametegwa kwenye miili ya Waafrika, siku yatakapolipuka, mtalia sana...

HARUFU YA KIFO

Zalisho la nne kutoka



JAMVI LA SIMULIZI
+255 672 160016 / +255 766 974865
jamvilasimulizi@gmail.com

© Richard R. Mwambe (Kamanda Amata)

MSANIFU JALADA
Emmanuel Kindo

MSANIFU KURASA
Robert Kiatu
+255 715 899495
rkiatu1@gmail.com

MHARIRI
Bahati Hoza

Kimechapwa na:
Gama Printers – Bagamoyo
+255 718 603654 / +255 764 596 554

Chapa ya kwanza 2020

ISBN 978 – 9987 – 9743 – 4 – 4

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili wala kuitumia kazi hii kwa namna yoyote ile bila ya idhini ya maandishi ya mwandishi. Kutekeleza kinyume chake itakuwa ni kosa, na sheria itachukua mkondo wake pasi na kujali cheo, umri wala aina ya mtu.

TUNU

Kwa watoto wangu, Jennifer na Richard Jr. Ninatunuku kitabu hiki kwenu wanangu wapendwa, ili kuwakumbusha uzalendo kwa taifa lenu. Leo hii ninapochapa kitabu hiki, bado umri wenu haujapambanua nini maana ya maisha. Lakini naamini, siku mtakapokuwa wakubwa na kusoma kitabu hiki kwa akili yenu wenyewe, kitawajenga kuwa Watanzania wa kweli. Mfanye kila mnachoweza kuacha alama katika taifa lenu ikiwemo kulitetea kwa njia yoyote ile.

Naamini mtaweza kwa kuwa mmekwishanionesha nia yenu katika umri huo mlio nao. Basi Mwenyezi Mungu awalinde, awakuze kwa kimo na akili na siku moja majina yenu yajenge makao katika vinywa vya wapenda amani. Siku zote za maisha yangu nitaendelea kuwaombea.

Nawapenda sana!

SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu, mweza wa yote. Kwani ni yeye aliyenipa pumzi na nafasi ya kuandika kazi hii na kuifikisha kwenu, na ndiye mwenye maamuzi juu ya maisha yetu.

Pili, shukrani zangu ziende kwa Madam Victoria Michael Ntara. Mama wa watoto wangu. Ulichangia Mawazo mengi ili kuifanya riwaya hii iwe bora kama ilivyo. Mungu akuzidishie moyo huo maradufu.

Kwa namna ya pekee namshukuru rafiki yangu mpenzi, Rehema Stanley Kamana, kwa mchango mkubwa alioutoa. “Rehema, nakushukuru kwa moyo wako. Mchango wako ulioutoa ili kuhakikisha kazi hii inatoka katika kitabu, umefanya kazi kusudiwa. Asante na Mungu akubariki na kukuongezea pale ulipopunguza. Aidha, mawazo na ushauri wako vimenipa moyo wa kusonga mbele. Asante sina cha kukulipa ila Mungu atakulipa vingi.”

Tatu, kwa wapenzi wote wa riwaya nchini. Kwa ajili yenu, nimewaleta kazi hii iliyotukuka, iwe burudani na kitulizo cha mioyo ya wenye huzuni.

Mwisho kabisa, shukrani zangu za dhati zifike kwa wana-UWARIDI. Kwa umoja mnaouonesha na mambo mbalimbali mnayoyafanya katika kuhakikisha gurudumu la fasihi Tanzania linafikia lengo lake. Asanteni sana na muendeleo kuwafanya watu waone thamani ya riwaya za Kiswahili.

Pia ninamshukuru kila atakayenunua kitabu hiki. Nyote mbarikiwe. Richard R. Mwambe, ninakupendeni sana.

06 April, 2020

Don Bosco , Iringa.

Katika maisha yangu nimejitoa kwa haya mapambano, kwa ajili ya Waafrika. Nimepambana kupinga tabaka la mtu mweupe, na nimepambana kupinga tabaka la mtu mweusi. Lengo kubwa kwangu lilikuwa ni kujenga jamii ya kidemokrasia ambayo watu wote wangeishi pamoja kwa amani na usawa. Ilikuwa ni muono wangu wa mbali ambao nilitamani kuufikia. Lakini kama inatakiwa kuwa, basi ni muono ambao nipo tayari kufa kwa ajili yake.

- **Nelson Mandela**



**HARUFU
YA
KIFO**

**Richard R.
MWAMBE**

UTANGULIZI

1962

WATANGANYIKA bado walikuwa wakisherehekea uhuru wa nchi yao. Ni mwaka huo, ndipo taifa hilo *'babe'* katika ukanda wa Kusini mwa Afrika lilikuwa jamhuri kamili baada ya Mwl. Julius Kambarage Nyerere kuwa Rais wa kwanza. Kitendo cha Nyerere kushika hatamu na kuiletea Tanganyika uhuru wake mwaka 1961, kilifurahiwa na Watanganyika na wapinga ukoloni katika Afrika kiasi kwamba kijana huyu machachari, msomi, akaonekana shujaa. Kijana wa Kizanaki, mwenye maneno mengi ya kumtoa nyoka pangoni, mwalimu wa shule ya upili. Wakati huo alikuwa ameweka kando taaluma yake na kuingia katika ulingo wa siasa, hakika, alihitaji kuwakomboa watu wake kutoka katika makucha ya wakoloni.

Mataifa beberu duniani ambayo mwaka 1884 yalikutana kule Berlin na kugawana Bara la Afrika kama *'kitoweo'* hayakufurahi hata kidogo, kwani azma yao ya kutawala haikuwa imefika kikomo isipokuwa tu falsafa ya Mwl. Julius K. Nyerere iliwakata kauli na kuwadhoofisha nguvu. Uingereza ikaja na kutawala mwishoni kisha ikatoa uhuru kwa Watanganyika. Ili iendeleo kunyonya ikaiweka nchi hiyo pamoja na nyingi ilizozitawala katika kile ilichokiita 'Jumuia ya Madola' chini ya utawala wa Malkia.

Mvutano haukuwa mdogo nyakati zile. Mwl. Nyerere, alipokuwa akipambana na mtu mweupe kwa maneno makali yaliyojaa hekima na busara, yenye kuua zaidi ya risasi. Maneno hayo hayo yaliwaunganisha Watanganyika, wakaweka nguvu pamoja na kuhakikisha wanamwondoa mkoloni na kuikomboa si tu Tanganyika, bali nchi zote Kusini mwa Afrika. Bahati mbaya sana mkoloni alikuwa mjanja kuliko babu zetu.

Aliondoka, lakini akatufanya kama kuku ndani ya banda lake, ambapo, akifurahi, anawanyima chakula, akiamua, anawanyima maji na ndivyo ilivyo hata sasa. Kiongozi yeyote wa Afrika akijifanya kujua tu, utasikia ‘tunakuwekea vikwazo vya kiuchumi’, tunagwaya na kufuata matakwa yao. Fanya hivi, fanya vile! Fanya vile, fanya hivi!

Pamoja na jitihada zote za Mwl. Nyerere na wapigania uhuru wengine waliozikomboa nchi zao na kuweka mikakati mizito ya kuzijenga na kuiimarisha Afrika, kama aliyekuwa Waziri Mkuu Mzalendo wa kwanza katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Patrice Lumumba, aliyekuwa Rais wa kwanza wa Ghana Kwame Nkrumah, mwanamapinduzi aliyeikomboa Msumbiji, Samora Machel na wengine wengi, bado tulishindwa kuikomboa Afrika na kuijenga vile tulivyotaka iwe. Badala yake tulishuhudia vifo tu, tena vyenye utata, visivyoeleweka mpaka kesho.

Mwaka 1972, tarehe 27 ya mwezi Aprili, huko Bucharest, Romania, mbali na nchi yake aliyoiipenda sana, aliyoiipigania na kuiletea uhuru. Mbali na watu wake waliomtukuza kila uchao, tukasikia, ‘Kwame Nkrumah amefariki dunia’. Wakasema ‘alikufa kwa ugonjwa usiotibika’, saratani, lakini kama haitoshi kuusimika uwongo wao, wakaongeza na kusema ni ‘kifo kisichoelezeka’.

Miezi michache tu tangu ailetee uhuru nchi yake ya Kongo, au Zaire ya zamani, tukasikia ‘Waziri Mkuu Patrice Lumumba kawekwa ndani’, mara yakafuatia mauaji ya kikatili kabisa dhidi ya kiongozi huyo. Na sababu ni msimamo wake wa kutokutaka kuruhusu namna yoyote ile ya unyonyaji na ukoloni mamboleo. Mataifa ya Ubelgiji na Marekani yakatajwa katika mauaji hayo. Miaka ikapita, mara, huko Uingereza, mbunge mmoja akatoa siri ya kifo cha Lumumba. Akasema kuwa, majasusi wa MI6 wamehusika. Mbunge huyu, Lord David Lea akaufichua ukweli wa mauaji hayo kwa kuliandikia barua jarida la *London Review of Books* toleo la March 21, 2013. Katika barua yake hiyo alieleza kuwa amedokezewa na Bi. Daphne Park ambaye alikuwa jasusi na balozi mdogo huko mjini Leopordville au Kinshasa ya sasa mwaka 1959 hadi 1961. Lumumba alipinduliwa katika njama iliyopangwa na mataifa ya Magharibi na baada ya mateso makali akapigwa risasi na kuuawa Januari 17 ya mwaka 1961.

Baada ya miaka kadhaa kupita, utawala wa kibaguzi ukaendelea huko Afrika Kusini. Viongozi wetu hawakuweza kukaa kimya. *‘Aluta Continua’*, mapambano yanaendelea, ilikuwa hotuba ya kuvutia na kihistoria

iliyowasilishwa na mpigania uhuru, Samora Machel. Nchi za mstari wa mbele ziliendeleza mapambano dhidi ya ubaguzi huu. Usiku wa tarehe 19 ya Oktoba 1986, Afrika ikapatwa na mshituko mwingine mkubwa. Mwanamapinduzi, mpiganaji wa Msumbiji, aliyekuwa rais wa nchi hiyo Ndg. Samora Machel, alikufa katika ajali mbaya ya ndege ambayo mpaka sasa haijapatiwa ufumbuzi kama ilidunguliwa, au ilikuwa ni matatizo ya kiufundi. Lakini uchunguzi wa awali ukatuambia kuwa ndege hiyo ilidunguliwa mita 200 kabla ya mpaka wa Msumbiji, ndani ya nchi ya Afrika Kusini.

Kwa ujumla, hatutakiwi kuwa huru, na hatuko huru hata sasa, tumepata uhuru wa maneno na bendera, hatujapata uhuru wa haki, uhuru wa kujiamulia nini cha kufanya. Wamewekeza kwenye vichwa na maamuzi yetu, wakatujengea ujinga wa kuamini kuwa; ‘ninyi hamuwezi, sisi tunaweza’, ‘chenu si bora, bali chetu’, ‘utamaduni wenu ni wa kishenzi, wetu ndiyo wa kisasa’, wanatutawala kama Mmasai anavyowatawala ng’ombe wake.

Tangu lini kitu kizuri kikatengenezwa Afrika? Wametunyima na kutunyang’anya uwezo wa kufikiri tangu Zama za Mawe za Kati. ‘Kizazi duni’, tukaitwa. Kizazi chetu hiki cha karne ya ishirini na moja kinashuhudia mapinduzi makubwa ya kiutawala Afrika, machafuko na mauaji ya kutisha. Huyu hataki kuachia madaraka, huyu anataka kuingia ikulu, ili mradi tu vurugu. Yote haya, ni yao, wala si yetu. Wanachukua almasi, wanatuletea bunduki. Ukitazama habari za kwao watakuonesha kila siku dokumentari za kutengeneza magari mapya, majumba ya kifahari, maisha ya raha kama wako peponi ilhali wakionesha upande wa Afrika ni mauaji, vita, njaa, ukame n.k

Na sisi tunajisahau au hatujielewi, tunashindwa kupigana vita hii ya kimamboleo. Tukionesha habari za weupe tunawasifia. Tukionesha habari zetu tunakandamizana. Tunasifia vita na kupiga kelele za njaa. Tunakimbilia kuomba misaada ilhali utajiri tunao. Tunawapa migodi, mbuga za wanyama na mengine mengi. Tunabaki kuangalia ndege zikiruka na kutua huku tunakenua, tukisema, ‘Ah! Mzungu bwana!’



SURA YA 1

SEHEMU FULANI HUKO MAREKANI

“Kama tulivyopanga. Mambo yetu lazima yaende vile vile. Kazi ya kuhakikisha kizazi duni kinatoweka duniani lazima ifanyike kwa kila hali na kila njia,” mtu mmoja mwembamba, mrefu, aliyesokota sharubu zake, akiwa kavalia suti ya vipande vitatu alisikika akiwaambia washirika wake walioketi kumsikiliza. Miguuni mwake, alisitiriwa na viatu virefu vilivyochongoka mbele na miwani yenye kioo kimoja, au wenyewe huiita *‘Monocle’*, iliyomkaa vyema katika jichole la kushoto. Bwana mkubwa huyo, aliyasema hayo huku akitembea tembea kuzunguka meza kubwa ya mtindo wa ovali iliyokaliwa na watu takribani kumi na tano hivi. Akavuta hatua mpaka upande mwingine wa meza ile. Akasimama na kuwatazama watu wale.

“Tutahakikisha tunawachonganisha wapigane, wauane na damu imwagike mpaka tone la mwisho ili tuendelee kufaidi rasilimali za Bara la Giza. Hawana akili wale! Wanafikiri sisi kuziachia nchi zao zijitawale tulikuwa wajinga? Tangu lini uhuru ukaupata kwa kumuomba anayekutawala? Hakuna!” akaendelea kusema na kuanza tena kuzungukazunguka na wajumbe wengine wote walikuwa kimya.

“Uhuru kamili ni kumfutulia mbali anayekutawala kama ni kwa sumu au kwa risasi, hapo utajitawala. Lakini kwa kumuomba anayekutawala, ujue bado atakupangia ya kufanya na utafanya kwa maana hiyo atakutawala tu...” aliposema hayo wote wakacheka na kisha ukimya ukarudi tena. Yule aliyekuwa akiongea akanyamaza na kusimama kwenye ncha moja ya meza hiyo akiwatazama wajumbe wote.

“Tumeongea mengi, tumejadili vya kutosha. Kama babu zetu walivyofanya kule Berlin, nasi hatuna budi kuendeleza mkataba ule

kwa mtindo wa kisasa. Lakini, jambo la kwanza ni kupunguza wingi wa Waafrika, kwa njia zote. Sina haja ya kuzisema. Na nataka kila mmoja ateleze jukumu alilolalo sasa, ili wajukuu wetu, miaka ijayo, wafaidi utajiri mkubwa kutokana na maamuzi chanya ya sisi babu zao,” akafunga mkutano na kila mjumbe akaondoka akijua nini anatakiwa kufanya.

SURA YA 2

1984

UGONJWA WA AJABU uliibuka afrika. Kasi ya vifo haikuwa ya kawaida. Kila mtu alijawa hofu na kumwogopa mwenziwe. Wanandoa wakaogopana, wapenzi nao vile vile. Ilikuwa ni misiba kila kukicha, makaburi yakaongezeka. Wataalamu wa madawa walikosa usingizi, kila walipokaa chini na kukuna vichwa ni jinsi gani wataukomesha ugonjwa huo, hawakufua dafu. Wakawasiliana na wataalamu wa nje, kwenye maabara kubwa za kisasa huko 'Ughaibuni'. Sampuli za damu zikapelekwa, lakini hakukuwa na jibu la maana lililotokea zaidi ya kutuletea jina tu la ugonjwa huo, *ADIOSIS*.

Hicho ndicho tulichoambulia kutoka kwao, jina la ugonjwa, hakuna kingine. Hakukuwa na la kufanya zaidi ya kuhimizana kumrudia Mungu na kuacha kuepuka maambukizi yasiyo ya lazima. Semina, warsha, makongamano, mikutano ya hadhara na mambo mengi yalikuwa yakihamasisha watu kujikinga na ugonjwa huo mbaya kuliko ubaya wenyewe. Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ukaathirika zaidi, kila aliyeishi ukanda huu aliihisi harufu ya kifo. *ADIOSIS!*

1996

PHILADELPHIA – MAREKANI

Katika moja ya maabara kubwa ndani ya jimbo hilo, mwanasayansi mmoja alikuwa akiumiza kichwa siku hadi siku. Mpaka wakati huu, alijikuta, anaaza kuzeeka kwa kujaribu kutengeneza kanuni fulani ya kikemia ili kupata dawa ya ugonjwa huo. Daima, alipenda kujifungia katika ofisi yake, na kufanya majaribio anuai kupata dawa hii au kinga

ile. Hata taifa lake lilimuelewa kwa kazi zake. Alikuwa amekwishagundua dawa na chanjo nyingi zilizotumika sehemu mbalimbali duniani, hata akapewa cheo kikubwa na Malkia wa Uingereza, 'SIR'.

Sir Dostrodof Fenegan, alijikuta anazeeka huku nywele zake zikiisha kichwani kwa kujikuna kila wakati.

People are so bastards! Akawaza wakati akiendelea kuchanganya kemikali hii na kuitazama ile kwa kutumia *microscope* yake kubwa na ya kisasa. Ilimchukua miaka kumi asubuhi na mchana, akiendelea kuandika na kuchora chora hesabu zake za kikemia katika kitabu kikubwa ndani ya ofisi yake. Hakupenda kubughuziwa wala kusumbuliwa. Uzuri ni kwamba, katika maabara hiyo kila mmoja alikuwa na kazi yake iliyomfanya akose hata muda wa kumtembelea mwingine. Lakini tabia ya huyu bwana iliwafanya hata wengine wapate wasiwasi, kwani, hata kula alikuwa akisahau mara nyingi. Yeye na kazi, kazi na yeye. Wakati wa vikao vya kikazi, kwa minajili ya kubadilishana mawazo ya kitafiti, yeye asingeweza kukaa zaidi ya dakika kumi, angekurupuka na kurudi ofisini kwake haraka kwani kilichomjia kichwani ndicho angenda kukiandika au kukifanya kwa wakati huo. Tabia hii haikuwapendeza wengine. Taarifa kuhusu mwenendo wake zikafika kwa uongozi naye akawekewa uchunguzi wa siri kujua nini hasa kinamfanya awe hivyo.

Na ili kumfanyia uchunguzi vizuri, Sir Dostrodof Fenegan, akapewa likizo. Idara ikamtaka kupumzika kwa kisingizio kwamba ni miaka mingi kafanya kazi bila likizo. Hakukataa. Cha kushangaza, hakukiacha kitabu chake, kwani hata nyumbani alikuwa na maabara yake ndogo ya chunguzi mbalimbali.

AIDIOSIS ulikuwa ni ugonjwa unaomuumiza sana kichwa na kumnyima usingizi. Kila alipotazama luninga, hususani, habari za Afrika, alizidi kuchanganyikiwa na hakujua nini atafanya kuukomesha ugonjwa huo.

"Ooooh! nimepata wazo, ngoja niende Afrika, nikaone mwenyewe, hii itanipa mwanga!" Asubuhi moja akajikuta akijisemea mwenyewe kana kwamba anaongea na mtu mwingine. Mara tu akaanza utaratibu wa safari kuelekea Afrika, nchini Tanzania ambapo ndipo alikuwa akipata habari nyingi sana za tatizo hilo.

Akiwa hajui kama nyuma yake anachunguzwa kwa kile kinachomfanya awe bize, Dr. Fenegan bado aliendelea kufanya kile alichokianza miaka kadhaa nyuma. Safari ya kwenda Afrika ilimjaa kichwani, alidhamiria

kuhakikisha anafikia mwisho wa tafiti yake na anaibuka mshindi kwa mara nyingine.

Ni vigumu kutegua mtego bila kufika mahali ulipo. Kama nahitaji kumsaidia Mwafrika sina budi kufika Afrika! Akawaza.

Mzee huyu, mkemia mbobevu, alikuwa akiishi peke yake ndani ya jumba lake kubwa lililo katika viunga vya jimbo la Philadelphia. Alikwishatalikiana na mkewe miaka mingi, na yote hayo yalisababishwa na kujali kazi kuliko ndoa. Mara nyingi, mkewe huyu, alimkuta mumewe ndani ya maabara yake kalala kwa uchovu huku akiwa kazungukwa na karatasi zenye michoro na kanuni za hesabu zisizoeleweka. Iliwahi kupita miezi mitatu bila daktari huyu kutimiza haki ya ndoa kwa mkewe, tatizo. Msongo wa mawazo uliomkabiri mwanamke huyo, ukamfanya atafute kile anachokikosa. Akashika mimba nje ya ndoa na kuiacha nyumba, akahamia kwa mwanamume mwingine. Hii haikumshtua daktari huyu, yeye faraja yake ilikuwa ni kuona aina anuai za wadudu anaowakusanya na kuwaweka kwenye vifaa maalumu wakiwa hai mara nyingine kutengeneza bakteria na vimelea vya ajabu. Ku toka kwa wadudu hao na mimea aliyoipanda katika eneo la nyumba yake. Huko, ndiko alikokuwa akigundulia dawa zake na kufanikiwa kumaliza kabisa magonjwa sugu yaliyomkabiri mwanadamu.

Lakini *AIDIOSIS* ilimfanya kukaa maabara zaidi ya miaka mitano pasi na kugundua hata robo ya kinga kama si dawa ya ugonjwa huo.

Kama ni mmea basi upo Afrika. Kama ni mdudu basi yuko Afrika pia. Cha muhimu ni kuwa na virusi halisi vya ugonjwa huu! Akawaza na kuandika kwenye kitabu chake.

* * *

LANGLEY MAKAO MAKUU YA C.I.A

Katika ofisi fulani, ndani kabisa ya jengo hilo kubwa na liliohifadhi kila nyaraka ya hatari, nchini Marekani, kijana mmoja aliketi kitini huku akichezea kitenesi chake kwa kukirusha ukutani na kukidaka. Mbele yake kulikuwa na kompyuta kubwa kiasi, iliyokuwa ikipakuwa kabrasha fulani. Akiwa ametingwa na mchezo huo, mlango ukafunguliwa na mwanadada mmoja Mwafrika akaingia ndani na kuufunga nyuma yake.

Yule kijana akagutuka na kuketi sawa kitini kwake huku akiacha kitenesi kikianguka sakafuni pasi na kukidaka kama mara zote. Akameza mate na kujiweka sawa huku akimtupia jicho yule mwanadada.

“Cindy kwa nini unaingia hivyo ofisini kwangu wakati sheria unaijua?” akamtupia swali huku ndita zikiwa zimeshonana kwenye paji la uso wake.

“Im sorry my boy!” Cindy akamwomba samahani huku akibakia amesimama akiwa katika suti safi na kitambulisho kinachoning’inia upande wa titi la kuume.

“Kelvin!” akaita kwa sauti ya upole, kisha akaendelea kusema, “kuna kazi ya mimi na wewe kufanya, umeshapata taarifa hiyo?”

“Hapana! Kazi gani na wapi?” akauliza huku akizungusha kiti na kumtazama vyema mwanadada huyo.

“Basi utapata taarifa...” akamwambia. Kabla hajaanza kusema kingine mara kengele hafifu ikasikika kwenye simu-janja yake, akainyakua na kukuta kuna ujumbe wa maandishi umeingia.

“...fika ofisi Q baraka...!”

* * *

Q ni ofisi ndogo iliyojitosheleza, yenye meza safi inayong’aa kwa umaridadi wake. Kompyuta moja, kubwa ya kisasa na vikolokolo vingine viliifanya meza hiyo kuwa na munekano mzuri. Viti vinne ndani ya ofisi hiyo viliashiria kuwa inatosheleza wageni wa idadi kama hiyo tu. Nyuma ya meza kubwa ambayo ilitengwa na hewa ya nje kwa kioo kipana kulikuwa na mtu mmoja; si mnene, si mwembamba. Mbele yake baada ya meza hiyo kulisimama vijana wawili, mmoja wa kike na mwingine wa kiume.

“Cindy!” akaita.

“Yes Sir!” Binti yule akaitika.

“Kelvin!” akamwita yule kijana.

“Yes Sir!” naye akaitika.

Baada ya kuwaita kwa majina yao, akajikohoza kidogo kusafisha koo kisha akendelea kusema.

“Nimewaita, kuna taarifa imekuja hapa siku kama nne zilizopita kutoka Philadelphia, katika kituo cha taifa cha utafiti wa madawa, PMRC,” akapiga kimya, funda moja la mate likafuatia na kisha

akaendelea, “Mmoja wa watafiti wa kitu kile, tena wa miaka mingi, tulimuweka kwenye uchunguzi. Na hapa tunavyoongea yuko likizoni...”

Cindy na Kelvin walitulia kimya wakisikiliza ujumbe huo pasi na kujibu chochote. Kisha yule bwana baada ya kuwatazama kwa zamu, akaendelea.

“Sasa kazi ninayowapa naweza kuiita kuwa ni awamu ya pili, maana ya kwanza imekamilika... Ninataka mumfuatilie, ili kujua hasa ni nini anafanya au anachunguza. Jopo limewachagua ninyi, kwakuwa, taaluma zenu binafsi zinaweza kuwasogeza na kuelewa kile afanyacho”. Akawatazama tena, “Wewe ni mtaalamu wa Kemia na wewe ni wa Baiolojia. So mnaweza kutambua nini anafanya kwa kuona ama makabrasha yake au nini anaongea. Mmenielewa?”

“Yes, Sir!” wakaitika kwa pamoja.

Cindy Brightone, mwanamke wa wastani, umri kati ya miaka thelathini na thelathni na mitano hivi. Mmarekani mwenye asili ya Afrika. Mtaalamu wa masuala ya Kemia, aliyechukua Shahada ya Uzamili huko *Victoria University of Wellington*. Kabla ya kujiunga na CIA, Cindy alikuwa ni mhazili msaidizi katika chuo kidogo cha huko Ontario, Canada. Alisifika sana kwa akili aliyokuwa nayo katika ukokotozi wa mahesabu hayo ya kikemia. Vyuo vingi na maabara mbalimbali zilikuwa zikimtumia katika hayo. Muda wake wa kwenda kulitumikia jeshi kama ilivyo kwa vijana wa nchi hiyo: Cindy alitumia mwaka mzima katika kikosi cha anga kinachojulikana kama *US AIR FORCE* na huko ndiko alikokutana na kijana huyu, Kelvin.

Kelvin Keagan, yeye tofauti na mwanamke huyu, tayari alikuwa mwanajeshi akihudumu katika hospitali kubwa ya jeshi upande wa maabara inayotembea angani ya jeshi la anga la Marekani. Ni mtundu asiye kubali kushindwa katika masuala hayo ya kibaiolojia. Alitokea kuwa rafiki mkubwa wa Cindy hapo jeshini. Na baadae wakakutana tena katika idara hiyo ya kijasusi ya Marekani, CIA.

“Picha yake hii hapa!” akawapatia, kila mmoja nakala yake. Cindy na Kelvin wakatazamana, kwa kuwa walimjua vyema mtu huyo. Jina la Sir. Drostdyhof Fenegan halikuwa geni kwa Wamarekani. Walimjua kwa tafiti zake, na sifa zake zilikuwa zikivuma huku na huko duniani, vitabu vingi, tafutishi nyingi, tafiti kedekede na gunduzi zisizo na idadi, zilichapichwa chini ya uhakiki wake achana na zile zilizoandikwa au kufanyiwa utafiti na yeye mwenyewe.

“Inatakiwa kuanzia sasa mumfuatilie, popote atakapokwenda, chochote atakachofanya na majibu yoyote yale muyafikishe *Unity X* haraka... Nimemaliza,” akawaambia kisha vijana wale wakaondoka baada ya kuuliza maswali kadhaa na kujibiwa.

* * *

Katika kituo cha utafiti wa madawa Philadelphia

“Watu wa namna hii ni wa hatari sana, yeye ni mwanasayansi aliyebobea, anayejua mahesabu mengi sana ya kikemia. Mtu kama huyu ni hatari, kwani anaweza kuunda hata silaha ya kibaiolojia na kututeketeza wenyewe. Isitoshe ugunduzi wowote lazima uwe chini ya idara ya usalama, kitengo kinachodili na maswala kama hayo, ili usilete madhara. Lakini Sir. Drostdyhof amekuwa kimya siku hizi tofauti na zamani, gunduzi yake hii au tuiite tafutishi, hataki kabisa watu waijue, unafikiri ni nini anakifanya?” mtu mmoja aliongea kwa sauti nzito huku akimtazama huyo aliye mbele yake, mtu mnene aliyejaa kitini, kinywani mwake alibana *cigar* kwa midomo yake miwili. Kila alichokuwa akiambiwa na mwenyeji wake, yeye, alitikisa kichwa tu. Baada ya mgeni wake huyo kumaliza ayasemayo, kwa ukimya wa dazani ya sekunde hivi, akajiweka vyema kitini na kuondoa ule mtemba wake mkubwa kinywani na kukung’uta jivu kwenye kibweta chake. Kisha akaupachika katika kifaa maalumu kwa kazi hiyo.

“*Good!* Mlipoichunguza ofisi yake mmegundua au mmeona nini?” akauliza na kutulia akisubiri jibu.

“Tumekutana na mahesabu magumu kueleweka, inaonekana safari hii anataka kugundua kitu kikubwa na cha siri sana. Tumeshindwa kuelewa kabisa *formula* zake za safari hii...”

Dakika kadhaa zilizofuata, akawekewa karatasi kadhaa mbele yake, akazikagua, zilikuwa kama kumi hivi zenye mahesabu na michoro ambayo ilimtoa jasho kuelewa. Akazichukua na kuzibana ndani ya faili na kuahidi kuzifikisha kwenye meza ya wataalam wa Shirika la afya duniani, ili wao nao angalau watambue nini kilikuwa kimeanza kutengenezwa na daktari huyo.

Yule bwana, mara tu baada ya kutoka Philadelphia aliondoka kwa

ndege, moja kwa moja mpaka New York. Hapo hakukaa sana akachukua ndege nyingine kuelekea Geneva yalipo makao makuu ya Shirika la Afya.

Huko karatasi zile zilipokelewa na kuingizwa chumba maalumu. Zikaskaniwa, na vivuli vyake vikaingizwa kwenye kompyuta kubwa ya kuweza kutambua mahesabu hayo. Jopo la watu kama sita hivi walikutana katika chumba hicho wakiwa na vitabu vya kutosha kila mmoja wao. Kanuni na mahesabu, achilia mbali michoro iliyokuwa ikionekana katika kompyuta hiyo kubwa ukutani viliwafanya watu hawa kukuna vichwa. Baada ya saa kama sita hivi ndani ya chumba kile ndipo mmoja wao alipoibuka na hoja.

“Ndugu wajumbe, baada ya kuunganisha na kukokotoa mahesabu haya naanza kupata picha ni nini profesa huyu anafanya...”

Wote wakashtuka na kumtazama, wengine wakavua miwani wakitega masikio wasikie ni nini ambacho mwenzao ametambua. Akatoka pale alipo na kwenda upande wa mbele na kusimama, akawatazama wajumbe wenzake na kisha akaanza kwa kuwaambia.

“Sir. Drostdyhof Fenegan, nafikiri anajaribu kugundua suluhisho la ugonjwa mbaya kabisa wa *AIDIOSIS* unaosumbua huko Afrika. Katika kuunganisha mahesabu yake kama tunavyoona hapa...” akatembeza kidogo ile kompyuta na kufikia katika aina fulani ya kanuni iliyozungushiwa duara kwa wino mwekundu, akawaeleza.

“Nimekuwa nikiangalia kwa makini hii kanuni, katika vitabu vya kikemia kanuni hii haiko sawa sana, kuna kitu kimeongezwa, na ndipo nilipoanza kuifuatilia kwa makini na kuona kuwa huyu mtu si wa kawaida. Ukiiangalia utaiona imekosewa lakini haijakosewa,” akawaambia na kila mmoja aliyekuwa amegemea meza akaketi vyema kitini. Maana wote walikwama hapo.

“Sir. Drostdyhof anakaribia kugundua kemikali mbaya kabisa zinazoweza kutengeneza virusi vipya ambavyo amefikiria kuviita *Amphibiot* kadiri ya maelezo yake ya mwishoni aliyoyaandika kwa Kigiriki. Katika kanuni ya mbele inaonekana wazi anataka kuona ni jinsi gani virusi hivi vinaweza kumuathiri mwanadamu kama vikipandikizwa mwilini mwake. Wasiwasi wangu ni kwamba anaweza kuwa anataka kutengeneza dawa ya kuumaliza kabisa ugonjwa wa *AIDIOSIS* duniani. Kwa maana, ukitazama hapa...” akaonesha, “na huku mwisho, nilichokifanya nilirejelea kitabu namba tano ndipo

nikagundua ukaribu wa unyume wa kanuni hizi. *He is a genious!*” Baada ya kusema hayo kila mmoja ndani ya kile chumba akapiga makofi huku akisimama. Hii ilimaanisha kwamba wamekubaliana na hilo na kumkubali Sir. Drostdyhof katika tafiti hiyo.

“Lakini nasikitika kusema kwamba, inaonekana hapa kuna kipande kingine cha kanuni hizi hakipo hivyo hatuwezi kujua kafikia wapi katika tafiti hii. Ila nitakuwa sahihi kuwaaminisha kuwa anatokomezwa *AIDIOSIS* au alikuwa na lengo jingine tu? Hakuna maelezo,” akasema na kurudi mahala pake huku akiacha minong’ono kati ya wajumbe wa kikao hicho.

* * *

PHILADELPHIA

Cindy na Kelvin waliwasili katika jimbo la Philadelphia asubuhi na mapema tangu waondoke usiku uliotangulia kule Virginia. Wakiwa kama wasiojuana, kila mmoja alichukua usafiri wake na kutafuta hoteli ambayo ingemfaa, huku wakikubaliana muda wa kukutana na mzee huyo nyumbani kwake pasi na miadi yoyote.

Ikawa hivyo. Saa sita mchana, Cindy alikuwa wa kwanza kuwasili katika vilima vya Minsi, East Srondburg ambako makazi ya Sir Drostdyhof yalikuwepo.

Nyumba yake ilijengwa peke yake, ikizungukwa na miti mingi. Gari lake lilionekana wazi tu, limeegeshwa mahala pake, lakini mlango mkubwa wa kutokea nje ulikuwa umefungwa. Wakati Cindy akiukaribia mlango huo, mara akasikia michakacho ya miguu ya mtu nyuma yake, akageuka na kukutana macho kwa macho na Kelvin.

“Vipi?” Kelvin akamtupia swali.

Cindy hakujibu kwa maneno bali kwa ishara ya mkono ikimaanisha, anahisi yupo ndani. Wakabonyeza swichi ya kengele mlangoni. Hakuna aliyekuja kufungua. Dakika kama kumi na tano hivi zikapita, hakukuwa na majibu. Kelvin akachukua funguo zake na kukitekenya kile kitasa, mlango ukafunguka pasi na ubishi. Wakaingia. Kila mmoja akakamata bastola yake tayari kwa lolote.

Ukimya wa nyumba hiyo, kwa kiasi fulani, uliwatisha vijana hao. Kila mmoja akapita upande wake na kukutana nyuma ya nyumba.

Walilakiwa na uwanja mkubwa wenye nyasi za kijani iliyowiva. Pembeni yake kulikuwa na kitu kama zizi dogo, ndani kulikuwa na maua mengi na vibanda vidogovidogo vilivyjengwa kwa umahiri na mpangilio uliyovutia. Cindy akaipachika bastola yake kiunoni na kutaka kusogelea zizi hilo. Kelvin akamzuia na kumpa ishara atazame juu kidogo, karibu na paa. Ndipo akaona kamera ya usalama. Iliyowekwa kwa kazi ya kumwona kila akaribiae zizi hilo. Kamera hiyo ingetoa taarifa katika vyombo vya usalama mara moja.

Kelvin akatumia darubini ndogo kutazama nini kilichopo ndani. Aliweza kuona mabanda yale vizuri na ndani yake kulikuwa na aina mbalimbali za wadudu kama, mijusi, nge, buibui na wengine wengi. Wadudu wote unaowajua wewe wenye sumu ya kufisha mwanadamu walikuwa ndani ya zizi hilo. Kelvin alihisi mwili ukisisimka akampa darubini hiyo Cindy. Alipoipachika machoni tu akaishusha mara moja.

“*Shit!!*” akang’aka.

Wote kwa pamoja wakaingia ndani ya nyumba hiyo na kuachana na lile zizi. Kelvin aliposukuma mlango ukasukumika. Akaita kwa sauti jina la mzee huyo, kimya! Wasiwasi ukawajaa na kukamata bastola zao tena. Wakapita kila chumba na kona ya nyumba hiyo, hakuna mtu.

“Hayupo,” Cindy akamwambia Kelvin huku akiishusha bastola yake. Wakaanza kupekua nyumba hiyo hapa na pale, hakuna cha maana walichokipata.

Kabla hawajaamua kuondoka, Cindy akakumbuka kutazama kompyuta iliyo juu ya meza ndogo, katika moja ya kona za nyumba hiyo. Akaiwasha na kufanikiwa kuvunja nywila zake, akapekuwa hapa na pale asione cha maana isipokuwa tu alipoamua kuingia katika barua pepe za daktari huyo.

“Kelvin!” akaita.

Kelvin ambaye muda huo alikuwa ametingwa, akitazama buibui aliyewekwa ndani ya dawa maalumu chupani, namna alivyokuwa akibadilika rangi; mara hii, mara ile. Akasogea kwa Cindy na kutazama kile anachomuonesha.

Nakala ya tiketi ya ndege aliyotumiwa kutoka shirika la *Qatar*.

“Amesafiri asubuhi hii ya leo,” Cindy akasema.

“Amekwenda wapi?”

“*Flight* yake ni kutoka Philadelphia mpaka Doha kisha anaelekea ... aaaaa Dar es salaam, Tanzania!” akasema huku akimgeukia Kelvin.

Kelvin akatikisa kichwa, na kuiangalia kwa makini tiketi ile. Akampa mwanamke huyo kadi mmweko ili ahifadhi nakala laini hiyo. Kisha wakaondoka zao na kuiacha nyumba hiyo kama walivyoikuta. Dakika kumi baadaye, wakapeleka taarifa *Unity X* kama walivyoamriwa. Na baada ya dakika chache tu wakupata ujumbe.

Follow him and find out what he is up to over there!

Ujumbe waliotumiwa uliwataka wamtafute na wahakikishe wanajua nini anakifanya huko alikokwenda.

SURA YA 3

DAR ES SALAAM

HALI YA HEWA ya jiji la dar es salaam ilikuwa ya joto kama kawaida. Hii haikufanya wakazi wa jiji hili kuacha shughuli zao. Lah. Bali ndiyo kwanza zilipamba moto. Mabaa yalisheheni walevi, madangulo yalijaa wazinzi na waasherati, iliimradi tu maisha yalikuwa yanasonga. Upande mwingine wa jiji hilo hilo, watu walikuwa wakilia na kuomboleza kwa kuondokewa na mpendwa wao. Nyakati hizo vifo vilikuwa si vya kuogopa tena, kwani kila wiki watu walizika na kikubwa ilikuwa ugonjwa mbaya kabisa wa *AIDIOSIS*.

Saa 2:30 usiku

Katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere, ndege ya shirika la Qatar ilitua salama salimini usiku wa manane wa jumamosi hiyo. Kati ya abiria waliofikishwa na ndege hiyo alikuwapo Sir. Drostdydhof Fenegan. Hakuwa na presha, kana kwamba analijua jiji hili kumbe hata kufika tu, ni mara yake ya kwanza. Baada ya ukaguzi wa kila kitu, akatoka nje na kukaribishwa na taa kali za uwanja huo. Mashanta wa magari ya kukodi walishamfikia na kumdaka hima hima. Aliwatazama kwa zamu kana kwamba hawaoni, lakini ukweli ni kwamba hakujua wanaongea nini kutokana na kutoijua lugha ya Kiswahili sawasawa.

“Kilimanjaro Hotel,” akamwambia kijana mmoja aliyemchukua kistaarabu katika gari lake.

“*Ten Dollars!*” Yule kijana akamwambia mgeni wake akimaanisha ni dola kumi tu kwa safari hiyo. Sir. Drostdydhof akatoa pochi yake na kuchomoa noti hiyo kisha akatulia kitini na kijana yule akafanya

kazi yake. Dakika kumi na sita hivi tayari walikuwa katika hoteli hiyo, kutokana na usiku huo kutokuwa na foleni za magari. Haikuwasumbua sana kufika japo dereva hakuwa anakwenda mwendo mkali.

“Karibu tena!” akamwambia mgeni wake naye akatikisa kichwa tu juu chini kuashiria kuwa ameelewa kumbe lah.

* * * *

Ndani ya hoteli hiyo hakuupata usingizi kabisa, kompyuta yake ndogo ilikuwa mezani akiendelea kufanya hiki na kile huku kitabu chake cha kumbukumbu kikiendelea kumeza michoro ya kutisha ya kisayansi.

Kati ya Watanzania Milioni arobaini, mzee huyu, alikuwa akimfahamu mmoja tu na huyo ndiyo hasa aliyelenga kumfikia na kuanza kazi yake. Lakini hakujua hata atampataje maana tangu walipoachana ni zaidi ya miongo miwili imepita.

* * * *

HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI

Siku iliyofuata

Kama ilivyo ada katika hospiatali hii, watu walikuwa wakipishana huku na huko kuja kutazama wapendwa wao wanaoendelea kuzipigania afya zao mahala hapo. Wapo waliotoka mikono kichwani huku wakilia, wapo waliotoka wakifurahi baada ya kukuta wapendwa wao wameruhusiwa kwenda nyumbani na kadhalika, ili mradi tu hali zote mbili za maisha zilikuwapo.

Katika wodi moja kulikuwa na wagonjwa mahututi, wengi wao wakiwa wamekonda na kufanya mifupa ya miili yao kuhesabika. Vidonda na malengelenge vikiwa vimewajaa midomoni na sehemu mbalimbali za miili yao. Dkt. Edward Minzi, mtu mzima, alikuwa akiwapa ishara wauguzi, zenye maana kuwa, ‘mfuniken huyu, hayupo tena’ yaani amekwishakufa. Kama kuna daktari aliyekuwa akiumiza kichwa na kuumia moyoni kutokana na vifo hivi basi ni huyu, Minzi. Hata ungepata nafasi ya kumuuliza angekwambia wazi kuwa ‘sijawahi kuona ugonjwa huu’.

Baada ya kuzungukia wodi yote na kumfikia mgonjwa mmoja mmoja alirudi ofisini kwake na kuketi kitako. Ni magazeti na vitabu vyake vya

kitabibu ndivyo vilikuwa faraja yake kwa kipindi hicho, maana hakuwa na msaada mwingine kwa watu hao zaidi ya kuwapa maneno yenye faraja wasubiripo vifo vyao.

Kutoka katika ukimya huo aligutushwa na mlango uliofunguliwa ghafla. Muuguzi mmoja akaingia na kusimama mbele ya meza hiyo.

“Dokta, kuna mgeni wako!” akamwambia.

“Mimi?”

“Ndiyo wewe”.

“Yukoje? Mwanamke au mwanaume?” akauliza huku akifunga kitabu chake.

“Ni mwanaume, mzee wa Kizungu!”

“Mzungu!” akanyamaza kidogo, “Mwambie aingie,” akaruhusu kisha akajiweka tayari kumpokea. Kweli, alikuwa Mzungu, mtu mzima, mvi chache za kuhesabika ziliota hapa na pale kichwani mwake na kuufanya upara ung’ao kuwa wazi. Akavuta kiti na kuketi kwa mtindo wa kutazamana na daktari huyo.

“Karibu sana, nikusaidie?” akamuuliza lakini kutokana na kuwa mzungu huyo alimtumbulia macho tu, akagundua kuwa haelewi lugha hiyo akabadili na kuanza kuongea naye Kiingereza.

“Ninakufahamu na nimekuja kukutafuta wewe mwenyewe, mimi ni Sir. Drostdyhof Fenegan.” akajitambulisha.

Dkt. Minzi hakuamini, akafurahi sana kumuona mzee huyu, profesa, ambaye kwa nyakati chache sana za masomo yake aliwahi kutumia vitabu vyake na kuhudhuria mihadhara kadhaa. Hakutegemea na wala hakuwahi kufikiri kama atakuja kukutana na mtu huyo maishani. Hapo juu ya meza yake tu, kati ya vitabu alivyovipanga kilikuwapo kilichoandikwa naye, daktari mbobevu katika masuala ya kemia.

“Karibu sana *Sir*! Umepajuaje hapa?” akamuuliza.

“Mtu hawezi kupotea mahala kama hapa, ukizingatia hii ni taasisi kubwa kiasi kwamba ukiuliza tu unaipata. Nimekuja usiku wa kuamkia leo, na asubuhi hii nimepata uelekeo wa wapi nitakupata, inaonekana unafahamika sana nchini!” akamwambia kisha wote wakaangua vicheko.

“Ndiyo! Ndiyo! Naona umekuja kula likizo kwetu!” Dk. Minzi akamwambia.

“Siyo likizo Edy, nimekuja kazini na nimekutafuta kwa kuwa najua wazi kuwa ni wewe wa kunisaidia,” akatulia na kumtazama daktari huyo ambaye naye, umri ulimchukua kiasi.

“Ndiyo...”

“Nipo kwenye utafiti mkubwa sana kijana...” alimwita kijana kwa kuwa kadiri ya umri wake, alimwacha miongo kadhaa, “...nafanya utafiti wa huu ugonjwa wa *AIDIOSIS*, chanzo na jinsi ulivyotokea,” akamwambia.

Dk. Minzi akajiweka vizuri kitini na kuendelea kumsikiliza.

“Na ninataka niipate dawa yake, kama si chanjo,” akaongeza kusema. “Lakini sitaki kuongelea hili swala hapa, kwani ni swala zito linalohitaji utulivu wa hali ya juu sana, upo tayari kunisaidia?” Sir. Drostdydhof akauliza.

“Bila shaka! Je ni wapi utapenda tukae tuzungumze hili?” Dk. Minzi naye akamuuliza.

“Edy! Waniuliza mimi tena? Nani mwenyeji kati yetu...”

“Aaah ok, sawa nimekuelewa. Eeennhh umefikia wapi?” akamuuliza.

“Kilimanjaro Hotel!”

“Sawa, mimi nina nyumba kubwa sana na unaweza kuishi pale, ni eneo tulivu ambalo litakufanya ufanye kazi yako vizuri,” Dkt Edward Minzi akamwambia mwalimu wake wa zamani.

“Itakuwa ni vizuri sana kijana. Ninachohitaji zaidi ni utulivu”. Baada ya mazungumzo machache, wakakubaliana kuwa Dkt. Edward akamchukue hotelini na kumuhamishia nyumbani kwake jioni ya siku hiyo. Sir. Drostdydhof Fenegan alifurahi sana kwenda kuishi kwa daktari mwenzake, kwani hakupendelea kabisa kuishi hotelini hata hivyo mpango wake ulikuwa ni kukodi nyumba nje ya mji itakayompa utulivu wa kazi yake.

* * *

Siku ya pili baada ya Sir. Drostdydhof Fenegan kuhamia kwa Dkt. Edward Minzi, ndipo usiku huo wakapata nafasi ya kuzungumza. Katika uwa mkubwa wa nyumba hii, kulikuwa na maua mengi sana na utulivu wa hali ya juu ambao ungeweza kumtuliza mtu yeyote na kumuondolea msongo wa mawazo aliyonao. Pamoja na umri aliyokuwa nao, Eddy hakuwahi kuoa au kuwa na mchumba.

Vikombe viwili vya kahawa vilikuwa vikijidai kati ya mtu na mwanafunzi wake.

“Yes! Sir,” Dkt. Edwardakaanzisha mazungumzo.

“Hujaacha kutumia jina hilo?” akamuuliza.

“Kamwe siwezi kuacha, kwani katika maisha yangu nimekutana na

mwanadamu mmoja tu mwenye hadhi hiyo ya 'SIR', najisikia furaha kukuita hivyo. Haya nipe mpango wako wa kazi..." Dkt. Edward akamtania mgeni wake.

"Sikia... ujio wangu huku ni wa kichunguzi kama nilivyokwambia, nipo kwenye uchunguzi wa siri sana kuhusiana na huu ugonjwa wa *AIDIOSIS*. Naumia tangu ndani kuona rafiki zangu Waafrika wanateketea kama inzi. Sijamshirikisha mtu, huu ni utafiti wangu binafsi. Na ninaweza kusema kuwa nilipofikia panaridhisha. Sasa nimekuja huku kwa mambo makubwa matatu; kwanza ni kuona mgonjwa aliyeambukizwa hivi karibuni, na kuchukua sampuli ya damu yake, pili nahitaji kuona mgonjwa aliyekwishaathirika kabisa, ambaye yupo kwenye hatua mbaya ambaye kila kitu kimejionesha, nahitaji kuona kwa macho maana kuna vitu navihitaji ili nikamilishe awamu ya kwanza ya uchunguzi wangu. Jambo la tatu ni kutafuta sasa mbadala wa virusi hivi, ili nitengeneze dawa ya kumaliza kabisa tatizo hili kwa Mwafrika. Tayari kuna aina ya virusi mbadala nilivyovipa jina *Amphibiot* ambavyo nimeanza kuvigenerate kinadharia ili vipingane na hivi. Vita ipigwe ndani ya mwili wa mwanadamu," Sir. Drostydhof Fenegan akamaliza na kuinua kikombe chake cha kahawa na kupiga funda moja, imepoa.

Dkt. Edward akajikuna kichwa, kisha akakitikisa kana kwamba kuna mdudu kaingia ndani yake, akajikohoza na kumtazama mzee huyo, "unafikiri ni jambo jepesi kupata suluhisho?"

Sir. Drostydhof akasitisha kunywa kahawa aliyoiongeza kikombeni; akashusha na kukiweka mezani.

"Ndiyo maana Waafirika mnakosa maendeleo!" akamwambia.

"Oh! *Sorry!*"

"...Kwa sababu kila kitu kwenu hakiwezekani, sivyo... kila kitu ni jitihada tu. Kama Waafrika mkijituma katika tafiti hizi mnaweza kuukomesha huu ugonjwa lakini mkiitegemea Ulaya kamwe hamtajitawala, na kamwe hamtajivunia Uafrika wenu. Sikia, nataka nikupe siri, na iwe siri yako tu. Huu si ugonjwa kama mnavyouona. Hili ni bomu au niite shambulio la kibaiolojia. Na bado yapo mengi yametegwa kwenye miili yenu Waafrika, siku yatakapolipuka mtalia na kusaga meno. *Life Span* yenu itakuwa miaka arobaini mpaka hamsini, Mwafrika hatoweza kuzaa tena kwa njia ya kawaida isipokuwa oparesheni, na kwa sababu hii vifo vya akina mama vitakuwa vingi kwa kukosa damu na kadhalika. Nimechunguza, na nimehakikisha hilo. Virusi hivi hatari vya *Ostrogonus*

vinadhoofisha kinga za mwili na kuzimaliza kidogo kidogo. Na baadhi ya dawa mnazowapa wahanga hao, zipo kinyume na virusi hivi. Kwamba ikiingia katika damu, haiwi sumu kwa virusi badala yake huwa chakula na kuwapa afya ili waendeleo kutenda kazi yao kwa ufanisi...” Sir. Drotydhof alimwambia Edward.

Ukimya ukatawala kati yao, Dkt. Edward Minzi akamtazama mzee huyo kwa nukta kadhaa na kisha akafungua kinywa chake.

“*Sir!* Hapo umenifumbua macho! Sasa wewe huoni hatari kwa kazi unayoifanya? Vipi wakikufuatilia, utajitetea vipi?” akamuuliza.

“Hawatoweza kujua, maana ninatumia *formula* za juu sana katika Kemia na Baiolojia,” akachukua kijitabu chake na kukifungua kurasa ya kwanza mpaka mia mbili hamsini.

“Umeona? Kuanzia moja, nimekokotoa hizi *formula* mpaka kurasa hii ya mia mbili hamsini. Nilipofika hapa sasa ili formula hii iendelee nahitaji hizo sampuli nilizokwambia nizifanyie kazi, nikimaliza hizo tu, inabaki kazi moja kubwa na ngumu kuliko zote,” akamwambia kisha akafunga kile kitabu chake.

“Nimekuelewa!” Dkt. Minzi akajibu, “Nitakusaidia,” akaongeza.

* * *

SIKU MBILI BAADAE

Cindy aliwasili Dar es Salaam akiwa katanguliwa na Kelvin kwa siku moja. Joto likamlaki akawa hana ujanja wa kulikwepa. Alipata faraja tu kwa kuwa gari alilopanda lilikuwa na kiyoyozi safi. Rangi ya mwanamke huyu iliuficha U-marekani wake, na upole nao ukatulua juu ya ukatili aliomezeshwa mafunzoni.

“New Afrika Hotel tafadhali!” akamwambia dereva naye bila kujibu akawasha gari na kuondoka kwa kasi kumuwahisha mwanadada huyo aendako.

Njiani hakukuwa na mazungumzo kati yao, kwani wakati mwingine ung’eng’e nao shida, hasa ukikutana na huu wa Kimarekani. Dakika arobaini na tano, taksi ikaegeshwa kwenye maegesho ya hoteli hiyo kongwe nchini iliyojengwa mita chache kutoka Mzunguko wa sanamu ya Askari, kando ya Barabara ya Azikiwe.

“*Here we are, madam!*” yule dereva akamwambia mteja wake huku macho

yake yakishindwa kujizuia kuangalia mapaja makubwa na matamu kwa macho, yaliyojaa nyama zenye kusesimua kila rijali. Mara baada ya malipo, Cindy akateremka na kupokelewa mizigo yake. Akangozwa chumbani pindi tu alipomaliza itifaki za mapokezi.

Ndani ya chumba cha hoteli hiyo, Cindy alijitupa kitandani, chali, bila hata ya kuvua viatu, kichwa chake kikachukuliwa na mawazo lukuki juu ya kazi aliyotumwa kuifanya Tanzania. Taratibu usingizi ukataka kumchukua lakini mlio wa simu yake ya mkononi ukamgutusha. Akajiinua na kuinyakuwa kutoka katika meza ndogo iliyo kando ya kitanda na kuiweka sikioni. Hakuwa mwingine bali Kelvin. Simu hiyo ilimtaka Cindy kukutana na kijana huyo kwa chakula cha jioni katika hoteli ya Jangwani Sea Breeze.

“Ok nitafika!” Cindy akajibu na kukata ile simu kasha usingizi ukamchukua mpaka sayari ya mbali.

* * *

JANGWANI SEA BREEZE

Saa mbili usiku iliwakuta Cindy na Kelvin katika hoteli hiyo. Sharubati ya embe na kukuchoma vilikuwa vikiteketea.

“Vipi umenusa chochote?” Cindy akamuuliza mara tu baada ya kujuliana hali.

“Ngumu. Nimehakikisha kuwa amefika hapa Tanzania, lakini bado sijajua ni wapi yupo. Katika fununu nilizopata, ni kwamba amefikia Hoteli ya Kilimanjaro lakini sijawahi kumwona akiingia wala kutoka,” Kelvin akaeleza.

“Na jamaa zetu je?” Cindy akachimba zaidi.

“Hawana taarifa ya mtu huyo, lakini wameahidi kutusaidia kujua ni wapi yupo,” Kelvin akaendelea kusema.

Baada ya Cindy kupiga fundu moja la sharubati akamtazama tena kijana huyo, kisha akachukua simu yake na kugusagusa hapa na pale.

“Sikia! Nilijaribu kutazama katika mtandao kama kuna *connection* yoyote huku kwa upande wa Sir. Drostdhof. Nimegundua kuwa kuna daktari mmoja aliyewahi kuwa mwanafunzi wake miaka kama ishirini hivi iliyopita, vipi hawezi kuwa yupo naye?” Cindy akauliza kwa mashaka.

“Umejuaje?” Kelvin akatikisa kichwa na kuuliza.

“Nilikuwa napitia mawasiliano na nyasifu zake, kwenye huu mtandao wa *LinkedIn* nimepata hilo!” Cindy Brightone akamwambia Kelvin. Mwanamke huyu alipokuwa safarini, kazi kubwa ailiyokuwa akiifanya ni kuchunguza mahusiano ya Sir. Drostdydhof na Tanzania kupitia mitandao ili walau aweze kujua kama ana ndugu au rafiki. Baada ya kuzama katika upekuzi huo kwa mtandao na kujaribu kuvunja kodi za mitandao fulani fulani ikiwamo huo wa *LinkedIn* ndipo alipogundua kuwa, kuna mtu mmoja ambaye ana mahusiano ya moja kwa moja naye ilhali Kelvin akijua kuwa mtu wao yupo Hoteli ya Kilimanjaro. Kila mmoja alikuwa sahihi kwa upande wake.

“Inawezekana,” akajibu.

“Basi tutafute wapi anaishi na tuanzie hapo, anaitwa Dkt. Edward Minzi ila haijaandikwa anafanyia kazi wapi, hiyo mpaka tuifanyie uchunguzi tena kwa vyanzo vya ndani,” Cindy akasema.

“Bila shaka, kesho tutaaulizia mpaka tumpate na kazi yetu tutaifanya na *partner*” Kelvin akaongeza kisha mazungumzo ya kawaida yakaendelea kati yao.

Siku iliyofuata...

Jengo la Shirika la Bima au wengi huliita ‘Kitega Uchumi’, lililopo katikati ya Jiji la Dar es salaam, juu, sakafu ya nane, mlango wa kwanza kushoto uliandikwa kwa maandishi ya nakshi za madini ya fedha *J & K Group of Companies*. Ndani ya ofisi hiyo kulikuwa na mtu mmoja mrefu mwenye mwili mkubwa aliyetambulika kwa jina la Johnson Kasalu. Johnson Kasalu ni kijana Mtanzania aliyezaliwa na kukulia huko Marekani. Wazazi wake walihamia huko miaka mingi sana wakitafuta urahisi wa maisha. Wakazeeka na hata kufia huko. Yeye alipokuwa kijana akapata elimu yake huko na kuchukua uraia wa nchi hiyo mara alipotimiza miaka kumi na nane kama ilivyo sheria au utaratibu wa nchi nyingi duniani kwa watoto ambao wazazi wao ni wahamiaji.

Akiwa huko Manhattam ndiko alikopata nafasi ya kujiunga na shirika hili la kijasusi la Marekani ‘CIA’. Na baada ya kufanya kazi nao kwa zaidi ya miaka kumi, akatumwa kuja Tanzania. Hapa nchini akaingia kwa kifuniko cha mfanya biashara na kufungua kampuni kubwa ya kupokea na kutuma mizigo duniani kote akaipa jina la J & K, lakini nyuma yake alikuwa na kazi maalumu aliyotumwa kuifanya na shirika

hilo.

Mlango wa ofisi hii ukafunguliwa, na karani wake akaingia ndani na kumpa taarifa ya ugeni.

“Waambie waingie!” akamwambia. Yule msichana akawaruhusu wale wageni waingie ndani, nao wakafanya hivyo. Walikuwa wawili, mwanamke na mwanaume. Mwanaume Mzungu na mwanamke Mweusi.

“Karibuni!” akawakaribisha viti, “Karibuni sana nawasikiliza,” akaongeza kusema huku akijiweka vema kitini.

“Asante, bila shaka ni Bwana Johnson Kasalu!” Cindy akawa wa kwanza kusema na yule bwana akatikisa kichwa huku akiwaangalia kwa zamu.

“Your brothers, from Langley?” Kelvin akatambulisha kikazi zaidi.

“Karibuni sana, *identity* please,”

Cindy na Kelvin wakatoa vitambulisho na kumpatia, Johnson akavitazama na kuvipachika katika kifaa maalum cha kielektroniki kilichfungwa kwa siri chini ya meza yake ya ofisini. Aliporidhika kuwa wapo sahihi, akawarudishia. Kisha akachukua mashine nyingine ndogo kwenye saraka ya meza yake. Akaiweka mezani. Akawataka kila mmoja kuweka kidole cha kati kwenye kifaa hicho. Cindy akawa wa kwanza kuweka na baadae Kelvin. Dakika moja baadaye taarifa za watu hao zikaonekana kwenye kompyuta yake. Taarifa zile ziliwatambulisha vijana hao kama wakala wa shirika hilo, wasifu wao na mpaka namba za utambulisho za siri.

“Sawa! Nafikiri ujio wenu una jambo japokuwa sina taarifa kamili,” Johnsona akaanzisha mazungumzo.

“Yeah, tumekuja kuna mzigo tunaufuatilia, mzigo huu umetokea Philadelphia,” Cindy akamwambia.

Johnson akamkatisha kwa kumwonesha mkono, “Sir. Drostdyhof Fenegan?” akamuuliza.

“Exactly,” Kelvin akadikia.

“Yeah! Huu mzigo upo hapa nchini kama siku tano sasa. Enhe, nipeni mpango,”

“Tumekuja kuufuatilia, lakini tumeupoteza. Sasa kuna huyu daktari anaitwa Edward Minzi, tunahitaji kujua anafanya kazi wapi na anaishi wapi. Hatutaki kuonana naye, sisi kazi yetu ni kuangalia tu mtu wetu anafanya nini,” Kelvin akasema.

“Mnamhisi?” akawauliza

“Ndiyo, ni sehemu pekee ya kuanzia kwa sasa,” Cindy akajibu.

“Sawa, hiyo ni kazi ndogo sana, japokuwa kwa nchi kama hii ya Tanzania, hawajaimarisha sana mitandao ya utambuzi wa watu kama kwetu, lakini tutampata. Sasa kuna uhusiano gani kati Sir. Drostdydhof na huyo Minzi?” Johnson akauliza.

“Ipo hivi, katika upekuzi wetu tumegundua kuwa huyu Sir. Drostdydhof anamjua raia mmoja tu wa Tanaznia naye ni huyu Dkt. Edward kwa sababu aliwahi kuwa mwanafunzi wake huko Moscow miaka kama ishirini na tano iliyopita. Sasa wasiwasi wetu ni kuwa kama hayupo pale Kilimanjaro Hotel basi anaweza kuwa yuko kwa huyu daktari,” Kelvin akaeleza.

“Ok, hisia yenu iko sawa, sasa huyu daktariiiiiiii.... Ngojeni kidogo,” akachukua simu yake na kuanza kuperuzi hapa na hapo na kisha akaiweka juu ya meza na kati yao mazungumzo yakaendelea.

Baada ya dakika kadhaa simu ya Johnson ikapata uhai, akaichukua, akatazama kwenye kioo, baada ya sekunde chache akaitua tena mezani na kuwatazama wageni wake..

“Dkt. Edward Minzi, anafanya kazi Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na anaishi eneo moja linaitwa Salasala,” akawaambia na kuwaonesha picha ya daktari huyo iliyotumwa kwenye rununu yake. Wote wakaitezama na kuihifadhi vichwani mwao. Dakika ishirini baadae wakaagana, na wawili hawa wakaondoka katika ofisi hiyo huku wakisindikizwa kwa macho ya Jonhson. Nje ya jengo hilo wakaingia katika gari lao na kuondoka kuelekea Muhimbili kwa kutumia kifaa cha mtandao kilichokuwa kikiwaongoza njia.

Tayari ilikuwa saa sita ya mchana walipowasili katika viunga vya hospitali hiyo. Kwa muda mfupi tu, walifanikiwa kujua ni eneo lipi ambalo madaktari hupenda kupata chakula cha mchana. Cindy akaingia mgahawani hapo huku akimwacha Kelvin garini. Mitego yao haikukaa bure kwani nusu saa baadae Dkt. Edward Minzi akifuatana na wenzake wachache wakaingia ndani ya mgahawa huo. Cindy alimwona vyema na kumkariri, tena akahakikisha kuwa ni yeye baada ya kusikia watu wakilitajataja jina lake.

Ingekuwa ngumu sana hata kwako kumtambua mwanamke huyu kwamba si Mtanzania. Muonekano aliokuwa nao ulikuwa wa Kiafrika haswa. Aliketi nyuma kabisa na kuagiza sharubati ya matunda mchanganyiko na kunywa taratibu huku miwani yake ikichukua picha

kadhaa za daktari huyu na kuzirusha mubashara kwa Kelvin. Ndani ya mgahawa huo, daktari huyu na wenzake walichukua kama dakika arobaini na tano hivi, kisha wakaondoka zao. Cindy naye akasubiri dakika kumi nyingine kisha akainuka na kurejea garini na kumkuta Kelvin akiwa bado anatazama kwenye luninga iliyokuwa ikimpa picha zote za daktari huyu.

“Kinachofuata,” akamwambia Cindy wakati akijiweka vyema kitini.

“Kunywa kwanza sharubati hii ya tunda halisi, siyo ya kwenu ya kutengeneza kwa umeme!” Cindy akamwambia huku akimkabidhi chupa yenye kinywaji hicho.

“Kwa tafutishi zangu za haraka, saa za kazi kwa serikali hapa, mwisho ni saa tisa na nusu, sasa ni saa nane kamili. Nafikiri tumsabiri ili tujue wapi anaishi,” Cindy akamwambia Kelvin.

“Sawa!” akajibu na kujiegemeza kitini, mshusho wa pumzi ndefu ukafuatia.

* * * *

Dkt. Minzi alimaliza kazi saa tisa na nusu alasiri. Akiwa hana hili wala lile, akatoka ofisini akiwa katika vazi la kinyumbani. Akaingia kwenye gari lake na kuondoka. Cindy na Kelvin nao wakalitua moto gari lao na kumfuata taratibu. Hawakuwa na lengo baya na daktari huyu isipokuwa walitaka kujua anapoishi ili wahakikishe kama ni kweli kuwa Sir. Drostdyhof yupo nyumbani kwake au la.

Baada ya kutoka pale Muhimbili, Minzi akachukua barabara ya Umoja wa Mataifa na kufika mpaka Daraja la Salenda. Akakunja kushoto kuitafuta Mwenge kwa kupitia Barabara ya Ally Hassan Mwinyi. Pale Morocco akaiacha barabara hiyo na kunyoosha ile ya *Old Bagamoyo*. Hakujua kabisa kama anafuatwa, aliendelea kupiga mluzi huku akiendesha kwa mwendo wa taratibu. Dakika kama sabini na tano hivi, akawasili Kunduchi na kuiacha Barabara ya Bagamoyo kisha yeye akakunja kushoto. Barabara ya vumbi na makorongo machache yaliyofanywa na malori mazito ya kubeba mchanga. Barabara hii mbovu ikamfikisha nyumbani kwake, Salasala. Kwa kutumia rimoti yake, akafungua geti na kuingiza gari lake ndani. Cindy na Kelvin wakapita kwa mwendo mdogo bila kusimama na kuizunguka nyumba hiyo kwa kupita mtaa wa nyuma.

Nyumba ilikuwa ya wastani. Sikubwa sana, wala si ndogo, yenye miti mingi kwa ndani ambayo baadhi yake iliweza kujitokeza juu ya wigo. Baada ya kuzunguka mtaa wa pili, wakatokea tena mtaa wa mbele na kuegesha gari kwenye duka moja linalouza vinywaji. Kutoka ndani ya gari lile waliweza kupata picha kadhaa za nyumba hiyo, kisha wakaondoka zao pasi na kuonekana kutokana na weusi wa vioo vya gari hilo.

* * *

Juma moja baadaye...

Sir. Drostdyhof Fenegan alikuwa ametingwa na kazi aliyokuwa akiifanya. Kitabu chake alikiweka kando kidogo. Macho yake yakiwa kodo katika vioo vya darubini. Darubini hii maalumu ya kisasa iliweza kumsaidia katika kazi yake bila shida. Katika uchunguzi wake huo aligundua aina ya virusi ambao humsababishia mgonjwa mateso makali ya vidonda au mapele. Virusi hao mamilioni walikuwa katika kioo kidogo ambacho tone la damu ya mtu aliyeathirika lilikuwapo. Virusi hivyo vilikuwa vikibadilika badilika maumbo hata rangi. Ndani ya kitabu chake aliendelea kuandika mahesabu yake na kuchora ile michoro ambayo kwayo ni yeye tu alikuwa akiielewa. Aligundua hatua zote tatu za virusi hao katika kumuathiri mwanadamu. Kilichomshangaza na kumshtua ni jinsi ambavyo kirusi huyo anavyojibadili na kufanana kabisa na chembe chembe hai nyeupe, wakati mwingine chembe sahani na kuweza kujiunga nazo katika utendaji ndani ya *plasma* ya mwanadamu.

Mara ghafla, mlango wa nyumba hiyo ukafunguliwa. Mwenye nyumba akaingia na kumkuta mzee huyo kaegemea meza kimya, kalala. Hakumsumbua kwani alijua wazi kazi za hawa watafiti hasa wa kisayansi jinsi zinavyokuwa ngumu na zinazokunyima usingizi. Hii kwake haikuwa ngeni kwani hata akiwa masomoni huko Urusi mara nyingi alimkuta mwalimu wake huyu akiwa kasinzia ofisini. Akaingia jikoni na kutayarisha chakula ambacho kingewafaa wote wawili. Baadae akaelekea katika chumba kile ambacho mzee huyo alikuwa akifanyia majaribio yake. Huko alishuhudia chupa nyingi ndogodogo zenye dawa aina mbalimbali, darubini ya kisasa ya kutazamia sampuli hizo za damu na vitu mbalimbali.

“Hapa kazi si ndogo!” alijisemea huku akizunguka zunguka bila

kugusa chochote. Alipojiridhisha akageuka na kuuelekea mlango ili kutoka katika chumba kile. Macho yake yakavutwa na miwani ya macho iliyokuwa juu kidogo ya meza kubwa ya TV. Kilichomvutia zaidi na kumshangaza ni kwamba ilikuwa ya kike. Akaiendea na kuichukua kutoka pale juu ya lile meza, akaitazama kwa kuigeuza geuza kisha akaitia mfukoni mwa shati lake.

Imetoka wapi? Akajiuliza huku akirudi sebuleni. Mara, akasimama ghafla na kutupa jicho pale alipomwacha Sir DrostdyHof, hayupo! Macho yakamtoka pima, akatazama huku na kule, hola!

“Sir! Sir! Drostdyhof!” akaita huku akiingia chumba hiki na kile. Hakumwona. Akachungulia hapa na pale, hakuna mtu. Dkt. Edward Minzi akaduwa katikati ya sebule yake. Akabaki wima bila kujitikisa kama nguzo ya chumvi ya mwili wa mke wa Lutu. Hakukuwa na yule mzee wala kile kitabu chake hakikuwepo pale. Akatoka nje na kuzunguka bustanini labda angemuona. Ah wapi! Hakuna mtu.

Ameenda wapi huyu mzee! Mbona ananishtua hivi? Akajiuliza na kufikia geti dogo la kutokea nje. Peupe! Hakuna mtu. Akarudi mpaka chumbani kwa Sir. Drostdyhof, akakuta kitanda kinamchekea! Kila kitu kilikuwa kama kilivyo, nguo zake, baadhi ya vifaa vyake na vitabu, vyote vilibaki bila kuguswa isipokuwa vitu viwili tu yaani yeye mwenyewe na kitabu chake alichokuwa akiandika tafiti yake. Havikuwepo

“Shiiiiiiitttt!” akang’aka na kurudi sebuleni, ndipo akaukuta ugeni asiyotarajia. Akasimama ghafla na kumshangaa huyo aliyemkuta hapo.

Mwanamke mwenye mwili wa wastani, aliyevalia fulana nyepesi na suruali ya jinzi ya buluu. Miguuni alikuwa na raba matata sana, *Saucony*. Alisimama kimya akimtaazama daktari huyo aliyeonekana kuweweseka. Hakuwa mwingine, Cindy.

“Tulia! Nipe hiyo miwani!” akamwambia pasi na kuonesha lepe la tabasamu usoni pake. Edward akaichukua miwani ile kutoka mfukoni mwake na kumpatia.

“Na kuanzia sasa, usimtafute Sir. Drostdyhof, na wala usimwambie mtu juu ya hili, ukikiuka, umejiweka pabaya, na roho yako itakuwa mkononi mwangu,” yule mwanamke akamwambia Edward, kisha taratibu akaanza kuuelekea mlango wa kutokea nje. Huku nyuma Dkt. Edward alikuwa akishuhudia mapaja yenye nyama za kutosha ndani ya suruali ile, makalio yaliyofanya mitikisiko ya wastani kadiri ya hatua za mwanamke huyo zinavyopigwa. Aligundua tu kuwa si Mtanzania kutokana na lugha aliyotumia, Kiingereza. Akabaki kasimama huku

akimwewesa midomo yake pasi na kutoa neno lolote. Aliporudiwa na fahamu akajitupa kochini na kushusha pumzi ndefu.

Huyu ni nani? Akajiuliza, kisha akaamua kutoka nje kutazama labda japo atapata kuziona namba za gari kama amekuja nalo. Nje ya geti la nyumba yake hakukuwa na chochote zaidi ya wapita njia wa kila siku. Akarudi ndani na kuingia tena kwenye kile chumba ambacho Sir. Drostdyhof alikuwa akifanyia uchunguzi wa zile sampuli za damu na kipande cha nyama ya mwanadamu aliyeathirika. Kila kitu kilikuwa kama kilivyo. Kichwa cha Edy kikajawa mawazo mengi.

Kwa nini wamemteka mzee wa watu? Kwani anachokifanya si ni kwa faida ya binadamu wote? Maswali hayakuwa na majibu. Zaidi ya hapo alikumbuka kauli moja tu ya mzee yule.

...Hili ni bomu au niite shambulio la kibaiolojia. Na bado kuna mabomu mengi yametegwa kwenye miili ya Waafrika, siku yatakapolipuka mtalia sana...'

Dkt. Minzi akatikisa kichwa kana kwamba kuna mdudu ndani yake.

Sasa naanza kuelewa kwa nini! Akawaza.

'...kama Waafrika mkijituma katika tafiti hizi mnaweza kuukomesha huu ugonjwa lakini mkiitegemea Ulaya kamwe hamtajitawala, na kamwe hamtajivunia uafrika wenu...'

Kila alipojaribu kutuliza kichwa chake alirudiwa na maneno yale ya Sir. Drostdyhof. Yakamtia uchungu sana lakini hakuwa na la kufanya. Baada ya muda mrefu wa ukimya, akapata wazo, wazo lililomfanya aruke kwa furaha.

"Nitaanzia alipoishia," akajisemea, "nitamshirikisha rafiki yangu, daktari mwenzangu mtaalamu wa mambo ya kimaabara".

* * *

NYUMBA NAMBA 9

"Vipi mmempata?" Johnson Kasalu akawauliza rafiki zake.

"Ndiyo, yupo mikononi mwetu, tutamfikisha panapohusika," Kelvin akajibu.

"Sasa mtatumia nyumba namba 5 au 9?" akawauliza.

"Nyumba namba 9 ipo salama sana," Cindy akawahi kujibu.

"Ok!"

Katika jengo moja kubwa la ghorofa tatu huko Masaki, lililotenganishwa na Bahari ya Hindi kwa Barabara ya Haile Selassie,

Cindy na Kelvin wakateremka garini wakiwa wamevaa makoti meupe ya kiganga huku mateka wao akiwa bado kalala usingizi. Wakamchukua kwa machela yenye magurudumu mpaka chumba kilicho chini ya ardhi. Hata walipopita naye mahali penye watu, hakuna aliyejua kama mtu huyo ni mateka bali walidhani kuwa ni mgonjwa mahututi aliyeletwa kwa matibabu. Jengo hilo kubwa lilikuwa ni hospitali ya kisasa sana iliyojengwa na raia wa Canada miaka kadhaa nyuma. Hospitali hii inayojulikana sana Tanzania na nje ya mipaka yake ilikuwa ikijawa wagonjwa kila kukicha kutokana na huduma zao nzuri na zenye ubora wa hali ya juu. Lakini chini ya jengo hili kulikuwa na nyumba maalumu, iliyopewa jina 'Namba 9'. Hii ni moja ya nyumba iliyokuwa ikitumika na jamaa hawa wa *CLA* ukanda wa Afrika Mashariki katika kazi zao za siri kama hii. Si kwamba mmiliki wa hospitali hii hakujua hilo. La hasha! Alilijua vyema kwa kuwa hata yeye alikuwa mmoja wao lakini aliyejiwekea kifuniko hicho cha ukurugenzi wa hiyo hospitali. Ni yeye pekee aliyejua juu ya nyumba hiyo, wafanyakazi wengine hawakujua hilo.

Saa mbili baadaye Sir. Drostdyhf alirudiwa na fahamu. Akafumbua macho na kukutana na watu wawili asiyowajua, huku yeye mwenyewe akiwa juu ya kiti maalumu ambacho hakukielewa sawasawa, alikifananisha na kile cha mganga wa meno, lakini hapana. Akawatazama kwa zamu watu wale ambao walikuwa kimya kabisa. Mzee huyu akafumba macho yake kwa nguvu na kuyafumbua tena.

"Nipo wapi?" akauliza.

"Philadelphia!" Kelvin akamjibu huku akimtazama usoni.

"Philadelphia?" akauliza.

"Ndiyo na wala usishangae. Umeletwa hapa kutoka Tanzania ili ueleze hasa ni kitu gani kilikupeleka huko?" Cindy akadakiza.

"Siwaelewi!"

"Tunataka tujue juu ya utafiti wako. Kwa kifupi imejulikana kuwa unafanya utafiti wa mbadala wa *program* ya *AIDIOSIS*. Na baada ya kupewa likizo kazini ukaamua kwenda kuufanyia Tanzania," Cindy akatulia kidogo na kumeza funda la mate, kisha akaendelea kuongea, "Unakumbuka kiapo ulichoapa, kwamba hautatoa siri wala kutafuta dawa kwa manufaa binafsi dhidi ya ugonjwa huu?" Cindy akaongeza.

Sir. Drostdyhf Fenegan akatulia kimya hata macho yake hakuyapepesa.

"Wewe mwenyewe unajua nini kinafuata baada ya kiuko hilo," Kelvin akamwambia. Sir. Drostdyhf akaendelea kutulia na kumezwa na

mawazo mazito.

Wamejuaje? Nimetumia kanuni ngumu sana kuficha siri hii! Wapi wamegundua? Wamenipataje? Akajiuliza maswali mfulurizo bila jibu. Akajaribu kukumbuka nini kilijiri lakini hakikuwa na msaada kwake.

* * *

Kumbukizi

Juma moja baada ya Sir. Drostdyhf Fenegan kuwepo katika nyumba ya Dkt. Edward Minzi, hakujua kama maofisa hawa wa *CLA* wamenusa pale alipo na walikuwa wakija jirani kabisa na nyumba hiyo. Kelvin na Cindy walipopata taarifa kutoka Langley kuhusiana na kipi hasa mzee huyo anafanya kufuatia majibu ya udadavuzi wa kanuni zake kufanyika huko Geneva, walipewa kibali kutoka *W.H* cha kusitisha maisha ya mtu huyo kwa njia isiyo ya maumivu kutokana na heshima yake kwa taifa hilo.

Wiki hiyo yote Cindy aliituma *camera* ndogo yenye umbo la mfano wa dondola. Sura na mvumo wa mbawa za mdudu huyo. Akamuingiza ndani kwa mfumo maalum wa kompyuta na kufanikiwa kumnatisha sehemu mojawapo ndani ya nyumba hiyo. Tangu hapo waliweza kufuatilia nyendo zote na utaratibu wa maisha wa mzee huyo akiwa ndani humo na kutafuta jinsi ya kumnasa. Baada ya betri kwisha kwenye kamera hiyo ndipo Cindy alipoingia kwa hila na kuweka miwani yake juu ya meza ya TV ambayo iliweza kumsafirishia picha jongefu moja kwa moja mpaka kwenye gari lao. Hayo yote waliyafanya kwa siku kama kumi hivi. Waliporidhika, siku ya kumi, ndipo Cindy akaingia ndani ya nyumba hiyo. Akamwekea mzee huyo dawa ya usingizi kwenye sharubati aliyokuwa anaipenda ambayo ilikuwa juu ya meza ya kusomea sebuleni hapo ambapo ni sekunde chache tu alikuwa ameketi. Yote hayo waliyafanya pindi tu mzee huyo aliponyanyuka ama kwenda msalani au kuingia mahala pengine. Cindy na Kelvin walitumia sekunde chache tu kukamilisha kazi.

Siku hiyo ambayo mzee huyo alikuwa amefikia pakubwa katika uchunguzi huo, alirudi sebuleni na kuchukua kinywaji chake, akaketi mezani na kujiburudisha ili ampe habari njema kijana wake Dkt. Edward pindi ataporejea. Ndipo alipoanza kuona kizunguzungu na nguvu zinamwishia, akatumia nguvu za mwisho mwilini mwake na

kuivua saa yake akaitupia upande wa pili wa meza.

Rejea Nyumba namba 9...

Kumbukumbu ya Sir. Drostdyhof iliishia hapo. Zaidi akajikuta ndani ya chumba hiki ambacho hakikuwa kigeni sana na macho yake. Kilimwaminisha kabisa kuwa yupo Philadelphia ilhali bado alikuwa ndani ya Jiji la Dar es salaam.

"Do you want to kill me?" akawauliza kama wanataka kumuua. Cindy na Kelvin hawakujibu kitu, walikuwa wakimtazama tu.

"If what you have done will cost your life! It will be," Cindy akamjibu, kama alichokifanya anajua kitagharimu maisha yake basi itakuwa hivyo. Sir. Drostdyhof akatulia. Kijasho chembamba kikamtiririka, akamkumbuka rafikiye mkubwa aliyekuwa naye ofisi moja katika maabara ile ya Philadelphia. Huyu bwana aliwahi kupingana na uongozi wake dhidi ya swala hilo la *AIDIOSIS* na kuahidi mbele yao kutafuta dawa yake. Nini kilitokea? Alipatwa ajali mbaya jioni ya siku hiyo ambayo haikumpa hata dakika moja ya kusema chochote au kuomba maji.

Taswira ya ajali hii mbaya ilimjia Sir. Drostdyhof Fenegan kwa nguvu na kutisha, akajua hana ujanja, kama ni kifo basi alikwishaanza kuinusa harufu yake.

"Hata mkiniua, sasa moto umewaka, hakuna Mwafrika atakayekubali kufa kikondoo. Nilipoishia mwingine ataanzia," akasema na kufumba macho. Mara akahisi kama sindano ikimchoma katika mkono wake. Alipofumbua macho, hisia zake hazikukosea. Dawa ya sindano ile ilipita kwenye mishipa ya damu na kumpunguzia uwezo wa kupumua kama mtu aliyebanwa pua. Mzee Sir. Drostdyhof akajitahidi kujitikisa kutafuta hewa safi, haikuwezekana. Yule mtu aliyemchoma ile sindano, (hakuwa Cindy wala Kelvin) akachukua nyingine na kumdunga kwenye mshipa uleule. Ndani ya sekunde chache tu, Sir. Drostdyhof akahisi unafuu kidogo. Mara baridi kali ikauvamia mwili wake, macho yake yakaanza kupoteza nuru, akamtazama kwa makini yule aliyedunga na kumuona akipotea kwenye giza nene.

Cindy akafumba macho yake alipomwona mzee huyo anamalizia dakika ya mwisho ya uhai wake kwa kuipigania rohoye. Sir. Drostdyhof alifanyiwa kifo cha huruma *'Euthanasia'*, mwisho wake ukafika, akajikuta katika ulimwengu mwingine kabisa ambao kwawo aliona vitu asivyovijua.

Baada ya nusu saa tangu tukio lile lifanyike, Kelvin na Cindy

waliusogelea mwili wa Sir. Drostdyhof na kuuchunguza kama kweli mtu huyo amekwishakufa au la.

"Is dead!" Cindy akasema huku akijifuta kamasi jembamba lililomsumbua puani mwake. Yule daktari aliyeendesha zoezi lile, akachukua faili na kumpatia Kelvin asaini, naye akasaini na kumpa Cindy naye akafanya vivyo hivyo. Wote wakasaini kuwa wameshuhudia Sir. Drostdyhof akiuawa kwa njia hiyo kama walivyoagizwa.

SURA YA 4

KATIKATI YA MSITU WA LONDO

MIEZI SITA ILIPITA TANGU TUKIO la kuuawa kwa siri kwa Sir. Drostdyhof Fenegan kutokea. Wamarekani na watu wengi walimlilia kutokana na mchango wake katika medani ya tiba. Walichoambiwa ni kuwa daktari huyo alikufa kwa malaria kali aliyoipata huko Tanzania. Makabrasha yake yote ya utafiti yakahifadhiwa huko Geneva na wengine wakakumbushwa kiapo walichoapa.

'Hatakinvi mtu yeyote kugusa chochote katika program hii ya AIDIOSIS mpaka malengo ya wakubwa yatakapotimia'.

Huo ulikuwa mstari wa mwisho kabisa uliofunga kabrasha la maagizo na maonyo juu yake.

Katika maabara kubwa ya serikali iliyojengwa katikati ya msitu mnene wa Londo mkoani Lindi, tafiti mbalimbali zilikuwa zikiendelea. Chumba kimoja hakikuruhusiwa kabisa watu kuingia na ndani yake kulikuwa na watu wanne tu, kila mmoja akiwa ametingwa kwenye meza yake akiendelea na kazi hiyo ya uchunguzi.

Katika meza moja ndani ya chumba hicho kulikuwa na mdudu mmoja mithiri ya mende. Mdudu huyu wa ajabu kidogo kwa jinsi alivyoumbwa alikuwa akijaribu kuruka huku na huku asiweze kwa kuwa alikuwa ndani ya chupa. Na wengine kama hao walikuwa wamekusanywa na kuwekwa katika chumba maalumu.

Dkt. Edward Minzi na timu yake walipata habari ya mdudu huyu kutoka kwa wanakijiji walipokuwa wakifanya utafiti wa mimea fulani huko msituni.

"Sisi huku waganga hutupaka majimaji ya mdudu huyu na tunapona vizuri tu!" Mama mmoja wa Kimwera alimwambia Minzi. Ilikuwa

ngumu kuamini, lakini wao kama watafiti, wakamchukua mdudu yule wa ajabu na kuingia naye ndani ya maabara hiyo. Baada ya mwezi mmoja wa uchunguzi wao juu ya mdudu huyo, waligundua kuwa ndani ya ugiligili wake kuna chembechembe hai ambazo zikikutana na damu ya mwanadamu huziathiri zile zote ambazo hazina asili ya mwanadamu na kuzifanya zisifanye chochote. Walipogundua hili, wakafanya zoezi la kukusanya sampuli hii ya wadudu ndani ya msitu huu na kuwekwa pamoja katika eneo maalum. Hatua nyingine iliyochukuliwa ni kuufunga msitu wote dhidi ya shughuli za kibinadamu kwani ilisemekana aina hiyo ya wadudu inapatikana hapo tu katika ulimwengu mzima.

“Vipi?” sauti ilimshtua Dokta Fabian aliyekuwa ametingwa kumwambia mdudu huyo.

“Sasa naweza kuchukua sampuli yake ili kuona ana wadudu gani,” akamwambia huku akichukua sindano moja ndefu na nyembamba zaidi ya ile ya kumdunga mwanadamu. Akamdunga yule mdudu na kufyonza ugiligili kutoka ndani ya mdudu yule kiasi cha kutosha.

Ugiligili ule ulikuwa mzito kiasi, akauweka kwenye kifaa maalumu kisha akachanganya dawa fulani na kuweka kwenye chombo kingine kinachozalisha joto la kiasi ili kuufanya ugande. Zoezi hilo halikuwa dogo kama unavyofikiria. Mafanikio yalianza kuonekana baada ya miezi sita mingine. Na baada ya kugundua ukweli kwamba aina hiyo ya mdudu haijawahi kuonekana duniani wakaamua kuipatia falme yake kisayansi kwa kuwa hakuwepo kwenye *Kingdom* yoyote inayojulikana. Jopo lile likaazimia kuita *Kingdom Londo* na kuweka kabrasha hilo tayari kuwasilisha kwenye taasisi maalumu za Umoja wa Mataifa ili kulifanyia utafiti zaidi.

* * *

Miezi tisa baadae...

Jopo la watafiti lilikutana katika chumba cha mikutano ndani ya maabara hiyo huko Londo. Lengo la kikao ilikuwa ni kutathmini wapi wamefikia katika utafiti wao dhidi ya ugonjwa wa huo. Walikuwa wanne, wawili walikuwa madaktari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kanali Kasiga na Meja Malege, wengine walikuwa ni Daktari Edward Minzi kutoka Idara ya kuhudumia waliothirika na ugonjwa huo na Ziada Kipele Teknolojisti wa maabara kutoka Wizara ya Afya. Jopo lilikamilika na Dk. Minzi ndiye hasa aliyetoa changamoto hii ya

kufanya utafiti huu. Hata walipoomba ruzuku serikalini wakapata bila kikwazo na ndipo wakaunda kikosi kazi na kujificha ndani ya maabara hii, kitengo cha utafiti huko Londo, katikati ya msitu mnene.

“Tumefanikiwa kiasi gani?” Dk. Minzi akamuuliza Ziada.

“Kiasi kikubwa sana, mimi na wenzangu Malege na Kasiga tumeweza kuunganisha *formula* mbalimbali kutoka vyanzo anuai na kutengeneza kitu ambacho hatuwezi kukiita dawa lakini chaweza kuwa chanjo,” akaeleza huku wengine wakisikiliza kwa makini.

“Ndiyo kwa sababu sote tunajua wazi kuwa *virus* huwezi kumuua na wala hana dawa, lakini tumegundua hii kitu ambayo itamfanya ashindwe kuishi kwenye damu ya mtu aliyedungwa dawa hii,” Kalege akaongeza.

“Kama tulivyoongea katika kikao kilichopita, hapa tumefanya kuunganisha vitu viwili vikubwa ambavyo kwavyo imetuchukua muda sana kupata majibu yake. Unga unga wa moyo wa mti wa *Ngomus Nditus*...”

“Ukisema moyo, unamaanisha nini?” Edward akamkatisha Ziada kwa swali.

“Oh samahani! Nikisema moyo wa mti namaanisha *pith of the tree*, yaani ile sehemu ya katikati ya mti. Sasa tulipo weka vitu hivi pamoja yaani unga wa *pith* ya mti wa *Ngomus Nditus* na ugiligili wa yule mdudu Londo tumepata matokeo chanya kabisa. Tulipoweka mchanganyiko huo na damu hai iliyoathirika tumeona udhoofu mkubwa sana wa virusi huyu, ijapkuwa hafi kabisa,” Ziada akaeleza matokeo namba moja ya utafiti wao.

Kisha Daktari Fabian, mbobevu katika maswala ya baiolojia akawasilisha ugunduzi mwingine, “Lakini pia kuna matokeo mengine katika hili, mchanganyiko huu tulipoweka katika damu hai ya mwanadamu isiyoathirika, kisha kuiwekea ile iliyoathirika, virus huyu hafanyi kazi kabisa! Yaani anaingia kwenye damu na kubaki kama alivyo...hana madhara,” akaeleza kwa mapana na marefu. Baada ya mazungumzo hayo, wote wakapiga makofi ya kujipongeza.

“Yeah! Hatuna budi kujipongeza kwa utafiti huu uliotuweka hapa takribani miezi kumi na tano, Sasa kilichobaki ni kufanya jaribio la kwanza kwa mtu asiye na ugonjwa huu kadiri ya matokeo namba mbili...”

“Ina maana tutamdunga?” Kasiga akamkatisha Minzi kauli yake.

“Ndiyo! Inabidi apatikane mtu asiye na maambukizi, tumdunge, kisha

mtu huyu awekewe damu yenye maambukizi ili tuone nini kitatokea!” Dkt. Edward akawaambia wenzake, ukimya ukatawala kati yao.

“Vipi? Mbona hamuonge!” akawauliza.

“Nawaza, nani wa kukubali kufanyiwa jaribio hilo?” Ziada akajibu na wengine wakatikisa vichwa kukubaliana naye.

“Itabidi apatikane tu! Kwanza kabisa, inabidi tutoe taarifa hii kwa Waziri wa Afya, ili aje ashuhudie nini tumekigundua. Kisha tutampa wazo letu tuone atasemaje, na ikibidi tutafanya jaribio hilo kwa mmoja wetu,” Dkt. Minzi akawaambia na wote wakatikisa vichwa kukubaliana naye.

Kikao kile cha jopo lenye mafanikio kiliendelea kuweka mambo sawa kwa saa kadhaa mbele na kufikia muafaka wa kufanya onesho hilo mbele ya Waziri wa Afya na maafisa wengine wa Serikali kabla hawajajaribu kwa mwananchi mlei kuona matokeo.

Miezi kumi na tano iliwaweka watu hawa ndani ya jengo hili wakikusanya sampuli na kutengeneza kanuni tiba mbali mbali za kupambana na virusi hao. Mwishowe, badala ya kugundua dawa, wakagundua kinga, ambayo ingeweza kumfanya mwanadamu asipate maambukizi ya ugonjwa huo. Hiyo ilikuwa hatua ya kwanza kubwa kwao ambayo haikuwahi kufikiwa popote pale duniani.

Kwanza kinga kisha tiba baadae! Dkt. Edward akawaza na kujipongeza moyoni. Daktari huyu aliingia katika chumba cha mapumziko na kuvuta kijidaftari chake cha kuandika mambo muhimu. Ndani yake aliandika mambo kadhaa kuhusu utafiti huo na moyoni alimshukuru mkufunzi wake Sir. Drostdyhof Fenegan kwa changamoto aliyokuwa amemwachia.

Nimeweza, nimefanikisha. Bila shaka, Sir. Drostdyhof atakuwa anatabasamu popote alipo! Akawaza huku akijiegemeza kitini na kuachia tabasamu la ushindi.

* * *

GENEVA

Siku iliyofuata...

Taarifa za ugunduzi huo zikafika katika Shirika la Afya duniani, nao wakitisha jopo lao kwa kikao maalumu. Kila mmoja katika kikao hicho sura yake ilisawajika kwa mawazo.

“Tumefanya nini?” kiongozi wa mkutano akasema hata bila ya salamu.

“Lakini wao hawajagundua dawa! Ni kinga tu!” mwingine akadakiza na kujibu kwa kujiamini.

“Sawa ni kinga, we huoni kama watazuia mpango? Malengo ya mpango yatafikwa vipi?” Yule kiongozi akauliza huku kajishika kiuno maana kiti kilikuwa cha moto.

“Aaaaa kwa nini mnaumiza vichwa? Tangu lini Mwafrika akagundua kinga au dawa, si zote tunawapelekea sisi! Hamna kitu hapo! Subirini muone, haitafanya kazi...”

“Sawa lakini kumbuka nao ni wanasayansi pia...”

“Hata kama! Kizuri hakitoki Afrika. Wao washazoea kurogana tu na kuuana kwa vita vywa wenyewe kwa wenyewe,” mwingine akadakiza na kusema kwa dharau, akibetua midomo yake juu.

Mvutano mkubwa ukatokea katika jopo hilo, wengine wakasema haiwezekani kwa Mwafrika kugundua kitu kama hicho. Wengine wakisema inawezekana na wasilifumbie macho. Mwisho wa yote muafaka ukafikiwa.

“Lazima jaribio hilo lizuiwe mara moja!” Kiongozi wa mkutano akasema, “Hatuwezi kuruhusu majaribio ya *vaccination* yoyote ambayo haijapita katika maabara zetu afanyiwe mwanadamu. Ni hatari, lazima chanjo hiyo ije hapa kwanza kisha tuifanyie uchunguzi wa kimaabara ndipo tutaruhusu majaribio kadhaa!”

Wote wakakubaliana na nukushi ya haraka ikaandikwa kwenda Wizara ya afya, Tanzania, kuwa chanjo hiyo isijaribiwe kwa mwanadamu kwani ni kinyume na haki za binadamu mpaka ifanyiwe uchunguzi upya katika maabara ya kisasa iliyo chini ya Shirika hilo na kupata kibali. Tunakandamizwa!

* * *

DAR ES SALAAM

“Hatuwezi kufanya kitu hiki peke yetu, hivyo wageni kutoka mashirika kadhaa ya afya huko ughaibuni waje pia kushuhudia nini Tanzania imekifanya chini ya watafiti wake,” Waziri wa Afya akamwambia katibu wake wa wizara wakati wakiandaa taratibu ya shughuli hiyo.

Katika nyakati zizohizo wizara ilipokea maombi kutoka vyuo kadhaa vya huko Uingereza na Marekani kuleta wanafunzi wao wachache

kujifunza zaidi ya nini kimefanyika katika utafiti huo. Pia nukushi iliyofika kutoka Shirika la Afya ikasema kuwa mara baada ya kuitangaza chanjo hiyo haina budi kupelekwa Geneva kwa uhakiki zaidi, ndipo iruhusiwe kutumika kwa mwanadamu. Nukushi hiyo ilijawa na sifa kedekede juu ya uvumbuzi huo, zaidi ikaahidi kufadhili pesa nyingi ilikuwezesha chanjo ifanye vizuri katika bara lote. Kumbe wahusika hawakujua kama wanapakwa mafuta kwa mgongo wa chupa.

Baada ya maandalizi kukamilika, ikatangazwa siku rasmi ya uzinduzi wa chanjo hiyo kama mwanzo wa kuelekea kuipata tiba kamili. Serikali ilijivunia hilo, ikaona kuwa sasa ni wakati wa kuishangaza dunia na viumbe vilivyomo.

Siku ilipowadia, wageni wengi na wataalamu kadhaa wakatuma Tanzania kuja kushuhudia hilo. Wengi hawakuamini, na wengine walitaka kusikia na kuona hasa nini kimefanyika katika uvumbuzi huo. Wanasayansi, wataalamu wa maabara, mafundi dawa, madaktari, viongozi wa serikali na waalikwa wengine wengi walifika kushuhudia uzinduzi huo. Hakika historia iliandikwa.

Karibu nchi nyingi za ulimwenguni ziliandika habari hii. Nachelea kusema, ilikuwa habari nzuri ya kwanza kutoka Afrika kuandikwa katika magazeti ya lugha tofauti katika nchi mbalimbali.

SURA YA 5

‘TANZANIA YAGUNDUA CHANJO YA AIDIOSIS’

KICHWA CHA HABARI katika ukurasa wa juu kabisa wa gazeti la Uhuru linalotolewa na serikali kilisomeka namna hiyo. Jumapili hiyo yenye pilika nyingi za watu; kwenda kanisani na wengine kutafuta mahitaji muhimu ya nyumbani, ilimkuta Kamanda Amata katikati ya Jiji la Dar es salaam akiwa anakata mitaa kwa baiskeli yake. Siku hii alijisikia tu kulitalii jiji hilo kwa kutumia usafiri huu ikiwa ni moja ya mazoezi ya viungo kwake. Simu zote zikiwa zimezimwa isipokuwa ile ya siri tu ambayo inaweza kukaa hata mwezi mzima isiite na ikitokea imeita basi ujue kuna ujumbe mzito.

Akiwa anakatiza Mtaa wa Mkunguni karibu na Hoteli ya Al-Uruba, akakuta kikundi cha vijana kikiwa kinapiga makelele ya furaha ilhali kukionekana kama kuna ubishani fulani. Akapunguza mwendo na kusikiliza kile wanachobishania. Ndipo akagundua kuwa wanabishana juu ya habari mojawapo katika gazeti la siku hiyo. Akavutiwa na kuiweka kando baiskeli yake. Akajongea karibu na meza hiyo ya magazeti. Akatoa noti ya shilingi 500 na kununua nakala moja kisha akapanda usafiri wake na kuendelea na mizunguko.

Mchana wa saa nane ukamkuta katika mgahawa wa Slip Way akipata kinywaji baridi baada ya uchovu wa utalii wake kwa mchana kutwa. Akafungua gazeti na kuisoma habari hiyo kwa kina sana na kuirudia mara kadha wa kadha ili imkae vyema akilini. Hata yeye alifurahi kuisoma kwani ilimsisimua kwa kuona jinsi wanasayansi na watafiti wa Kitanzania walivyopiga hatua kubwa katika hilo. Mwisho habari ile ilisema kuwa siku ya jumatatu, yaani keshoye, ndipo uzinduzi wa chanjo hiyo utakapofanyika huko Lindi katika msitu wa Londo ndani ya ukumbi mdogo wa maabara hiyo wenye uwezo wa kukukua watu kama mia mbili hivi. Wageni mbalimbali wa ndani na nje ya nchi

watahudhuria. Taarifa hiyo iliandika.

Mgeni rasmi wa uzinduzi huo akatajwa kuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amata hakujua kwa nini habari hii imemsisimua sana, akakata shauri la kuhudhuria hata kama hana mwaliko.

Akainua simu yake tayari kumpa taarifa bosi wake Selina au kama anavyopenda kuitwa, Madam S, kumwambia kuwa atahudhuria shughuli hiyo akiwa kama mgeni wa kawaida tu. Mazungumzo ya dakika chache yalipita. Baada ya simu hiyo, Madam S hakuwa na kipingamizi, akamruhusu kufika huko.

* * *

Muda huo huo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere, ndege ya shirika la *Swiss* ilikanyaga ardhi ya Tanzania na kushusha wageni waliyoabiri ndani yake. Ndani ya ndege hii kulikuwa na wasafiri mbalimbali. Kama kawaida, miongoni mwao, watu kama sita hivi walikuwa wakija kuhudhuria tukio hilo pasi na wao kufahamiana. Wote wakasambaa kwenye hoteli tofauti na kujipanga kwa safari hiyo ya kuelekea mkoani Lindi asubuhi ya siku inayofuata. Ndege nyingi za kukodi zilikuwa zimeshakodiwa na watu wa mashirika mbalimbali. Na wale ambao walikosa ndege tayari walishaanza safari kwa kutumia magari ya watalii.

Wakati yote haya yakitokea huku duniani, huko angani kulikuwa na ndege ndogo ya kisasa sana ikiendelea na safari. Ndani yake kulikuwa na watu wapatao wanne tu; marubani wawili na abiria wawili.

“Nilijua tu itatokea!” Cindy akamwambia Kelvin wakiwa ndani ya ndege hiyo ambayo ilikuwa ikiwapeleka moja kwa moja mkoani Lindi.

“Unafikiri ni ile ile?” Kelvin akarudisha swali.

“Bila shaka, si unaona kwenye jopo la wagunduzi yupo Dokta Edward! Na huyu si ndiye alimhifadhi Sir Drostdyhof!” Cindy akaeleza.

“Kwa hiyo kaanzia ambapo marehemu kaachia?”

“Yeah!”

“Haiwezekani. Umesahau kuwa ni wewe uliyepekua ile nyumba kila kona na kuhakikisha kila aina ya nyaraka ya uchunguzi umeichukua? Umesahau kuwa ni wewe ndiye uliyeichukua *notebook* na kompyuta ndogo ya marehemu? Sasa aliacha nini nyuma yake! Umekosea Cindy, tena ukiwaza hivyo unajiweka pabaya sana katika kazi yako maana itakuwa na maana kuwa wewe ni mzembe!” Kelvin akamwambia. Cindy akabaki kimya hajui nini cha kujibu huku moyoni mwake akiona kuwa ni kweli akifikiri hivyo basi yeye ni mzembe katika kazi yake.

Saa kumi na moja jioni waliwasili katika uwanja huo mdogo uliotelekezwa na serikali miaka mingi. Wakateremka na kwa kuwa waliomba kibali cha kuiweka ndege hiyo kwa saa kumi na mbili basi haikuwa na taabu. Wakaicha hapo. Pamoja na rubani wao wawili, wakaelekea hotelini. Ni siku hii tu uwanja huu kama ulifufuka kwani shirika la ATC nalo lilileta watu kwa ajili ya kazi za hapa na pale, zima moto nao hawakuwa mbali.

Hoteli ndogo ya Mingoyo, kilomita chache kabla ya kufika Lindi mjini ndipo wakafikia na kukuta usafiri umekwishatayarishwa wa kuwafikisha huko waendako siku inayofuata.

“Kwa nini wanaitaka hii chanjo, si wawaachie tu nao wajivunie ugunduzi wao!” Cindy akalalama.

“Cindy, fumbuka macho, siri za ndani za kimataifa huzijui? Wataalamu waliketi tangu miaka hiyo kutengeneza silaha za kibaiolojia, na moja kati ya nyingi ni hii. Sasa wao walishaamini kuwa hakuna mwanadamu mwenye akili ya kutegua kanuni hizo walizotumia. Daktari Mitlass alikufa kwa ajali katika harakati zake. Haikuwa ajali ya kweli, ilitengenezwa kwa kuwa yeye alishaenda kinyume na matakwa ya wakubwa kutaka kutoa siri hii. Wewe mwenyewe, Cindy, umeshuhudia Sir. Fenegan akiondolewa maisha yake kwa sindano tu, kwa sababu alikuwa anaelekea kutegua kitendawili hiki. Sasa mara hii wanasema wamegundua chanjo, si rahisi kuwaachia hiyo chanjo abadani!” Kelvin akasema. Cindy akashusha pumzi na kugeukia upande wa pili.

* * *

SIKU YA TUKIO

Watu takribani mia mbili; weusi kwa weupe, walijazana katika ukumbi wa mkutano. Wote wakisikiliza kwa makini sana, muadhara, juu ya ugunduzi wa chanjo hiyo uliokuwa ikiwasilishwa na Daktari Edward Minzi kama ‘Mkuu wa Kikosi’. Baada ya maneno mengi sana yaliyozungukwa kwa misamiati ya sayansi ya tiba na kitafiti, daktari huyu akaketi na kumpisha mshereheshaji aendeleo na ratiba. Katika mstari kama wa nne hivi, Kamanda Amata aliketi kimya akifuatilia muadhara huo. Licha ya hilo, macho yake hayakuacha kupepesa hapa na pale na mara kadhaa yalikuwa yakigongana na macho ya Cindy aliyeketi upande mwingine katika mstari wa pili.

Huyu ni nani? Akajiuliza mwenyewe, lakini hakukuwapo wa kumjibu. Mara kwa mara akaendelea kumtazama na kumsoma zaidi. Amata alivutiwa na mwanamke huyo aliyevalia suti safi ya rangi ya ugolo na

viatu virefu. Kifua chake kilipambwa na matiti ya wastani yaliyotulia kimya, yaliyojaa vyema na kumjengea umbo la kuvutia. Akashusha macho na kumtazama vyema maeneo ya kati. Si haba, kijungu kipo, ijapokuwa ameketi lakini kilijitokeza. Mapaja yaliyojaa vyema katika suti hiyo yaliufanya moyo wa Amata kutapatapa. Kijana akameza mate na kuapa kumtafuta mara baada ya hafla hiyo.

Wataalam wa Kemia kutoka Shirika la Afya duniani walikuwa wametulia wakifuatilia dokumentari iliyokuwa ikieleza kisayansi zaidi juu ya chanjo ile. Na baada ya dakika kama ishirini hivi ikamalizika. Watu wote ukumbini humo wakapiga makofi huku wakiwa wima kuonesha kuwa wamekubaliana na hilo.

Dk. Stith akamtazama mwenzake, wakatikisa vichwa pamoja. Mara baada ya Mheshimiwa Rais kuongea machache hafla ile ikafungwa na baadhi ya wataalam wakatoka ukumbini na kuingia katika chumba fulani. Hawa walikuwa watafiti kutoka idara ya utafiti wa madawa ya shirika la afya duniani, wakakutana na wale watafiti wa Tanzania pamoja na Waziri wa Afya na wadau wengine wa maswala kama hayo nchini. Wakati huo tayari Rais alikuwa hewani kwa helikopta kurejea Dar es salaam moyoni akiwa na kila tone la furaha kwa jambo hilo. Huku tayari ameshatia saini kuwa chanjo ile ipelekwe Geneva kama Shirika la Afya lilivyoomba na kuahidi kuirudisha punde tu wakimaliza uhakiki wao.

Wakati yote hayo yakiendelea, Kamanda Amata alikuwa nje ya jengo lile kubwa. Hakuna cha maana alichokuwa akikisubiri, hata mwenyewe alikuwa akijishangaa lakini kila alipotaka kuondoka moyo wake ulisita akaendelea kusubiri. Labda angemwona mwanamke yule.

“Hey! Shughuli imeisha unapaswa kuondoka, hili si eneo la kusimama simama ovyo!” sauti ya askari anayelinda eneo hilo ikamshtua. Akageuka nyuma na kumwona kijana huyo wa *FFU* aliyening’iniza bunduki ya *SMG* kifuani mwake. Amata akajiondoa taratibu na kuchukua gari lake alilolikodi hapo Lindi mjini. Kwa mwendo wa taratibu sana huku akipiga mruzi akampita yule askari na kushika njia kurudi kijijini.

Alipofika katika kijiji cha Londo kilicho nje kidogo ya msitu huo, alitafuta eneo zuri na kuegesha gari lake, moyoni mwake alitaka kuhakikisha kama yule mwanamke yupo bado mle ndani au keshatoka. Tamaa ilimponza fisi!

* * *

Kule maabara ndani ya chumba kile kidogo, kikao kifupi kilikuwa kikiendelea kati ya wageni kutoka idara ya utafiti wa madawa ya shirika

la afya na wadau wa serikali wenye dhamana kwa hilo.

“Sisi hii chanjo tunaichukua na kuipeleka tena kwenye maabara yetu kubwa, kama tulivyokubaliana. Pale itafanyiwa majaribio kwa mwanadamu endapo tu itapata baraka za shirika la afya na si vinginevyo,” Dkt. Stith akamweleza waziri mwenye dhamana, pamoja na wale madaktari wagunduzi wote wanne.

“Mnachosema ni sawa, na sisi tunaheshimu sana shirika la afya kwani wao ndiyo kila kitu katika maswala ya afya duniani. Lakini kama ninyi wenyewe mmesema kanuni tuliyoitumia kisayansi inaonesha ipo sawa, kwa nini mtie mashaka na tafiti yetu?” Dkt. Minzi akahoji huku uso wake ukionekana kujikunja kwa hasira.

“Kilichoamriwa kimeamriwa!” akazungumza Stith, mtaalamu wa maswala ya kimaabara na magonjwa korofi ya mwanadamu. Dakika chache baadae, Cindy na Kelvin wakiongozwa na Dkt. Ziada Kipele, wakaingia katika chumba maalum kilichohifadhiwa sampuli hiyo ya chanjo. Hakukuwa na chupa nyingi, ni kama kumi na sita hivi, ndogo ndogo. Kwa kuwa ilitakiwa izationalishwe zaidi baada ya kuifanyia majaribio kwa mwanadamu. Zikakusanywa na kupakiwa salama kwenye sanduku maalumu la kisasa lenye uwezo wa kuhifadhi barafu kavu kwa muda mrefu. Lakini pia, lilikuwa na kiungo cha umeme ambacho ukiunganisha kwenye umeme basi lina uwezo wa kujizalishia baridi lenyewe. Zikawekwa katika mianya yake kuepusha zisigongane. Kabrasha lenye kanuni ile yote pamoja na laptop iliyolishwa kabrasha laini navyo vikawekwa ndani ya sanduku hilo katika upande mwingine. Pale ilipowekwa laptop hiyo pakafungwa kwanza ili kuzuia baridi isiiathiri, kisha sanduku likafungwa kwa namba maalum za siri. Sanduku lile likafungwa katika mkono wa kuume wa Cindy kwa mnyororo. Msafara wa Waziri na wataalamu wale ukatoka kuelekea mjini huku ukilindwa na vijana wa *FFU* na kuongozwa na pikipiki kubwa ya askari wa usalama barabarani..

* * *

Amata akashusha darubini yake ndogo mara tu msafara ule ulipopita, akavuta hatua na kuingia kwenye gari lake, akalitia moto na kuondoka huku akiufuatilia msafara huo kwa mbali. Dakika hamsini zilizofuata, ule msafara ukaingia katika uwanja wa ndege mdogo wa Lindi. Cindy na Kelvin wakashuka na lile sanduku wakiwa chini ya ulinzi mkali na kuingia kwenye ndege ile waliyokuja nayo. Wale wengine wakaingia kwenye ndege ya kukodi kurudi Dar es salaam. Kamanda Amata aliishuhudia ndege ile ikiacha ardhi ya Tanzania na kukata mawingu

kuelekea Ulaya.

Alipohakikisha uwanja umebaki na ndege moja tu ya ATC, akateremka garini na kumuendea mmoja wa vijana walioketi katika mabenchi uwanjani hapo. Mazungumzo ya dakika chache yakapita, akamkabidhi funguo ya gari na kuagana naye. Hii ilikuwa ni ndege ya mwisho ambayo ilimchukua Waziri wa Afya pamoja na wajumbe wachache, na Amata alipata nafasi humo. Akiwa katika siti yake, akiliye haikutulia kabisa kwani taswira ya mwanamke yule ilimrudiarudia mara kwa mara na hakujua kwa nini. Wakati wengine wakiwa na mazungumzo ya hapa na pale, yeye aliketi kimya huku macho yake yakitalli bahari safi na pwani ya mji wa Lindi ilivyokuwa ikionekana kwa juu.

* * *

“Are you ok?” sauti ya rubani ikawauliza Cindy na Kelvin kama wapo sawa.

“Yes!” wakaitikia kwa pamoja. Lakini nukta hiyo hiyo Cindy na Kelvin wakajikuta wakitazamana na mitutu miwili ya bunduki.

Wale marubani wakatoka kwenye viti vyao na kusimama wakiwaangalia Cindy na Kelvin, mmoja wa wale marubani akamwamuru Cindy ampe lile sanduku. Mwanamke yule akiwa anatetemeka akamwonesha mkono wake ambao ulifungwa pamoja na sanduku hilo. Yule rubani akakenua kwa kutabasamu kisha akachomoa funguo iliyoweza kufungua kifungo kile bila tatizo.

“And now you are finished!” akawaambia kisha akamimina risasi ndani ya ndege ile na hitilaafu kubwa ikatokea.

Sekunde chache tu ile ndege ikalipuka vibaya ikiwa angani.

SURA YA 6

DAR ES SALAAM

Saa 12 jioni...

KAMANDA AMATA akatoka nje ya Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere akiwa yeye tu bila ya mzigo wowote. Akavuta hatua ndefu ndefu na kuvuka eneo la kusubiria wageni. Hatua zake hizo zilimfikisha katika maegesho ya uwanja huo. Kwa kuwa aliliacha gari lake hapo tangu asubuhi, alitegemea kulikuta. Na kweli. Kama alivyofikiri, ndivyo ilivyokuwa. Alilikuta palepale alipoliacha. Alipolikaribia, mwiliwe ukasisimka, akasita kwanza. Alipotupa jicho vizuri ndani, hakuamini kile anachokiona. Akatazama vizuri kutoka pale alipo, bado hakukubaliana na macho yake. Akaukaribia mlango na kutazama pasi na kuufungua. Naam! Sasa, akakubaliana na kile ambacho macho yake yanakiona.ndani ya gari lile. Katika kiti cha abiria, nyuma, kulikuwa na fupa la kichwa cha mwanadamu. Na kati ya meno ya juu na ya chini ya fuvu hilo kulibanwa karatasi.

Akarudi nyuma taratibu na kuliacha lile gari. Badala yake akachukua taksi na kuelekea mjini. Ndani ya taksi hiyo kulikuwa na ukimya wa dakika kama ishirini hivi. Baadae dereva ndiye akawa wa kwanza kuuvunja ukimya huo.

“Vipi brazal Mbona upo kimya?” dereva wa taksi akauliza.

“Hapana nimechoka tu!”

“Umesikia hiyo ajali ya ndege iliyotokea muda mfupi uliyopita?” akampiga swali.

“Yeah! Nimeisikia,” Amata akajibu tu ili yaishe, kwa maana alikuwa anakumbuka maneno ya muziki uliopigwa na Magereza Jazz wana Mkote Ngoma yasemayo ‘Kubali yaishe’.

“Halafu Boss hujanambia tunaenda wapi?” yule dereva akauliza tena.

“Nifikishe Mgahawa wa Hard Rock!” akamwambia. Yule dereva akaiacha Barabara ya Nyerere na kuchukua ile ya Nkurumah, akanyoosha mpaka mzunguko wa Mnara wa Saa na kuukamata Mtaa wa India. Katika makutano ya Mtaa wa India na Indira Gandhi akakunja kulia na kupita Makunganya, haikumchukua mwendo mrefu kwani ni kipande kifupi tu. Jirani na jengo la Wizara ya Katiba na Sheria akaegisha gari na kuliacha likiunguruma, akageuka na kumtazama mteja wake. Amata akafungua mlango na kutoka nje, akampa ujira wake na yeye akaingia ndani ya mgahawa huo. Akatafuta mahala pazuri akaketi huku bado akiweza kuiona ile taksi ikiwa pale pale. Akamwona dereva akiwa ametingwa na simu kwa takribani dakika nzima, machale yakamcheza. Baada ya dakika kama mbili hivi ile taksi ikaondoka na kumwachia maswali kadhaa. Amata akaona hapo si mahala pa kukaa, akanyanyuka na kutokea mlango wa pili akavuka barabara na kukuta gari jingine limeegeshwa, akachukua funguo yake na kulifungua, kisha akajitoma ndani na kulitia moto. Haya ni maeneo nyeti ambayo watu wa idara hii hupenda kuacha magari yao, ili ukibanwa na shida wakati wowote unafika na kuondoka nalo. Kila mmoja katika idara ya TSA alikuwa na funguo moja ambayo inawasha magari yote haya, lakini pia kuna kitu cha siri cha kufanya ili gari hilo liweze kuondoka. Hiyo ilikuwa ni siri yao.

Akiwa anaiacha Barabara ya Agha Khan na kuchukua ile ya Ocean kuelekea Upanga, simu katika gari hilo ikaita, akainyakua na kuiweka sikioni.

“Ofisi ndogo tafadhali, haraka sana. Tena Sana Aisee, ova!”

“*Copy!*” akajibu na kutazama huku na huku, hakuna gari, akapiga norinda moja matata sana na kurudi alikotoka.

* * *

Ofisi Ndogo

Madam S alikuwa kimya ofisini kwake. Mashavu yake yalionesha wazi uzee unaomnyemelea. Ilikuwa ngumu kujua kama ni kwa mawazo au kwa umri mpaka uso wake kusawajika namna hiyo. Luninga kubwa ya ukutani ilikuwa ikionesha moto mkubwa uliokijaza kioo chake.

Mlango wa ofisi ukafunguliwa baada ya kugongwa kwa mtindo wa

kipekee. Kamanda Amata akajitoma ndani na kuketi kitini. Kwanza akamshangaa bosi wake, maana hata hakumpa makaribisho ya kawaida. Alipomtazama akagundua kuwa luninga hiyo imemchota vyote, mawazo na akili. Naye akageuza shingo kutazama huko, akalakiwa na picha ile ile. Picha ya moto mkubwa uliokuwa ukionekana kuwaka kwa hasira.

Madam S akazima ile luninga na kumtazama Amata.

“Karibu!” akamkaribisha.

“Asante. Nimeitika wito,” naye akaitikia.

“Yeah! Nipe habari za Londo,” Madam akamwambia. Amata akamweleza mengi tu kuhusiana na safari hiyo lakini hakumgusia juu ya yule mwanamke maana alijua hatoweza kukwepa *madongo* ya mkuu wake.

Baada ya taarifa hiyo akamwambia kuhusu lile fuvu ndani ya gari lake pale uwanja wa ndege. Hili likamshtua sana Madam S, akamkazia macho kijana wake.

“Sijakuelewa!” akamwambia.

“Nimekuta fuvu ndani ya gari langu pale *Airport!* Kati ya meno ya juu na chini kuna kijikaratasi, nikaamua kuliacha bila kutoa taarifa yoyote na wala sikuangalia kama karatasi hiyo ina ujumbe gani...”

“Ok!” Madam akamkatisha na kuinua simu yake, akabofya namba fulani fulani na kuiweka sikioni.

“Ndiyo Simbeye, kuna mzigo ndani ya gari letu pale uwanja wa ndege naomba ushughulikiwe,” akamwambia Inspekta Simbeye kwa simu hiyo, kisha baada ya kupata jibu la upande wa pili akakata na kumtazama Amata.

“Ngoja tusubiri jibu! Nani anayethubutu kufanya jambo kama hilo? Wanakubip? Basi ukiwagundua wapigie,” akamwambia.

“Ndiyo Madam! Nina shauku ya kutaka kujua nini umeniitia!”

“Amata, Kamanda wangu, usione ninaongeaongea hivi, hapa nimechanganyikiwa. Amata huna budi kurudi ulikotoka...”

“Nilikotoka!” akashangaa.

“Ndiyo! Hiyo ndege uliyosema imepakia sampuli ya zile chanjo imelipuka angani kama saa moja iliyopita...”

“*What!*” Amata akang’aka na kujikuta kasimama wima huku mikono kichwani, akili yake ikafanya kazi haraka na kuunganisha matukio.

Ina maana walioweka fuvu lile walikuwa wakinipa taarifa hii kwa mtindo ule? Haiwezekani! Akaongea peke yake moyoni kisha akaketi tena na kumtumbulia macho Madam S.

“Na huo moto uliokuwa unaouona hapo ni ile maabara ya Londo. Imelipuka na kuteketea vibaya. Mpaka sasa jeshi la Zima Moto na Uokoaji wanasema huo ni moto wa kemikali,” Madam akaeleza.

Kamanda Amata, akatikisa kichwa. Akajipiga piga upande huu na ule. Haikuingia akilini. Akasimama tena, akaegemea meza kwa mikono yake miwili huku akimtaazama bosi wake. Mwili wake ukatetemeka kwa hasira na uchungu. Akapiga ngumi mezani, kisha akaliendea jokofu dogo lililo ndani ya ofisi hiyo na kutoka na chupa kubwa ya VAT 69 na bilauri mbili. Akajimiminia na kummiminia mkuu wake. Akamsogezea yake, naye akachukua ya kwake na kuipeleka kinywani. Hakunywa, bali akainusa tu na kuishusha.

“Vipi?” Madam akauliza huku tayari bilauri yake ikiwa tupu.

“Nahisi harufu ya kifo kama si damu,” akamwambia kisha akaiinua na kuinywa yote. Akachukua chupa na kujimiminia nyingine

“Najaribu kuvuta kumbukumbu ya watu niliowaona kule. Labda nitagundua mmoja au wawili wenye sura ovu,” akaongeza kusema na kupiga fundu moja kubwa na kushusha bilauri ikiwa tupu.

“Tumehujumiwa!” Madam S akasema, huku naye akiendelea kujimiminia bilauri ya pili, na ya tatu, “Tafiti yetu wameichukua na kutufanya sisi mabwege. Wamechoma maabara washenzi hawa, wanataka kupoteza aina yoyote ya uchunguzi iliyobaki nyuma,” akaongeza kusema na kupiga bilauri ya tatu kavukavu.

“Lazima sanduku lile lipatikane. Nina uhakika huu ni mpango uliopangwa kitaalamu,” Amata akasema na kujimiminia kinywani bilauri ya nne. Mara simu ikaita katika ofisi ile, Madam akainyakua na kuiweka sikioni.

“Yes!” akaitika na kukaa kimya kwa dakika kama moja hivi, “Ok, sawa!” akakata simu.

“Amata!” Madam S akaita, “Hakuna chochote kwenye gari lako...” akamwambia.

“Unasema? Haiwezekani. Hawa watu kama si mashetani, wananitafutia nini mimi?”

“Usijali, achana nao, hebu tutazame hili la moto maana hii ni idara nyeti sana ya serikali. Tafiti zote za madawa na magonjwa zimehifadhiwa hapa. Sasa imewaka moto, unategemea ni hasara kiasi gani tumeingia? Hata kama ni moto wa kawaida, na ijulikane chanzo hasa cha moto ni nini na nataka nijue kwa nini moto huo usiwake jana au kesho, ukawaka leo?” tayari pombe kali ilishaanza kumchanganya Mwanamama huyo

na kuanza kuropoka mambo mfululizo. Kamanda Amata naye alikuwa akihisi kichwa kinamzunguka kwa pombe ile. Akainua chupa na kuiangalia kisha akapiga tarumbeta mpaka ikabaki tupu.

“Unywaji gani huo Kamanda! Utakufa...”

“Wangekufa waliotengeneza kwanza,” akamjibu kwa sauti ya kilevi na wakati huo simu nyingine ikaita. Madam akainyakuwa na kuitazama, kisha akamtupia jicho Kamanda.

“Mbona unaniangalia? Au *dushbelele* linakupigia, nenda bwana ukapunge mashetani!” Amata akamwambia Madam S.

“Huna adabu!” akamjibu kisha akaipokea simu ile.

“*Sierra One...!*” akaitika namna hiyo kisha akatulua kusikiliza. Amata aliposikia neno hilo akajua simu imetoka wapi, akanyamaza kimya.

“Sawa, sasa hivi!” akajibu na kuirudisha mahala pake. Akainuka na kuelekea kwenye heng’a iliyo pembeni tu ya kabati la vitabu. Akachukua koti na kulivaa, kisha akavuta saraka kutoka katika rafu hiyo ya vitabu, akachukua bastola mbili na kuzipachika katika mapaja yake ambako kuna mikanda maalumu kwa kazi hiyo.

“Nimeitwa kilingeni, kuna kikao cha Kamati ya Usalama ya Taifa. Tulia sehemu moja mpaka nitakapokupa taarifa nyingine,” akamwambia Amata.

“Kwa hiyo nikusubiri hapa au?” Amata akauliza.

“Kanisubiri gesti nakuja,”

“Ah! Ina maana unataka kumaliza siku ya leo na mimi?”

“Haswaaaa! Tena juu ya kitanda kimoja, si kama siku ile! Haya toka ofisini kwangu!” Madam akamwambia.

SURA YA 7

Sehemu fulani huko Mtwara

KATIKA MOJA ya mashamba ya mpunga, Kusini kabisa mwa mkoa wa Mtwara, karibu na mpaka wa Tanzania na Msumbiji. Watu wawili walitua kwa parachuti katikati ya matope mengi. Kila mmoja akakunja parachute lake. Lakini kutokana na matope hayo wakaamua kuyaacha kwa kuificha vyema.

“Vipi unalo?” mmoja akauliza.

“*Yes!* Nililifunga vizuri kabisa,” mwingine akajibu. Yule wa kwanza akachukua kitu kama kurunzi na kukibofya upande wa chini. Kitu kama mlipuko kikatokea na kuruka angani. Sekunde kadhaa baadae nao wakaona kitu kama kilekile kikitokea upande wa pili.

“*Vamos!*” yule wa kwanza akamwambia mwenzake akimaanisha waende kufuata hiyo ishara ilikotokea. Wakaongozana huku lile sanduku likiwa imeshikwa vizuri. Mwendo kama wa dakika kumi na tano hivi wakakutana na magari mawili, meusi, Land Rover Defender. Yakasimama mbele yao. Hawakuuliza. Wakafungua milango na kuingia, yakageuzwa na kurudi yalikotoka.

“*Everything is ok?*” dereva akauliza kama kila kitu kipo sawa.

“*Yes!*”

“Vizuri, mkuu anawasubiri hekaluni,” yule dereva akawaambia huku akibadilisha gia na kuingiza ya nne, safari ikaendelea na lile Defender lingine likiwa nyuma yao.

* * *

Iliwachukua Mwendo wa saa tatu hivi kufika katikati ya msitu mkubwa kilomita zaidi ya mia mbili kutoka mpaka wa Msumbiji na Tanzania.

Eneo lilijulikana kama Cabo Delgado. Katikati ya msitu mkubwa kulikuwa na jumba kubwa la kifahari. Uwanja mkubwa wa mchezo wa *golf* uliwakaribisha. Mara tu baada ya magari yale kuwasili, mzee mmoja wa makamo, mwenye nywele nyeupe za kuhesabika katika kichwa chake, akaacha kucheza mchezo ule. Akavuta hatua taratibu na kufika mbele ya jumba hilo huku nyuma yake akisindikizwa na wanadada wawili waliokuwa wamevalia *Charlatan black crochet high neck bikini* na juu yake makoti mepesi meupe. Wote hawa walikuwa Wazungu. Eneo hilo hakukuwa na Mwafrika zaidi ya mmoja tu aliyekuwa bawabu katika himaya hiyo.

"Welcome back my heroes!" Yule mzee akawakaribisha kwa sauti yake kavu na ya kukwaruza. Akalipokea lile sanduku na kumkabidhi mmoja wa wale wanadada. Nao wakatangulia ndani, na yeye akafuatia huku nyumaye wakija wale vijana. Ndani ya jumba hilo lenye kila aina ya ufahari, wakaingia kwenye lifti na kuteremka chini ya ardhi kama mita ishirini hivi. Wakatoka na kujikuta ndani ya chumba kikubwa chenye mitambo mbalimbali ya kikemia, kwa kifupi ilikuwa maabara kubwa na ya kisasa. Pale kulikuwa na watu wengine wawili waliovalia mavazi meupe juu mpaka chini, huku sura zao pia zikiwa zimefunikwa kwa jinsi hiyo hiyo. Mmoja wao akasogea na kulichukua lile sanduku, akalifungua na kutoa zile chupa zote na kuzihifadhi jokofuni.

"Kesho tutafanya jaribio letu la kwanza kisha mambo mengine yataendelea," akamwambia yule mzee naye akatikisa kichwa kuitikia.

Katika ghorofa ya juu, yaani kule walikokua mwanzo, yule mzee akakutana kwa siri na vijana wake waaminifu wanne na wale wanawake wawili ambao walionekana kuwa ni walinzi wake wa karibu.

"Tumeweza!" akawaambia, "Sasa utajiri wetu utaongezeka maradufu," akaongeza kusema. Akiwa katika kuongea huko, msichana mwingine, achilia mbali wale wawili, akamletea bilauri iliyojaa pombe kali na kumwekea mezani.

"Kila kitu kipo sawa?" akawauliza huku akiwatazama kwa macho makali

"Ndiyo Mkuu, kila kitu ni sawa kabisa, na mtu wetu atafikishwa hapa muda si mrefu," wakamjibu.

"Sawa, nitawaona baadae kwa mipango mingine," akawaambia na wale jamaa wakainuka na kuondoka.

Baada ya kuhakikisha wale vijana wamekwishaondoka, akainuka na kuingia katika chumba chake cha siri ambacho ni yeye tu huingia.

Akaketi na kuwasha luninga yake kubwa ya ukutani, kisha akasogeza kinasauiti.

“Kagueni sampuli!” akasema kupitia katika kile chombo, na sauti hiyo ikasafiri mpaka maabara kule chini ya ardhi kwa wale wataalam.

“*Ok! Sir!*” akajibu mmoja na kuchukua kichupa cha chanjo ile iliyoletwa kutoka Tanzania, na kufyonza kwa sindano matone kadhaa kisha akakirudisha jokofuni. Akadondosha yale matone kwenye mashine nyingine. Akabonya hapa na pale na kuaza kuangalia mambo ambayo ni yeye tu alikuwa akiyaelewa.

“Hii ndiyo yenyewe!” akasema, na yule mzee akasikia.

“Sawa andaeni *specimen* nne za kufanyia majaribio, jinsi ya kike mbili na ya kiume vivyohivyo. Kati yazo, mbili za jinsi tofauti ziwe *negative* na mbili ziwe *positive*, ili tuhakikishe kama kweli chanjo hii inafanya kazi. Tukipata jibu basi tutafanya hatua nyingine,” akatoa maagizo.

“*Work in process Sir,*” wakaitikia wote wawili kuwa kazi ipo kwenye mchakato.

“*Thank you. Waiting for progress,*” Dimens akajibu na kuzima kile chombo cha mawasiliano.

* * *

Dar es salaam

Katikati ya Jiji la Dar es salaam, Kamanda Amata akaegesha gari lake na kuingia katika ukumbi mkubwa wa burudani. Tayari giza lilikuwa limeshamiri na usiku ukizidi kuyoyoma, lakini vijana bado walikuwa wakiendelea kuserebuka na miziki mbalimbali waliyoipenda.

La Tarven, ndivyo ulivyojulikana ukumbi huo. Ulijengwa kisasa sana, kiasi kwamba ukipita nje huwezi hata kujua kama humo ndani kuna muziki, ila ingia ndani, ndipo ushuhudie. Si muziki tu bali hata dhambi zilizosheheni ndani humo, zilifanyika pasi na kificho. Amata akachagua siti ya peke yake na kuketi, akaagiza kinywaji na kutulia kimya huku akiangalia *dance floor* inavyopata shida. Dakika kumi baadae akiwa ametingwa na simu yake, akiperuzi hiki na kile, akajikuta hayuko peke yake. Alipotazama akakutana uso kwa uso na Madam S.

“*Yes! Mom! Kikao kimeisha?*” akauliza.

“Ndiyo maana niko hapa!” Madam S akajibu huku macho yake yakitalii ukumbi ule kwa namna ya pekee sana.

“Niambie!” Kamanda Amata akaanzisha mazungumzo.

“Kikao kilikuwa kizito sana! Vuta nikuvute haikuwa ya kawaida. Hapa ninapokwambia ni kuwa nimepewa *D.O! Direct order* kutoka kwa Mh. Rais ya kuhakikisha hili linapatiwa ufumbuzi,” Madam S akamwambia Amata.

“Ndiyo!”

“Kutokana na matukio haya mawili; kuungua kwa ile maabara kule Londo, na mlipuko wa ndege ambayo ndani yake kulikuwa na ile sampuli ya chanjo. Muafaka tuliofikia ni kuwa; kwanza kabisa hii ni hujuma ama ya ndani au ya nje ya nchi. Tumepewa kazi ya kufanya uchunguzi wa kina kujua chanzo cha moto na kwa nini. Pia kutafuta maana ya mlipuko wa ndege ile,” akatulia kidogo, kisha akaendelea, “Kazi hii inatakiwa ianze mara moja”.

“Sawa! Yaani hapa ninapomalizia tu kunywa hii bia ndipo kazi itaanza,” Amata akasema.

“Kwa hiyo bado unakunywa?” madam akamuuliza kijana wake.

“Yap! Lazima nipige kinywaji ili niweze kuunganisha matukio,” akamjibu mkuu wake. Madam S akatulia na kumwangelia kijana wake akipiga tarumbeta bia iliyokuwa mezani. Alipoishusha, chupa ilikuwa tupu, akabeua, kisha akamtazama boshi wake.

“Sikia Madam! Yaani kwa maono yenu ya kikao kuwa hii ni hujuma, ninakubali kwa asilimia fulani na sikubali pia kwa asilimia nyingine. Kuhusu ajali ya ndege, nayo vivyo hivyo... Sasa jambo la kwanza kwangu ni kusecure sampuli zilizobaki...”

“Sampuli zilizobaki?” Madam akamkatisha Amata.

“Yes! Sampuli zilizobaki...”

“Sampuli gani wakati nakwambia ndege iliyobeba imelipuka!”

“Madam! Mmesema ni hujuma! Kama ni hujuma, basi hiyo ndege haijalipuka, bali imelipuliwa... na ina maana kama imelipuliwa basi aliyelipua yuko hai,” Amata akaongea.

Mwanamama yule, akatikisa kichwa huku akimtazama Kamanda Amata kwa jicho kali lenye kila dalili za kukubaliana naye.

“Una akili sana, sikuwa nimefikiri hilo...”

“Tumshukuru Mungu!” Amata akajibu.

“Enhe, kwa hiyo unasemaje baada ya kufikiri hilo, au niseme nipe maana ya sentensi yako...” Madam S akadadisi.

“... Safi! Simaanishi kusecure hizo zilizokuwa ndegeni, nimesema zilizobaki, na kama huzijui nitakuonesha nikizipata,” Amata akaeleza

huku akiinuka.

“So?” Madam S akauliza huku naye akisimama.

“Naingia kazini sasa! Si mmenipa kazi... ndiyo naingia hivyo! Lakini safari hii nitamiss sana kampani yangu!”

“Usijali, nitahakikisha wanamaliza kazi na kuja kukuunga mkono kwa sababu naelewa ugumu wa kazi yako!” akazunguka kutoka kiti alichokaa na kwenda upande aliyosimama Amata. *Zero distance*. “... Amata, nahitaji umalize kazi hii salama, ulisaidie taifa kwa mara nyingine. Kama nilivyokwambia wakati ulee! Nakupenda zaidi ya mume wangu”.

SURA YA 8

Msanga Mkuu - MTWARA

ALFAJIRI YA SIKU ILIYOFUATA, iliwakuta wavuvi wakiwa kwenye vuvi zao kama ilivyo ada. Wakiwa katika kazi yao hiyo, mmoja wao alishtuka kuona kitu kama mwili wa binadamu kikielea majini.

“Oya! sio mtu yule?” mmoja akauliza na kumfanya mpiga kasia kusitisha zoezi lake.

“Tusitishane Mudi, unajua tuko baharini hapa, na bahari zina mauzauza hizi ohoo!” mwingine akamjibu.

“Jamani mwili wa mtu ule,” mwingine akaongeza. Akawasha kurunzi yake na kushuhudia kweli mwili wa binadamu ulikuwa ukielea. Wakasogeza chombo kile mpaka jirani kabisa na kile walichokiona.

Hawakukosea, mwili wa mwanadamu, mwanamke, ulikuwa ukielea, haukuonekana kama una uhai.

“Amekufa?”

“Ndiyo!”

“Tumwache... tutanunua kesi bure!”

“Nuksi leo, mi sivui tena, hii ishara mbaya!” mwingine akadakiza.

“Hapana! We bwege nini! Kwani mtu akifa, ndiyo hasaidiwi? Tumtoe nchi kavu, tutoe taarifa polisi, ndugu zake waje kumtambua,” akawaambia wenzake. Baada ya mabishano ya robo saa nzima, mwafaka ukafikiwa. Wakasaidiana na kuupakia ule mwili, wakaugeza geuza na kuona baadhi tu ya majeraha na nguo yake iliyongua huku na kule. Michaniko hiyo na majeraha vilionekana wazi kuwa mtu huyo kafikwa na janga la moto.

“Nyie! Huyu mzima huyu! Mtu anayekufa kwa maji hawi hivi

bwana, mbona kama hamjui jinsi bahari inavyomfanya marehemu, tumuwahisheni,” aliyekuwa nahodha wao akawaambia. Kile chombo sasa kikawekwa mashine badala ya makasia, na kuwashwa. Kisha kikakimbizwa mpaka nchi kavu karibu kabisa na kituo cha polisi cha wanamaji katika pwani ya Mtwara.

“Vipi?” kijana mmoja aliyevalia kiaskari na bunduki yake kifuani aliwauliza wavuvi wale.

“Tumemwokota huyu mwanamke akielea majini, hatumjui,” wakajibu. Yule kijana akamtazama yule mwanamke akiwa kalala kimya.

“Hajafa huyu?” yule polisi akajiuliza kwa sauti ya chini. Akaingia ndani na kutoka na wenzake, mmoja wao akapiga picha kadhaa, kisha wakampakia katika gari la polisi na kumkimbiza hospitali. Askari waliobaki huku nyuma wakachukua maelezo ya wavuvi wale na kufungua faili. Mwanamke yule alifikishwa Hospitali ya Ligula na kupatiwa matibabu ya haraka baada ya kugundulika kuwa kweli aliksalia na uhai kidogo.

* * *

Siku hiyo hiyo...

Saa sita mchana wa siku hiyo. Kamanda Amata aliwasili Londo kama mchunguzi aliyetumwa na serikali. Hakuna alichokikuta zaidi ya vijana wa Zimamoto waliokuwa wakifanya hiki na kile. Maabara hiyo kubwa na ya kisasa ambayo ilijengwa kwa pesa nyingi sana za serikali ilisalia kuta chache tu. Kemikali na makabrasha yote vilikuwa vimeteketewa kwa moto. Ndani ya ofisi iliyotengenezwa kwa muda, Kamanda Amata aliingia na kukutana na wakuu wa jeshi hilo, maafisa kadhaa wa polisi na Jeshi la Wananchi.

“Karibu sana!” sauti ya kike ikamkaribisha. Alipogeuka upande huo, akakutana na mwanamama aliyejaa mwili kwenye sare yake ya Zimamoto ambayo usipoangalia vizuri unaweza ukafikiri kuwa ni *FFU*. Akaitikia karibisho hilo na kuketi katika kiti kilichowazi. Baada ya hapo kikao kifupi kikaendelea na mazungumzo ya kina na kitaalamu yakawaumiza vichwa watu hao.

“Kwa hiyo ni kwamba chanzo cha moto huu ni mlipuko wa Kemikali?” Amata akauliza baada ya kusikiliza kila lililozungumzwa.

“Ndiyo, uchunguzi wa awali unaonesha hivyo. Mtaalamu wetu amegundua hilo baada ya kuona aina yenyewe ya moto iliyokuwa

ikiwaka...” yule mama akasema.

“Inawezekana uchunguzi ukaonesha hivyo kwa kuwa jengo zima lilijazwa na kemikali za aina aina...” Amata akaliambia jopo, “Lakini kemikali hizo zisiwe chanzo cha moto huo,” akamalizia.

“Kitaalam, umakini wetu wa kwanza huwa ni kuangalia uwezekano wa nini kinaweza kusababisha... Hii ni maabara, na maabara daima inabeba kemikali nyingi. Hivyo cha kwanza kukiangalia hapa ni uwezekano wa kitu tunachokiita *Chemical Reaction*... Kuna kemikali ambazo hutengeneza joto kitaalam tunaita ‘*exothermic*’. Hizi zinaweza kusababisha moto muda wowote. Kemikali za mtindo huu zikisababisha moto basi nyingine hutenda kama mafuta na kuufanya moto kuwa mkubwa na wa kasi sana. Kadiri ya dokumenti ya *NFPA 921*, inasema, inaweza kuwa vigumu kugundua chanzo kwa sababu chanzo huweza kujificha kwenye majivu, lakini kwanza huwa tunaangalia nini kilikuwa ndani ya eneo athirika...” akaongea askari mwingine aliyekuwa na kabrasha mbele yake.

“Nikukatishe! Kulikuwa na watu ndani ya maabara wakati moto ukitokea?” Amata akarusha swali.

“Ndiyo, kulikuwamo watu na wote wameteketea kwa moto huo,” akajibiwa. Habari hii ikaupa ganzi mwili wa Amata, akahisi nywele zikimsimama.

“Mmewahi kujiuliza kwa nini moto huo haukuwaka siku nyingine zaidi ya jana?”

Ukimya ukapita na kila mmoja akawa akimtaazama mwenziwe.

“Ni ajali tu!” akajibu Mkuu wa Zimamoto.

“Ni ajali tu! Je mmejiuliza kwa nini moto huo umeanza wakati mmoja sawa sawa na ile ndege ambayo ilibeba sanduku lenye sampuli ile? Au hamkukitazama hicho”

Kwa maswali hayo mawili wajumbe wa kikao kile wakabaki kimya. Hakukuwa na mwenye jibu. Walitazamana kwa nukta kadhaa na kurudisha macho mezani. Wote waliona kweli hawakuawahi kufikiri juu ya hayo mawili.

“Kwa ukimya wenu ina maana haya hamkuyatilia maanani. Sasa, serikali inahitaji kupata taarifa kamili kama ifuatavyo: Inahitaji kujua idadi kamili ya vifo na majina ya marehemu na utambulisho wao, pili, chanzo cha moto, yaani moto ulianza wapi hasa, kama ni stoo, jikoni, chooni nk. Inahitaji kujua hayo yote mpaka kufikia kesho asubuhi,” Amata akatoa oda, na kwa kuwa wote walimpokea kama mkaguzi

kutoka serikalini, waliamua kuanza kazi upya huku yeye akiendelea na mambo mengine.

Baada ya kikao hicho, akatoka na kuwaacha wataalamu hao wakijadiliana kwa kina, akaingia katika gari lililomleta tayari kwa safari ya mjini. Safari yake hii ilikuwa ni kwenda kumwona Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Lindi. Dakika tisini hivi baadae aliwasili katika ofisi hiyo, kwa bahati akamkuta anayemhitaji.

* * *

Ofisi hii iliyopo ndani ya jengo la ghorofa tatu, ilimkaribisha Amata kwa ukarimu wa hali ya juu ambao ulioneshwa na afande wa kike aliyeketi nyuma ya kompyuta, chumba kimoja kabla ya kile cha mkuu huyo wa polisi.

“Karibu, pita moja kwa moja, mkuu anakusubiri,” yule afande wa kike akamwambia Amata huku akimwonesha mlango ulio pembeni yake.

“Asante mrembo!” Amata akajibu na kukinyonga kitasa cha mlango huo. Ndani ya ofisi hiyo pana, Amata alikaribishwa na mwanaume wa makamo aliyevalia sare nadhifu za jeshi la polisi. Mabegani mwake alikuwa na vyeo vinavyompa hadhi na heshima aliyonayo; S.A.C.P yaani *Senior Assistant Commissioner of Police*. Sura yake haikuwa na tabasamu hata kidogo, makovu ya hapa na pale usoni yalimtambulisha kama mtu mkorofi au tuite ‘nyani aliyekwepa mishale mingi’.

“Karibu kijana!” akakaribishwa na kuingia, kisha wakaketi katika mtindo wa kutazamana. Kati ya RPC huyo na Kamanda Amata palikuwa na meza kubwa yenye *formica* maridadi kabisa. Simu ya waya, kabrashacha na kalenda ya mezani viliipamba meza hiyo, bila kusahau gazeti la siku hiyo, Mfanyakazi.

“Asante sana, naitwa Jaffari,” akajitambulisha, “Nipo hapa Lindi kwa ajili ya uchunguzi wa mlipuko ulitokea huko Londo,” akamwambia.

“Ndiyo, ndiyo, habari yako ninayo kijana, na nimeambiwa nikupe msaada wowote ukihitaji,” yule RPC akamwambia Amata. Kwa haraka Kamanda akamsoma kiongozi huyo kuwa ni mtu asiye na maneno mengi, anaongea kile tu anachotakiwa kuongea, basi.

“Sawa! Ninalohitaji mimi kutoka kwako ni hili; askari namba PC 1876B, nahitaji awekwe ndani sasa hivi!” akamwambia kisha akamtupia jicho la wizi.

Yule RPC akajikuta akibaki kinywa wazi pasi na kujielewa, akaiondoa

miwani yake usoni na kuitua mezani.

“Kwa nini sasa kijana?” RPC akauliza mara tu akiliye iliporudi.

“Si kwa nia mbaya, ila ukishamweka ndani uniambie, ndipo nitakwambia kwa nini,” Amata akamweleza. Kamanda yule akabaki bado haelewi mantiki haswa ya ombi lile. Akachukua simu yake ya mezani na kubonyeza tarakimu kadhaa, kisha akasubiri.

“Hello!” sauti ya kike upande wa pili ikapokea.

“Fika ofisini mara moja!” akaamuru na kukata simu. Akashusha pumzi ndefu na kujiegemeza kitini.

Haikupita muda, mlango ukasukumwa na mwanadada mfupi, mwenye mwili uliojaa nyama za kutamanisha wakware, akasimama kikakamavu kabisa na kutoa salamu ya kijeshi kwa mkuu wake.

“Wasiliana na Kamanda wa kikosi cha FFU, mwambie PC namba 1876B, akamatwe na awekwe ndani...”

“Sawa Afande!” yule WP akajibu na kupiga saluti kisha akageuka na kutoka katika ile ofisi.

“Kijana!” Yule RPC, mtu mzima, akamwita Amata na kumgutusha kutoka kwenye hali aliyokuwa nayo, ya kumtazama mwanadada huyo.

“Ndiyo kamanda!” Amata akajibu na kujiweka sawa kitini.

“Dakika chache tu...” akamwambia Amata au Jaffari wa bandia, kisha, kati yao, yakapita mazungumzo kadha wa kadha. Wakiwa katikati ya mazungumzo hayo, simu ile ya mezani ikapata uhai, yule bwana akainyakuwa na kuiweka sikioni.

“Yes!” akatamka na kubaki kimya kwa sekunde kadhaa.

“...sawa, asante!” akajibu na kukata simu kisha akamtazama Kamanda Amata.

“Tayari,” akamwambia, “Kuna lingine?”

Amata akashusha pumzi na kutuliza akili yake kwa nukta kadhaa.

“Nahitaji kufika kumwona, nina mazungumzo naye!”

“Sawa!” RPC akajibu na kuinua simu yake ya upepo, akaongea maneno matatu tu ya kutoa amri huku na huko. Na muda mfupi baadaye, mwanadada yuleyule akaingia tena kupewa maagizo na bosi wake.

“Twaweza kwenda,” akamwambia Amata kisha wakainuka na kutoka nje, hapo wakachukua gari la ofisi, Land *Cruiser GX* lenye vioo vya giza na kuelekea kituo cha FFU Mitwelo. Ndani ya gari hilo, kulikuwa na watu watatu tu; dereva mwenye cheo cha Koplo, yule WP aliyemchukua kule ofisini na Amata aliyekuwa ametulia katika kiti cha nyuma. Kama walivyotoa oda, askari yule walimkuta *lock up*.

Walifika na kuteremka, moja kwa moja wakapelekwa kwa mkuu wa kituo hicho. Baada ya mazungumzo mafupi, Amata akaongozwa mpaka chumba maalum cha mahojiano.

* * *

Kilikuwa chumba kidogo, chenye meza moja ya mbao na viti viwili vya chuma, Amata alikutana uso kwa uso na askari yule, kijana, mwenye sura ya kitoto, lakini machoni alionekana mwerevu sana. Amata akaketi naye mkabala. Baada ya yule aliyemuongoza kutoka, Amata akabaki na mtu wake tu.

“Nafurahi tumeonana tena! Unanikumbuka?” Amata akamuuliza.

“Sura si ngeni ila sikumbuki ni wapi tumeonana,” yule askari akajibu.

Kamanda Amata akachomoa kitambulisho bandia cha upolisi, yule afande akakisoma na kisha akamrudishia.

“Usihofu afande, ni mimi niliyeomba uwekwe hapa kwa sababu maalumu, hakuna baya lililosababisha hili...” Amata akamwambia na yule afande akatikisa kichwa.

“Unaitwa nani?”

“Aizaki Maneno,” akajibu.

“Jana mchana, saa saba, ulikuwa wapi?” Amata akamchapa swali.

“Nilikuwa kazini, lindoni katika maabara ya utafiti kule Londo,” Aizaki akajibu.

“Umejibu kwa usahihi kabisa afande, na kule ndiko tulikoonana mimi na wewe!” akamwambia.

“Unajua kuhusu moto uliotokea kule Londo?”

“Kabisa!”

“Unaweza kunambia wakati moto unaanza wewe ulikuwa wapi?” akaongeza swali.

“Aaaa kwa kweli pindi moto ulipokuwa ukianza mimi nilikuwa zamu, na nilikuwa kwenye kibanda chetu cha kupumzikia...”

“Unaweza kunambia moto ulianza wapi hasa, kadiri ya ulivyoona?” Amata akamsaili.

“Aaaaannhhhh... Ule moto mi niliuona upande wa stoo, na tulipopiga king’ora ili watu kujiokoa ukweli ni kwamba watu wanne tu ndiyo waliokuwapo kazini na hawa hawakuwa ndani, ofisi zao ziko nje,” Aizaki akaeleza kinagaubaga na Amata alikuwa akimsikiliza kwa tuo.

“Je unaweza kuhisi chochote juu ya moto huo, ama umesababishwa

na mtu au ajali ya kawaida?”

“Kwa kweli hapo siwezi kukudanganya, nafikiri ile ni ajali ya kawaida,” akajibu. Amata akajiweka vizuri kitini.

“Unajua nini! Mimi nipo kwa ajili ya uchunguzi wa moto ule, si unajua kuwa kile ni kitengo nyeti sana serikalini, na kwamba siku hiyo tu ndipo uzinduzi wa chanjo ya *AIDIOSIS* ulifanyika...”

“Ndiyo najua!”

“... na umesikia kuwa ndege iliyobeba maafisa wa *WHO* pamoja na sampuli za ile chanjo imelipuka....”

“Ndiyo nimesikia!”

“We unaonaje hapo? Hii ni kawaida au...”

“Sikuwahi kufikiri ila sasa unanipa wasiwasi...”

“Achana na hilo, wewe kama askari, mwenye mafunzo, pale getini najua ulikuwa makini sana kuangalia wote wanaoingia kwenye hafla ile, wawe Wazungu au Waafrika. Najua kuwa kwa uaskari wako umeweza kuzikariri sura chache kama si zote. Vipi kuna sura yoyote umeitilia mashaka?” Amata akaendelea kumtwanga maswali huku saa yake ikirekodi mazungumzo hayo. Aizaki akabaki kimya kwa jozi la sekunde, kisha akainua uso wake kumtazama Amata.

“Braza, jana ni siku yangu ya saba kulinda pale na ilikuwa ndo namaliza lindo langu. Kiukweli kabisa, kuna Wazungu kama watatu hivi walikuja siku nne nyuma...” Amata akatega sikio kusikiliza nini kitasemwa... “Dakika chache kabla ya mlipuko ule, hawa jamaa walikuwa wakisaini kutoka,” akaeleza. Hili jambo likamstua Amata, tena likamvutia sana kulihoji kwa makini, akatulia kwa sekunde kadhaa kisha akamtupia swali lingine.

“Wakati mlipuko umetokea wazungu hao walirudi au la?”

“Walirudi kwa sababu hawakuwa mbali, lakini baada ya kama saa hivi sikuwaona na sijui waliondoka saa ngapi,” Aizaki akasema.

“Sawa Aizaki, majibu yako yatasaidia sana uchunguzi wa kazi hii. Nikikwambia kuwa hawa jamaa wanahusika kuchoma moto maabara, nitakuwa nakosea?” Amata akauliza.

“Kwa hilo siwezi kujibu, maana ni wanafunzi na walikuja kujifunza zaidi juu ya kazi zao za kimaabara,” Aizaki akajibu.

“Wewe umejuaje kama ni wanafunzi?” Amata akamgeuzia kibao.

“Mmoja wao mwanadada anaitwa Varie Masquet alinieleza, maana kuna siku nilimuuliza,” Aizaki akajibu.

“Sawa, una fununu yoyote ya wapi walikuwa wanaishi?” akamuuliza.

“Hapana, sikuwahi kujua, walikuwa wakija asubuhi na kuondoka saa nane mchana. Labda naweza kusema tu walikuwa wakitumia gari aina ya *Jeep Cherokee* jekundu namba LD 750,” akajibu na kuongeza kitu kingine.

“Aizaki, nashukuru kwa majibu yako, naomba usizungumze lolote juu ya hili hata kama utaulizwa na *IGP*. Swala hili utakuwa ukinijibu mimi tu kama nikihitaji. Kaa tayari, muda wowote nitakuhitaji Dar es saalam kama itabidi, na taarifa zote utakuwa unazipata kupitia *RPC* na siyo mtu mwingine yeyote. Usikubali ofa ya bia wala chakula,” Amata akamweleza na kutulia, kisha akamtazama na kumtwanga swali, “Umeoa?”

“Ndiyo!”

“Sawa! Sasa ni hivi, mpeleke mkeo kwao kwa muda, na ubaki peke yako. Nina maana yangu kukwambia hivi. Na maana hii utaijua siku nyingine. Kama huna pesa, utaniambia, kadi yangu ya mawasiliano ni hii...” akampa kadi iliyoandikwa namba za simu, “Kila utembeapo hakikisha kadi hii unayo” akanyanyuka kitini na muda huo kijana mwingine akaingia ndani ya kile chumba na kutaka kumchukua Aizaki, Amata akamzuia.

“Huyu si mhalifu, sasa yupo huru! *By the way...* Aizaki! Mimi ni yule mtu uliyemkaripia na kumfukuza pale Maabara baada ya wageni kuondoka..”

“Ha! Braza! Samahani sana braza, sikujua kama upo kazini...”

“Usihofu, nilipenda jinsi ulivyo makini na kazi, tutawasiliana”.

* * *

‘LEKA TULINGE EXECUTIVE LODGE’. Maandishi ya kumetameta yaliyosomeka namna hiyo yalimkaribisha Amata usiku huo. Akavuta mlango na kuingia mpaka kwenye dirisha kubwa la mapokezi. Akiwa katika kumsubiri mhudumu, luninga ya pembeni hapo ikawa ikirusha habari ya saa mbili usiku ambayo ilimvutia kusikiliza.

Mtwara; mwili wa mwanamke umeopolewa katikati ya Bahari ya Hindi kilomita kadhaa kutoka Msanga Mkuu. Taarifa za kipolisi zinasema, mwili huo ulioonekana kama hauna ubai, uliopolewa na wavuvi alfajiri ya leo na kukimbizwa Hospitali ya Ligula kwa uchunguzi. Aidha, mganga mfawidhi wa hospitali

hiyo amethibitisha kumpokea mwanamke huyo akiwa hajitambui, ila vipimo vinaonesha kwamba bado ana ubai... Duru za kiusalama zinasema kuwa huyu anaweza kuwa mmoja wa abiria waliokunwamo kwenye ndege iliyoungua jana ikiwa angani."

Kamanda Amata alitulia na kusikiliza kwa makini habari hiyo na ilipokwisha, akafikiri kwa sekunde kadhaa.

Hapana, lazima niende! Akajisemea na kuiacha ofisi hiyo ya mapokezi pindi tu mhudumu alipowasili. Akaingia garini na kuanza safari ya kuelekea Mtwara usiku huo huo.

* * *

Katika ofisi za Mamlaka ya Viwanja vya ndege(TIAA) jijini Dar es salaam, watu wanne walikutana usiku huo kwa kikao kifupi. Mkutano huu ulikuwa ni mmoja kati ya mingi ambayo inafanyika kuhusu tukio hili.

"Inaweza kuwa kweli imetunguliwa?" mmoja akauliza.

"Kwa kweli ni ngumu kueleza, lakini tumefanikiwa kupata kisanduku cha kukusanya taarifa za mruko wa ndege..."

"Zinasemaje?"

"Taarifa kutoka kwenye *Black Box* inasema ndege haikuwa na hitilafu yoyote. Hata hivyo bado wataalamu wanachunguza zaidi," akaeleza.

"Zaidi ya kifaa hiki, taarifa ya kibinadamu tutaipata zaidi kwa mmoja wa abiria aliyeokotwa leo asubuhi huko Mtwara," mjumbe mmoja akaeleza wazi.

"Tuna uhakika gani kama ni yeye? Yaani ni mmoja wapo?" mwingine akauliza.

"Aaaah... unajua taarifa kutoka katika rada ya jeshi, inaonesha ndege ile bado ilikuwa katika anga yetu ikielekea Kusini Mashariki. Ni dakika chache tu tangu iruke pale Lindi," akazidi kueleza. Wakati kikao hicho kikiendelea, simu ya ofisi hiyo ikaita, mmoja wao akaiendea na kuipokea.

"Ndiyo nakusikia..."

Kutoka upande wa pili.... "*Rescue 2!* Tumegundua baadhi ya vipande vya mabaki ya ndege katikati ya bahari, kilomita kadhaa karibu na Kisiwa cha Mafia. Hali kadhalika tumepata mwili mwingine uliyoungua vibaya ukiwa umeshikana na mabaki ya kiti, tumegundua hilo baada ya kuona mkanda wa ndege uliofungwa kiunoni na kuunganika na vyuma

vya kiti hicho. Tunaendelea na uchunguzi wa eneo hili kwa kina, taarifa zaidi tutawapatia, *over and out!*” ile simu ikakatika. Yule mzee akarudi na kuwapa habari wajumbe wa kikao hicho.

Ukimya ukatawala kwa sekunde chache kisha mmoja akajikoholesha na kufungua kinywa kusema, “Vijana wa jeshi wako vizuri sana!”

“Haswa, na wamefanya kazi kubwa sana tangu jana usiku, hatuna budi kuwashukuru...” dakika hiyohiyo akakatishwa na simu ile ile, akaindea tena na kuiweka sikioni.

“Makao Makuu TIAA, unaongea na mkurugenzi...”

Akasikiliza simu ile kwa sekunde chache kisha akaishusha na kuvuta pumzi ndefu.

“Vipi?” mwingine akauliza kwa shauku.

“Naomba tuahirishe hiki kikao, nitakuiteni baadaye, nimeitwa wizarani kuna kikao cha dharula,” akawaeleza na kuafikiana. Kikao kile kikahairishwa kwa muda na wazee hao wakatawanyika kuendelea na majukumu mengine.

SURA YA 9

KAMBI YA JESHI LA ANGA NGERENGERE

KATIKA KITENGO maalum cha rada, vijana watatu wa jeshi walikuwa wametingwa na kazi yao wakirekodi mienendo na taarifa za kila ndege inayoingia. Hii ndiyo rada kubwa na yenye nguvu inayoweza kuona hata ndege ikiingia tu Afrika. Mtambo huu wa aina yake ulikuwa ukimilikiwa na Jeshi la Wananchi kwa usalama wa mipaka yetu.

Wakiwa hawana hili wala lile, mlango ukafunguliwa na mkuu wa kikosi hicho, Meja Jenerali Kilowoko. Kwa heshima ya kijeshi wakasimama na kutoa salamu, naye akaijibu kisha wakaketi.

“Enhe vijana! Mmegundua kipya kutoka jana? Au kilekile?” akawauliza.

“Mkuu, vikosi vya maji vinaendelea na operesheni, na kuna tafutishi ambazo wamezipata. Kwa upande wetu sisi hapa hatuna jipya katika hili,” akajibu mmoja.

“Sawa, sasa sikieni, msitoe taarifa yoyote nje kwa lile mliloliona, kwa maana linaweza kuleta mtafaruku. Ibaki kuwa siri ya ofisi hii mpaka nitakapowapa amri nyingine, sawa?”

“Sawa mkuu!!” wakajibu na kila mmoja akaendelea na kazi yake katika mtambo huo, akichakata hapa na pale katika kompyuta yake.

* * *

Madam S aliwasili katika kambi hiyo asubuhi ya siku iliyofuata. Baada ya kuruhusiwa kuingia, akapelekwa moja kwa moja katika ofisi ya Meja Jenerali Kilowoko. Na ni muda huo tu alikuwa akiingia ofisini humo kuanza majukumu yake ya siku mpya. Hakuutegemea ugeni huo.

“Karibu mama!” akamkaribisha, na wote wawili wakaketi ofisini humo kwa mazungumzo.

“Naitwa Sellina au Madam S kama vijana wangu wanavyoniita!” akajitambulisha, “Natokea ofisi za usalama wa taifa, TISS,” akamwonesha na kitambulisho halisi cha kazi ambacho si mara nyingi hukionesha, isipokuwa kwa watu maalumu tu.

“Karibu sana!” akamkaribisha na kuanza mazungumzo yao na kubwa zaidi lilikuwa ni juu ya ajali ile ya ndege. Madam S alifika kambini hapa kuona kama kuna kitu cha ziada kilichogundulika katika ajali hiyo. Hii ni kwa sababu alijua na alikuwa na uhakika kuwa kikosi hicho kitakuwa na taarifa zote za ajali kutokana na uwezo wa rada waliyonayo. Baada ya mazungumzo kama ya nusu saa hivi, wakainuka pamoja na kuingia katika gari la jeshi. Safari yao ilikuwa ni katika msitu mdogo, pembezoni mwa kambi hiyo. Katika msitu huu ndiko mitambo ya rada hii ilifungwa tena kwa kificho cha hali ya juu sana. Kama si mjuvi wa medani hizi, kamwe usingetambua, ungeishia kuona uwanja tu na mapori yasiyo na maana, ndege vita mbovu na chopa zilizoliwa na kutu.

Ndani ya chumba hicho, Madam S alipata nafasi ya kuongea na vijana wale ambao walimweleza na kumwonesha kile ambacho wamekiona na kurekodi. Kisha akamtazama Bwana Kilowoko na kumshukuru, pia akachukua rekodi ya picha zile na kuondoka nazo kwa kibali maalumu kutoka Ikulu.

* * *

LANGLEY – USA

NDANI YA JENGO la makao makuu ya idara ya ujasusi ya Marekani, CIA, kikao cha siri na nyeti kilichukua nafasi alfajiri moja ya siku hizo. Watu wanne, wazee, waliyobobea kwenye medani za kijasusi waliketi katika mtindo wa duara.

“I don’t know what happened in Tanzania!” mmoja akaeleza kuwa hajui nini kimetokea huko Tanzania kuhusiana na ile ajali ya ndege.

“Tumechezewa akili, tena na watu wajuzi wa kazi, najaribu kufikiria Mellania si mtu wa kuzidiwa akili, hata mwenzake Doddy. Lakini imekuwaje? Tuamini lipi, kwamba Mella’ na Doddy ndiyo wamefanya hujuma hii?” mwingine akaonesha wasiwasi wake.

“Mnawazungumzia Mellania na Doddy? Wao ni marubani tu; kwa nini hamuwatazami Cindy na Kelvin, ambao tangu mwaka jana wamekuwa wakifuatilia swala hili? Na kama kabrasha walikabidhiwa wao...”

“*They are dead! We can't speak about dead men here!*” Yule mzee wa kwanza akamkatisha mjumbe huyo kwa kumwambia kuwa hao wamekufa, hawawezi kuzungumzia wafu mahali pale. Wote wakatulia kimya.

“Ndugu! Mellania na Doddy ndiyo waliorusha ndege kutoka hapa Langley na kuwachukua Cindy na Kelvin kwenda Tanzania kwa ajili ya kuhakikisha wanarudi na ile chanjo. Na mpango ulikuwa ni kupeleka Geneva. Sasa kilichotokea mnajua. Sanduku lile lilikuwa *secured* mkononi mwa Cindy ili ahakikishe linafika salama. Ndege imelipuka, tuhuma yetu ya kwanza ni kwa marubani, Doddy na Mellania, hawa ndiyo wa kuwasaka sasa, mamluki!” mjumbe ambaye juu ya meza alipokaa palisomeka ‘No 4’ aliongea.

Ukimya ukatawala tena kila mmoja akipekua kabrasha lake kutazama taarifa iliyowafikia na kuandikwa ndani yake. Zaidi ya yote taarifa ilieleza wazi kuwa watu watatu wametumwa Tanzania kwa uchunguzi wa siri juu ya kadhia hiyo.

“Wao watakutana na mtu wetu pale Dar es salaam, Bwana Johnson Kasalu ambaye tayari ana taarifa fulani fulani za siri ambazo zitawasaidia ni vipi watategua kitendawilia hiki,” mjumbe namba moja ambaye katika kikao hicho alionekana kuwa kiongozi alilieleza jopo.

“Vipi kuhusu picha za Satelaiti? Hazijaonesha chochote?” mwingine akauliza, “Maana sioni katika taarifa hii,” akaongeza huku akifunga lile kabrasha na kulisukumia kando.

“Picha za satelaiti hazijaweza kuonesha chochote. Na hapo ndipo utata unapojitokeza, ina maana hii ishuru kuna watu walikuwa wanaijua, hivyo walijipanga haswa, na ili tusipite kwenye nyayo zao, wamefuta kwa kuitia moto ile maabara, *bullshi!* Tutawatia mkononi hata kama ni miaka mia,” akajibu namba moja na kuzungumza huku kauma meno.

“Idara ya usalama wa taifa ya Tanzania inasemaje au niseme imechukua hatua gani?” akauliza mwingine kwa kuwa naye hakuona kitu kama hicho katika kabrasha lile.

“Mjumbe! Kumbuka kanuni zetu, kila nchi tuna vichwa vyetu, hivyo hatutumii idara za nchi hiyo katika kupeleleza. Unajua unapofanya hivyo amini usiamini kazi huwa ngumu kwa sababu ni vipi kama ni wao wamefanya hujuma hii ili wabaki na hiyo chanjo? Hivyo sisi tunafanya kwa maslahi ya Taifa la Marekani na Utukufu wa *White House*,” akajibu namba moja.

Baada ya majadiliano marefu na mazito yaliyochukua takribani saa nne, wakaweka maazimio ya kazi. Wadau hawa wakagawana majukumu ya kufanya katika uchunguzi huo. Mjumbe mmoja kati ya hao alipewa kazi ya kuunda kikosi kazi cha kufanyia uchunguzi nyendo za Mellania na Doddy ili kujua kama walikuwa na uhusiano na vikundi vyovyote vya kigaidi. Walitakiwa kuchunguzwa simu zao, barua pepe na za kawaida, marafiki na familia zao. Katika wajumbe wengine, yupo aliyepewa jukumu la kufuatilia mchakato mzima unavyofanyika huko Tanzania na wengine kuratibu maswala mbalimbali katika hilo.

DAR ES SALAAM

JOHNSON KASALU alishusha miwani yake na kuwatambua mara moja wageni wanne walioingia uwanja wa ndege wa Dar es salaam mchana huo. Akajitoa pale alipo na kusogea jirani, kisha akakohoa mara tatu na wale jamaa, mmoja wao akafanya vivyo hivyo. Kasalu akatoka na kuelekea kwenye maegesho na kuingia kwenye gari alilokuja nalo. Punde si punde wale wageni nao wakaingia katika gari hilo hilo na Kasalu akalitia moto na kuuacha uwanja huo.

“Karibuni Dar’! Jiji la joto na mvua zisizokwisha,” akawakaribisha, na hiyo ndiyo ilikuwa sentensi ya kwanza kwa wageni wake. Wakati huo tayari alikuwa akiacha Kipawa na kuitafuta Vingunguti akiwa juu ya Barabara ya Nyerere.

“Asante, pole na majukumu,” mmoja akaitikia kwa Kiswahili safi na Kasalu akajibu kwa kichwa. Kila walichokifanya ndani ya gari hilo kilikuwa na maana yake. Ukimya ukaendelea garini. Kasalu akakunja kushoto mara alipoifikia Barabara ya Nkurumah, akachukua ile ya Lumumba mpaka Umoja wa Vijana, akakunja kushoto na kuchukua ya Morogoro kisha Umoja wa Mataifa na moja kwa moja wakafika Masaki kwenye ile nyumba namba 9, iliyojengwa chini ya hospitali kubwa ambayo Sir. Drostdyhof ndipo alipokatishiwa uhai wake. Si yeye tu na wengine wengi ambao walihukumiwa kabla kwa makosa yao chini ya kanuni ya S.A, yaani *Secret Assassination* kadiri ya serikali yao na kuuawa kwa siri ndani ya nchi hii pasi na yenyewe kujua.

Kasalu akaingiza gari katika chumba maalumu na lango lake likajifunga. Wakateremka, naye akawaongoza kwenye mlango mwingine na kuingia humo. Ilikuwa lifti ambayo inauwezo wa kubeba watu hata kumi. Wakateremka mpaka chini na kuifuata nyumba namba tisa iliyojengwa chini mita kumi na tano kutoka katika uso wa nchi.

Ndani ya nyumba hii kulisheheni kila kitu, silaha, ukumbi wa

mazoezi ya viungo, chumba cha kulenga shabaha, chumba cha mateso, kliniki, mawasiliano na vingine vingi. Ungeweza kuishi humu hata miaka mitano bila kutoka nje lakini usipitwe na hata jambo moja la huko duniani.

“Tunapambana na wajuzi!” Johnson akawaambia wakati vijana hao wakijitupa kwenye makochi.

“Tutawatia mkononi, tuna watu wa kuwakamata hai na kuwaleta hapa, lakini zaidi ya yote ni kupata lile sanduku,” Jesse, mmoja wale wageni mwenye mwili mkubwa wa mazoezi akajibu. Kutoka katika mfuko wake wa koti akatoa picha mbili akaziweka mezani. Johnson akazitupia jicho na kutikisa kichwa.

“Doddy na Mellania!” akasema.

“Yes! Lazima wafike hapa, hii ni amri ya moja kwa moja,” Jesse akasema kisha akazirudisha mfukoni.

Kikao cha mikakati kikachukua kama dakika thelathini hivi na mambo yakawekwa sawa na kila mmoja akawekwa katika kitengo maalumu. Mmoja alitumwa kufanya uchunguzi katika Wizara ya Afya kujua nini kinazungumzwa juu ya sakata hili. Mwingine alipewa Muhimbili naye kusikia na kunusanusa nini kinazungumzwa juu ya hilo. Mwingine akapelekwa Lindi akitakiwa kufuatilia nyendo za uwanja mdogo wa ndege wa mkoa huo, kuchunguza kujua nini kilijiri. Jesse akaelekea Mtwara kumwona Cindy kwa kuwa Johnson alimpa taarifa hiyo. Johnson Kasalu akabaki ofisini kwake akiratibu kila taarifa kwa kuwa alikuwa mwenyeji wa mazingira.

* * *

MTWARA

Kamanda Amata aliwasili katika hospitali ya Ligula saa nne asubuhi na kuonana na mganga mfawidhi. Baada ya kujitambulisha kwa utambulisho bandia, akaeleza shida yake, haikuwa ngumu. Akaruhusiwa kumwona mgonjwa huyo. Ndani ya chumba hicho kulikuwa na Cindy peke yake kama mgonjwa mahututi. Muuguzi mmoja alikuwa kando akiratibu mwenendo wa mapigo ya moyo ya mwanamke huyo, na kuhakikisha mambo mengine yako sawa.

“Anaendelea vyema ila hawezi kuongea!” muuguzi akamweleza Amata ambaye alikuwa kimya akimwangalia mgonjwa huyo. Alimkumbuka, kwani ni yuleyule ambaye alimhusudu mara tu alipomwona kule kwenye hafla lakini mara hii hakuwa na mwili ule wa kutamanika.

Moto ulimwuunguza sana maeneo mbalimbali ya mwili wake mpaka kufanya nguo yake kuungana na sehemu za nyama yake. Sura yake haikuathirika, ilibaki na urembo uleule, hata akiwa katika barakoa ya kumsaidia kupumua, Cindy alionekana akitabasamu.

“Kuna vifaa vyovyote mliyomkuta navyo?” akauliza.

“Tumemkuta na saa tu ambayo tumemuhifadhia, zaidi ya hapo hakuna kingine,” muuguzi akajibu. Amata akatikisa kichwa kukubaliana naye.

“Naomba kuiona!” akamwambia yule muuguzi na baada ya muda tu akaletewa. Ilikuwa saa ya kisasa sana, *Tommy Tech*. Alipoiweka kiganjani mwake, Amata akamtazama tena Cindy pale kitandani, hakuamini.

Ina maana mwanamke huyu ni Spy? Akajiuliza kutokana na saa iliyokuwa mkononi mwake. Haikuwa tofauti sana na hii ya Cindy. Kamanda Amata akajikuta sasa anataka kumjua zaidi mwanamke huyu. Akaifyatua ile saa kwa nyuma na kuchomoa kadi sakima ndogo, akaitia mfukoni pasi na mtu yeyote kumwona kisha akamrudishia ile saa yule muuguzi.

“Ihifadhi, na usimpe mtu yeyote! Akiamka mrudishie saa yake,” akamwambia.

“Samahani, nahitaji, kupata picha yake kwa kumbukumbu za Wizara, unaweza kumtoa hiyo barakoa kwa sekunde mbili tu?” akaomba.

“Sawa ijapokuwa siruhusiwi kufaya hivyo!” yule muuguzi akajibu.

Amata akachukua picha kwa haraka na kisha wakamrudishia ile barakoa ya oksijeni kama mwanzo.

“Asante nitakununulia soda kama hutojali...”

“Eee soda tena, lazima nijali,”

“Unaitwa nani?”

“Somoe!” akajibu.

“Basi ukitoka unitafute,” Amata akamwambia na kumpa kadi yake ya kibiashara, kadi kama ileile aliyompa Aizaki.

* * *

Katika hoteli ya Msimbati *Sea View* iliyojengwa kilomita nyingi nje ya mji huo, Kamanda Amata aliketi katika nyumba ndogo ya chumba kimoja aliyopanga kwa siku hiyo mara baada ya kutoka kule hospitali. Akiwa ameketi kwenye mlango mpana wa kioo uliotazama baharini, tayari kadi ile ilikuwa katika simu yake akijaribu kupekua taarifa zilizomo. Hakukuwa na mambo mengi zaidi ya picha na video fupifupi ambazo hazikuwa na maana kwake. Akaendelea kupekua mpaka video ya mwisho hii ndiyo iliyomvutia.

Picha zake hazikuonekana vizuri, mara ilionekana miguu,

ikapita haraka, mara *dashboard* ya ndege nayo haikukaa hata sekunde ikapita. Kwa ujumla kulikuwa na mvurugano wa matukio, hii ilionesha kuwa ndani ya ndege hiyo kulikuwa na hali ya kugombania kitu, na nyendo za huku na kule. Moyo wa kijana huyu ukajikuta ukiingiwa na ubaridi wa ghafla. Hii ikamvuta umakini wa kuitazama na kupekuwa zaidi. Akarudi ya nyuma iliyokuwa na sauti akaisikiliza tena.

'Are you ok?'

'Yes!'

'And now you are finished!'

Maneno haya yalisikika vizuri na hata picha ilikuwa imetulia, ilionekana Cindy alipoona hilo akainua mikono na hii ilifanya saa yake kurekodi picha ya mtu aliyekuwa akisema maneno hayo, lakini haikumpata sura sawasawa. Amata akalaani, maana alijua angeiona sura yake kazi ingekuwa ndogo.

'Noooo! Nooo!'

'You can't do that bast....'

'Paaah!! Paah! Paaah!'

'Kelviinnnnn!'

'Shut up, bitch, and you will die with fire, fuc you,'*

Sauti hiyo ilisikika vyema ijapokuwa iliambatana na kelele za vitu vingine, na picha ambazo hazikutulia hata kidogo. Hakuna sura iliyooneka kwa utulivu, ni mara moja tu sura ya mmoja wao ilipita kutoka upande mmoja wa *screen* na kwenda mwingine.

'Time! Time! Time! Here we go!'

'I'm burningggggg!!!!'

Sauti hizo zilikuwa zikisika haraka haraka kwa kuingiliana. Amata alikuwa makini kusikiliza na kung'amua sauti mbili za kiume na moja ya kike ambayo hakuwa na wasiwasi nayo, alihisi kuwa lazima itakuwa ya Cindy. Baada ya ile ya kiume kusema *'Time! Time! Time!'* ukafuata mvumo wa kitu kama upepo mkali. Sauti ya kike iliyosema *'I'm burning!'* ikamalizwa kwa kishindo kikubwa.

Bila shaka kishindo hiki ni cha mlipuko! Akawaza Amata.

* * *

Asubuhi iliyofuata, akiwa amejilaza katika ubaraza wa nyumba hiyo ndogo. Juu ya kitanda kidogo cha kamba, huku akipigwa na upepo wa baharini, kati ya kundi kubwa la watu waliokuwa katika ufukwe wa eneo hilo, kulikuwa na mtu mmoja aliyekosa utulivu. Akili ya Amata

iliganda kwa kijana huyu kwa dazani ya dakika. Kila mara kijana yule alikuwa akionekana kuongea na simu yake ambayo ilifungwa katika saa. Kengele za hatari kichwani mwa Amata zikalia, akahakikisha ampotezi katika upeo wa macho yake huku akijifanya amelala.

Ina maana kuna watu wananifuatilia! Wamenijuaje? Akajiuliza. Akili yake ilikimbia haraka haraka kubadilisha wazo hili na kuweka lile. Alipomwona yule jamaa kazubaa kidogo tu, akajiangusha upande wa pili wa kile kijitanda cha kamba na kujiviringa mpaka katika mlangoni na kuingia ndani kwa ufundi mkubwa na kufika karibu na begi lake. Akachukua bastola na kuiweka sawa kisha akaibana kwenye mkanda wa suruali. Yote haya aliyafanya bila kusimama, akachukua fulana na kuivaa, akatoka ndani ya ile nyumba kwa mtindo wa mbwa, na huko nje akainuka na kupotelea katika miti iliyoota hapo kwa wingi.

Kule ufukweni yule jamaa akageuka kwa chati kutazama pale alipokuwa akimwona Amata yaani pale kibarazani. Hayupo! Akashtuka na kusimama kutoka pale mchangani alipoketi. Akageuka huku na huko na kuinua mkono wake mpaka karibu na kinywa kisha kuongea na baadae akaushusha.

Shiiiiit! Nilikuwa nafuatilwa, ningeekufa kibwege. Nani hawa wanaojua kumfuata mtu kwa ukimya namna hii? Bila shaka napambana na wataalamu wa mambo, safari hii kazi ipo! Kamanda Amata akawaza kisha akatoka pale nyuma ya mti alipoegemea na kujichanganya na watu huku akivuta hatua kumwendea yule jamaa kwa hadhari kubwa, akiangalia huku na huko, nyuma na mbele kwa wizi aone kama kuna kiumbe kinamfuata. Hakuna.

Yule kijana alikuwa bado akishangaa shangaa, kutahamaki, akahisi kitu kikimgusa kwenye mbavu zake.

“Tulia!” Amata akamwambia.

“We nani?” yule bwege akauliza.

“Usitake kujua! Ongoza upande wa miti, ukileta vurugu nitayasitisha mapigo ya moyo wako,” akamwambia na kumsukuma taratibu kuelekea upande wa pili ambapo palikuwa na miti mingi na mabafu ya watu kuoga pindi watokapo kwenye maji chumvi.

“Ingia humo!” akamwamuru, na yule jamaa akaingia ndani ya bafu mojawapo. Kabla Amata hajafunga mlango, yule jamaa akageuka ghafla na kumpelekea pigo moja lililoitoa ile bastola mkononi. Alipotaka kupeleka pigo la pili akadakwa mkono na kunyongwa,

mifupa ikaachana kwenye maungio. Jamaa akapiga yowe la uchungu na Amata akampa pigo takatifu. *Karate* moja iliyotua katiwa ya utosi na kumwacha akijibwaga upande wa pili wa lile bafu. Alipotaka kuiwahi bastola, jamaa kama umeme akaiwahi na kupiga teke, ikaenda upande mwingine. Amata akaona lile pigo halikumpata sawasawa, akiwa bado anashangaa, jamaa akamchota mtama Amata, naye akabwagika kwenye sakafu kama mzigo.

Yule jamaa akainuka haraka kumkabili Kamanda. Kisu mkononi. Akaja kasi, Amata akainua miguu akamchota ngwala iliyompeleka chini huku kisu kikimtoka mikononi. Wakati akianguka alipigiza kichwa kwenye sinki la maji na kutoa mguno wa maumivu. Amata akaiwahi bastola yake na kuiweka kiunoni kisha akajiinua na kumkamata ukosi wa shati na kumtumbukiza kichwa kwenye ndoo ya maji kwa sekunde kadhaa, akamwopoa. Yule mtu alipiga chafya mfululizo, akipumua kwa nguvu na haraka.

“Nani bosi wako, nambie!” akamwuliza huku akimtumbukiza tena na kumwibua.

“Si-si-siwezi ku-kwa-mbia!” akajibu kwa taabu na kufuatiwa na chafya mfululizo. Amata akamtumbukiza tena na safari hii akamwona jamaa akilegea, akamwopoa na kumwachia. Akaanguka chini mzima mzima. Marehemu.

“Shenzi kabisa!” akamsindikiza marehemu huyo kwa tusi kisha akamwendea na kumpekua. Kwenye shati hakuna kitu. Kwenye suruali, akatoa kadi moja ya kibiashara na kijitabu kidogo cha kumbukumbu. Kiunoni mwake bastola moja ndogo, akavitia mfukoni mwake. Akamvua saa na kuitia mfukoni. Amata akahisi kitu kama kimiminika kikitiririka kichwani mwake. Akajishika, akagundua kuwa ana jeraha, maana matone ya damu yalikuwa yakimtiririka. Akawahi kutoka na kuufunga mlango kisha akavunja kitasa kwa nje na kuondoka zake. Hatua moja, ya pili, macho yake yakatua kwenye mlango mwingine wa bafu bovu, na kulining'inizwa kibao chenye maandishi, ‘*Out of use*’ yaani hakitumiki. Akakichomoa haraka na kukipachika kule kwenye mlango wa bafu alilomwacha yule jamaa, kisha akaondoka zake.

Sasa mchezoni utanoga najua nitawachanganya tu kwa hili! Akawaza. Kabla hajafikia mlango wa chumba chake, simu yake ikaita. Simu ya marafiki, akainyakua na kuiweka sikioni.

“Hello!” akaita.

“Hello mi Somoe wa Ligula,” akaitikiwa.

“Ndiyo umemaliza *duty*?”

“Ndiyo, nimeshakabidhi ripoti kwa anayeingia mchana. Halafu yule mgonjwa tumemrufaa kwenda Dar, Agha Khan,” akamwambia Amata. Taarifa hii kidogo ikampa kigagaziko.

Rufaa! Akawaza. Hakutilia maanani sana kwa sababu rufaa kwa mgonjwa ni jambo la kawaida sana.

“Oh, sawa, sasa mimi nipo Msimbati, hatuwezi kuonana jioni ya leo? Maana kesho naweza kuondoka!” Amata akaanzisha swaga zake.

“Mmmmh! Nije huko? Mbali sana!”

“Usijali, basi nitakuja mimi...”

“Sawa! Basi ukifika maeneo ya Faya nipigie,” Somoe akamaliza na kukata simu.

Afadhali nitapata wa kuniondolea upweke! Akafunga simu yake na kuirudisha mfukoni. Hakuwa na haja ya kukaa. Akainua mkoba wake mdogo akautupia mgongoni na zile tafutishi zake zote akaziweka humo humo na kutoka. Akili ya haraka ikamtuma kuacha gari lake, hivyo akapita mbali kabisa na kutafuta daladala la kawaida tu akaelekea mjini.

* * *

Katika jumba moja maeneo ya Shangani vijana watatu walikutana kwa kujadiliana jambo. Ilionekana wazi kuwa jambo lenyewe halikuwa la heri hata kidogo kwa jinsi tu walivyoonekana.

“Oya jamaa kapotea hewani!” mmoja akawaambia wenzake.

“*What!* Kapoteaje sasa?” mwingine akadakia.

“Naona kimya tu hapa, kila nikim*trace* simpati...”

“*Shii!* Asije kuwa jamaa kamnasa... maana tulishaambiwa kuwa huyu jamaa hafai, ni wa kumwangelia kwa jicho ng’avu...”

“Sasa! Hatuna budi kwenda”.

Vijana hawa baada ya kuona mwenzao hapatikani katika mawasiliano ikabidi wafunge safari kuona kulikoni. Kwa mwendo wa kasi sana, walichukua kama dakika thelathini hivi kuwasili Msimbati. Wakateremka na kugawana njia kila mmoja akiwa ametingwa kumtafuta mwenzao na kuangalia usalama wao pia.

Baada ya kuzunguka eneo lote hilo hawakufanikiwa kumwona ndugu yao huyo.

“Atakuwa wapi? Au ametekwa?” mmoja akauliza.

“Sijui, hawezi kutekwa kijinga hivyo, Shebby namjua makeke yake!” mwingine akaongeza. Baada ya kutafuta kama saa nzima hivi wakakubaliana kutoa taarifa kwa kiongozi wao. Hakuna hata mmoja aliyewaza kupekuwa chooni. Wakatoka na kuingia garini kisha safari ya mjini ikaanza.

* * *

Bwana Torres Kazumari, mwenye uhotara wa Kimakonde na Kireno alikuwa barazani kwake akitazama mandhari safi ya Bahari ya Hindi. Hakuwa na wasiwasi wa maisha, kwani kama pesa alikuwa nayo nyingi ya kutosha. Watu wengi wenye *deal* walipenda kumtumia mzee huyu wa makamo ama kuua au kufuatilia kitu. Alikuwa na mawasiliano na watu wengi sana kutoka sehemu mbalimbali za dunia, wazuri kwa wabaya, wema kwa wenye dhambi.

Pasipo na kutarajia akapokea ugeni huu wa vijana watatu ambao aliwatumia kazi tangu siku iliyotangulia. Akaushusha mtemba wake maana haukuwa muda muafaka wa kukutana na watu hawa.

“*Yes guys!* Nipeni taarifa, nini kimewarudisha sasa?” akawauliza huku akiwatazama kwa jicho kali.

“Shebby amepotea!” akajibiwa. Yule mzee akashtuka kidogo na kuwatazama mmoja mmoja.

“Mnasemaje? Kapoteaje yani kwa mfano!” akawauliza.

“Alikuwa akifuatilia nyendo za yule mtu huku tukiwasiliana naye kuwa tunakwenda kumfungia kazi, mara hakupatikana hewani tumekwenda eneo lile hatukumwo...”

“*Stop!*” akamzuia kusema, akainua mtemba wake na kuuvuta pafu kama tano hivi akauweka mezani.

“Mnajua ninyi ni wazembe sana! Mmeshaharibu kazi yaani! Nimewaambia huyo mnayemfuatilia sasa si sawa na wale wajinga wajinga wa huko nyuma, huyu ni mjuzi, mtaalamu wa mambo mengi. Sasa nina uhakika, kama Shebby hajauawa basi yupo katika hali mbaya, na kama yuko mikononi mwa huyu jamaa basi sasa tunaingia msambweni, yaani patanuka hapa Mtwara,” akasimama na kuifuata simu yake ya mezani, akabofya namba fulani, akazungumza kwa Kireno kisha akakata simu hiyo na kuwarudia vijana wake.

“Hakikisheni mnapata taarifa ya Shebby kama kafa au yuko wapi mniletee kabla ya saa nne usiku,” akatoa amri na wale vijana wakatimka zao.

* * *

“Yaani najishangaa tu jinsi ulivyouteka moyo wangu, ulipoondoka tu nikahisi kukumiss...” Somoe alilalama akiwa chini ya kifua cha Kamanda Amata huku mavazi yao yakiwa kando sakafuni.

“Mmmh acha uongo, nyi’ warembo waongo sana ee!” Amata akamjibu na kumbusu kinywani, “Kwa nini hukusindikiza mgonjwa Dar?”

“He! Ndugu yake alikuja!” Somoe akajibu.

“Ndugu yake!” Amata akashangaa.

“Ndiyo, kaka yake anayeishi Marekani, hajui hata Kiswahili, wamemchukua kwa ndege ya kukodi kwenda Agha Khan. Wamekuja na muuguzi kabisa,” Somoe akaeleza. Taarifa hii ikamwingia akilini sawia kabisa. Akainuka na kumwacha Somoe pale kitandani.

“Bebi wapi teeeena?”

“Subiri, narudi,” Amata akamwambia Somoe. Akachukua simu yake na kubofya hapa na pale, akatuma taarifa kwa Madam S kuhakikisha kama mgonjwa huyo kafikishwa Agha Khan. Kisha akarudi kitandani na kuanza upya mchezo wao. Somoe alionekana kuwa stadi sana kitandani kiasi cha kumpagawisha kijana huyu wa TSA. Lakini msichana huyu naye alipata taabu na huyu bwana maana alikuwa na maguvu kiasi kwamba alisukuma kwelikweli mpaka Somoe kujikuta hoi.

Nusu saa baadae walikuwa hoi kila mtu upande wake.

“Yule mgonjwa mlimpa jina gani?” akamuuliza Somoe.

“*Unknown!*”

“Sawa hamumjui, mlimpa jina gani la utambulisho?”

“*Unknown!* Tulimwandika kwenye faili hivyo hivyo yaani ‘*Unknown*’”.

Dakika chache baadae Somoe akachukuliwa na usingizi mzito. Hii ikawa nafasi kwa Amata kufanya mambo yake. Kwanza akaiendea suruali yake na kuchomoa saa ya Shebby, kijana aliyemuua bafuni huko Msimbati. Akaitazama na kugundua kuwa ilikuwa na simu ya upepo iliyotengenezwa ndani kwa ndani. Mara nyingi sana si rahisi kumkuta raia wa kawaida akiwa na saa kama hii vinginevyo ana kazi maalumu. Akaiweka pembeni na kuchukua kile kijitabu kidogo cha kumbukumbu

na kukipekua ndani, hakukuwa na la maana sana zaidi ya miadi mingi ya siku za nyuma. Kurasa ya mwisho ndipo kidogo palimsisimua.

Kuna kazi nyeti!

Onana na Brixton Bandeko,

Mtwara Club saa mbili usiku leo!

Ujumbe huu ulikuwa katika kikaratasi tofauti na zile za kijitabu hicho. Tarehe ya miadi hiyo ilikuwa ni siku moja nyuma yaani baada ya kufikiri akagundua kuwa ni jana yake tu..

Hii inaweza kuhusiana na sakata bili? Akajiuliza. Akaweka pembeni hicho nacho, kisha akaitoa ile kadi ya kibiashara na kuisoma.

'...Toress Alexis Kazumari,

CdG Marine Tour...'

Kisha kukafuatiwa na namba kadhaa za simu na barua pepe. Amata akazitazama namba zile, mbili zilikuwa za Msumbiji na moja ya Tanzania. Akataka kukiweka pembeni, hisia yake ikamkatalia, akakitia kwenye mkoba wake pamoja na vile vingine.

Labda vitanisaidia mbele ya safari! Akawaza na kisha akaingia bafuni kuoga. Yote hayo yakifanyika, Somoe alikuwa akikoroma kwa usingizi mzito wenye ndoto tamu tamu. Alikuwa akijigeuza tu kutoka upande huu kwenda ule kule huku mwili wake wa kibantu usio na nguo ukifanya umbo la kupendeza ambalo lingemsisimua mwanaume yoyote yule.

Akiwa mbele ya kioo akichana nywele zake mara baada ya kutoka maliwato, Amata akashtuliwa na simu yake ya kazi, simu ambayo daima haipigwi na ikipigwa ujue kuna ujumbe mzito. Simu hii ilikuwa ya kawaida sana lakini haikuingiliana na mtambo wowote wa simu, iliweza kuwasiliana kwa satelaiti tu.

"Amata, huyo mgonjwa unayemsema hajafikishwa Agha Khan...!" sauti ya Madam S ilimpasha habari. Amata akatulia kidogo kisha akamtazama Somoe, bado alikuwa kalala fofofu.

Kama hajafikishwa Agha Khan, yuko wapi? Akajiuliza pasi na jibu.

* * *

Dar es salaam

Cindy alifikishwa Dar es salaam akiwa katika mikono ya Jesse. Katika hospitali ya Ligula, Jesse aliruhusiwa kumchukua mgonjwa kama alivyoomba kwa kujitambulisha kama kaka yake na kutakiwa

kuimfikisha Agha Khan. Pamoja naye alikuwa na vibali vyote stahiki vya kumchukua mgonjwa huyo. Lakini hiyo ilikuwa danganya toto kwani Cindy alifikishwa Nyumba namba 9, Masaki. Moja kwa moja akaingizwa katika kliniki ndogo chini ya ardhi ambako juu yake kulikuwa na hospitali kubwa na ya kisasa. Mwanamke huyo alianza kupatiwa matibabu ya hali ya juu kwa sababu Jesse alijua wazi kuwa akiamka basi angeweza kuwapa mwanga mkubwa wa sakata hili.

Kumbe jambo hili sasa ndilo Kamanda Amata alilolikosea, yeye akilini mwake alikuwa akiwaza kuwa mwanamke huyo, ‘*Unknown*’ akiamka apate nafasi ya kumhoji mawili matatu, na alipopewa taarifa kuwa khamishiwa Agha Kan, akashtuka. Taarifa kutoka kwa Madam S kuwa hata Agha Khan hayupo ikamfanya ajione bwege aliyechezea shilingi chooni. Sasa tayari kazi mpya ya kumtafuta Cindy, yuko wapi, ilianza kujiunda upya katika moyo wake.

“Hakikisha anaamka, nina mazungumzo naye kisha atapelekwa Marekani,” Jesse alitoa amri kwa daktari na muuguzi waliokuwa kwenye hekaheka za kumtibu.

“Tuombe Mungu maana huyu mtu yupo kwenye hali mbaya, vipimo vya awali vinaonesha amepata matatizo kwenye ubongo. Ama alijigonga au alipigwa kwa nguvu, na hata akiamka sidhani kama atakuwa na akili sawasawa...”

“Kwa hali hiyo atapona kweli? *Come on!*” Jesse aliposikia jibu hilo akahisi kuchanganyikiwa, akajishika kichwa na kuzunguka ndani ya chumba kile.

“Inawezekanaje awe kwenye hali hiyo?” Jesse akabwata.

“Sikia Jesse! Huyu kapata ajali, tazama alivyongua vibaya, na inaonekana hapa ubongo wake umepata shida kubwa mbili; damu haifiki kwa kiwango cha kawaida katika mfumo wa ubongo kwa sababu hii sasa ubongo wake haupati oksijeni ya kutosha, na hakuna njia yoyote ya kumwamsha mpaka Mungu aamue,” yule daktari akaeleza kwa kifupi.

Maneno haya yakamfanya Jesse kusimama na kumtazama yule daktari kwa jicho kali. Ukimya ukachukua nafasi, kila mtu akiwaza lake. Jesse akajitupa kwenye kochi katika korido ndogo karibu kabisa na mlango wa kuingia katika chumba hicho, akashusha pumzi na kufikiri kwa kina nini hasa ambacho anaweza kufanya.

SURA YA 10

CABO DELGADO

DAKTARI EDWARD MINZI alirudiwa na fahamu. Akafumbua macho taratibu na kupambana na mwanga mkali machoni mwake. Akajaribu kupepesa huku na huko lakini ile taa ilikuwa kali sana kiasi kwamba ilikuwa vigumu kwake kuweza kufungua macho moja kwa moja. Akajaribu kujitikisa, akatikisika, kilichomshangaza ni kuwa nguo alizovaa hazijui wala hajawahi kuziona hapo kabla.

Niko wapi? Akajiuliza. Alipoinua kichwa kutazama vizuri upande wa mbele, ile taa kubwa ikazimika na kubaki zile za kawaida. Hakufungwa. Akajiinua kwa taabu na kuketi kitandani. Uchovu ulikuwa dhahiri shahiri mwilini mwake. Dakika hiyo hiyo mlango ukafunguliwa na mwanadada mrembo akaingia ndani ya chumba hicho. Edward akabaki kumtolea macho hasa kwa nguo aliyovaa. Mwanadada huyu, maji ya kunde, mwenye shingo nyembamba na mwili usio mnene sana akaufunga mlango nyuma yake.

“We ni nani?” Dkt. Edward akauliza.

“Usijali! Utanijua tu, nipo hapa kwa ajili yako, kukupa huduma zote utakazo...” akajibu kisha akaanza kuchojoa kivazi chake ambacho mpaka hapo tayari alikuwa nusu uchi.

“... najua una mawazo na maumivu mengi kuhusu ajali ya moto, usijali, nitakufanyia masaji, nitakuliwaza kwa kila unachokihitaji kama mwanaume,” akamsogelea Edward pale kitandani.

“Hebu niondolee ushetani wako!” Dkt. Edward akaongea kwa sauti ya kichovu. Yule mwanadada akasimama na kumshangaa mwanaume huyo.

“Nimepewa pesa nyingi kwa ajili yako... unajua? Na siwezi

kumwanguka mteja wangu.” Yule mwanadada akasema huku akiwa karibu kabisa na pale alipoketi daktari huyo.

“Hata ungepewa dunia, we unafikiri kila mtu anapenda kufanya upumbavu kama huo na mtu asiyemjua?” Dkt. Edward akalalama.

“Huu ni upumbavu! Ingekuwa upumbavu basi Adam na Eva wangebaki wenyewe na kufa kisha dunia kubaki tupu. Wewe umezaliwa kutoka hapa, katika hili, ina maana mama na baba yako ni wapumbavu?” akamwambia.

“TOKAAA!” Dkt. Edward akang’aka huku mkononi mwake tayari alikuwa na chupa ya mvinyo aliyoinyakuwa katika meza ndogo pembeni mwa kile kitanda. Almanusura, kumrushia mwanamke huyo kama hasingechelewa kutoka nje ya chumba kile.

“Shenzi kabisa!” Edward akatukana, kisha akainuka na kujikokota kuliendea dirisha labda kutoka hapo angeweza kuona au kujua ni wapi alipo. Alipolifikia dirisha akajikuta yuko juu kadiri ya mita hamsini hivi, kumbe chumba kile kilikuwa katika ghorofa ya sita katika jengo moja lenye urefu wa wastani. Akaangaza macho ili aone kama anaweza kutambua ni wapi. Hakuweza. Zaidi ya machoye kujazwa na taswira za majumba mafupi kwa marefu. Akarudi kitandani, na kuketi kwa kujiinamia. Mawazo yakamrudisha siku ya tukio la moto, jinsi watu walivyokuwa wakijaribu kujiokoa na wasifanikiwe.

‘Doc’ This way pleaseee!’

‘...this way pleaseee!’ akaikumbuka hiyo sauti iliyomfanya apate njia ya kutoka katika jengo hilo. Mara hii, ikaja na mwangwi kichwani mwake, akatikisa kichwa na kutulia.

Niko wapi? Kwanini niko hapa? Tumebujumiwa? Akajiuliza na kisha akaanza kuanguka chozi. Akajaribu kuvuta kumbukumbu tena kuelewa nini hasa kilitokea.

Moto ulianzia stoo, ndiyo, stoo, nani wa mwisho kuingia? Aaaa nimemsabau jina, bakuwa Mtanzania, tumebujumiwa, tumebujumiwa! Akawaza kwa uchungu, kumbukumbu hii ilianza kuja kwake namna hii. Dkt. Edward akaanza kupata kumbukumbu ya tukio lile.

* * *

Kumbukumbu ya tukio ...

“Unatoka wapi huko?...” Dkt. Edward alimuuliza kijana mmoja wa kizungu mara baada ya kukutana naye kwenye korido moja ambayo

hatakiwi mtu kuingia huko kama huna shughuli maalumu.

"Aaaa excuse me Sir, is my mistake..." alimjibu hivyo kuwa kakosea tu.

"The place is only for authorized people! Don't do it again!" akamkanya kuwa asirudie kwani hilo eneo ni kwa watu wanaohusika tu.

"Ok Doc'!" alimjibu kisha akaondoka huku akisindikizwa na macho ya daktari huyu wa makamo.

Nyendo za hawa watu sizielewi! Kuna tatizo, mara tu ugeni utakapoondoka yapasa niliripoti bili! Aliwaza huku bado akimtazama kijana yule akiishia kwenye mlango mwingine.

* * *

Rejea chumbani...

Kutoka pale kitandani alipoketi, aliendelea kutulia, akijaribu kuvuta kumbukumbu zaidi. Mara mlango ukafunguliwa na wanaume watatu wakaingia, mmoja kati ya hawa sura yake haikuwa ngeni kwa daktari huyu. Akainuka alipoketi na kusimama akitazamana naye.

Ni buyu! Ni buyu buyu! Kumbukumbu ikarudi akamkumbuka kijana huyo aliyemwokoa katika moto ule.

"Mr. Datsun! What have you done to my country?" Dkt. Edward akampigia kelele huku akimsogelea kwa hasira akimuuliza nini amekifanya kwa nchi yake (yaani Tanzania).

Jamaa huyo aliyekuwa ndani ya suti maridadi, nyeupe, iliyompa utanashati na mwonekano wa kipesapesa, na vijana wake wawili akabaki kumtazama daktari huyo.

"Una shida gani?" akamwuuliza kwa Kiswahili safi kilichonyooka. Hii ikamfanya Dkt. Edward kushtuka, hakuwahi kumsikia hata siku moja mtu huyu akiongea Kiswahili kabla ya hapo.

"Nimekuokoa kwenye moto, nimekuleta hapa mahala salama, pazuri. Tazama panavyopendeza! Nimekuolea mke mzuri, mrembo, maana najua kuwa wewe hujaoa, akupe raha zote za dunia. Umemkataa, ukataka kumpiga na chupa ya mvinyo. Huku kwetu mvinyo tunakunywa hatutumii kama silaha... Isitoshe, mwanamke mrembo hapigwi kwa chupa ya mvinyo, bali kwa mabusu na mapenzi mwororo." Datsun akamwambia Edward.

"Kwanza hapa nipo wapi, nambie!" Dkt. Edward akang'aka huku akionekana wazi kutweta kwa hasira.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Utajua tu, usijali. *Doc’ This way please!*” Datsun akamwambia Edward. Sentensi hii ya mwisho *Doc. This way please!* ikamkumbusha tena Edward tukio lile la moto.

* * *

Kumbukumbu ...

Dkt. Edward alishtushwa kwa kelele za king’ora cha kuashiria hatari ya moto. Alitazama huku na huko, akawahi kwenye swichi ya dharula ambayo ukiiminya milango yote ya jengo hilo hufunguka na kubaki wazi huku vifaa maalum vikiwa vinamwaga maji kusaidia kuupunguza moto huo. Siku hii ikawa sivyo. Edward akaminya na kuminya milango haikufunguka wala vifaa vya kuzima moto havikufanya kazi. Daktari huyu akachukua shoka dogo karibu kabisa na mlango, akakipiga kioo cha mlango wa ofisi yake. Kikapasuka na kuacha uwazi, alipotaka kutoka, mlipuko mkubwa ukatokea katika chumba kingine cha kuhifadhi madawa ya maabara na kusababisha moto mbaya kabisa uliokuwa ukisambaa kwa kasi.

“*Nooooo!*” akapiga kelele. Mara akajikuta kashikwa mkono kutoka nyuma yake, hakuwa mwingine alikuwa Datsun. Cha kushangaza kijana huyu alikuwa kavalia mavazi maalum ambayo hayakuweza kuathiriwa na moto ule. Mkononi mwake alikuwa na koti jingine linalofanana kabisa na lile vazi lake. Akamvika haraka Edward kisha akamvuta mkono.

“*Doc’ This way pleaseee!*” akapiga kelele na kumvuta kwa nguvu. Hapakuwa na mlango ila dirisha kubwa. Datsun aliruka teke moja la maana na kukitawanya kioo hicho kisha akatoka na daktari yule, akapotea naye msituni. Wakiwa katika kukimbia huko, Dkt. Edward akaanza kujihisi uchovu, mwili unakosa nguvu, akasimama na kuhisi giza nene, akageuka nyuma hakuna kingine alichokiona zaidi ya moshi mzito kwenye mipenyo ya matawi ya miti. Nuru ikampotea, akaanguka chini na kuchukuliwa na usingizi mzito.

Datsun, akambebea Edward begani mwake na kuvuta hatua katikati ya msitu huo, mwendo wa kama dakika kumi na tano hivi akatokea barabarani. Upande huu aliotokea haukuwa na nyumba kwani kijiji cha Londo kilikuwa upande wa pili. Kando tu ya barabara hii, kulikuwa kumeegeshwa gari la kisasa aina ya *Jeep Cherokee* lenye usajili wa namba

LD 750. Kutoka ndani ya gari hili, akateremka kijana mwingine wa kizungu na kufungua buti wakamuweka humo Dkt. Edward na kuingia garini, likatiwa moto na kuondoka kwa kasi.

* * *

Rejea chumbani...

Dakika kumi na tano baadae, Dkt. Edward alikuwa ndani ya suti mpya, nyeusi. Akatoka katika sebule ndogo na kuwakuta wale watu wakimsubiri akiwamo Datsun. Pamoja na kukaa ndani ya chumba kile hakuwahi kufikiri kama mlango huo ungemfikisha sebuleni. Ni dakika hiyo ndipo alipogundua hilo.

“Waoh! Sasa umekuwa mtu mwingine kabisa, twen’ zetu!” Datsun akamwambia Edy kisha wakainuka na kutoka ndani humo. Wakaingia kwenye kambarau na kupanda ghorofa sita juu zaidi, huko wakatokea katika eneo pana, ilikuwa ni juu kabisa ya ghorofa. Dkt. Edward alishangaa kukuta helkopta kubwa imeegeshwa huko, akasita na kusimama.

“Vipi?” Datsun akauliza.

“Mnanipeleka wapi?” akamuuliza.

“Usijali, hatuna haja ya kukudhuru, tumekuchukua wewe kwa kazi maalumu na utalipwa pesa nyingi na kupewa mahali pa kuishi milele,” Datsun akamjibu huku akimshika mkono.

‘*Dimens – LabTech*’, akapachikwa kitambulisho juu ya koti lake kilichosomeka namna hiyo.

“Hiki ni kitambulisho chako cha kazi mpya, kazi yenye pesa nene sana daktari. Usijali, sasa unakwenda kuonana na Lord Dimens mwenyewe. Inawezekana umewahi kumsikia au kuona chata zake kwenye vifungashio vya kemikali na madawa mbalimbali. Basi, leo hii utakuwa Mtanzania wa kwanza hata ikiwezekana kupeana naye mkono...” Datsun akamweleza Dkt. Edward aliyebaki kimya.

“Usinipake mafuta kwa mgongo wa chupa!” Edward akajibu na kutulia kitini. Helkopta ile ikaruka na kuondoka zake. Edy, kama mwenyewe alivyopenda kuitwa akabaki kutazama jiji lile kutoka juu. Kila kitu kwake kilikuwa kama ndoto, akabaki kimya akitafakari hili na lile. Akawakumbuka maswahiba wake, walioteseka pamoja katika utafiti wa chanjo ile ndani ya msitu wa Londo kwa miezi takribani kumi na

tano na ushei. Taswira ya Kanali Kasiga na Meja Malege, madaktari wa jeshi la Tanzania ilimjia, akamkumbuka Teknolojisti Ziada Kipele. Chozi likamdondoka.

Helikopta ilikuwa hewani ikipasua anga, Dkt Edward Minzi aliendelea kuutazama mji ule ulivyoziidi kusukumwa mbali. Majumba yaliyoujaza yakatoweka na kumezwa na msitu mnene. Msitu huo haukuwa tafauti sana na ule wa Londo. Akaendelea kutazama chini na kuona uoto huu wa kupendeza na mito iliyokatisha katikati yake.

Baada ya mwendo wa takribani saa mbili hivi. Katikati ya msitu ule. Akaona kitu kama nyumba au jengo, kikianza kuonekana. Moyo wake ulipiga kwa nguvu, na kuhisi kijasho chembamba kikimtiririka.

“Doc’ Tumefika maskani... Hapa utaendelea na kazi yako uipendayo, yaani ya uchunguzi wa kimaabara,” Datsun akamwambia Edward.

“Hapa ni wapi?” yule daktari akauliza.

“Hutakiwi kupajua, ila bado upo nchini kwako Tanzania. Utaongea Kiswahili, lugha unayoipenda, utakula ugali unaoutaka na dagaa wa Kigoma na mengine mengi,” akajibiwa. Punde tu ile ndege ilikuwa imekaribia kabisa lile jengo ambalo kutoka juu lilionekana katika umbo pembe sita yaani *hexagone*. Dakika kama tano baadae, ile helikopta ikatua juu kabisa ya paa la jengo lile kama kule ilikotoka. Wakateremka.

* * *

MTWARA

Nina mambo mawili ya kuanza nayo; kumtafuta mmiliki na kuijua CdG Marine Tour na kumpata Brixtone. Nikimaliza haya, vyovyote ivavyo, nianze kufanya uchunguzi wa tukio la mlipuko wa ndege na kujua yule mwanamke ‘Unknown’ kapelekwa wapi. Dah! Yaani saa 24 hazitoshi kwa siku, sijui nifanyeje... namhitaji Chiba na Gina, katika sakata bili. Nitaanzia wapi kumwingia yule bibi anipe hawa watu? Akawaza, akiwa chali kitandani.

Amata akajiweka tayari kwa kutoka, mara baada ya akili yake kuwa tayari kwa kazi. Akachukua kila anachokiona kwake kuwa kitamfaa kwa usiku huo. Alipohakikisha kuwa yupo kamili, akatoka na kukiacha chumba hicho. Nje ya hoteli hiyo akakodi taksi tayari kwa safari.

“Wapi kaka?” dereva akauliza.

“Mtwara Club!” Amata akajibu kisha akatulia kitini.

“Club ya wenye pesa hiyo kaka, asee!” Dereva akaanza lugha ya utani.

“Ni ya kawaida tu! Ni mbali sana?”

“Hapana, ni hapo mbele tu”.

Haikuwachukua muda mrefu, ile taksi ikawasili nje ya kilabu hicho. Hakika ilikuwa ya kisasa. Taa za rangi rangi zilikuwa zikiwaka na kubadili sura ya kila mtu. Muziki laini ulikuwa ukisikika upande wa chini. Upande wa juu ilikuwa ni sehemu ya watu wanaokunywa pombe huku wakiwa na mazungumzo yao. Hakukuwa na kelele ila utulivu, na muziki ule kutoka chini ulikuwa ukifika kwa kiwango kidogo sana.

“Karibu!” Sauti ya mwanadada wa kimakonde ikamkaribisha. Akamgeukia na kuitikia karibisho hilo. Amata akamsanifisha kwa kumtazama; kuanzia nywele mpaka kanyagio.

Si mbaya sana, analipa! Akawaza, kisha akatoa tabasamu lenye nguvu ya kumlegeza kila mwanamke au tuseme kila mrembo.

“Samahani! Unamjua Brixtone au ushawahi kumsikia?” Amata akamuuliza huyo dada pasi nakujali jibu atakalopewa.

“Unamhitaji?”

“Ndiyo, mimi ni mgeni wake,” Amata akaunganisha jibu huku moyoni mwake akiwa na uhakika kwamba kwa swali hilo la mwanadada huyo basi kampata anayemtaka.

“Njoo huku!” akaambiwa. Naye akafuata kama fisi aliyeambiwa ‘huku kuna mfupa!’.

* * *

Brixtone Bandeko, kijana mwenye pesa. Mwanachama mkubwa sana wa kilabu hiki. Mrefu, mwenye tambo na wajihi unaomuonesha kama ‘dume’ mbele ya macho ya wamtazamaye. Kutokana na pesa alizokuwa akimiliki, wapo waliosema kuwa ni jambazi. Wengine walisema kuwa ni *Freemason*. Basi, ili mradi tu kila aliyeweza, alisema lake. Kiuhakika, alikuwa na pesa, alimiliki nyumba mbili kubwa sana huko Magomeni ya Mtwara. Magari kadhaa ya abiria yaani daladala na taksi za kutosha. Jambo moja tu ambalo wengine walimhisi kuwa labda jogoo hapandi mtungi, ni hali yake ya ukapela. Hakuwa ameo lakini alikuwa na wanawake wasiopungua wanne na wote walikuwa wakimiliki maduka ya nguo na vyakula ila hawakuwa na watoto. Kama ni kutumia, basi kijana huyu alikuwa akijua vyema kufanya hivyo. Hakuwa bahili, lakini kwa wanaomjua vyema alikuwa mtu katili sana kwao. Kwake kutoa roho ya binadamu mwenzake ilikuwa ni kama kuvunja biskuti tu.

Katika kilabu hiki cha usiku, Brixtone alikuwa na sehemu maalumu ya kukutana na vijana wake. Alikuwa akimiliki kundi la vijana ‘wakora’, wanaojua vyema kutumia silaha. Walikuwa wakupora magari, au pesa kwenye maduka makubwa. Mara kadhaa wameteka mabasi ya abiria na kupora mali. Na hapa ilikuwa ni sehemu yao ya kugawana nyara. Lakini pia alikuwa akikodishwa na watu mbalimbali katika kufanya uhalifu kama wa kuua na kadhalika. Watu walimjua yeye lakini nyuma yake naye alikuwa akimilikiwa na mtu. Mtu mwenya pesa kuliko unavyofikiri, mwenye marafiki wema kwa wabaya kutoka pepo zote nne za dunia.

Siku hii haikuwa ya kijana huyu kuwa hapa kilabuni, ila alikuja kwa sababu maalumu. Kuomboleza. Kumuombeleza kijana wake, Shebby. Shebby alikutwa bafuni amekufa baada ya mfanya usafi kugundua tofauti iliyopo katika milango ya mabafu kadiri ya alivyoacha mara ya mwisho.

Nikimtia mkononi huyu mshenzi, nitamtafuna nyama! Alijiwazia Brixtone, kisha akainua chupa yake ya pombe kali, *‘Jackie Daniel’* na kugugumia kama mafunda manne na kuishusha mezani kwa kishindo. Alipojiegemeza kwenye kochi hilo, mlango ukafunguliwa.

“Niambie Somoe mpenzi!” Brixtone akamwambia mhudumu huyo aliyekuwa sasa kaingia ndani na mlango ukiwa wazi nyuma yake.

“Una mgeni!”

“Mgeni!”

“Ndiyo, inawezekana ni muhimu kwako,” Somoe akamwambia kijana huyo naye akatoa ishara ya mkono ‘mwambie aingie’.

Somoe akatoka na kumpisha Amata kuingia ndani kisha mlango ukafungwa. Kamanda Amata akaketi katika kochi linalotazamana na kijana huyo. Brixtone akainua uso na kukutana macho kwa macho na mtu asiyemjua. Hawakuwahi kukutana kabla, hata jinsi macho yao yalivyokuwa yakitazamana utazani madume ya chui yaliyodhulumiana jike. Huyu akipeleka poo poo zake kulia na huyu anapeleka kushoto, zinakutana. Ila mara nyingi Amata alikuwa anawahi kuzifikisha mwisho kabla ya mwenyeji wake.

“Wewe ni nani?” akamuuliza.

Amata hakujibu, akatoa ile saa ya Shebby na kuiweka mezani, kisha akaegemea kochi alilokuwa amekalia. Brixtone akaitazama ile saa na kushusha pumzi.

“Was it you?” Brixtone akapiga kelele za hasira na kuinuka kutaka kumvamia Amata. Akiwa kwenye hali hiyo akakutana na konde zito

lenye kilo nyingi lililotua katika chembe, akarudi na kujibwaga kitini huku akipumua kwa shida kidogo. Alihisi kama mifupa yote ya mwili imekusanyika sehemu moja.

"Yes! It was me!" Amata akajibu.

Ukimya ukachukua nafasi kisha Brixton akajitahidi kuongea, "ume-mu-u-a Sheb-b-by!"

"Ndiyo! Nataka unambie kazi gani ulimtuma juzi?" akamjibu na kumuuliza swali, "Na nahitaji kumjua Torres!"

Brixton akatoa macho baada ya kusikia jina hilo likitajwa. Huwa si rahisi Torres kujulikana kirahisi namna hiyo. Mkodoo huo ukamjua jambo Kamanda.

"Huwezi..." Brixton akamwambia Amata. "...Nimeshakujua, nimepewa pesa nyingi sana kukuua wewe mshenzi," akaongeza kumwambia Amata.

"Maumivu ya hiyo ngumi yamekutoka, sivyo? Nitakupa nyingine ambayo itasimamisha moyo wako," Amata akaongea kwa sauti ya chini lakini iliyofika vyema kwa kijana huyo.

"Kutaka kumwona Torres ni kukitafuta kifo chako," Brixton, akamwambia Amata na ghafla akachomoa bastola yake. Kamanda Amata alilijua hilo lakini akabaki kochini katulia.

"Mshenzi wewe! Sasa jeuri yako na ujanja wako vimekwisha, nitakuua hapa hapa! Sali sala ya mwisho..."

"Brixton umekuwa mchungaji mpaka kunitaka mimi kusali sala ya mwisho?"

"Acha maneno yako ya kijinga wewe! Hapa umekutana na Brixton Bandeko, au niite BriBa!" akajigamba huku akisimama taratibu na bado domo la bastola likiwa linamtazama mgeniwe.

"Nipe majibu yangu kwanza..." Amata naye akamtunishia misuli

"Ee nilimtuma akuue, hata hivyo una bahati tu ulimuwahi, la sivyo usingemuweza..."

"Hah! Hah! Hah! Najua kuna aliyekutuma kufanya kazi hiyo, napenda kumjua kabla hujaniua!" Amata alicheka kwa dharau na kumwambia Brixton.

"Pumbavu sana wewe..." nukta hiyo Brixton alipotamka hayo, Amata aliinua mguu wake na kuukita kwa kisigino juu ya meza, kisu kidogo kikachomoka mbele ya kiatu hicho na kudidimia chini ya kidevu cha Brixton.

"Aaaaaaggghhh!" Brixton akatupa bastola na mikono yake ikakamata kile kisu na kukichomoa huku kikifuatiwa na bubujiko la damu. Nukta

hiyo hiyo akajikuta akipata pigo moja la judo, likampeleka kitini. Amata akamkandamiza na goti lake kifuani.

“Nambie, unamfanyia kazi nani?” akamhoji huku mkono mmoja akiukamata ule wenye kisu.

Brixton alikuwa akitapatapa, hakuweza kusema lolote, kisha akatulia kimya uhai ukamtoka.

“Shiiiiit!” Amata akajitoa na kumwacha jamaa huyo akidondoka kochini. Akaingiza mikono yake mifukoni na kumpekua kuona kama kuna chochote, akachukua simu na ubamba uliyokuwa juu ya kochi. Pesa akamwachia. Akamwinua na kumkalisha kama mwanzo huku damu zikiwa zimechafua kifua chote.

“Upumzike kwa amani kama unastahili! Kwa maana, kila kitembeacho, hufa,” akatoka na kuufunga ule mlango, kwa nguvu zake zote akavunja kitasa kwa upande wa nje, na kuondoka zake.

Nusu saa baadae akawasili chumbani kwake na kukuta patupu, Somoe hakuwepo.

Kaenda wapi hyu mwanamke? Akajiuliza. Na kusogea hadi kitandani, akaketi juu yake. Nukta hiyo hiyo simu ikaita juu ya kitanda kile. Amata akashtuka na kuitazama. Ilikuwa simu ya Somoe. Aliikumbuka vyema. Akainuka na kwenda maliwato, hakumwona. Akapekua hapa na pale, asimwone. Kidogo akili ikamhama, akaanza kuzunguka huku na kule ndani ya chumba hicho.

“Somoe! Somoe! Somoe!” Akaita. Lakini ukweli ni kwamba hakuwepo. Ile simu pale kitandani ikaendelea kuita, akachukua kitambaa na kutumia hicho kuishika kisha akaweka sauti kubwa.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Unaogopa hata simu? Najua upo Mtwara na umeshaua vijana wangu wawili mpaka sasa. Nakufuatilia tu! Na mwisho wako upo mikononi mwangu saa si nyingi. Kitu unachokifuatilia kitakugharimu maisha yako mjinga wewe. Huu ni mpango na mkakati wa kimataifa, usijidanganye kijana kama utauweza, la hash! Wewe ni takataka tu, CIA na FBI wapo hapa Tanzania, mimi najua lakini wewe hujui... Na nakwambia mkakati wa kuwamaliza umeanza, asubuhi ya kesho tazama kipindi cha Kumekucha usikie...”

“Wewe ni nani?” Amata akaingilia mazungumzo hayo.

“Hah! Hah! Hah! Unataka kunijua? Usijali tutaonana tu, najua wazi kuwa katika akili yako kesho utanitafuta na utakuwa umeingia mwenyewe kwenye domo la mamba. Hao uliyowaua usifikiri wanahusika na mtandao huu, ni vibaraka tu vya kutumwa. Kama hivyo umeviua basi,

ila nakusifu kwa kuwa una silaha mwili mzima umemuuaje Brixton? Kwa kiatu chako! Asee.” Sauti ile ya dharau ilikuwa ikimuuzi Amata, alitamani mtu huyo awe hapo mbele yake lakini haikuwezekana. Jambo pekee alilojiona mjinga ni kuwa ndani ya chumba kile alichomuulia Brixton hakufikiri kama kuna kamera mficho, ‘hidden camera’.

“Nimekuuliza wewe ni nani? Wanaume huwa hatupigani kwa maneno, jitokeze hadharani tupambane ...” Amata akang’aka.

“Huyo mwanamke aliyekuwa chini ya pua yako saa moja iliyopita, hakuwa hapo bure. Kwa kumtongoza na kulala naye basi ujue ndiyo mwanamke wako wa mwisho, hah! Hah! Hah...! Na habari zako zote ametuletea, Malaya wa kiume wewe! Kenge maji!”

Amata akashikwa na hasira na kuipiga chini ile simu, nayo ikatawanyika vipande vitatu. Akaketi tena kitandani na kujiinamia kwa muda akifikiri jambo.

Nani mshenzi huyu, anayenifuatilia kila hatua? Amata akajikuta katika wakati mgumu sana. *Tutaona mwisho wake!* Akajisemea moyoni kisha akachukua simu ya Brixton na kuanza kuipekua, hakukuta cha maana. Majina yalikuwa matano tu likiwemo la Shebby. Akaiweka pembeni na kuanza kupekuwa ule ubamba. Humu mulikuwa na mambo mengi ambayo kidogo yalimfurahisha. Picha ya mpenzi wake, iliyopambwa kwa maneno matamu matamu, akaangalia mazungumzo yao na kubaki kucheka tu. Zaidi ya hapo, ni picha za maswahiba, sura zao hakuwahi kuziona, alichokifanya yeye ni kuzituma kwenye simu yake ya siri na nyingine ziliingia moja kwa moja katika mashine yao ya utambuzi kule Shamba.

Je nikimpata huyu ataweza kunambia siri ya mpenziwe? Hapana, nitakuwa nimekosea, wacha nibadili mbinu ya mashambulizi. Kabla sijarudi Dar, kesho lazima nifike CdG Marine Tour. Baada ya hapo, nitarudi Dar kesho hiyo hiyo, kwa maana shujaa akiona shimo haruki mara moja, bali hurudi nyuma na kuvuta kasi kwanza! Akawaza na kufikia uamuzi.

* * *

Jonson Kasalu akamtazama Jesse, kijana mwenye misuli iliyojaa kimazoezi.

“Kwa hiyo!”

“Nimefanya kazi nyingi sana ila hii kuna vitu vinanishangaza na kunichanganya. Kwanza Bwana Johnson ieleweke kwamba kazi yetu

haitakiwi iingiliwe kabisa na serikali,” Jesse akamwambia Kasalu.

“Sasa Jesse unafikiri mimi na wewe tutafanyaje? Kumbuka tukio hili limetukia hapa Tanzania, kwa nini wanaintelijensia wa hapa wasifanye kazi? *Unless otherwise* itoke oda kutoka Langley...”

“Na ndicho nilichotaka kusema...” Jesse akamalizia, “Kwani mpaka sasa wamefikia wapi? Maana najua wao watachunguza kienyeji tu na kuchukulia swala hili kirahisi rahisi. Tanzania haina intelinjensia ya kupambana na mtandao wa kimataifa kama huu, hawana. Sanasana vijana watapoteza maisha au wataharibu na kuifanya kazi iwe ngumu zaidi”.

Johnson akashusha pumzi, akatazama meza yake kwa sekunde kadhaa kisha akamtazama Jesse, “Sawa!” akamjibu.

SURA YA 11

NUKUSHI KUTOKA SHIRIKA la kijasusi la Marekani, *CLA*, ilifika sehemu husika katika idara ya usalama wa taifa. Baada ya hapo ikawasilishwa Ikulu kwa Rais kwa kuwa yeye usalama wa taifa zima u mikononi mwake.

Baada ya kuisoma na kuona jinsi ilivyo na utata, akaitisha kikao cha dharula cha baraza la usalama la taifa. Wajumbe wote wakakutana katika ofisi maalum ndani ya jengo la Ikulu kuijadili taarifa hiyo. Kila aliyeisikia alishangazwa kwayo.

“Ina maana *CLA* washafika hapa na wanajua kuwa sisi tunachunguza?” mmoja wa wajumbe akauliza.

“Kwa mujibu wa maelezo hapa ni kuwa ‘kwa kuwa tayari serikali ya Tanzania ilikabidhi chanjo ile kwa Shirika la Afya Duniani, hivyo ni jukumu lao kufanya huo uchunguzi. Hivyo idara ya upelelezi ya Tanzania isihusike kabisa katika kulichunguza hilo kwani itavuruga upelelezi’, ina maana hata kama hawajaingia basi wapo kwenye uchunguzi”, akaelezwa na Waziri wa Ulinzi. Kila mtu akabaki kimya kutafakari.

“Hivi kwa nini hawa jamaa wanapenda kutuona hatujui sana au?” mjumbe mwingine akadakia.

“Hatukatai kwamba wao wana utaalam na teknolojia ya kisasa katika kufanya uchunguzi, lakini huwezi kutuambia tuache wakati hilo swala sisi ni la kwetu...”

“Watawala wa dunia!”

Baada ya majadiliano marefu, Mheshimiwa Rais akajiweka sawa na kutoa neno lake, “Sikilizeni, maadam wamekubali ni uzembe wao, na wanataka kulichukua wao, basi mi nafikiri tuwaache tuone watafikia wapi...”.

“Sawa Mheshimiwa Rais, lakini mimi kama mimi siipendi hii tabia ya hawa jamaa kutudharau sisi na vyombo vyetu vya usalama. Mikasa mingapi wao wenyewe wameshindwa kuinusuru nchi yao?” Mkuu wa majeshi, CDF, akatoa kauli yake.

“Lakini maadam Amiri Jeshi Mkuu umesema. Basi! Nasi tutafuata, lakini bado nina hoja kuwa idara yetu ya usalama wa taifa ikae tayari kwa lolote muda wowote!” akasema IGP.

Rais akafunga mkutano, na viongozi wote wakaondoka katika ukumbi huo kila mmoja akilaumu hatua hiyo.

Baada ya wote kuondoka ndani ya chumba kile cha mkutano, Rais alibaki na *Aide de Camp* na walinzi wake watatu. Ilimchukua kama dakika kumi hivi kutafakari jambo kisha akainuka na kutoka. Akavuta hatua na kuipita milango kadhaa mpaka katika chumba kingine ambacho hupenda kukaa kama ana mambo ya kufikiri au mazungomzo yanayohitaji faragha kubwa. Chumba hiki kilijulikana kwa jina ‘*Kilimanjaro Square*’.

Ndani ya chumba hicho, daima huingia peke yake au na mtu anayemuhitaji tu. Walinzi wake wakabaki nje na yeye akaingia ndani ya chumba kile, akaketi kimya akitafakari.

Hakuna kazi ngumu kama hii, ila sijui kwa nini tunaipenda! Urais ni mzigo, yaani bata huna muda wa kufurahi na mkeo, loh! Akawaza. Dakika tano baadae akapata jibu, akachukua simu ya mezani na kupiga kisha akamtaka mtu wa upande wa pili kufika mara moja ndani ya ofisi hiyo na kuleta taarifa ya kazi mpaka ilipo.

* * *

Madam S akaegesha gari lake katika viwanja vya Ikulu, akateremka na kabrasha lake mkononi, moja kwa moja akavuta hatua na kuzipanda ngazi za jengo hilo mpaka ndani.

“Mzee anakusubiri!” akaambiwa na afisa usalama ambaye huwa na jukumu la kujua ratiba zote za dharula na za kawaida za Mkuu wa nchi. Madam S akatikisa kichwa na kumfuata kijana huyo mpaka kwenye mlango maalumu, akamfungulia na kuingia kisha ukafungwa nyuma yake. Mlangoni hapo kulikuwa na walinzi wawili waliosimama pasi na kutetereka, na yule kijana aliyemleta Madam S akasubiri sehemu nyingine ila si mbali na mlango huo.

Ndani ya chumba kile, Rais alimkaribisha Selina kwa ukarimu wote.

Daima akutanapo na mama huyu, moyonimwe huona katua mzigo mkubwa, kwani alimwamini na kumheshimu kama mama au dada yake.

“Sellina! Nashukuru umekuja, najua ni wewe tu unayeweza kunitoa katika hofu hii...” akaanza kwa kusema.

“Ndiyo mkuu!” Madam S akajibu.

“Niliipa kazi ofisi yako kushughulikia swala la mlipuko wa ile maabara ...” akamwambia.

“Na sisi tukaenda mbele zaidi kuchunguza juu ya mlipuko wa ile ndege iliyobeba zile chanjo...” Madam S, *Head Of TSA*, akasema.

“Yes! Madam, nahisi una taarifa nzuri sana za kunipa, nakusikiliza!” Mkuu wa nchi akamwambia mwanamama huyo.

Akafungua kabrasha lake na kuliweka mezani kisha akaanza kutoa taarifa fupi ya nini kimegundulika katika uchunguzi wa awali.

“Mheshimiwa Rais, kama tulivyojadili katika kikao cha Baraza la Usalama kuwa hii ni hujuma, mpaka sasa tumeliona hilo kwa asilimia sitini na tano. Ulitupatia kazi ya kuchunguza juu ya moto uliozuka katika maabara yetu ya kitafiti huko Londo. Ndani ya siku hizi kijana wetu alikuwa akifuatilia kwa ukaribu na kwa kuwa, taarifa za awali zinasema hakuna aliyetoka ndani ya maabara ile, uchunguzi umeanzia kwa mmoja wa walinzi waliokuwa zamu siku hiyo anayejulikana kwa jina la Aizaki, PC namba 1876B wa Kikosi cha FFU Mkoa wa Lindi. Kutoka kwake kuna tafutishi tulizozipata; kwanza wageni, yaani wanafunzi wa Kizungu waliokuwa wakifanya mazoezi na kujifunza maswala mbalimbali ya kitafiti. Wote walitoka katika maabara hiyo salama na moto ulizuka dakika kama kumi baadae...”

“Oh! Asante Mungu, maana hapo tungeanza mada nyingine za kidiplomasia...” Rais akasema.

“Enhe...” akamtaka mwanamama huyo kuendelea.

“... Taarifa hii inasema zaidi kuwa wakati moto ule ukiendelea, walirudi na kuondoka tena na mpaka sasa hawajulikani walipo...”

“*What?* Yaani wakarudi na kuondoka? Inawezekana walisahau baadhi ya vitu vyao,” akasema. Na Madam S akaendelea na taarifa yake, “Pamoja na taarifa hii kuna majina yao na vyo wanavyosoma pamoja na nchi watokazo. Sisi hatukuishia hapa, tumeingia pia katika uchunguzi wa mlipuko wa ndege. Katika taarifa hii ya kwanza hili hatukuliweka ila litakuwa katika maandishi ndani ya saa 24...”

Rais akapiga makofi ya pongezi na kumtazama mwanamama huyu, “Hongera sana, naona wazi tupo hatua kadhaa mbele, basi nitasubiri

hiyo taarifa ya pili kesho lakini kwa kifupi ni kwamba, shirika la kijasusi la Marekani *CLA*, wametutaka kusitisha uchunguzi wowote juu ya sakata hili...”

“Kwa nini?” Madam S akauliza.

Hakumjibu, akachukua ile nukushi na kumpatia ajisomee mwenyewe. Madam S akapitisha macho haraka haraka na kuitua mezani.

“Sawa!” akajibu.

“Sawa! Nani umemtuma kwa kazi hii?” Rais akauliza.

“Amata Ric...”

“Kamanda Amata!” akamalizia mheshimiwa, “Vizuri, yule kijana anajua kazi na namwamini sana kwa sababu huwa makini katika kazi yake, ingekuwa inawezekana tungemtoa fotokopi, ili tuwe na mwingine kama yeye...” akaongeza kusema, kisha wote wakaangua kicheko.

“Ndiyo, na ameshafanya kazi kubwa sana katika hili. Kesho utaona taarifa tutakayoandika,” Madam S akamwambia mkuu wa nchi huku akifunga kabrasa lake, akalisukuma kwa Rais naye akalipokea na kulifungia kwenye saraka ya meza yake.

“Kesho, ukija hapa, uje na Kamanda Amata, nahitaji kumuona *personal*”.

“Bila shaka!” Madam akajibu na kuinuka, wakapeana mikono, akafungua mlango na kutoka. Kijana aliyemsindikiza kumleta ndani, ndiye huyo huyo aliyemsindikiza kumtoa nje.

* * *

Asubuhi ya siku iliyofuata ilimkuta Amata katikati ya mji wa Mtwara, huku akijua wazi kuwa anafuatiliwa, hakuonesha kuwa na wasiwasi wowote kwa kuwa pia kwake ilikuwa ni sehemu ya maisha yake. Nje tu ya wigo wa Kanisa la Watakatifu Wote, akaingia kwenye taksi, kisha akatulia huku akipepesa macho kujihakikishia usalama wake. Alipoona hakuna, akamwamuru dereva kuondoka.

“Wapi mzee?”

“We twende tu, nipeleke kivukoni mi naenda Msanga Mkuu,” akamjibu.

Yule kijana akawasha gari na kuondoka zake, akachukua Barabara ya Port kama anakuja Shangani kisha akaiacha hiyo na kukamata ile ya kuelekea soko la samaki. Haukuwa mwendo mrefu, dakika kumi na saba tu zikawafikisha eneo hilo.

“Hapa utapata usafiri kaka, kuna viboti vitakuvusha mpaka upande wa pili,” yule dereva akamwambia.

“Asante nashukuru,” akatoa noti ya shilingi elfu tano na kumpatia kisha yeye akapotea zake na mkoba wake mkononi. Hatua kama ishirini na tisa hivi akafika kwenye kijiduka kidogo pembezoni tu mwa soko hilo. Akasubiri ile taksi iondoke. Dakika moja kama si mbili, ikaondoka na muda huo huo likaingia gari moja jeusi, *Ford Cortiner*, likaegeshwa hapo. Hakuna mtu aliyeshuka. Amata akajibanza nyuma ya kile kiduka huku akihakikisha anatazama kila kinachoendelea. Dakika tatu nyingine zikapita, hakuna aliyeshuka kwenye lile gari. Hapo mwili wa Kamanda ukasisimka kidogo, akajua wazi kuwa sasa kuna kazi.

Ndiyo hawa wanaonifuatilia? Akajiuliza. Kisha akapita katikati ya watu na kuingia chooni, akajifungia. Akavua shati lake na kulifunga vifungo, kisha akaligeuza ndani nje na nje ndani akalivaa tena. Kutoka shati sasa ikawa fulana ya kisasa ya vijana wa mjini na usingeweza kugundua kama mguo hiyo kwa ndani ina sampuli nyingine ya nguo. Akavua suruali yake na kuitia begini kisha akavaa nyingine iliyotengenezwa kwa malighafi ya mpira, nywele na ndevu za bandia akajiweka kwa haraka kisha akajibandika sunzua mbili juu kidogo ya jicho lake. Alipohakikisha yupo sawa, akatoka ndani ya kile choo huku mkoba wake badala ya kuwa mkononi sasa umekuwa wa kuweka mgongoni.

“Kaka hujalipa bado!” sauti ya kike ikamshtua, akasimama, kumbe hakujua kama choo kile ni cha kulipia. Akampa Shilingi hamsini kisha akajichanganya na watu mpaka katika ukingo wa bahari. Hapo kulikuwa na mashua nyingi sana. Pembeni kabisa kuliegeshwa moja iliyoonekana ya kisasa. Ndani ya mashua hiyo kulikuwa na Wazungu kama wanne hivi, wawili wa kike na wengine wa kiume.

“Oya!” akamwita mmoja wa wavuvi.

“Vipi kaka, nina samaki kibao tu yaani wewe tu ntu wangu,” yule kijana akamwambia Amata. Na kwa lafudhi yake tu, akagundua kuwa ni Mmakonde.

“Sihitaji samaki kijana...”

“Sawa, nankahitaji nini sasa?” akauliza.

“Nahitaji kuvuka...”

“Unaenda Nsanga Nkuu au?”

“Ndiyo Msanga Mkuu, shilingi ngapi?” Amata akauliza.

“Aaaa shilingi 5000 tu,”

“Twende,” Amata akamwambia kisha wakatoka na kuingia katika

moja ya mashua ambayo inatumia injini ya dizeli na safari ikaanza.

Katika mashua hiyo, mazungumzo kati ya Amata na yule mvuvi yalipamba moto ikiwamo lile la kuokotwa Cindy. Yule mvuvi akaeleza habari yote kadiri anavyoifahamu na Amata akawa anachuja kujua lipi muhimu na lipi si muhimu. Lakini bahati mbaya katika yote aliyoyasikia kwa kijana huyo hakukuwa na muhimu kwa kazi yake. Dakika chache baadaye, ile injini ikawa juu na ile mashua ikawa ikitembea peke yake juu ya maji.

“Huwa tunashushia hapa kaka,” yule kijana akamwambia Amata.

“Asante sana, mimi nitakuwa hapa kwa siku moja tu, nitakutafuta uje unichukue,” akamlipa na kuchukua namba ya simu yake kisha wakaagana.

* * *

‘*CdG Marine Tour*’, bango kubwa lenye maandishi ya buluu lilimkaribisha. Hatua kumi nyingine akafika ndani ya ofisi hiyo.

“Karibu sana!” sauti nyororo ya msichana ilimkaribisha. Kama kawaida yake mbele ya viumbe hivyo hutoa tabasamu la akiba. Lakini akawaza ghafla kama anaweza kumnasa malaika huyo kutokana na badiliko la sura yake hii. Kamanda Amata akajilaumu kwa kutojua nini atakutana nacho mbele ya safari.

“Habari mrembo!” akamsabahi mwanadada aliyemkuta katika dirisha la mapokezi.

“Nzuri kaka, karibu *CdG Marine*, nikusaidie tafadhali...”

“Samahani, nimesoma juu ya hii kampuni yenu kupitia mtandao nikapenda kuwatembelea ili nipate maelezo zaidi kwani napenda utalii wa majini,” Amata akaeleza. Kwa sababu mrembo huyo hiyo ilikuwa ni kazi yake hakuona tabu, akampa habari nyingi za kutosha juu ya kampuni hiyo. Katika chokonozi zake, Amata akamuuliza hasa mmiliki wa kampuni hiyo ni nani, na ndipo akatajiwa jina lisilo geni masikioni mwake.

“Mr. Torres Alexis Kazumari, Mtanzania mwenye asili ya kireno,” akajibu.

Akiwa katika mazungumzo na mwanadada huyo, simu yake ikaita, akajua wazi mwito huo ni kutoka Ofisi Ndogo, akaichukua na kuweka sikioni uku akitoka nje.

“Ndiyo mama!” akaita.

“Asee kijana hebu ishia hapo hapo, njoo nyumbani kuna mambo ya kuweka sawa, fanya hima, Tena Sana Aisee,” kisha ile simu ikakatika, baada ya kuhakikisha ameiweka vizuri, akarudi pale mezani.

“Samahani, nimepata dharula, ninaenda mjini kikazi, si vibaya nikipata namba yako ya simu, nitakupigia siku nikija hata tupate soda pamoja!” akamwambia.

“Bila shaka!” akamjibu na kumpa kadi ya mawasiliano. Kamanda Amata akatoka eneo lile na kurudi upande wa kivuko, hapo akakuta mashua nyingi na ile iliyomleta ilikuwa imekwishaondoka. Hakujali. Akachukua simu yake na kupiga ofisi ya shirika la ndege la Tanzania, ATC. Alipohakikisha kuna ndege adhuhuri ya siku hiyo akaweka nafasi. Ijapokuwa hata yeye alikuwa amepanga kurudi Dar es salaam siku hiyo, simu hii ilimharakisha tu, na alijua hilo kutokana na uzito wa taarifa yenyewe. Ikambidi akatishe kila kitu. Alipenda kumchimba na kumteka kimawazo mrembo yule lakini haikuwa hivyo.

Mashua iliyomfikisha ng’ambo ilikuwa nyingine kabisa na hii ikamshushia upande wa pili kama alivyoomba. Jambo la kwanza alilolifanya ni kutazama kama lile gari ‘*Ford Cortiner*’ lipo au halipo. Hakuliona. Akatembea kwa mguu kama umbali wa mita mia mbili hivi ili aone kama kuna mtu anayemfuatilia. Alipohakikisha hakuna, akaingia kwenye taksi aliyokutana nayo ikitoka na safari zake nyingine.

“Uwanja wa ndege!” akamwambia dereva naye akatia gia na kuondoa gari.

* * *

“Imekuwaje tumempoteza?” jamaa mmoja ndani ya lile Ford akawauliza wenzake, “Mnajua mtu kama yule kumpoteza ni hatari sana kwetu. Maana hujui ni wapi ataibukia, kumbuka alipotupotea kule Msimbati akaondoka na uhai wa Shebby. Kabla hatujamwona tena akaondoka na uhai wa Brixton, tutamweleza nini Torres?” akauliza. Ukimya ukatawala huku lile gari likibadili barabara.

“Lakini mi si nilisema tubaki palepale ninyi mkang’ang’ania tuondoke. Yule jamaa aliingia chooni mi nilimwona, na mpaka tunaondoka, yeye hajatoka...”

“Kwa hiyo atakuwa amefichama chooni sivyo? Unafikiri hivyo!” Yule jamaa wa kwanza akamkatisha na kumuuliza swali.

“Ndiyo anaweza kuwa kajificha chooni mle!” akasema. Ukimya

ukachukua nafasi huku dereva akiendelea kuifukuza barabara.

“Huu ni ugomvi na Toress!”

Nusu saa baadae lile gari likamezwa ndani ya wigo mkubwa wa jumba moja la kifahari. Jumba hili daima hutumiwa kwa vikao tu vya Torres Alexis Kazumari na vijana au watu wake. Wakamkuta kichwa kikimuwanga kwa mawazo, akienda huku na kurudi kule.

Akiwa ndani ya lindi la mawazo akagutushwa na gari lililoingia katika uwa wa jumba hilo. Akawasha luninga yake, ikamwonesha ni gari gani lililongia. Akavuta hatua na kuketi kitini. Vijana wanne wakaingia sebuleni hapo na kila mmoja akaketi mahala pake.

“Mmefanya nini?” Torres alianza kwa swali. “...niliwaambia hakikisheni hamumpotezi, ina maana kuwa mmekosea mahali mpaka kawagundua na kuwatoroka...” akalalama.

Hakuna aliyejibu kwa kuwa mioyoni mwao wote walijua uzembe walioufanya. Torres akatazama chini kisha akawaangalia wale vijana.

“Kamleteni yule mwanamke wake!” akamwambia mmoja wa wale vijana. Dakika tu! Somoe akaletwa akiwa hoi, akatupwa sakafuni. Naye akaanguka sakafuni kama mzigo kutokana na hali aliyokuwa nayo.

“Good!” Torres akasema huku akitikisa kichwa chake, “...bwana ‘ako ametutoroka! Na wewe u mikononi mwetu. Tunataka tukutumie wewe mwenyewe kumleta hapa, kama plan A ilishindwa basi plan B lazima uifanikishe. Najua namba yake ya simu unayo maana ile ya kwako tuliyoiacha chumbani kule haipatikani,” akachukua simu na kumpa mmoja wa vijana wake.

“Nina uchungu sana na huyu mshenzi, kaniulia Shebby na Brixton! Namuhitaji, na kama hanijui nitamwadhibu mwenyewe,” akasema kwa ukali, “Taja namba yake haraka!” akamwambia Somoe, aliyekuwa sakafuni, huku tayari mkononi mwake akiwa na mjeledi alioletewa na kijana wake muda huohuo. Somoe alibaki kimya, nywele zake zilizokuwa timtim zilimfanya aonekane kama msukule. Uso wake uliosawajika kwa misukosuko ya usiku uliotangulia ulionekana kuvimba.

“Taja! Nahesabu mpaka tano... moja...mbili...tatu...” Somoe akabaki kimya, “...nn...”

“Hata unitese vipi haitakusaidia. Sijaikariri namba yake. Namba ipo kwenye simu ile mliaoiacha...” Somoe akaongea kwa sauti iliyojawa uchungu na maumivu.

“Wewe ni jeuri!” Torres akashusha mjeledi uliopiga sawia kwenye mgongo wa Somoe. Akapiga kelele za uchungu, lakini chotara huyo

hakujali akamtandika wa pili.

“Unamjua yule wewe? Kwa taarifa yako yule ni kachero wa serikali, mpelelezi hatari ... amekuingiza matatizoni.... Tupe namba yake kabla hasira zangu hazijakuishia...” Torres akaongea kwa hasira. Somoe alibaki kulia kwa vikwifukwifu, huku mgongo wake ukionekana kubadilika rangi na kuvimba kwa vipigo hivyo vilivyoanza tangu usiku uliotangulia. Torres akaanza kumtandika mijeledi mfululizo mpaka vijana wake wakaingiwa na huruma kwa mwanadada huyo. Somoe alipiga kelele za nguvu na kunyamaza ghafla kisha akalala chini kimya. Chotara huyo hakujali, akaendelea kumtandika mijeledi na kisha akampiga teke la nguvu ubavuni.

“Mtoeni mkamtupe baharini aliwe na samaki, malaya mkubwa huyu!” akatupa na ule mjeledi kisha akaelekea mlango mwingine, kabla hajaingia kwenye mlango huo akasimama na kugeuka.

“Kibisa! Mkimtupa huyu, mrudi hapa bila kuchelewa! Hali imeshakuwa mbaya, hatujui mnyama huyu ataibukia wapi,” Torres akaingia ndani ya chumba kile huku akiubamiza mlango nyuma yake na kusababisha kishindo kikubwa.

* * *

DAR ES SALAAM

Saa 11:05 jioni...

ABIRIA WA MWISHO kushuka katika ndege ile ya *ATC*, *Focker Friendship*, alikuwa Kamanda Amata. Ndani ya suruali ya *cardet* na fulana ya njano. Kiatu cheusi na miwani ya macho, vilimfanya awe nadhifu, atamanike na yeyote ambaye angekutana naye. Hatua kadhaa zikamfikisha katika jengo la *VIP*. Siku hii aliamua kutumia jengo hili akiwa anajua wazi huenda akawa na mtu anayemsubiri upande ule wa kawaida. Kutoka katika jengo hilo akapita geti dogo na kutembea mwendo wa dakika kama mbili hivi na kufikia maegesho ya magari. Gari lake aliloliacha siku tano nyuma alilikuta palepale. Hii ilimaanisha si Chiba, Gina wala Scoba aliyekuwa amerudi nchini kutoka kwenye kazi zao nje ya nchi. Kwa maana yeyote angeweza kulitumia kama angewasili uwanjani hapo. Haya ni magari ya ofisi, huwa wanayaegesha katika sehemu nyeti na muhimu kama hapo uwanja wa ndege, bandari ya Zanzibar jijini Dar es salaam, baadhi ya mahoteli katika jiji hilo na

sehemu kama Kariakoo sokoni na zingine ni siri kukwambia.

Mara tu alipolifikia, akatoa kidubwasha chake kidogo mfano wa simu ya mkononi, akakiwasha na kulizunguka lile gari mpaka pale alipotoka. Kifaa hiki kinachojulikana kama *Handheld Explosive Detector* kina uwezo wa kutambua aina mbali mbali za milipuko. Mara kinapotambua hutoa mlio fulani wa ishara. Mara hii hakikufanya hivyo, si kwamba betri iliisha, la hasha, bali gari hilo lilikuwa salama. Akaingia na kuketi nyuma ya usukani, akapachika funguo na kutia moto injini, ikakubali, akaiacha iungurume kwa dakika kadhaa kisha akatia gia ya kwanza na kutoka taratibu.

* * *

“Yes Madam!” Amata akaongea kwenye simu iliyofungwa ndani ya gari hilo.

“Umerudi?”

“Ndiyo mama!”

“Tuonane haraka iwezekanzavyo, fika nyumbani Masaki,” Madam akamwambia.

“Copy!”

Katika Barabara ya Nyerere kuelekea mjini kati, Kamanda Amata akaongeza mwendo na kuipita njia panda TAZARA huku akisikiliza Redio Tanzania, Idhaa ya Taifa. Baada ya mwendo wa kama dakika ishirini hivi, akaiacha Barabara ya Nyerere na kuchukua ile ya Msimbazi, akaendesha mpaka katikati ya barabara hiyo baada ya kituo cha polisi cha Msimbazi, akaingia kushoto na kupita Mtaa wa Swahili, akaambaa nao mpaka Faya, akavuka na kukamata Barabara ya United Nations mpaka Daraja la Salender.

Ilimchukua kama dakika hamsini hivi kuwasili Masaki, kandoni kabisa mwa Bahari ya Hindi. Mbele ya lango la nyumba hiyo akapiga honi kwa mtindo wa pekee na kusubiri. Kutoka ndani Madam S akajua kuwa kijana wake amewasili. Akafungua geti kwa kutumia swichi maalum ambayo imefungwa sehemu ya uficho ndani ya nyumba hii.

Amata akaingiza gari ndani huku lile lango likijifunga nyuma yake. Akatafuta sehemu nzuri na kuegesha gari hilo. Akateremka na kukutana na bosi wake, kila mmoja akamtabasamia mwenzake, wakakumbatiana kwa sekunde kadhaa.

“Karibu!” Madam akamkaribisha Amata naye akaitikia na kuingia ndani.

“Vipi mbona inaonekana pombe zimenyweka!” Amata akaanza maswali ya ajabu kwa bosi wake.

“Acha umbea! Kila kitu unataka ujue? Haya, alikuja baba yako...”

“Waoh!”

“Hebu keti kwanza, tunatakiwa kuonana na Rais, Ikulu,” madam akamwambia.

“Saa ngapi? Mbona wanitisha?” Amata akamwambia.

“Muda wowote, kasema ukifika tu twende...” akamwambia huku akimmininia kinywaji kwenye bilauri.

“Lakini kabla hatujaenda lazima taarifa yote iwe katika maandishi; haya nipe yaliyojiri Mtwara kabla sijakupa yangu,” akaongeza huku akikaa kwenye kochi kubwa la vono. Amata akainua bilauri yake na kupiga mafunda kadhaa kisha akaiweka mezani.

“Nashangaa sana kwa nini umenirudisha nyumbani mapema. Nilipanga nirudi leo, ila umeniwahisha masaa mawili ... kwanza nimepata *data* nyingine kutoka kwa yule PC wa Lindi ambaye siku hiyo alikuwa lindo. Naweza kukwambia tu kuwa hii ni hujuma, nimeinusa zaidi, tena kutoka kwa mtu mweupe. Ndani ya maabara ile kulikuwa na watu kama kumi na tano hivi, wamekufa kumi, watano hawajulikani walipo na hawa watano wote ni Wazungu, wanafunzi kutoka vyuo vya Marekani ambao walikuja kujifunza zaidi juu ya tafiti hii.”

“Ndiyo ambao kwenye taarifa ya kwanza walionekana kutoka na kurudi baadae?” Madam akachomekea swali.

“Yes! Lakini kwangu mimi siwaweki kwenye kundi la wanafunzi bali ni majasusi waliokuwa wanajua kazi yao, na wameikamilisha...” Amata akamwambia Madam na kunyanyua bilauri yake, akapiga funda moja na kuishusha.

“Amata, hiyo ni habari mpya kabisa, inaiongezea nyama ile ya kwanza ili inoge zaidi... Enhe nambie...” Madam akajiweka vyema kitini kama mjukuu anayesubiri kusikia kisa cha sungura na fisi kutoka kwa babu yake.

“Uhakika ambao ninao ni kuwa waliotoka dakika kama kumi hivi kabla ya mlipuko ule ni hao Wazungu, tena walikuwa wanne tu, kwa maana hiyo tungepaswa kuokota maiti kumi na moja...” akasema. Lakini kabla hajamaliza kusema hayo, Madam S akamzuia na kuonesha

sura ya mshangao.

“Mama yangu!” akapiga kite.

“Nini Madam?”

“Kamanda, hapa kuna ishuru nzito. Maiti zilizotolewa baada ya moto ule kuzimwa ni tisa tu, kadiri ya taarifa iliyofika Ikulu jana na hakuna kabisa mabaki hata ya mfupa wa mwanadamu mwingine, ina maana watu wawili wamemiss...”

“Hiyo mpya! Na siipingi kwa sababu nilikuwa naumiza kichwa juu ya hilo,” Amata akadakiza kusema. Kisha Madam S akaendelea kuandika kwenye kompyuta yake ndogo yote ambayo Amata alimtaarifu mpaka hapo.

“Nyongeza!” akamwambia.

“Nilikwenda Mtwara kuona yule mwanamke aliyeopolewa baharini, hakika nilimwona kwenye hafla ya uzinduzi. Lakini sasa sikujua hasa yuko upande wa nani. Nilikuwa nasubiri apate fahamu tu nianze kubanana naye angetupa mwanga sana wa tukio hili. Nikiwa nasubiri hilo nikasikia kuwa kaja mtu anayejifanya kaka yake kamchukua kuja Agha Khan...”

“Oooh *come on!*” Madam akahisi ganzi kwa swala hilo, “...ina maana kuna mtu kamteka, kwa sababu mara tu uliponambia nilikwenda mwenyewe mpaka pale wakakiri kuwa hawajapokea mgonjwa wa namna hiyo ... Amata! Sasa atakuwa amepolekwa wapi?”

“Umeona ee? Sasa hapa kuna mtu anaitwa Torres Alexis Kazumari. Nilikuwa najaribu kumfuatilia kujua ana *connection* gani katika sakata hili! Maana aliniwekea watu waniue, na bahati mbaya na mimi nimewavunja wawili lakini kati yao hakuna aliyenipa siri ila jina hili nimelipata katika kumbukumbu zao. Kuna mwanamke ambaye nilikuwa naye jana, sikujua kama ni mtu wao au wamenicheza shere. Walitaka kunizubaisha naye, wanidake, lakini nikawawahi mimi. Baadae wakatimia simu ya mwanamke huyu kunipa vitisho... Walitumia mbinu za kitoto. Nikiwa tayari nimezama katika ufuatiliaji huu ndipo ukanipigia, nikarudi. Kwa ujumla nahisi hawa akina Torres ndiyo wamemteka yule mgonjwa kwa sababu huyu mwanamke ni muuguzi pale Ligula... hii ni tafutishi ya awali, sasa sijaupata ukweli wa niliyokwambia...”

“Pole! Nimekuelewa, hapa nimeandika tu kwa kifupi kwa sababu Mheshimiwa anahitaji kujua... bado tuna kazi ngumu maana *data* tumepata ila kazi ni kuzifanyia *analysis*. Sasa ipo hivi, twende kwa Rais

tukaonane naye kisha mimi na wewe tuna mengi ya kuchanganya ili habari ikae sawa.”

Baada ya kuweka tayari kila kitu, wakatoka pamoja jioni hiyo na kuelekea katika jengo jeupe huko Magogoni.

* * *

Saa mbili usiku, walikuwa tayari ndani ya chumba cha mikutano ya siri *‘Kilimanjaro Square’*. Mheshimiwa Rais alikwishaketi tayari mara tu alipoambiwa kuwa watu hao wamewasiri hapo. Baada ya makaribisho na kila kitu, taarifa fupi kutoka kwa Amata ikawasilishwa na Madam S. akajitahidi kuichambua kwa kuwa kuna mambo ambayo hakutaka yafahamike kwanza kwa sababu za kiusalama.

“Pole kijana kwa misukosuko, lakini najua wewe ni shupavu na hivyo ni vitu vidogo kwako,” Mheshimiwa akamwambia Amata, naye akatabasamu tu, hakujiibu.

“Nimesikia taarifa yako lakini kwa sasa hatuna budi kusitisha uchunguzi huu na kuwaachia wataalam zaidi kutoka Marekani, ndiyo maana umerudishwa hapa. Hivyo endelea na kazi ambayo bosi wako atakupangia, ila kama kuna lingine basi utapewa taarifa,” Mkuu wa nchi akamwambia Amata.

“Sawa mheshimiwa!”

Hakikuwa kikao kirefu, ila mazungumzo ya kiusalama yalizungumzwa kwa kina, kisha wakaagana na kuondoka. Wakiwa ndani ya gari Amata alikuwa kimya kabisa.

“Vipi mbona huongei?” Madam akamuuliza.

“Ah! Nafikiria juu ya swala hili, unajua nilishakuwa nakaribia mahala fulani hivi, mmeninyang’anya tonge mdomoni...”

“Usijali, nakuacha nyumbani kwako, kisha kesho asubuhi tukutane shamba tuyaweke vyema, mimi ndiyo bosi wako,” Madam S akamwambia Amata.

Majira ya saa nne hivi za usiku, Madam S alimfikisha Amata Kinondoni na kumwacha hapo kwa miadi ya kukutana asubuhi kwa mambo kadhaa ya kikazi. Kamanda akamshukuru na kumuaga, kisha akaliendea geti la nyumba hiyo, akafungua na kuingia katika uwa mkubwa wenye maua mengi. Akaangaza macho huku na kule, kupitia vivuli vya maua hayo, akaona kila kitu kipo sawa. Akavuta hatua mpaka mlango wa nyumba. Kabla hajatumbukiza ufunguo tunduni, akasita na kusimama. Kwa sekunde kadhaa akatulia kusikiliza kwa makini kama

kuna sauti au chochote ambacho angekihisi si salama kwake. Hakuna. Akafungua mlango taratibu na kutembea kwa hatua za kimya mpaka sebuleni, hakushika kitu chochote zaidi ya kitasa. Akasimama na kuwasha taa, akatazama kila kitu kwa jicho la kikachero.

Akili yake ikahisi kuwa hapo hapakuwa na usalama. Palionekana pamepekuliwa kiufundi sana. Akajua wazi kuwa mpekuzi ni mtu ambaye anaijua kazi yake vyema. Akaendelea kutembeza macho sehemu zote zilizoweza kuonekana kisha akaanza kupita chumba kimoja baada ya kingine. Kila alichopita kilikuwa vile vile, yaaani kimepekuliwa kiufundi sana. Alipokikaribia chumba chake cha kulala mwili ukamsisimka na nywele zikamsimama. Hii ikampa ishara kuwa humo ndani hakuko sawa. Akachomoa bastola yake ndogo na kuiweka tayari kwa lolote kisha akafungua mlango na kuusukuma taratibu, haukufungwa, ukafunguka bila matata. Ilimchukua sekunde kama thelathini hivi kwa Amata kuvuta hatua kuingia ndani ya chumba hicho.

Ghafla akageuka nyuma ya mlango huku domo la bastola yake likitazama mahali hapo. Hakuna mtu. Akageuka upande wa pili, mambo ni yale yale. Geuko la tatu, akatazama kitandani, shuka lilionesha wazi kufunika kitu.

Mtu? Akajiuliza. Kwa mkono mmoja akakamata bastola na ule mwingine akauweka tayari kufunua lile shuka, akasogelea kitanda. Kama ni mtu aliyekuwa amelala kitandani hapo basi alionekana wazi kuwa hakuwa na uhai kwani jicho la Amata lilitua katika maeneo ya tumbo hakuona kuvutwa pumzi. Akavuta shuka kwa ghafla na kuikamata bastola kwa mikono miwili.

“Shiiiiitt!” akatoa ukelele dhaifu na kupiga hatua moja nyuma. Hakuamini akionacho, mwili wa binadamu, mweusi kama mkaa. Alipoutazama kwa haraka haraka, aligundua kuwa mwili huo ni wa mwanaume, umeungua kwa moto. Akautazama kwa makini zaidi, lakini kwake ilikuwa ni ngumu kutambua ni wa nani. Akashusha pumzi na kuirudisha bastola yake kiunoni. Akainyakuwa simu yake na kumpigia Madam S na kumtaka arudi mara moja.

Sasa huu mwili ni wa nani tena? Akajiuliza. Utata!

* * *

Madam S aliwasili na kumkuta Amata kaketi kwenye kiti kimoja ndani ya chumba kile. Alipotupa macho kitandani akashtuka kwa kuuona ule mwili.

“Nini hiki?” akauliza.

“Ni hicho unachokiona!” Amata akajibu.

Akavuta hatua na kutazama vizuri, akatikisa kichwa kisha akamgeukia Amata aliyekuwa kimya kitini.

“Nani anayefanya haya yote? Inaonekana anakufahamu vyema sana!”

“Sio ananifahamu, anatufahamu,” Amata akajibu.

“Haya, anatufahamu,” akatulia kimya kwa nukta kadhaa, akautazama ule mwili, kisha akamtazama Amata kwa mara nyingine. Akasogea jirani na kijana huyo aliyekuwa amejinamia kimya.

“Amata!” Madam akaita kwa upole.

“Yes Mom!” Amata akaitika na kuinua uso.

“Who did this?”

“I don’t know!” akajibu na kuchomoa bastola yake, akaiweka mezani.

“Madam! Nakwambia wazi hili sakata la kupotea kwa chanjo si la kuliacha, sijui kumuachia nani, hii ngoma lazima tuicheze, wale jamaa ni hatari sana na nahisi ndiyo wanaofanya michezo hii...”

“Umejuaje?” Madam akamkatiza.

Amata hakujibu akabaki kimya. Madam S akainua simu yake na kupiga kwa Inspekta Simbeye, kumhitaji mahala hapo haraka. Kisha yeye akaendelea na mazungumzo machache na kijana wake. Haikupita hata dakika kumi na tano, Inspekta Simbeye akawasili na vijana wake kama sita hivi waliosheheni silaha za moto. Mara tu baada ya kupokelewa na Madam S, akafikishwa katika chumba hicho na kushuhudia kile wanachokishuhudia. Hakuongea mengi, akawaita vijana wake, wakachukua picha za mwili huo na walipokamilisha, wakautia katika machela tayari kuondoka nao. Wakati wanauinua kuutoa pale kitandani, kutoka katika kiganja cha mkono wa ile maiti, kikaanguka kitu kama rikoda ndogo sakafuni.

“Peleka! Peleka!” Simbeye akawaamuru. Wale vijana wakaendelea na safari yao. Madam S akawa tayari amekwishakiokota kile kifaa na kukitazama. Akabonyeza moja ya kitufe na kuruhusu ujumbe ulio ndani usikike.

“...Huu ni ujumbe wangu kwako na kwa wengine wote wanaojaribu kutafuta sanduku hili... kwanza usitegemee kulipata, pili kama unapenda maisha yako baki na kaofisi kako, mimi si mtu wa kutafutwa kijinga binyo. Najua ulikuwa Lindi siku ya uzinduzi, umekwenda Mtwara kunitafuta, umenikosa. Hakika huwezi kunikamata na kabla ya kunipata mimi nitakupata wewe. Amata Ric, kachero wa siri wa serikali, nakufahamu kama ninavyokifahamu kidole changu.

Najua kuma CIA wapo na wanataka kazi hii waifanye wao! Kwa taarifa yao hakuna mtandao wa kunigusa, iwe CIA, BOSS, KGB, MOSSAD, NCA na yeyote yule...

Hii ni biashara, na biashara lazima ibeshimiwe. Ili kukuhakikishia kuwa najua kila mnachokifanya sikiliza nini kitatokea kesho hapo Dar es salaam. Na mwisho nakupa tabadhari, bata sasa unaposikia ujumbe huu ninakutazama, na nitakutia mkononi pindi tu utakapojaribu kufuatilia nyendo hii...

Ule ujumbe ukakatika hapo, Madam S akashusha pumzi na kuitazama ile rikoda, akaizima na kuichunguza kwa makini.

“Anajiamini nini?” akauliza.

“Jiulize! Mi napenda sana watu wenye dharau kama hawa niwafunze adabu. Kwa nini mnakubali kuachana na hili? Madam, umezeeka, sivyo? Watu kama hawa si wa kuwaacha wakitushikashika mpaka makalio namna hii...” Kamanda akalalama.

Madam S akavuta hatua tatu na kusimama kwenye kona moja ya chumba, akafikiri jambo kisha akatoka na kuelekea sebuleni. Kamanda Amata akamfuata huku nyuma yao kukiwa na Inspekta Simbeye.

“Vipi?” Simbeye akauliza.

“Nipelekee ule mwili Muhimbili, waambie wasiuguse hata kwa vipi nakuja mwenyewe kesho kuushughulikia,” Madam S akamaliza na Inspekta Simbeye akatoka baada ya kuagana naye.

“Hii dharau Madam!” Amata akamwambia mkuu wake wa kazi.

“Usijali, we pumzika tuonane kesho,” akamwambia Amata aliyeonekana kuchanganyikiwa kwa namna moja au nyingine.

“Siwezi kulala hapa, lakini nakuhakikishia aliyeweka huu mwili nitamjua kesho na nitamwonesha kuwa mimi ni nani! Shubaamit!” Naenda kulala kwa Gina.

“Gina hayupo!”

“Hata kama hayupo, najua funguo anaweka wapi”. Baada ya hapo wakatoka wakifuatana. Madam S akamchukua Kamanda Amata kwenye gari lake huku Simbeye akiondoka na vijana wake. Njia nzima, hakuna aliyeongea, zaidi ya muziki laini na Amata aliyekuwa akivuta kamasi mara kwa mara. Madam S aliijua vyema hali hiyo ya kijana wake, kuwa akishikwa na hasira ya kudharauliwa basi hupata makamasi ya mtindo huu. Baada ya mwendo wa takribani dakika ishirini kama si ishirini na tano, akaegesha gari mbele ya lango la nyumba kubwa aishiyo Gina, TSA 5.

“Natumaini umefika!” Madam akamwambia Amata.

“Kesho nayo sikul! Alamsiki,” Amata akamuaga Madam S, naye akaingia ndani ya jumba hilo. Kwa kuwa alijua funguo hukaa wapi, haikumsumbua kuzipata na kuingia ndani.

SURA YA 12

CABO DELGADO

SIKU HII ILIKUWA ya pekee sana katika msitu huu mnene ndani ya mji wa Cabo Delgado huko Msumbiji. Wageni kama ishirini hivi walikuwa wamewasili katika jumba hilo la kifahari ambalo chini ya ardhi kulijengwa maabara kubwa sana na ya kisasa. Jengo hilo lililojengwa katikati ya msitu na mwekezaji mmoja wa Kizungu, lilikuwa la kifahari sana na lilibeba siri nyingi ndani yake.

Hakuna aliyefika katika jumba hili kwa gari. Kila mmoja alishushwa kwa helikopta na kisha ikaondoka na kumwacha hapo. Mkuu wa itifaki aliyeandaliwa, aliwapokea wageni hao na kuwafikisha wanapotakiwa kufika.

Ukumbi mkubwa wa mikutano, wa kisasa, ulikuwa umewekwa viti ishirini na moja tu. Juu ya meza ndefu ambayo ilizungukwa na viti hivyo kulikuwa na kila aina ya kinywaji kikali na kitamu bila kukosa chupa za maji yaliyozalishwa hapo hapo katika jumba hilo. Dakika kama tano baadae ule ukumbi ukawa umebeba watu kama thelathini na mmoja hivi. Wageni ishirini, mwenyeji wao Lord Dimens na walinzi kumi waliovalia suti nadhifu kabisa.

“Jisikieni mpo nyumbani!” Mwenyeji wao akawakaribisha na kila mmoja akajiweka sawa.

“Nimekuiteni wateja wangu. Mara nyingi tumekuwa tukifanya biashara huku na kule na si ajabu hatukuwahi kukutana na kuketi namna hii,” akawaambia na kuwatazama kwa zamu, kisha akaendelea. “Basi, leo ndiyo siku maalumu kwetu, yaani kwa mimi na ninyi...” Akaongea taratibu huku mikono yake ikiwa imeshikana pamoja chini

ya kidevu chake. Wageni wale walikuwa kimya wakisikiliza, kila mmoja akiwa na shauku ya kujua nini wameitiwa na tajiri huyo.

“Kwanza kabisa leo nataka niwaoneshe ufanisi wa maabara yangu, ambayo mpaka sasa inashika nambari moja Afrika na si ajabu hata duniani. Inafanya nini, watenda kazi wake na tuna mpango gani na dunia hii. Karibuni!” Alipomaliza kusema hayo, mara, vile viti vikageukia upande mmoja vyote kisha upande ule vilikotazama ukuta ukafunguka kana kwamba kuna mlango. Hapo kikaonekana kioo kikubwa ambacho kilikuwa na nembo kubwa ya *Dimens – LabTech* ikizungukazunguka. Baadae kukafuata dokumentari iliyoonesha ubora na viwango vya maabara hiyo. Ikaonesha ni bidhaa gani za dawa na kemikali ambazo viwanda na mahospitali mbalimbali duniani wanatumia vinavyozalishwa na maabara hiyo. Ikaonesha jinsi ubora wa tafiti zao za madawa, mafanikio na usambazaji duniani kote. Ilichukua kama dakika ishirini hivi na kumalizika kwa ujumbe uliojiandika juu yake.

‘Tupo kwa ajili ya kuokoa maisha’

Ule ukuta ukajifunga na vile viti vikarudi kama mwanzo. Kila mmoja akajiweka sawa tayari kusikiliza jambo jingine. Lord Dimens akatabasamu kwa jozi la sekunde, kisha akavunja ukimya kwa kuzungumza.

“...Leo niliamua kuwaonesha hili, hakuna mwanadamu aliyeko duniani anayejua maabara hii, ninyi ni wa kwanza na mna bahati sana. Lakini hili si nililowaitia, na najua nyote hamjui ni nini nimewaitia, nisikilizeni kwa makini...” akainua bilauri ya maji na kunywa mafunda kadhaa.

“Dunia, na zaidi Afrika, sasa hivi inateseka kwa ugonjwa wa *AIDIOSIS*, hakuna kiumbe awaye yote asiyejua hili. Wataalamu mbalimbali wameshindwa kupata dawa au kitulizo tu cha ugonjwa huu. Maabara kubwa za ulimwengu zimeshindwa kugundua chanzo na suluhisho la tatizo hili. Leo hii nataka niiambie dunia kuwa tatizo hili limekwisha na litakuwa historia...” Baada ya kusema hayo, wageni wale wakampigia makofi ya kutoa kongole kedekede. “... Maabara yangu iko mbioni kugundua chanjo ya *AIDIOSIS*... ambayo tukimdunga mtu asiye na maambukizi, hatoambukizwa kamwe... Huu ni ushindi kwetu! Tukiwa mbioni kupata dawa itakayowaponya kabisa hata wale ambao wameathirika kwa viwango tofauti. *Viva Dimens Lab Tech*...” akaweka ukimya kidogo na kuwatazama wageni wake walioonesha sura

za mshangao au tuite za kutoamini wasikiacho.

“*What!* Hivi we una wazimu au mzima?” mmoja wa wageni akaongea kwa jazba huku akiwa kasimama.

“Sawa! Haujakosea, wazimu wangu umenifanya nigundue hili. Na nimewaita ninyi kwa kuwa ni wadau wakubwa wa mambo ya madawa duniani, mnaojali afya na kuthamini uhai. Sikutaka wala kupenda kuwaambia wengine *formula* hii, bali nilitaka ninyi muijue kwanza, na kama shirika lolote kati ya yale mnayoyamiliki litahitaji kuinunua *formula* hii basi sasa ni muda wa kuweka dau, kabla ya tarehe husika ya uzinduzi,” akatabasamu. “Ila kabla hatujaanza kuifikiria biashara hii basi ngoja niwaoneshe jinsi inavyofanya kazi ndani ya mwili wa mwanadamu,” akawaambia na kisha moja ya picha kubwa ukutani ikasogea kando na kitu kama lifti kikafungua milango. Ndani ya kijichumba hicho akatoka mtu mmoja mwenye sanduku kubwa na nyuma yake akifuatiwa na kijana mmoja wa kizungu, mkakamavu aliyetuna misuli.

“Huyu anaitwa Dkt. Hammon Sekela, mtafiti mkuu wa chanjo hii ambaye ameshirikiana na watu wangu kwa kutumia teknolojia tanzu ya Dimens Lab Tech na kufanikiwa kama timu. Nimemwajiri hapa miaka mingi na sasa kafanikiwa kufikia lengo tulilolitaka. Yeye atawaeleza kila kitu, kwa jinsi gani chanjo hii inafanya kazi,” akawaambia kwa kujiamini wakati huo Dkt. Edward, aliyepachikwa jina jipya alikuwa akiumia moyo kwa uongo huo. Alitamani kumzaba makofi lakini haikuwezekana. Ni kwa vile tu hawakuwa wakijua kuwa daktari huyo ametekwa na chanjo hiyo imeibwa kabla ulimwengu haujajua chochote.

Dkt. Edward Minzi akwasalimu wageni wale, walioonakena wazi kushiba pesa, kisha akatulia na kulifungua sanduku lile ambalo ndani yake kulikuwa na chupa ndogondogo tisa kwa idadi yake, huku nyingine chache zikiwa zimehifadhiwa. Nyuma yake ikafunguka luninga nyingine kubwa naye akaanza kuielezea ile *formula* kiutaalamu sana. Kati ya wageni wote hao hakuna aliyekuwa akijua kuwa daktari huyo amefungiwa bomu hatari mwilini mwake. Alishaambiwa kuwa akipindisha maelezo tu basi kinobu kitafyatuliwa na yeye angeweza kupasuka vipande vipande. Hivyo, alikuwa akielezea na kufanya kazi zote katika hali hiyo, hakuwa na jinsi, ilibidi afuate kile anachoamriwa. Edy, kama alivyopenda kujiita mwenyewe, akaeleza kwa ufasaha sana juu ya chanjo hiyo na wageni wale wakamsikiliza kwa makini huku

wakifuatilia kile ambacho walikuwa wakikiona kwenye luninga.

Ilichukua dakika arobaini na tano kufuatilia maelezo hayo ambayo yalipangwa kitaalamu kabisa. Isingewezekana kwa mtu wa kawaida kusikiliza na kuelewa nini ambacho daktari huyu alikuwa akikieleza. Alipomaliza, akapigiwa makofi ya nguvu. Yule kijana aliyeingia naye, akamsogelea, sanduku lile likafungwa, na wote wakaondoka na kuwaacha wale wageni palepale. Mazungumzo ya wao kwa wao yaliendelea kwa dakika nyingi tu na mwenyeji wao aliwaacha waendeleo kufanya hivyo. Dakika kumi baadae akawanyamazisha na kuwatazama.

“Hayo ni yote kwa leo! Kikao chetu kitaishia hapa, mwenye kuhitaji mzigo huu atanitafuta baada ya uzinduzi. Uzinduzi utafanyika miezi mitatu mbele mtataarifiwa nyote naye atakayefika dau atapata mzigo, asanteni!” Kabla hawajaongea lolote, kiti cha mwenyeji wao, kikaanza kudidimia chini na sekunde ishirini tu sakafu ikajifunga, wakabaki peke yao.

“This way please!” sauti ikawaambia na wote wakainuka na kuingia kwenye mlango uliofunguka katika ukuta wa chumba hicho kipana. Baada ya kupita mlango huo, wakaingia kwenye lifti iliyowapeleka wote juu kabisa ya jengo na huko wakaondoka kwa helikopta kurudi makwao.

* * *

“Dkt. Edward! Tutafanya biashara nzuri sana miezi mitatu ijayo, na wewe utakuwa ni mtu muhimu sana katika hii...” Lord Dimens, mmiliki wa maabara ile akamwambia Edward. Mzee huyu, jeuri, aliyetiacha nchi yake kwa miongo mingi na kuingia Afrika, alikuwa tajiri ambaye aliamini kuwa anaweza kufanya lolote katika sayari hii. Aliingia Msumbiji kama mwekezaji hasa upande wa madawa. Serikali ya Msumbiji ikamuuzia msitu huu mkubwa kwa shughuli zake za kitafiti, naye akajenga maabara hii ambayo ndani yake kulitengenezwa madawa mbalimbali ya binadamu. Hakuna aliyejua nyuma ya pazia kuna nini. Hakuwa mwingine ila Lord Dimens, walimwita ‘*Lord*’ kumtukuza kwa utajiri wake.

Dkt. Edward akabaki kimya huku uso wake kauinamishia chini, hasira na uchungu vikautafuna mtimawe, akainua macho na kumtazama huyo aliyeongea.

“Kwa nini? Unafikiri kitu ulichokifanya ni sahihi? Watu wangapi

umeua kwa sababu hii!” Edy akalalama.

“Hilo halina nafasi kwa sasa na kule kwenu Waswahili mnasema ‘Lawama hazijengi’ sivyo? Sasa ngoja nikwambie jambo ambalo wewe hulijui na nikikwambia utaelewa kwa nini nilifanya tukio lile,” Dimens akamwambia Dkt. Edward. Katika chumba hiki walikuwa wanne tu, yeye, yaani Dimens na Dkt. Edward pamoja na walinzi wawili tu.

“Nikwambie?”

“Nambiel!” Edy akajibu kwa upole, huku uso wake ukiwa umesawajika kwa mawazo.

“Nisikilize kwa makini. Kwanza kabisa ujue kuwa *AIDIOSIS* si ugonjwa kama wengi mjuavyo, ile ni *program* au ningeita mradi, kwa lugha nyepesi...” Dkt. Edward akashangaa kidogo. Dimens akabaki kimya kumpa tafakuri hiyo ambayo alijua wazi kuwa inampasua kichwa.

“Sasa basi, miaka mingi nyuma kati ya 1935 na 1940 kuna jopo la matajiri ambao wao wanaamini kuwa kwa pesa zao wanaiongoza dunia. Matajiri hawa ni kama ukoo au familia, waliorithi na kurithi ukwasi wa karne na karne. Miaka hiyo walikaa kikao kizito huko Melbourne ya zamani. Katika kikao hicho waliazimia mengi, ila hili ni moja kubwa yaani kuanzisha *program* itakayoteketeza maisha ya Waafrika au kama wao walivyoita ‘kizazi duni’ kwa njia ya mkusanyiko wa magonjwa mfano Kifua Kikuu, vidonda, majipu, utapiamlo na mengine mengi. Lakini shabaha yao kuwa haikuwa tu kuteketeza bali pia kufanya biashara nyuma yake... Walijuwa wazi kuwa, dunia ikishaona kasi ya vifo hivyo, basi ingehitaji dawa. Na wao wangeitoa kwa awamu na kupata pesa ambayo hata wajukuu wao wangeirithi tena na tena.”

Daktari Edward alikuwa kimya akimsikiliza bwana huyu kwa tuo, huku maneno au habari hiyo ikimwingia vyema akilini. Dimens akaendelea.

“Watu hawa kumbuka walikuwa ni matajiri sana wakati huo ee... Basi, baada ya kuafikiana kutengeneza *program* hiyo, wakatafuta wataalamu wanabaiolojia na kuwaeleza. Walipokubali kuingia mkataba na matajiri hawa wakaanza kazi ya kuitengeneza hiyo. Wao kama wanasayansi waliamini kuwa Mwafrika ana kinga zenye nguvu sana dhidi ya maradhi, na hakuna maradhi yasiyo na dawa huku Afrika. Walichokifanya wakatengeneza *formula* katika mtindo wa *virus*...Wewe ni daktari, unajua, *virus* hasikii dawa kwa kuwa hana umbo maalumu. *Virus* huyu akiingia katika mwili wa mwanadamu anaenda kuua au kudhoofisha

kinga za mtu huyo kwa kujigeuza kuwa kama kinga yenyewe, anaua na kushambulia chembe chembe hai zote hatua kwa hatua, baada ya hapo hata atumie dawa gani hakuna itakayomponya,” akatulia kidogo. Dkt. Edward akameza mate.

“Aaaah usimeze mate kupoza kiu, utakaukiwa zaidi hah! hah! hah!” akacheka kipesapesa na kubonya kitufe fulani. Pale alipoketi Edward, kwenye meza yake, pakafunguka, chupa ya maji na bilauri ya plastiki ngumu vikajitokeza na kutulia kana kwamba kuna mtu aliyewiweka. Hakuwa na la kusema aliitazama chupa ile.

“Eh! *Have a fresh water please!* Hayo ni maji spesho yenye virutubisho na vitamins za kutosha. Duniani kote yanapatikana hapa tu,” akamkaribisha huku akimwonesha kwa mkono. Edward akanywa maji na kutulia kitini tayari kusikiliza maelezo hayo.

“*Good!* Sasa kwa kifupi naweza kukwambia kuwa *AIDIOSIS* ni silaha mbaya ya kibaiolojia ambayo haijawahi tokea duniani. Na watu hawa waliwekeana kiapo kabisa kuwa yeyote atakayejaribu kutengeneza mbadala wake, halali yake ni kifo. Hati hiyo ipo, imehifadhiwa Washington, chini ya jengo moja muhimu sana la serikali. Baada ya kuifanyia majaribio mara kadhaa na haikufanya kazi, walikuja kufanikiwa miaka ya 70 na kuipandikiza kwa Mwafrika wakidai chanjo kumbe la. Walipohakikisha iko sawa na imeanza kazi, huwezi kuamini Edward, wale wataalamu wanasayansi waliuawa wote ili tu wasije kugeuka na kutengeneza mbadala kwa maana kwao ingekuwa rahisi tu! Lazima ujue kwamba, unaweza kutengeneza kitu kwa faida yako ya leo na ukajuta kwa athari yake baadae”.

Dkt. Edward Minzi alikuwa akisikiliza kwa makini kila ambacho Dimens alikuwa akiongea, hapo akavuta kumbukumbu ya mwalimu wake, Sir. Drostdyhof Fenegan.

‘...*Sikia nataka nikupe siri, na iva siri yako tu, huu si ugonjwa kama mnavyouona. Hili ni bomu au niite shambulio la kibaiolojia. Na bado kuna mabomu mengi yametegwa kwenye miili ya Waafrika, siku yatakapolipuka mtalia sana...*’

Sauti hii ilimrudia Edward, akatikisa kichwa na kutulia.

“Sikiliza kwa makini, mi nakupenda sana Edward na ukinisikiliza utajua nani mwema na nani mbaya...” kisha akaendelea na habari yake, “Tangu hapo, *formula* na maandishi yoyote yaliyohusiana na ugonjwa huu yakafichwa mahali ambapo hakuna binadamu wa kawaida anaweza kupafikia. Ni mtu mmoja tu mwenye *codes* na *fingerprints* zinazoweza

kufungua saraka hiyo. Na ikapitishwa sheria ya siri kuwa mtu yeyote atakayejaribu tena kutengeneza formula mbadala atauawa mara moja. Edward, wapo watu waliojaribu akiwamo Sir. Drostdyhof Fenegan...”

“Unataka kunambia Sir. Drostdyhof amekufa?” Edward akashtuka na kusimama.

“*Cool down man!*” Dimens akamwambia Edward, kisha akamjuza, “*You are right!* Sir. Drostdyhof Fenegan alikwishauawa kama miezi kumi na sita hivi iliyopita. Sasa wakajitokeza watu wanne kutoka Tanzania waliojizatiti na kujitoa mhanga kuwaokoa Waafrika wenzao, nao ni wewe na wale madaktari wa jeshi... ukasukwa mpango wa ninyi kuuawa na hiyo chanjo kuchukuliwa. Ndiyo chanzo cha ule moto mara tu baada ya ninyi na serikali yenu kukubali swala la Shirika la Afya la Dunia kuchukua sampuli ile...” Dimens akaongea kwa mapozi ya hali ya juu sana kiasi kwamba hata kama ni wewe ungembubali kwa kile asemacho.

“Ina maana ulikuwa unajua kuhusu Sir. Drostdyhof ?” Edward akauliza.

“*Yes!* Mimi nina serikali! Nina majasusi kila kona! Si rahisi mtu kunifanyia njama nisimng’amue. Na haya nakwambia wewe kwa sababu umekuwa mtu muhimu kwangu, utakayeniongezea utajiri maradufu kwa ujuzi wako,” akamwambia, kisha akanyamaza ghafla na kubadilika sura, akainama kidogo na kuongea kwa sauti ya chini.

“Na hapa tuna sheria niliyoiweka. Yeyote akayetoa siri ya kinachoendelea hapa, tunamyeyusha kwa *acid* na kumpoteza kabisa katika uso wa dunia. Yaani tunayeyusha mpaka roho yake, hamwoni shetani wala Mungu, hata Toharani hafiki... *this is the Lord Dimens’s order,*” akamaliza.

Dkt. Edward akatuliza akili, akafikiri mara mbili, “Shenzi sana hawa jamaa, wanatufanya hivi?” akapiga ukelele.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Sio hivi tu wanawafanya zaidi ya vile...”

“Anhaaaa! Na wewe ni nani hata ujue haya yote?” Edward akatupa swali.

“Enheeeee! Sasa ndiyo tunaingia upande wa pili wa hii simulizi yetu ya kuvutia. Naitwa Lord Dimens, mmiliki na Mkurugenzi wa *Dimens-LabTech*. Sisi hapa kwa miaka mingi sana tulikuwa tukifanya utafiti juu ya mbadala wa *AIDIOSIS* kwa siri, ndo mana nikajificha huku. Nilivyosikia tu juu ya kuwa ninyi mmegundua chanjo na wakati huo huo nikasikia mabwanyenye wanaihitaji nikasema ‘haiwezekani’. Mimi

nawapenda sana Waafrika na ndiyo maana nikaja kuwekeza huku. Taarifa hizo za shirika la afya na washirika wao wa Langley iliponifikia, nikasema ‘*the time is now and the place is there*’, ndipo nikaingiza watu wangu kuja pale kujifanya wanafunzi wa mambo ya maabara. Hakuna! Mimi nikafanya hujuma ya kuiiba hii chanjo ili isiingie mikononi mwa wale jamaa zaidi ya hapo nikamwambia kijana wangu akuchukue wewe baada ya wale wengine kushindwa kuwaokoa! Na hii yote nilifanya kwa sababu nawapenda Waafrika. Naomba tuishie hapa kwa leo...” Dimensi akamaliza na mara hiyo hiyo wakatenganishwa na kitu kama pazia katikati yao. Dkt. Edward akabaki na mawazo mengi sana juu ya swala hili, hakujua kipi ni kipi katika hilo, faukani, akili yake ilikwishatekwa na *propaganda* za Dimens na roho yake kubaki katikati. Amuamini Dimens kuwa ameiiba ile chanjo kwa ajili ya kuwasaida Waafrika? Eti ikienda Geneva haitapatikana tena. Au awaamini Shirika la afya kuwa wanataka waiingize maabara kuifanyia uchunguzi kabla ya kuitumia kwa mwanadamu. Kazi ipo!

* * *

Dar es salaam

Siku tatu baadae...

Katika ofisi za siri, *Safe House*, au kama wenyewe waiitavyo ‘Shamba’, ni Madam S na Amata tu walikutana kwa mazungumzo.

“Kazi hii inazidi kuwa tamu hata kama sitakiwi kujihusisha,” Amata akamwambia Madam S wakiwa wawili tu katika meza ya mkutano huko Shamba.

“We liache hilo! Nina uhakika ulipofika wewe hakuna wa kufika, mtandao unaofanya swala hili ni mkubwa na wa hatari sana, sijui, *anyway*, ngoja tuone,” Madam S akaeleza.

“Sawa mi nikuache nikampokee Jasmin, najua atanihitaji tu siku ya leo,” Amata akasema huku tayari amekwishasimama.

“Acha umalaya wako, utakufa!” Madam S akamwambia huku akimtazama kwa jicho kali.

“Ningeshakufa muda mrefu mama, hata mzee wetu, Willy Gamba, alituambia ‘kazi na dawa’ he!” Amata akamwambia mkuu wake na kuanza kuvuta hatua kuuelekea mlango wa kutoka nje ya chumba kile.

“Sawa, sasa ukimpokea tu Jasmin nipigie tafadhali kuna mambo tuyaongee,”

“Sawa *mom!*”

“*Ok! Bye!*” wakaagana na Amata akaingia garini na kuliacha jumba hilo.

* * *

Juma moja baadae...

LANGLEY - MAREKANI

CIA Makao Makuu

“Narudia tena! Siwezi kuvumilia unyama huu! Kwa sasa huyu bwana Dimens ameshakuwa mwiba kwetu,” aliongea Mkurugenzi wa idara maalumu ya kushughulikia ‘matatizo’ ya nje. “Hapa kuna *deal* kubwa, na mshenzi huyu amekuwa akitusumbua sana miaka na miaka sasa... safari hii lazima roho yake iwe mali yangu,” akaongea kwa ukali akiizunguka ofisi yake huku na huko. Watu wengine ambao walikuwa ndani ya chumba hicho walibaki kimya kila mmoja akiwaza lake. Mwingine alikuwa tayari keshamzika Dimens katika udongo uliochanganyika na mawe, huku mwingine akiendelea kumfumuafumua na kumchanachana vipande ilimradi tu asiweze kufufuka na mwingine naye aliwaza baya zaidi ya hao wenzake. Basi ilimradi tu kila mmoja aliwaza cha kwake. Dakika moja baadae, yule mkurugenzi akasimama kimya na kuwatazama wajumbe wake.

“Mpo! Au naongea peke yangu?”

“Tupo mkuu!” wakaitika na kila mmoja akarudisha mawazo mezani pale.

“Cindy amekufa hapa katika hospitali yetu. Ina maana, amekufa na jambo kubwa moyoni ambalo tulikuwa tunalihitaji sana. Isitoshe vifaa vake vya siri vyote havijapatikana, walau tungeng’amua kitu. Lakini taarifa ya kichunguzi iliyoletwa hapa asubuhi hii na Jesse ni kwamba wanamhisi Dimens katika swala hili,” akasema, kisha akavuta kiti na kuketi.

“Cindy amekufa?” mmoja wa wajumbe ambaye tayari ngozi yake ilianza kufanya makwinyanzi ikiashiria kuwa uzee unagonga hodi alisimama na kuongea kwa hofu huku akitetemeka.

“Yeah! Ilikuwa siri ya ofisi lakini sasa yabidi tushirikishe vitengo vingine, ipo hivi...” akakohoa kusafisha koo kisha akaendelea “... Katika ajali ya ndege, wote wamekufa, twaweza kusema hivyo. Cindy alirudishwa hapa kwa msaada wa Jesse na timu yake, yaani *team number 2*. Amefia hapa Langley siku tatu nyuma. Amekuwa katika *coma* tangu alipookotwa huko Afrika. Kelvin mpaka sasa hajulikani alipo, kafa au hajafa, taarifa haijasema kinagaubaga, Mellania rubani wa ndege haijulikani kafa au mzima, yuko wapi, taarifa haina majibu...”

“Sasa wamejuaje kama ni Dimens?” mjumbe mwingine akadakia kwa swali.

“*Dimens ... is... a... devil!*” Yule mkurugenzi akajibu huku akiuma meno na kupiga ngumi mezani akimfananisha Dimens na shetani.

“Wameshamjua alipo?” mwingine akauliza.

Ukimya ukatawala, na sekunde chache baadae, yule mkurugenzi akatamka.

“Naomba tuishie hapa ili nipate muda wa kufikiria nini cha kufanya...”

“*No, Sir!*” mwingine akapinga, “...Hatuwezi kuacha kikao hiki kinaelea namna hii, Kelvin hajulikani alipo, Mellania hajulikani alipo, Cindy amekufa, nani sijui amefanya nini mi sijui! Ni nani huyo shetani anayeitwa Lord Dimens, tumeang...”

“*Nooo! Do not call him Lord!... He ... Is ... just a devil, bullshit!*” mkurugenzi akamkatisha kauli mdau wa kikao maana hakutaka kabisa Dimens kuitwa ‘Lord’ yeye aliamini kuwa ni shetani fulani tu.

“Nilikukata kauli, endelea...” akamruhusu.

“Nasema hivi, sisi ndiyo idara kuu kabisa ya juu katika upelelezi na ujasusi popote duniani, nani siyepua CIA? Hii ni aibu, kiumbe kama Dimens anatusumbua vipi mpaka tunamkosa, anaishi *Mars? Neptune? Venus au Pluto...* ? kama anaishi ndani ya dunia au niseme sayari hii kwa nini tumkose? Wangapi tumewaangusha na kuwatoa maisha iwe kwa kificho au kwa siri? Nani alitisha kama Carlos *The Jackal*? Nani alitisha kama yule Mbrasil mmiliki wa shamba kubwa aliyetusumbua katika biashara ya dawa za kulevya, nani? Hata Lucifer tukimtaka tuna uwezo wa kumteketeza... Dimens au *demons...* *Sir, kill him. Team 1* imewahiwa, sasa *Team 2*, tuna uhakika gani na timu hii?” mjumbe yule akaongea mpaka machozi yanamtoka.

“Sasa tufanye nini?” Mkurugenzi akamwambia.

“Nilikuwa nasubiri hapo hapo,” akadakia mjumbe aliyekuwa kimya muda wote akitafakari, “...Kwanza kabisa tumeingia kwenye hili swala

kimakosa, na tumefanya kosa kubwa sana kuwataka Tanzania wasitishe uchunguzi wao... naiona hatari! Hatari kubwa! Dimens, siyo mjinga. Kama alijua kuwa mnatuma mpaka ndege hatoshindwa kujua kuwa vijana wetu wapo Tanzania kwa kazi hii. Katika orodha yetu ya wapelelezi hatari duniani na wakuogopwa, yupo mmoja, Mtanzania,” aliposema hayo, watu wakaanza kunong’ona, ishara ya kutokubaliana naye.

“Niacheni nimalize!” Akawaambia.

“Kama mnakumbuka jasusi la KGB lililoasi, na kutokea kuwa muuaji hatari, Bill Van Getgand, kule Ujerumani, ni huyu mpelelezi wa Tanzania aliyemkamata, FBI walikuja mwishoni. Na kabrasha hilo ninalo mimi. Kama mnamkumbuka Sir Robinson Quebec, ni nani kati yetu aliujuu uovu wa huyu mtu? Hakuna, wote tulimwona rafiki huko Canada, ni mpelelezi huyu aliyegundua uovu wenye udhalimu wa mwanadamu huyu, ndiye aliyemwona mbwa mwitu ndani ya kondoo, sitaki kuongea *apocalipsis*... bali nawaambieni...”

“*Quite!* Naona mjumbe huna hoja, ni lini umesikia mwafrica anaweza kutatua mgogoro mkubwa na mzito kama huu? Nchi zao kila siku zinapigana, kwa nini wasitatue matatizo yao kwanza?” Mkurugenzi akaongea kwa ukali.

“Hicho si kigezo!”

“Hawawezi!”

“Wanaweza!”

Kile kikao kikavunjika baada ya wajumbe hawa wa ngazi za juu kushindwa kuafikiana. Wakapanga miadi ya kukutana siku inayofuata ili kuendeleza mjadala wao. Dimens alizidi kuwaumiza kichwa na kuwanyima usingizi.

* * *

Kandokando ya Jimbo la Manhattam, katika makaburi ya St. Peter’s Park, mwili wa Cindy ulisubiri kuteremshwa kaburini huku askari waliovalia nadhifu kabisa wakiwa wamesimama imara, wakifanya gwaride lile la maazishi. Gwaride maalum ambalo hufanyika tu anapokuwa mwanausalama amefariki. Cindy alipewa heshima hii ambayo alistahili kutokana na kazi yake. Miongoni mwa waombolezaji, Jesse alikuwapo kimya kabisa mwenye uso wenye huzuni.

Baada ya buluji ile kumalizika, bendera ya Marekani iliyokuwa juu ya sanduku la mwanamke huyu ikakunjwa kwa ustadi kabisa na vijana hawa kisha amri ikatolewa na kupisha taratibu za kidini.

Saa moja iliyofuata, watu walitawanyika katika uwanja huu, shughuli ya maazishi ilikuwa imekwisha..

“Jesse!” Yule mkurugenzi aliyekuwa na kikao siku chache zilizopita alimwita kijana huyu.

“*Yes Sir!*” akaitika.

“Nambie ukweli, hali ilivyo huko Tanzania!” akamwambia.

“Hali ni tete kama nilivyokuandikia kwenye taarifa. Tunamtafuta mtu asiyetabirika, mpaka sasa tunafikia mahala pa kupata vibaraka wake, sio kwa kuwakamata la, ni kwa kuhisi lakini tunashindwa kufuata nyayo za mtu huyu. Lakini bila kumung’unya maneno si mwingine ni Lord Dimens...”

“*Do not call him Lord!*” akang’aka.

“*Ok Sir!*”

“Sikiliza. Hakikisheni mnajua wapi anapatikana”.

Hatua mbili mbele, Jesse akasimama na mkuu wake akafanya vivyo hivyo.

“*Sorry sir!*”

“Enhe!”

“Tumtafute Dimens au tutafute ile chanjo? Maana naona kama unaenda kinyume na faili ulilotupatia...”

“*Oh come on Jesse, sure! Recover the ‘SEC’*” akamwambia na kumwacha. Jesse akabaki dakika chache kimya akimtazama. Akatikisa kichwa na kuingia ndani ya gari lake, akalitia moto na kuondoka zake taratibu. Jesse alikuja tu mara moja kwa mazishi ya Cindy, na mara baada ya shughuli hiyo tayari alikuwa akielekea uwanja wa ndege kwa safari ya Dar es salaam.

* * *

Dar es salaam

Jua la jioni lilipendezesha anga la jiji hilo. Pilikapilika ndani ya Uwanja wa ndege wa Mwalimu Nyerere zilikuwa si haba. Watu walijaa katika eneo la mapokezi wakisubiri kuwalaki ndugu zao. Wakati wengi wao wakiwa na hamu ya kuwaona tena wapendwa wao, upande wa maegesho kulikuwa na mipango mingine ikiendelea.

“Nyote mnajua nini mnapaswa kutenda. *Shoot on the spot!*” jitu moja, nene, lilikuwa likimpa maelekezo kijana aliyeshikilia bunduki aina ya AK 47 akiwa ndani ya Land Cruiser lililokuwa katika maegesho ya

uwanja huo. Yule bongе аlichukua darubini yake na kuiweka machoni pake huku аkipumua kwa nguvu na yule kijana naye tayari jicho lilikuwa kwenye lensi iliyofungwa juu ya bunduki hiyo ya Kirusi.

“Wanatoka sasa, *attention!*” Yule bongе akamwambia kijana wake kisha akainua simu yake ya upepo akabofya kitufe fulani na kuiweka karibu kabisa na kinywa chake.

“Kama tulivyopanga, hapa ni vita tu, hatakiwi mtu kupona leo. Tukikamilisha, kila mmoja anatakiwa atoroke kwa njia aliyopangiwa, fanya kazi kitaalamu. Hakikisha hadhuriki mtu asiyehusika. Kila mmoja ana picha ya mtu anayetakiwa kuuawa, uhakika wa wote kuwa wako hapa upo na mmewaona, sasa kazi ni moja tu. Mwisho wa yote tukutane chimbo, sawa?” Yule bongе akawapa taarifa wenzake, kila mmoja akajibu kuwa yupo tayari kwa shambulizi.

* * *

Upande wa pili wa uwanja huo huo katika maegesho mengine maalumu, gari aina ya Jaguar lenye rangi nyeusi lilikuwa limeegeshwa na vioo vyake vikiwa juu kabisa huku ndani kiyoyozі kikiendelea kupoza hewa. Ndani ya gari hili kulikuwamo watu watatu tu, dereva, mwanamama mmoja mtu mzima na kijana shababi kando ya dirisha.

“Umewasikia?” Yule mama akasema.

“Nimewapata vyema, sasa unasemaje?” Yule kijana kando ya dirisha akajibu kwa swali.

“Fanya unachoweza lakini hakikisha, unaokoa watu hawa maana wamekuja kichwa kichwa sana hapa mjini wakijifanya wanajua kila kitu...”

“*Their souls are served...* Ukiwa na mimi amini kuwa kifo huletwa na Mungu tu!” Yule kijana akajibu kwamba roho zao zi salama na kuinua ‘*short gun*’ yake tayari kwa kazi. Mikononi mwake alivaa *gloves* za ngozi, usoni akashusha soksi nyeusi, dereva wake akafanya hivyo pia na yule mama akateremka na kuufunga mlango wa lile gari.

“Hapa kazi tu,” akawaambia. Na wale jamaa wakaonesha vidole gumba juu, huku kioo cha mbele kushoto kikiwa kimefunguka kidogo pa kuweza mtutu wa *shortgun* ile kufanya kazi.

“Shabaha unayo? Maana wewe ukiona mwanamke mzuri tu utalenga maua badala ya mlengwa...”

“Hah! Hah! Hah! Hah! Scoba usinichekeshe bwana tupo kazini...”

“Haya, nitakwenda mbele ya wale jamaa na kisha nitapiga norinda kuligeuza gari ilikotoka, kumbuka kushoto kwako kuna watatu na walioshuka ni wawili ambao watawapa ishara wenzao. Nikienda mbele piga wale watatu, nikipiga norinda piga mmoja kisha wa mwisho Madam S anajua cha kufanya naye ndani ya sekunde kumi tu za breki....” Scoba akatoa maelekezo.

“Umesomeka kijana,” hakuwa mwingine ni Kamanda Amata, TSA 1, alijibu kauli hiyo.

* * *

Jesse aliteremka ndegeni na kumaliza taratibu zote ndani ya uwanja huo. Sasa alikuwa tayari kutoka nje. Kila alipotaka kutoka nafsi yake ikamkataza kabisa. Aliheshimu sauti hii. Jua kwamba ili uwe mpelelezi mzuri au jasusi mzuri sifa kubwa ni kuweza kuwa na sensi au tuite mlango wa fahamu wa sita. Hii ndiyo sifa kubwa ya shushushu. Jesse akaingiza mkono mfukoni na kutoa kifaa maalumu akakipachika sikioni na kujaribu kutafuta mawasiliano kama kuna watu wake upande huo.

Akafanya mawasiliano na kukuta watu wake anaowategemea wapo hapo akiwamo Johnson Kasalu. Baada ya kumhakikishia usalama, kijana huyo akatoka nje kwa kupita katika mlango wa *‘Arrivals’* kisha kuelekea kwenye maegesho ya magari. Akiwa bado hajavuka barabara, akimuona Johnson Kasalu anakuja upande wake ndipo aliposhuhudia kitendo hasichokitegemea. Land Cruise moja lililokuwa likiunguruma likashushwa kioo na mtutu wa bunduki ukajitokeza.

“Dooooonnnnnnn!” Jesse akapiga kelele na Johnson kwa kitendo cha haraka akajitupa chini huku akichomoa bastola yake. Jesse wakati akijitupa chini alihisi kitu kama msumari kimepenya begani na kufuatiwa na maumivu makali. Akiwa pale chini akaona gari jingine jeusi, hakuweza kulitambua haraka, likitoka mahala pake kwa kasi, na kupiga *u-turn* moja ya hatari sana mita chache karibu na lile Land Cruiser na lilipogeuka kurudi lilikotoka zikasikika kelele za watu huku wakikimbia huku na huko. Lile gari ikafunga breki na mkono wa mtu mmoja ukajitokeza huku mlango ukifunguliwa. Kijana mmoja aliyekuwa akishangaa tukio hilo huku mkono wake ukiwa ndani ya koti alichapwa kofi la macho na kunyakuliwa kuvutiwa ndani ya gari lile. Kisha likaondoka kwa kasi sana kuelekea mjini. Kitendo cha kama

sekunde thelathini hivi haya yote yalikwishatokea.

“Nani hawa?” Jesse akauliza huku bega lake likivuja damu nyingi sana.

“Siwajui, na hata sikutegemea wao kutushambulia!” Johnson akajibu huku akimfunga jeraha kwa shati lake baada ya kulivua. Lile Land Cruiser, lilibaki palepale lilipoegeshwa na hakuna mtu aliyetoka. Askari walikuwa wamelizunguka na bunduki zao mikononi wakiwataka walio ndani kujisalimisha. Walipoona kimya wakasogelea na kufungua mlango, walishuhudia maiti tatu za vijana. Moja imelalia usukani na risasi ikiwa imefumua vibaya kichwa chake. Nyingine imejitupa pembeni kwenye kiti cha nyuma ikiwa na jeraha kifuani usawa kabisa wa moyo, na nyingine ikiwa kitini huku mkononi imeshika bunduki ya kivita AK 47 nayo ilikuwa imefumuliwa kichwa kwa risasi.

“Yamekufa!” askari mmoja mwenye cheo cha koplo akawaambia wenzake. Wakashusha bunduki zao na kusogelea eneo lile, wakafungua milango na kutazama maiti hizo. Haraka wakazungusha utepe wa njano eneo lile na taratibu za uchunguzi zikaanza.

“Hawa watakuwa magaidi kwa vyovyote vile,” mwingine akadakia na wakati huo tayari watu walishazunguka eneo hilo kila mmoja akizungumza lake.

“Tutawajua tu, hakikisheni mnawasaidia wale majeruhi kisha wao watatuambia vizuri maana watakuwa wanajua. Hivi ni visasi tu!” Askari mwingine mwenye ‘mbavu tatu’, aliyekuwa na *radio call* mkononi akawaambia wenzake. Mmoja wao akatoka kuelekea kule aliko Johnson na Jesse, hakuwakuta. Alipouliza akajibiwa kuwa hakuna aliyeona wameondoka wakati gani.

* * *

Scoba aliiacha Barabara ya Nyerere na kuingia ile ya Kilwa kuelekea Kurasini. Madam S akageuka nyuma kumwangelia Amata.

“Vipi?” akamwuliza.

“Amezimika!” Amata akajibu.

“Hongera, naona bado una shabaha sana!” Madam akamtania.

“Jana nilifanya mazoezi makali sana kule shamba, unafikiri mchezo. Nilikwambia nitatumia risasi tatu tu yaani moja kwa kila mmoja na ndivyo ilivyokuwa,” Amata akaeleza.

“Halafu yule jamaa aliyetokea kwenye maegesho kuja kumpokea huyu mgeni mbona kama namjua?” Scoba akauliza huku akiingia Barabara

ya Shimo la udongo na kupita UDA kisha akakunja kushoto na kuingia Daraja la Nyerere.

“Yule ni mfanyabiashara mmoja hivi anaitwa Johnson Kasalu,” Amata akajibu.

“Umemjuaje?” Madam akadakia.

“Unakumbuka sakata la dawa za kulevya lileeee...”

“Enhe!”

“Nilimwona na nikaamua kumfuatilia, ila nina mashaka sana na biashara zake, na hili la leo, hapana! Kuna kitu nyuma yake,” Amata akasema.

“Hii vita ni kubwa sana! Unajua tumeingia tu lakini tumeshazuiwa kufanya, hivyo sisi ni kama wahalifu...” Madam akasema.

“Hatukuwa na budi mama kufanya hili. Kama tulinasa mazungumzo yao, basi kazi yetu ni kuzuia uhalifu. Hakuna furaha kubwa ya mwanausalama kama anapofanikiwa kuzuia uhalifu na hakuna maumivu mabaya kwake kama uhalifu unaohatarisha usalama wa taifa unatendeka na yeye ameshindwa kuzuia, maumivu yake huwa hayaishi...”

“Mmmm! Unakumbuka mafunzo eee,” Madam akamwambia.

“Sana tu, wakufunzi walini *train* sawasawa,”

“Tumshukuru Mungu!”

“Amin!”

* * *

Inspekta Simbeye aliwasili katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere akiwa na vijana wake. Vijana wa kazi, wasiocheka na mtu. Mazungumzo yote ya watu katika uwanja huo yalikuwa ni juu ya tukio lililopita nusu saa tu. Moja kwa moja akaingia katika kituo kidogo cha polisi. Ndani ya kituo hicho alikutana na askari mwenye cheo cha Sajini. Yule askari alipomwona Simbeye akasimama na kutoa heshima ya kijeshi kisha wakaketi.

“Ndiyo afande, nipe taarifa ya kilichojiri, maana ndicho kilichonitoa ofisini...” Simbeye akaanzisha mazungumzo kwa mtindo huo.

“Hapa kumetokea shambulio la kijambazi au kigaidi sijui niliweke vipi. Kuna msafiri mmoja ambaye aliingia hapa na ndege ya KLM ndiye aliyeshambuliwa na vijana ambao walikuwa ndani ya Land Cruiser lenye rangi ya nyeusi...” akaeleza.

“Amekufa?”

“Hapana hajafa, ila ameumia begani,” yule kijana akaeleza. Simbeye akatulia kidogo kama anayefikiri jambo.

“Lakini mkuu hapa kuna jambo la kushangaza kidogo...” kauli hii ikamshtua Simbeye.

“Unasema!” akagutuka.

“Nasema katika shambulio hili kuna mambo ya kushangaza sasa bado najaribu kuyachanganua nione kipi ni kipi...”

“Kwa nini?” Simbeye akauliza.

“Wale jamaa waliomshambulia huyu msafiri wameuawa wote...”

“Sasa kipi cha kushangaza, ninyi mlitakaje?” Simbeye akauliza.

“Tatizo si wao kufa, tatizo ni aliyewaua! Inaonekana kuna kikundi kingine kimewaua hawa jamaa kisha wakakimbia na gari lao mpaka sasa tumetoa taarifa, hilo gari halijaonekana,” akasema.

“Unataka kunambia kulikuwa na makundi mawili?”

“Ndiyo. Kundi moja lilitaka kumuua huyu msafiri na lingine liliwafuata hawa,”

“Huyo majeruhi yuko wapi?” Simbeye akauliza.

“Sasa mkuu hilo nalo ni lingine, huyu majeruhi hajulikani alipo mpaka sasa na hakuna mtu aliyemwona kaondokaje,”

“Kijana unanichanganya,” Simbeye akasema. “Naomba uniandikie hilo jalada na chunguzi zenu za awali, kisha nifikishiwe pale *Central* leo hii, mengine tutaongea huko huko,” akanyanyuka na yule kijana naye akanyanyuka kisha wakapigiana saluti na kuagana.

Hali ya hewa ya uwanja huo ilirudi katika utulivu na shughuli zikaendelea kama kawaida huku askari polisi wakiwa makini kuangalia usalama. Simbeye na vijana wake wakaondoka, ila mmoja alimwacha kwa siri aendelee kukusanya habari hizo.

* * *

Nyumba Namba 9

Katika nyumba yao ya siri, Jesse alikuwa akipatiwa matibabu, na Johnson alikuwa pembeni yake akimtazama daktari wao akifanya kazi. Haikuwa kazi rahisi kama unavyofikiria, risasi ilikuwa imenasa ndani, na kuvunja bega hilo kiasi kwamba halitoweza kufanya kazi kwa kipindi fulani.

“Vipi dokta?” Johnson akauliza.

“Nimeitoa risasi, ila huu mkono hautaweza kufanya kazi kwa sasa inabidi akae angalau siku tisini ili mfupa uunge sawasawa,” yule daktari akamwambia. “Ni nani aliyewashambulia?” akamuuliza Johnson.

“Kwa kweli bado sijajua, lakini nitawatia mkononi tu,” Johnson akajibu na kujinasibu.

“Utawatia mkononi wakati nao wameuawa!” Yule daktari akamwambia na kumwacha kijana huyo kakodoa macho.

“Johnson!” akaita, naye akageuka upande ule kumwangukia daktari yule, “Kundi mnalopambana nalo ni kundi lenye weledi mkubwa sana wa mambo haya, kama ni intelijensia na wao wanajua. Muwe makini sana na mambo yenu kuanzia sasa. Kwa tukio hili ina maana kuwa wanawajua mlipo na mnafanya nini na kwa wakati gani. Hakuna adui hatari kama yule aliye miongoni mwako. Si ajabu hata mipango yenu wanajua...” yule daktari akamwambia Johnson huku akiwa tayari kuondoka.

“Inabidi kujipanga upya!” akasema Johnson kisha akamwangukia Jesse aliyekuwa ametulia kitandani.

“Waambie akina Tetty warudi kambini haraka!” Jesse akamwambia John, naye akachukua simu yake na kuwapa taarifa watu hao ambao walitumwa Tanzania kama *‘Team 2’*.

* * *

LINDI

Mlango wa Tetty uligongwa katika hoteli aliyokuwa akiishi huko Lindi. Muda huo tayari alikuwa bafuni kujiandaa kwa safari ya kurudi Dar es salaam kama taarifa ilivyomfikia. Lakini walionywa wasitumie ndege kutokana na kile kilichompata Jesse siku hiyo. Wakaonywa wasisafiri pamoja wala wasitumie gari binafsi bali wapande mabasi au usafiri mwingine wowote. Baada ya kupata taarifa hiyo, akawaambia na wenzake hivyo wakapanga kukutana Dar es salaam kwenye nyumba yao ya siri.

Hodi ikaendelea kubishwa na Tetty akiwa bafuni alikuwa akitafakari ni nani atakuwa anagonga mlango huo. Tangu afike katika mkoa huu kwa uchunguzi wa siri hakuwahi kuwa na mazoea na mtu kiasi kwamba

amfuate chumbani. Akajifunga taulo lake juu kidogo ya maziwa, kichwani akavaa kofia kama mfuko wa plastiki na kuzihifadhi nywere zake ndefu za kizungu. Akatoka taratibu na kuliendea jagi kubwa lenye ua ndani yake. Akaingiza mkono na kuchukua bastola yake, akaiweka sawa.

Maana sasa hivi bakuna kuaminiana! Akawaza huku akiuendea mlango.

“Yes! Who are you?” akauliza kutaka kujua ni nani anayegonga huku taratibu akiukaribia mlango. Akashika kitasa tayari kufungua.

“Just open, here is your anvelope!” akajibiwa kutoka nje na kujulishwa kuwa kuna bahasha yake hivyo afungue tu. Akafungua mlango na kuacha kaupenyo kadogo. Kijana mweusi mwenye ndevu nyingi, mwili mkubwa, akasukuma mlango kwa nguvu na Tetty akapigwa kikumbo na kuangukia upande wa pili huku taulo lake likiuacha mwili na bastola yake ikitoka mikononi. Akajaribu kuiwahi na alipotaka kuitumia tayari akajikuta akitazamana na bunduki kubwa na kasha lililokuwa na maua likiwa chini sakafuni.

“Kama ulikuwa hujui, basi jua sasa kuwa umebaki peke yako!” Yule jamaa akamwambia Tetty huku akimsogelea. Mwanamke huyu alikuwa akihema kwa nguvu na hasira zilionekana dhahiri shahiri usoni mwake. Kwa kasi ya ajabu, akajizungusha na kumchota mtama, yule jamaa akatua sakafuni kama mzigo wa kuni. Tetty akawahi kuinuka na kumweka chini ya ulinzi huku bado akihema kwa nguvu. Akaipiga teke ile bunduki ikasogea mbali.

“Ulifikiri utaniokota kama wengine, sasa humuhumu chumbani ndimo maisha yako yatakapoishia...” Tetty akasema.

Mara akasikia tena mlango ukigongwa kwa nguvu, Tetty hakuwa na muda wa kupoteza, akamtwanga risasi ya kichwa, yule bwege, akalala kimya. Mwanamke huyo kwa haraka, akavaa jinzi lake. Hakujali kama katanguliza nguo ya ndani au la. Akavalia travota zake na kujiweka tayari kwa safari. Akanyakua kabegi kake ambako kalikuwa kamefungwa tayari kwa safari. Akafungua dirisha na kuchumpa nje. Huko akakwea ukuta kwa sekunde tatu tu akawa nje akitua bila kishindo.

Wale jamaa wakavunja mlango na kuingia ndani, hakuna mtu zaidi ya marehemu ndugu yao tu.

“Huyu jamaa atakuwa alishaanzisha mapenzi huyu, mi namjua sana!” kijana mmoja aliongea kwa jazba japo kwa sauti ya chini.

“Keshatutoroka, tumuwahi nje!” mwingine akapiga ukelele na wote wakatoka nje na kuzunguka huku na huko wasimwone Tetty.

* * *

“*Team 2 imeanguka Sir!*” Mkuu wa kitengo cha operesheni za nje cha CIA alimwambia boshi wake. Siku hii aliitwa yeye tu ofisini na endapo ukipata wito huu wa kuonana na ‘*Top*’ kabisa wa idara hiyo, basi ujue kuna jambo kubwa. Hii ilikuwa Siku nzito sana kwa mkuu huyu wa kitengo cha operesheni za nje aliyejulikana kwa jina moja tu la Brandon, baada ya kukuta ujumbe mezani pake kuwa anatakiwa kuonana na ‘*Top*’. Ukimya ukatawala kati ya wawili hawa kisha yule ‘*Top*’ akakohoa kidogo na kufikicha macho yake yaliyofichwa nyuma ya miwani. Alikuwa mtu mzima kadiri ya miaka sitini hivi, lakini macho yake makali yalionesha jinsi ambavyo mtu huyo alivyo makini katika kazi yake.

“Mr. Brandon, *you have failed!*” Yule boshi akamwambia mgeni wake kuwa ameshindwa.

Brandon hakujibu kitu badala yake aliishia kumtazama tu kwa macho makavu, “Nilitegemea ungeifanya kazi hii kwa ustadi na weledi wa hali ya juu kama kawaida yako, lakini sijui ni nini kimetokea,” akaongeza kusema.

“Sasa huyu adui yako anakujua mpaka unakunywa chai saa ngapi, huoni kama ni hatari hiyo? Tushapoteza vijana karibu watatu wa *team 1*, Cindy, Kelvin, Mellenia, Doddy... yaani dah! Na sasa *team 2*. Brandon, hawa vijana tunawatrain kwa gharama sana, mwenyewe unajua...” akashindwa kusema, akamtazama tena Brandon.

“*Abort the mission please!*” akamwambia asitishe kazi hiyo iliyokuwa ikiendelea huko Tanzania.

“Sasa tukisitisha si ulimwengu utatushangaa?” Brandon akauliza.

“Wacha utushangae, kwani ni mara ya kwanza kusitisha *program* kama hii? Mbona mara nyingi tu. Ile ya Cambodia umeisahau? Watu wetu waliuawa kwa wakati mmoja wakiwa miji tofauti, tulisitisha. Maana kikitokea kitu kama hiki basi ujue adui unayemtafuta yupo ndani yako hapo hapo...”

“Unataka kunambia Dimens ana watu wake humu ndani?” Brandon akadakia kauli.

“Au we unaonaje?” badala ya kumjibu akamuuliza swali lililomuacha kimya, “Nenda na fanya nililokwambia!”

“*Ok Sir!*” Brandon akaitikia na kuondoka katika ofisi ile huku moyo wake ukiwa umejaa donge la kumsaka Dimens. Ndani ya ofisi yake alijibwaga kitini na kutulia kwa muda. Akili ilipomkaa sawa akamwita katibu muhtasi wake na kumpa jukumu la kutuma nukushi ya haraka kwa Bwana Johnson Kasalu kuwataka vijana wake warudi nyumbani. Brandon hakulizika kabisa na uamuzi huo lakini hakuwa na jinsi zaidi ya kutii amri ya mkuu wake wa kazi.

Yule mwanadada naye hakucheleva kuitimiza kazi hiyo. Alipoketi tu kitini pake, kazi ya kwanza ikawa ni kutayarisha nukushi hiyo na kuituma kwa wakala wao Johnson Kasalu kwamba kazi hiyo imesitishwa na jamaa wanatakiwa kurudi Marekani.

* * *

Huko katika *House 9*, Jesse alikutana na watu wake. Usiku wa manane kila mmoja alihakikisha amefika mahala hapo na hilo lilitimia lakini Tetty peke yake alikuwa hajawasili mpaka muda huo.

Kila mmoja akajawa na wasiwasi na hasa kufuatia tukio la siku hiyo la kushambuliwa kwa Jesse.

“Nini kitakuwa kimempata?” kijana mmoja wa Kizungu alirusha swali pasi na kujua nani atajibu. Ukimya ukatawala na hofu pia, “Ni ngumu kujibu swali lako maana hapatikani hata simuni, ila ninavyomjua Tetty, atafika tu ila lazima yupo matatizoni,” akajibu mwingine. Wakati huo wote Jesse alikuwa kimya kitandani akifikiri jambo.

Simu ya Johnson Kasalu ikapata uhai, akainyakuwa na kuitazama ni nani anapiga, akatikisa kichwa baada ya kujua kuwa kuna nukushi imeingia ofisini kwake na alitakiwa kuipata haraka na kuitekeleza. Akawaaga vijana hao na kuwaacha kwa muda ndani ya nyumba hiyo ya siri. Hakuna aliyetamani kufanya chochote. Kila mmoja alikwenda huku na kurudi kule, Tetty hakuonekana, seuze kupatikana kwenye simu!

Baada ya subira ya dakika thelathini hivi, usiku huo huo, Johnson Kasalu akarudi na kuwakuta katika hali ile ile. Walipomwona wote wakamzunguka na kusikiliza kama ana ujumbe wowote. Kasalu hakuonekana mwenye furaha bali mshangao uliochanganyika na woga au hofu.

“Vipi?” Jesse alikuwa wa kwanza kuuliza.

“*Bastard!*” akatamka na kujitupa kitini kisha akatoa kijifuko cha

karatasi na kumwaga vilivyopo mezani.

Wote wakakodoa macho kutazama. Pete, heleni, bangili na kidani kimoja ambacho nyuma yake kimeandikwa Tetty Hudson, maandishi ambayo si rahisi kuyagundua kama hujui kuwa yapo katika kidani hicho. Hii kwao ilimaanisha kuwa mwanamke huyo amekwishakufa.

“Siwezi kuamini!” Jesse akalopoka na wengine wakamwunga mkono. Baada ya mjadala mrefu juu ya kufa au kutekwa kwa mwanamke huyo ndipo Kasalu akampa Jesse ile nukushi iliyofika ofisini mwake.

Jesse akaisoma na kuwapa wengine wote nao wakaisoma kila mmoja kwa wakati wake.

“Tunaondokaje bila kuhakikisha usalama wa mwenzetu?” akauliza mwingine.

“Si unajua kanuni, kwa hiyo hakuna cha kushangaa, ni kwamba upatapo tu ujumbe kama huo hauna mjadala hata kama mwenzako anakufa huna budi kumwacha kwani ni bora kufa mmoja lakini si kundi zima. Hatuwezi kujua nini wameona mpaka wakaamua hivyo. Cha kufanya ni kuondoka na wao wanajua nini watafanya. *Mission aborted!*” Jesse akawaambia vijana wake na kila mmoja akaanza kuandaa safari ya kuondoka katika jiji hilo.

Jesse akajiinua kitandani na kuketi, baada ya dakika kama mbili hivi akainuka na kumchukua Johnson pembeni wakaongea machache.

“Johnson, tunaondoka, lakini tunamwacha Tetty mikononi mwako awe hai au amekufa, tunamhitaji,” akamwambia.

“*Don't worry comrade!* Nasikitika sana kazi hii inakufa katika kanda yangu. Najua nina wajibu wa kufanya kitu kikubwa katika hili,” Kasalu akamwambia Jesse.

“Usijali, kazi zetu ndivyo zilivyo lakini naamini kila kitu kitakwenda sawa. *Ciao!*”

* * *

Alfajiri ya siku iliyofuata kila mmoja aliondoka kwa njia yake, hii ilikuwa ni kumchenga adui kama alikuwa bado akiwafuatilia. Hakuna aliyetumia uwanja wa ndege wa Dar es salaam na wala hakuna aliyemwambia mwenzake kuwa atafikaje Marekani bali waliagana na kila mmoja akaondoka kwa wakati wake huku Jesse akiwa bado kabaki saa kadhaa Dar es salaam.

Siwezi kuamini kama kazi hii imeshindikana, bado tulikuwa kwenye kutafuta

datum hii na ile. Wamewahi kusitisha, tunahitaji kujua zaidi juu ya Mellania, Doddy, Kelvin na sasa Tetty! Jesse aliwaza sana mpaka akahisi kichwa kuuma.

Bega lake likiwa na bandeji kubwa, akatoka katika nyumba hiyo kwa mlango wa siri na kuibukia katika stoo ya vifaa tiba. Akapita hapa na pale, akufika katika ofisi ya daktari mfawidhi wa hospitali hiyo. Daktari huyu, Mhindi, ambaye hata yeye yupo hapo kwa kifuniko cha udaktari ila nyuma yake alikuwa shushushu hatari na wakala wa CIA, akamtazama kijana mkakamavu anayeingia katika ofisi yake.

“Are you ok?” akamuuliza Jesse

“No!”

“Why?”

“Tume ‘abort’ misheni yetu...”

“Nina taarifa tayari. Jesse! Najua umechukia ila rudini nyumbani kwanza mambo yawekwe sawa kisha tutajua cha kufanya,” yule daktari akamwambia.

“Usijali, ila ... Tetty!!”

“Atapatikana tu. Be carefully!” wakaagana, na Jesse akatoka nje ya jengo lile na kuchukua usafiri wa pikipiki kuelekea Posta ambako alipanda boti mpaka Zanzibar huko akakodi ndege mpaka Nairobi na kuondokea huko.

SURA YA 13

CABO DELGADO

Majuma marwili baadae

NDANIYA CHUMBA kimoja chenye mitambo tiba isiyoelezeka, kulikuwa na watu wawili mwanamke na mwanaume. Watu hawa walikuwa wamefungwa bila wao kujua au kutaka. Mwanamke alikuwa mzungu na mwanaume Mwafrika. Kwa juma zima waliwekwa humo. Hakuna kati yao aliyejua kaingiaje ila kila aliyepata fahamu alijikuta ndani ya chumba hicho. Chumba cha siri, chini ya ardhi, katika jumba kubwa la Lord Dimens. Hawakujua hata wako wapi lakini pia hawakuwahi kuongea kila mmoja alikuwa kimya kabisa.

Kwa mara ya kwanza waliona mlango ukifunguka na watu watatu wakaingia; mmoja mtu mzima na mwingine kijana mkakamavu mwenye nywele nyeupe kana kwamba ana mvi kichwani mwake lakini sivyo, na wa tatu alikuwa mwanamke. Mwanamke huyu alikuwa na chano mikononi mwake. Ndani ya chano hicho kulikuwa na chupa moja ndogo ya dawa na sindano kadhaa na soksi za mipira, maalum kwa kuvaa mikononi.

Wale mateka, kila mmoja, akatolewa na kufungwa kwenye kiti kikubwa chenye mikanda huku na huku. Mwanamke akiwa kavuliwa brauzi na yule mwanaume akiwa kavuliwa shati. Wote wakabaki vifua wazi. Matiti mekundu ya msichana huyu yalisumbua wanaume ndani ya chumba hicho.

“Mmmmmh! Unaonekana una ladha ya pekee binti ee!” Yule mzee akasema huku macho yake yakitalii kifua cha mwanadada huyo. Akavuta kiti, na kukaa juu yake.

“Nimewaweka hapa, si kwa nia mbaya ila tu kwa kufanya majaribio

kadhaa katika miili yenu. Ninyi ni watu muhimu sana duniani. Kwanza mtaingia katika historia kwa kufanyiwa jaribio hili, hah! Hah! Hah!” Yule mzee akaongea na kutoa cheko la kifedhuli.

Kutoka pale alipofungwa, yule mwanamke mzungu akatoa tusi baya kabisa na kumtemea mate mzee huyo. Mara yule mlinzi akapiga hatua tayari kumtia adabu, akazuiwa.

“No! no! no! usifanye hivyo. Wanawake wazuri kama hawa huwa hawaadhibiwi kwa ngumi, au kofi,” akamwambia mlinzi wake.

“Sikilizeni,” akawaambia wale mateka.

“Tupo hapa ku*introduce* chanjo makini kabisa ya *AIDIOSIS* iliyovumbuliwa katika maabara yetu kubwa kabisa duniani, Dimens Lab-Tech. Ninyi ndiyo mtakuwa mashuhuda wa kwanza duniani. Kwanza tutawapima kama mmeshaathirika na ugonjwa huu. Kama ndiyo hamtatufaa na kama siyo basi mtatufaa sana kwa zoezi hili,” yule mzee akawaambia.

“Acha ushetani wako! Na nikitoka hapa utapata shida!” Yule mwanamke aliendelea kulalama.

“Ha! We shetani unamjua? Kwa taarifa yako tukimaliza kazi yetu hii tunawaua, kisha tunawasagasaga na kuwapa nguruwe nyama tamu ya binadamu, wala hutopata muda wa kufanya hayo unayoyafikiria. Anza kazi!” akaamuru. Yule mwanamke aliyebeba chano naye akavaa *gloves* na kuchukua sindano maalumu kwa kutoa damu katika mishipa. Dakika tatu tu tayari sampuli za damu za viumbe hawa zilikuwa kwenye kibompoli maalumu kwa kuhifadhia. ikatiwa katika mashine na kusubiri kidogo.

“Tutakapomaliza jaribio la kwanza litafuata la pili, hilo litahitaji utulivu sana. Tunataka manii za huyu kijana na mayai ya wewe msichana kisha tutatengeneza mtoto kwenye mashine maalumu na tutamuweka kila tunachokitaka. Maabara yetu ni kubwa ina uwezo wa kutengeneza mwanadamu kama wewe na kumkuza kwa miezi sita tu. Jiandaeni!”

“*Never!*” Yule mwanamke akadakiza kusema huku akijaribu kujitikisa kwenye kile kiti kikubwa kilichojilaza na kuwa kama kitanda.

“*Never?* Mbona damu tumechukua! tutashindwa kupata mayai yako? Hah! Hah! Hah! Lazima ujue kuwa watu wako wamekutelekeza. Hivi tunavyoongea, wamepewa na kazi nyingine za kufanya na hiki kioperesheni chenu kimefungwa wiki mbili zilizopita,” yule mzee akaendelea kumwambia yule mwanamke maneno ya kukarahisha. Akajitikisa lakini wapi!

“Dunia hii haiwezi kufanya chochote mi nisijue... Hakuna wa kunizuia kama ni hiyo kazi yako basi hata mimi nilikuwa CIA miaka mingi sana nyuma kabla sijaachana nao. Nimetumikia MOSSAD na KGB kwa nyakati tofauti. Sasa naendesha shughuli zangu hapa, umesikia mwanamke? *So! Never say never again!*” akamwambia.

“Sir!” akaitwa kutoka uande wa nyuma.

“Yes!”

“Kazi ya kwanza tayari, mwanaume ameathirika, mwanamke hajaathirika!” Yule mtu aliyevaa kiganga akamwambia Dimens.

“Oh good, nini kinafuata?” Dimens akauliza.

“Sasa huyu mwanamke tutamdunga ile chanjo, kisha baada ya saa sita tutamwekea damu iliyoathirika kisha tutaangalia nini kinatokea mwilini mwake...”

“Damu zao zinaendana?” Dimens akadakiza swali.

“*Yes, Sir!* Tumepata bahati sana kupata *specimen* zinazomatch kundi la damu,”

“Vizuri sana, endelea tu, mi nasubiri nione sayansi yetu imefikia wapi!” Dimens akasema na yule mganga akachukua kile kichupa na kudunga sindano kwenye kizibo chake cha mpira kisa akainua juu na kufyonza kiasi cha dawa anachohitaji, akaishusha na kuirudisha kwenye chano. Akachukua pamba kwa kutumia kishikio maalumu kitaalam huitwa *forceps*. Pamba hii ilikuwa na spiriti kali kabisa, akampaka yule mwanamke kwenye mkono wake kati ya kiwiko na bega.

“Oh! Samahani huyu mwanamke mmesema anaitwa nani?” Dimens akauliza.

“Tetty Hudson!” mganga akamjibu kisha akaendelea na kazi yake, akamdunga sindano kwenye nyama ya mkono. Tetty akafinya macho kwa maumivu wakati mganga huyu akisukuma ile dawa mwilini.

“Tayari...”

“*Good! Next?*”

“Baada ya saa sita tutamwenkea damu iliyoathirika kisha tutaendelea na ile *process* ...”

“Sawa! Asante sana, basi tutaonana wakati ukifika,” Dimens akamwambia mganga kisha akainuka katika kile kiti. Tetty akiwa bado juu ya kile kiti na mikanda ile imemfunga barabara. Mwanamke yule alijikuta ameloa jasho lisilo la kawaida. Yule mganaga akasukuma kile kiti na kutoka nacho katika mlango mwingine kisha akateremka ghorofa ya chini kabisa huku macho yake yakiwa yamemtoka pima

kutazama matiti ya Tetty huku akijilambalamba midomo yake.

Chumba alicholingizwa sasa kilikuwa tofauti kabisa na kile, hiki kilikuwa kikubwa na kilionekana hasa kuwa ni maabara kwani vikorokoro vilivyojaa na mitambo yote ilikuwa ikifanya kazi. Watu watatu wenye nguo nyeupe wakapokea kitanda alichokuwa Tetty na kukisukuma bila kuongea mpaka mahala maalumu na kukiweka huku msichana yule akiwa juu yake. Hakujuu kinachoendelea. Yeye alichooona ni mitambo tu ikiunganishwa kwenye mwili wake, mashine zilianza kupiga kelele mara tu zilipounganishwa naye, zikaanza kuonesha mwenendo mzima wa damu na vitu vingine kama moyo, mapafu na kadhalika. Kwa ujumla ni kama uhai wote uliahamishiwa kwenye mashine hizo. Hakuwa na la kufanya, kwani alikuwa amefungwa barabara kabisa katika kitanda kile.

Saa Sita baadaye...

Chumba kipana chenye viti kama kumi hivi kilikuwa kimebeba idadi hiyo ya watu. Mbele ya chumba hicho kulikuwa na luninga kubwa ambayo ilitosha kwa wote hao kuona nini kinatokea kule kilikokusudiwa. Ilikuwa ni chumba maalumu kwa kutazama matokeo ya kisayansi ya chunguzi mbalimbali duniani kote au ndani ya maabara hiyo. Lord Dimens aliketi mbele kabisa ya chumba hicho na watu wengine tisa. Katika hao watu tisa alikuwapo Dkt. Edward Minzi, naye alikuwa hapo pasi na kujua nini kinakuja kutokea.

“Are you ready for the show?”

Sauti kutoka kwenye vyombo maalum ikauliza kisha ile luninga ikawaka na kujiweka sawa kwa sekunde kadhaa na baadae ikaonesha maandishi makubwa yaliyotambulisha zoezi litakaloendelea sekunde chache zijazo. Mara ikaanza kutokea historia ya ugonjwa wa *AIDIOSIS* kuanzia mwanzo mpaka hapo ulipo. Ikaelezwa jinsi watu mbalimbali walivyojaribu kutafuta dawa na kinga dhidi ya ugonjwa huo lakini ikashindikana. Na mwisho wa maelezo hayo ikaeleza kuwa maabara ya kisasa ya Dimens imeweza kugundua kinga thabiti na kuwa sasa Mwafrika hatoteseka na ugonjwa huo. Ikazidi kueleza kuwa baada ya kufanya utafiti wa kina katika misitu minene ya Cabo Delgado, taasisi hiyo ya kutengeneza madawa na kinga imefanikiwa kutegua kitendawilizi hiko baada ya miaka mingi ya mateso miongoni mwa mtu mweusi.

Dkt. Edward Minzi akamtazama kwa jicho pembe mzee huyo jeuri

anayejifanya kuwa sasa yeye na maabara yake kuwa ndiyo wamegundua hiyo chanjo.

Ni mpumbavu sana, ni nini anachokivaza shetani buyu? Eti kagundua chanjo yeye! Dkt. Minzi akawaza na kuwazua huku akianza kuhisi kijasho chembamba kinamtoka kwapani. Alipotembeza macho huku na huko akakuta walinzi wote wakimkazia macho. Ikambidi atulie huku hasira ndani ya moyo wake ikizidi kupanda.

Yaani watu tumeteseka msituni, wengine wamepoteza maisha, buyu mzee anasema hii chanjo ni yake! Dkt. Minzi alizidi kuwaza.

'And now have a look in how it works in human body...'

Sauti hii kutoka kwenye ile dokumentari iliyotaka watazamaji waangalie jinsi chanjo hiyo ifanyavyo kazi katika mwili wa mwanadamu ikamshtua na kurudisha akili yake katika ile luninga. Picha kubwa ya mwili wa mwanadamu ikaonekana kwa mfano wa 'X-ray' ioneshavyo. Maelezo yaliyofuatia yakaelezea kwanza virusi wa *AIDIOSIS* wanavyoweza kuingia kwa mwanadamu na ni nini hutokea baada ya siku tisini. Onesho lile likaonesha jinsi ambavyo virusi vile hatari vinavyojigeuza kuwa sehemu ya chembe hai za mwili. Kisha wakaonesha dawa tofauti ambazo ziliwahi kugunduliwa na kusifiwa kuwa zinamaliza kabisa tatizo hilo na jinsi gani zilikuwa zikishindwa, na kwa vipi.

Hii kidogo ilimrudisha Dk. Minzi darasani kwani hakuwahi kufikiri juu ya hilo lakini hata hivyo halikuwa na maana kwa wakati ule. Akatulia kufuatilia, kilichokuwa kikimuuma zaidi kuhisi dhahiri kuwa 'tumeibiwa'.

Tumeibwa! Akawaza.

Baada ya picha ile kumaliza kuelezea jinsi dawa zingine zilivyoshindwa kazi kusudiwa, sasa ikaanza kuelezea juu ya kinga mpya iliyovumbuliwa na maabara hiyo ya Dimens Lab-Tech. kwanza wakaisifia maabara yao kisha wakaanza kuonesha mwili uleule, sasa ukiwa tayari umedungwa chanjo hiyo na baadae wakaonesha jinsi virusi vinavyoingia na kupata upinzani mkali kiasi kwamba haviwezi kufanya kazi yake. Ikaeleza kisayansi sana na mwisho ikawataja tena kwa utukufu mkubwa Dimens Lab-Tech.

"Noooooo!" Dkt. Minzi akapiga kelele. Kabla hajainuka kama alivyotaka kufanya akajikuta mikononi mwa manjemba kama manne hivi. Dimens alishtuka sana kwa kelele zile, akasimama ghafla akitetemeka.

"Lock up and make him uncomfortable!" Dimens akasema kwa hasira, akitaka afungiwe na kupewa adhabu kali. Wale vijana wakaanza

kumburuza Dkt. Minzi kumpeleka kwenye chumba maalumu.

"Noooo! It's not yours! You stole it from us! You are a thief! You hav..." Edward aliendelea kupiga kelele huku akiburutwa na jamaa wale.

"Shut up, dirty monkey!" Dimens akamkatisha Dkt. Minzi aliyekuwa akiburuzwa huku akipiga kelele kwa kumfananisha na nyani mchafu.

"Even if I am a monkey, but you stole it from us, you are a thief, a robber, a terrorist, a Satan, son of bitch, bastard!" Dkt. Minzi alikuwa akipiga kelele kwa nguvu na kile kikao kikavurugika. Edward alikuwa akitokwa na machozi. Akatupwiwa ndani ya chumba kimoja cha wastani na kisha wale jamaa wawili wakaingia naye ndani na wengine wakabaki nje.

Huko ndani, Dkt. Edward alipigwa sana mpaka kushindwa kutembea. Alipigwa kiasi kwamba alikuwa hata kutoa sauti hawezi tena, akapoteza fahamu na kulala kimya. Dakika kama nne hivi wale vijana wakarudi ukumbini na kukuta ukimya ule wa mwanzo ukiendelea na ile picha bado ikilalama kwenye ile luninga. Dakika kumi nyingine zilizofuata, ikamalizika na Dimens akainuka tayari kwa kuondoka. Akawageukia wataalamu wake na viongozi wa ngazi za juu ndani ya taasisi yake na kuwatazama kwa zamu. Hawa walikuwa ni watu anaowaamini sana kuliko mtu mwingine yeyote. Hawa ndiyo waliokuwa wakijua kila kinachoendelea na kupanga mambo mengi ya siri na hadharani.

"Uzinduzi wa chanjo hii nataka ufanyike baada ya miezi minne, wapi tutafanyia na vipi, hilo niachieni mimi, nitaandaa na kuwapa mpango kazi, sawa?" Dimens akawaambia.

"Sawa" wakajibu na kisha akaondoka zake. Hatua chache akafika katika chumba kile alichofungiwa Dkt. Edward Minzi na kumkuta akiwa karudiwa na fahamu lakini bado hakuwa hata akiweza kuketi.

"Dkt. Edward..." Akaita kwa sauti yake nzito na kukwaruza kiasi, akajikohoza na kujiweka sawa. Kutoka pale chini Edward akamtazama mzee huyu kwa jicho lililololowa damu, lililogubikwa na uchungu usiofichika.

"Huwezi kusitisha kile ninachotaka kufanya," akamwambia, "Umenikosea sana ni lazima uniombe msamaha..."

"Never!" Na serikali ya Tanzania itakutia mkononi tu mtoto wa kahaba we!" Dkt. Minzi akaongea kwa hasira na shida.

"Hah! Hah! Hah! Hah! Hah! Seriakali ya wapi? Tanzania? Ingekuwa inaweza kunizuia, basi ingefanya hilo palepale. Lakini hakuna wanachojua zaidi ya mlipuko tu, na hiyo idara yenu mnayoitegemea mpaka sasa imeambiwa isifanye uchunguzi kwani haiwezi chochote,"

akamaliza kusema na kuvuta hatua kutoka nje, kisha akasimama kama amesahau kitu. Akageuka taratibu kumtazama daktari yule... “Aaaahhhnnn *by the way!* Ngingekuua siku nyingi ila nina kazi na wewe, miezi minne ijayo tutafanya uzinduzi wa hii chanjo na wewe unatakiwa ujibu maswali ya wageni waalikwa yatakayojitokeza baada ya kuona hii dokumentari, sawa?” akamuuliza. Lakini hakujibiwa, akatikisa kichwa na kutazama chini, “Unajua, ni pesa nyingi sana yaani, nitakuwa kama Mungu mdogo hapa duniani,” akatoka na kuubamiza mlango nyuma yake.

* * *

Mwezi mmoja baadae...

Sakata la wizi wa chanjo ya *AIDIOSIS* liliumiza sana vichwa vya wanausalama hasa katika mataifa makubwa. CIA baada ya kurudisha kikosi chake nyumbani mwezi mmoja uliopita, hawakuishia hapo wakaamua kufanya uchunguzi wa kimya kimya kujua nini kinaendelea. Ijapokuwa wakati mwingine uchunguzi wa mtindo huu huchukua muda mrefu kubaini tatizo, wao hawakujali, kwani ilikuwa ni moja ya mbinu zao za mstari wa mbele. Kazi nzima ya uchunguzi ikachukuliwa kutoka mikononi mwa Bwana Brandon na kukabidhiwa kwa mtu mwingine kwa siri sana. Baada ya Brandon kuonekana ameshindwa na *‘Team 2’* yake kugundulika kirahisi, kabrasha lile likafungwa kabisa na kuandikwa *‘Closed’* juu yake. Likafungwa kwenye chumba cha siri kabisa chenye usalama wa hali ya juu zaidi ya benki.

Hii nayo ilikuwa ni moja ya mbinu kwani, mkurugenzi wa idara hiyo nyeti duniani, aliitwa katika Ikulu ya *‘White House’* na kutakiwa kutoa maelezo ya kina juu ya sakata zima. Na agizo alilopewa na bosi wake, yaani Rais wa Marekani ni kuhakikisha chanjo hiyo inapatikana na huyo Dimens anashughulikiwa. Zaidi ya hapo aliambiwa kuwa ni operesheni ya siri hivyo mtu yeyote hata wa ndani ya jengo la *Langley* asijue.

Kufunga kabrasha lile hakukuwa *‘kufunga’* bali ni moja ya mbinu za kichunguzi hasa kumchunguza adui wa ndani kwa maana ilijulikana kuwa kuna *‘mamluki’* ndani yao ambaye anatoa siri kwa Dimens na kufanya operesheni hiyo kuwa ngumu kupita kiasi. Hivyo likafungwa jalada na kuhifadhiwa katika chumba hicho katika mfumo wa kielektroniki. Ndani ya chumba hicho ni mtu mmoja tu mwenye

uwezo wa kuingia. Na ili afike katika sehemu hiyo, angetakiwa kuweka saini yake kwenye chombo maalumu, kikiitambua, angetakiwa kuweka nywila, ikitambulika, angetakiwa aweke kiganja cha mkono wa kulia na kisha macho yake yangetambuliwa kwa mwanga maalum kisha taarifa zote hizo zikikusanywa picha ya mhusika hutokea kwenye kioo maalumu. Hapo mlango ungefunguka. Zaidi ya hapo hakuna mtu mwingine ambaye angeweza kuingia katika chumba hicho.

SURA YA 14

Miezi Miwili Baadae

DAR ES SALAAM

KAMA KAWAIDA ya jiji la Dar es salaam; foleni za magari, jua kali, joto la ajabu, vyote vilijenga umaana wa jina hilo. Siku hii ilikuwa bize sana kwani viongozi wa Nchi za Maziwa Makuu walikuwapo nchini kwa kikao maalum cha maswala ya kijamii. Na swala kubwa lilikuwa ni juu ya ugonjwa mbaya kabisa wa *AIDIOSIS*, ambao ulikuwa ni zaidi ya vita. Viongozi hawa hawakuwahi kuzungumzia hili, lakini kwa sasa iliwabidi, baada ya idadi ya vifo kupanda kwa kasi sana. Hii ilishtua wizara husika za afya katika nchi hizi na ndipo kikao hiki cha marais na watu wa wizara hizo kiliitishwa na kukutana katika jiji hilo. Miongoni mwao, kulikuwapo wajumbe wa Shirika la afya duniani wakisikiliza na kuchangia hoja anuai ambazo zilikuwa zikichagizwa.

Malumbano hayakuwa madogo na muafaka ulikuwa ni ndoto kufikiwa. Hali tete! Siku ya kwanza kikaahirishwa na kuendelea siku iliyofuata. Nayo ikaisha kwa kuweka mikakati ya kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kwani ilionekana wazi kuwa hakuna suluhisho lingine. Siku ya tatu ambayo ilikuwa ni ya mwisho maazimio yakapitishwa, hakukuwa na jipya zaidi ya elimu kwa Waafrika. Wajumbe hawa wa Shirika la afya nao wakachagiza nguvu zao zote na kupiga chapuo wa maana kuwa uelimishaji rika ndiyo dawa pekee. Wakaahidi kusaidia nchi hizi kwa kuleta mashirika zaidi ya misaada ya kutoa elimu hiyo, kuleta mashirika ya kusambaza mipira ya kufanyia ile wanayoiita ‘ngono salama’. Ndani ya kikao hicho, viongozi wetu wakapiga makofi na kushangilia kuwa sasa wamepata suluhisho litalosaidia kupunguza vifo hivyo. Kauli mbiu mbalimbali zikasambazwa huku na kule. Mabango makubwa yakawekwa mabarabarani, makundi ya kijamii yakaanzishwa

na kufadhiliwa pesa nyingi. Lakini pia, mashirika mengi yaliyokuwa chini ya mataifa makubwa yakaingia katika nchi hizi na kuwekeza miradi mingi ya kupambana na ugonjwa huo huku wataalamu wao wakijazana kila kona ya nchi. Hili ndilo walilokuwa wanalisubiri kwa hamu na sasa likatimia.

Baada ya kikao hiki kwisha, huko Langley, Marekani, taarifa zote za kikao zikafika kama zilivyo bila kughoshiwa. Nani kapeleka? Halikuwa swali labda kama ni hoja tu, maana jamaa hawa walikuwa na masikio kila upande.

“Yes!” Ndivyo walivyotamka.

Sasa operesheni ikabadilika, kwa nafasi hii ndipo majasusi wengi wakajipenyeza kama madaktari, wauguzi, sijui wanini wanini sijui. Wakati huu sasa mashirika mengi yaliingiza watu wengi, chini ya haya yote kulikuwa na utafiti mpya uliokuwa ukiendelea kwa siri sana kama maagizo yaliyotolewa miezi mitatu nyuma.

* * *

Baada ya mkutano huo...

Wadau wa Wizara ya Afya walikutana kwa kikao cha utendaji kazi ndani ya Hoteli ya Golden Tulip siku saba baadae. Hawakuwa wengi, bali kama watu ishirini hivi. Miongoni mwao kulikuwa na wajumbe kutoka mikoa mbali mbali ya Tanzania. Waziri wa wizara husika na katibu wake walikuwapo na ndiwo walikuwa waongozaji wa kikao huo.

Katika kikao hiki, ajenda kuu ilikuwa ni kutoa taarifa na maazimio ya mkutano ule wa viongozi wa nchi za maziwa makuu. Taarifa na maafikiano vikasomwa, na wajumbe wakatikisa vichwa kuonesha wameelewa.

“Hivyo msishangae kuona mashirika mbalimbali ya kimataifa yanaingia nchini mwetu, ama kijijini kwako au wilayani. Maazimio makubwa ndiyo haya, kuruhusu mashirika ya misaada ya kibinadamu kuja ama kutoa elimu au kusaidia katika hili na lile ili kuimarisha vita hii dhidi ya gonjwa hili hatari la *AIDIOSIS*. Licha ya hiyo, serikali imepokea msaada mkubwa wa fedha za kigeni kutoka Umoja wa Mataifa na nchi wahisani ili kuzitumia katika vita hii. Baada ya bodi ya wizara kukaa tumeona kuwa pesa hizi zitagawanywa katika wilaya na halmashauri zote nchini ili kufadhili vikundi vya kijamii vitakavyokuwa tayari kupambana na ugonjwa huu kwa kuendesha semina, warsha, makongamano na matamasha mbalimbali yenye kuhamasisha vita hii.

Kwa hiyo, ndugu wakurugenzi mlijue hilo na mlifanye kwa uadilifu...”

Baada ya katibu wa wizara kusema hayo kulifuata kipindi cha maswali na majibu ili kila mtu aweze kuelewa kinaganaga. Na mwisho makasha makubwamakubwa yaliyosheheni *condom* yakagawiwa ili kusambazwa katika halmashauri na kuhamasisha watu kutumia ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huu.

Miongoni mwa watu waliokuwa wakihudumu ndani ya hoteli hii, hususani katika ukumbi huu kwa wajumbe wa mkutano, Gina alikuwa mmoja wao. Mara kwa mara alikuwa akiingia ndani ya ukumbi huu na kusikia kile kinachozungumzwa. Na katika pitapita ya hapa na pale kusambaza maji kwa wakubwa hawa, alifanikiwa kupachika kinasa sauti chake nyuma ya pazia moja la dirisha. Kifaa hicho kiliweza kusafirisha mazungumzo hayo mpaka katika gari moja lililoegeshwa nje ya hoteli hiyo.

* * *

Volkswagen Transporter, lililofungwa bodi lote na kuruhusu madirisha matatu tu kuwa wazi, yaani la mbele lenye kioo cha kuonea dereva, na ya pembeni upande huu na ule kwenye chumba cha dereva. Gari hili la rangi ya njano lilikuwa na ngazi nne za *aluminium* juu ya bodi lake na maandishi makubwa yaliyolipamba ubavuni *TANGANYIKA TELEPHONE COMPANY*. Hakuna aliyelitilia shaka kwani kampuni hiyo ya serikali ilijulikana sana nchini. Nyuma ya usukani wa gari hilo aliketi kijana mmoja mwenye mwili wa wastani lakini ukimwangelia tu mkono wake ulioning'inizwa nje utajua ni wa mwanamazoezi kwa jinsi misuli yake ilivyojaa vyema. Mtu huyu hakuwa mwingine bali Scoba. Nyuma ya usukani huu alikuwa amesinzia kabisa na kumezwa na usingizi wa kina lakini alikuwa kazini kwani milango yake ya fahamu ilikuwa wazi kabisa na kudaka hisia zote. Alijua kuwa kuna mtu anapita, au anasogelea gari na kila kitu. Hakuwa amelala haswa ila ni moja ya mbinu za kazi yake.

Ndani ya bodi la gari hilo ambapo ungeliona kwa nje ungejua kuwa kuna nyaya na zana nyingine za kazi za watu wa simu, au ungefikiri kuwa kuna vikombe vipya na vya zamani vya simu kwa ajili ya kubadilisha hapa na pale. Haikuwa hivyo. Badala yake kulikuwa na kompyuta mbili na mitambo kadhaa ya kunasa sauti za mawasiliano yoyote yapitayo eneo hilo, iwe simu, TV, redio n.k

Chiba alikuwa hapo ndani kimya, akifuatilia kikao chote kwa kutumia

kinasa sauti kilichowekwa na Gina ndani ya chumba kile cha mkutano. Katika mashine nyingine alikuwa akinasa simu zinazopigwa katika eneo hilo, au jumbe fupi za maandishi za simu zinazorushwa na kupita kwa kutumia mnara wa jirani katika eneo hilo. Hapo masikio na hisia zake zilikuwa zikifanya kazi nyingi kwa wakati mmoja. Kwake haikuwa tatizo sana tofauti na kama ungekuwa wewe. Alisikia hoja za mkutano pia alisikia simu zinazobadilishana katika mashine yake kwa wakati huohuo. Uwezo aliokuwa nao Chiba katika hili ni binadamu wachache sana ambao wanao. Akiwa ametulia kimya kabisa akichambua mambo hayo akashtuliwa na simu moja wapo iliyokuwa ikiongea kwa Kireno. Mwanzo aliipuuza kwa kuwa pia hakuijua lugha hiyo sawasawa, lakini baadae akaamua kuiunganisha na kompyuta yake na kuitia sauti hiyo katika softiwea ambayo inauwezo wa kupokea sauti na kuitafsiri kwa maandishi kwa lugha uitakayo. Simu hii ilimfanya Chiba kuacha kila kitu na kuelekeza masikio yake huko.

"...bado wapo kikaoni..." mtu mmoja akasikika.

"...Hakikisha kama kikao hicho kina madhara kwetu au la!" mwingine akasikika akimhimiza yule wa kwanza.

"...Yes Sir! Nitakupi mrejesho..."

"...Kwanza umeshajua nani na nani wameingia humo ndani? Kama kuna yoyote mwenye madhara kwetu unambie..." aliyeitwa 'Sir' akaonesha wasiwasi.

"Hakuna mtu wa hatari, hawa ni wakurugenzi wa balmashauri na wilaya tu, zaidi sana ni katibu wa wizara na waziri mwenye dhamana. Hakuna nyoka isipokuwa mijusi tu ambayo ni kawaida yao kuvapo..." yule mjumbe akajibu.

"Ok kijana, nitakupigia wakati mwingine, kama kuna lolote hakikisha unanijua, do you read me?"

"Yes, Sir"

"Over and out!"

Chiba akashusha pumzi ndefu na kuigeukia kompyuta yake nyingine aliyoiacha ikirekodi kinachoendelea na kuikuta ikiendelea kufanya hivyo.

Hawa jamaa wamejipanga sana, ina maana wanajua kabisa kila kinachoendelea! Ni akina nani hawa? Tena inaonekana ni kundi kutoka nje, kama si Ureno basi ni kati ya nchi zinazoongea Kireno. Wanatujua bata kwa sura si ajabu, hapa kazi ipo. Lakini hawatuwezi, mbona wameshindwa kumtambua Gina kama ni mwanasalama au nyoka kama wanavyoita nao? Shit! Chiba akajiwazia kisha akajiegemeza kwenye kiti chake kilichompa mneso wa kutosha ndani

ya gari lile. Baada ya kuwaza machache akajivuta mpaka kwenye ile kompyuta yake inayokamata mawimbi ya simu. Akaingiza nywila zake za siri, akafanikiwa kuvunja kilindo cha mtandao wa kampuni husika ya simu kisha akatafuta kujua watu hawa wawili walikuwa wakiongea kutoka wapi na wapi. Haikumpa shida, kwa kuwa daima ni kazi yake.

Sekunde kadhaa zikampa majibu, *subject 1* alikuwa Mtwara na huyu ndiye aliyekuwa akiitwa ‘*Sir*’ katika mwito huo wa simu. *Subject 2*, huyu alionekana hayuko mbali sana na eneo la mkutano, lakini wapi hasa? Hii ikawa kazi nyingine ya kuchunguza, kwanza hujui kavaaje au ana muonekano gani. Chiba akahisi akili yake ikifa ganzi, akapachika kidole chake kwenye *earpiece* yake na kumpa ujumbe Gina.

“*Alfa! alfa!*”

“*Omega! Omega!*”

Hii ilikuwa ishara yao ya mawasiliano waliyokubaliana. Hawakutakiwa kutajana majina ili kujenga usalama kati yao kama kuna mtu anadukua mawasiliano hayo.

“Kuna kondoo anatawanya majani nje ya zizi, sijajua kama yupo zizini au nje yake, lakini si mmoja wa kondoo wetu. Ninajua kila mnyama aliyekuwa zizini kwa majina na vyeo...”

“*Copy!*”

“Ukimwona mtie kamba achinjwe!”

“Ujumbe umefika na unashughulikiwa...”

“*Ova!*”

Alipomaliza mazungumzo hayo na Gina akatulia kimya kitini akiangalia mwenendo wa kila kitu. Mara hii akawasha kompyuta nyingine na kuunganisha na camera ndogo zilizofungwa kwa siri katika taa za mbele na nyuma ya gari hilo, pia kwenye viakisi mwanga vya pembeni, upande huu na ule. Kutoka katika kamera hizo aliweza kuona pande nne bila shida, akatumia hizo kuchunguza kama kuna mtu atakayemtilia shaka kati ya wapita njia au wafanya biashara ndogondogo ukiachilia mbali madereva taksi.

* * *

Johnson Kasalu akaegsha gari lake nje tu ya hoteli hiyo. Akateremka na kuufunga mlango kwa kusukuma kwa mguu wake wa kulia. Akaweka mikono yake karibu na shingo na kurekebisha tai, ili impe mwonekano sahihi autakao. Alikuwa mpana wa mwili, mrefu kiasi, mweusi na mwenye ndevu zilizozunguka midomo yake. Upana wa kifua chake,

ulifanya ajulikane kuwa ni mtu anayependa mazoezi, hasa ya kunyanyua vitu vizito. Kijana huyu, mfanyabiashara maarufu, wengi walimjua hivyo, hasa wafanyabiashara wenzake. Lakini nyuma yake alikuwa *undecorver agent* kutoka CIA. Mtanzania wa kuzaliwa aliyekulia Marekani na kupata elimu yake yote huko, huku akipitisha maisha yake kwenye vitongoji tata vya jimbo la Los Angeles.

Akavuta hatua kuelekea katika hoteli ile huku mkononi akiwa na *briefcase* ndogo. Kabla hajamaliza kupita katika ujia ule aingie hotelini, ukasikika mlio wa risasi iliyopigwa hewani. Nukta hiyohiyo, gari moja aina ya Range Rover likasota kwa breki na kusimama jirani kabisa na miguu yake. Watu wawili wakashuka na kumdaka Johnson. Bila kutegemea. Johnson alimtandika ngumi nzito mmoja wao, akaenda chini. Kisha kwa kutumia ile *briefcase* akampiga mwingine kichwani na kumpotezea malengo kisha akamshindilia sumbwi la tumbo, naye akajikuta anasahau kila kitu na kukamata tumbo. Teke maridhawa la mtindo wa tik tak likatua usoni mwa yule aliyejishika tumbo. Likamwinua na kumtupa kando mzima mzima huku Kasalu akitua ardhini kwa miguu yake miwili.

Polisi waliokuwa nje ya hoteli ile wakawa tayari kutoa msaada lakini kilichoshuhudiwa ni wote wawili wakipaishwa hewani na kutupwa kwenye bustani ya maua. Sasa kelele zikaanza kusikika. Kelele hizo zikamtoa Johnson umakini, akajikuta akipigwa kwa kitako cha bunduki kisogoni kwake na kupoteza nguvu na fahamu. Ilikuwa ni sekunde kama ishirini na tano hivi kwa tukio lile kumalizika na Johnson Kasalu akachukuliwa katika lile gari.

Tukio lile liliwaacha askari polisi wawili wakiwa wamelala bila uhai juu ya maua huku bunduki zao zikiwa huku na huko. Raia wema wakasogea taratibu kutoa msaada unaowezekana, lakini badala yake wenye mioyo myepesi waliangusha vilio.

Ndani ya ukumbi, mlio mmoja tu wa risasi ulisikika, tena kwa mbali kiasi kwamba hakuna hata aliyeshuka. Kikao kikaendelea. Gina akiwa katika sehemu maalumu iliyokuwa na vinywaji na vitafunwa ambavyo vingetakiwa kupelekwa kwa wageni hao, aliisikia ile risasi kwa uwazi kabisa. Akageuka na kuvuta pazia pembeni kisha akashuhudia kila kilichoendelea huku akichukua picha ya matukio hayo kwa simu yake. Kwa kuwa yeye alikuwa na kazi nyingine, hakulitilia maanani hilo. Lilipotulia naye akaliacha.

Miongoni mwa watu waliokuwa wakishangaa maiti za wale askari,

alikuwapo kichaa mmoja, naye akitupia macho huku akiongea vitu visivyoeleweka.

“Oooh, *yes! Yes!* Wamekufa hawa, eeeee wamekufa hawa, wamekufa kabisa!” alijisemea huku akitema mate huku na kule na kuwafanya watu wawe na kinyaa na kumpisha.

“Hakuna! Hakuna! Aaaaa hakuna kabisa ni hawa hawa tu, wamekufa hawa.... Bado bado mmmm hapana wamekufa,” aliendelea kuongea, kisha akajivuta na kukata ua moja la uwaridi na kulirusha juu ya zile maiti. Akatembea taratibu na manguo yake machafu huku akiwa amebeba makolokolo mengi. Alikuwa ananuka, nywele chafu zilizoshikana shikana huku na huko, viatu visivyotamanika. Kichaa huyu alikuwa amejifunga matambara mengi katika mwili wake.

Baada ya kila kitu kutulia, Scoba akateremka taratibu na kuvuka barabara mpaka upande ule ulikotokea tukio lile. Akapishana na yule kichaa, kisha akafika kwenye kundi la watu lililokuwa likishangaa maiti za wale askari.

“Samahani, nini kimetokea hapa?” akamwuliza mmoja wa akina mama waliokuwa wametoka eneo hilo punde tu.

“Majambazi mwanangu, yamemteka baba wa watu sijui! Na wanaomjua wanasema kuwa yule baba ni mfanyabiashara, sasa inawezekana katika mkoba wake kulikuwa na pesa, yaani hata sijui... mi nasikitikia hao vijana askari tu, yaani bado wadooogo....” akasema.

“Aisee nchi hii imeharibika, watu hatuogopi kuuana!” Scoba akasema huku akivuta hatua, na wakati huo huo gari la polisi liliingia eneo hilo na kutawanya watu wakiwataka wake mbali. Scoba alikuwa mmoja wa waliosogezwa mbali. Akaangaza macho yake huku na huko hakuna aliyemhisi kuhusika, akaitazama saa yake tayari ilikuwa ni saa tano na nusu asubuhi. Akaamua kurudi garini, alipoketi kitini nyuma ya usukani, kidirisha kidogo mgongoni mwake kikafunguka.

“Vipi Scoba!” Chiba akauliza.

“Ah, watu washafanya yao kaka,” akajibu.

“Umechelewa Scoba, hapa kuna jambo zito nalinusa, siyo majambazi wale! Kuna utata...”

“Unasema...!”

“Umemuona yule kichaa...?”

“Ndiyo! Na nimepishana naye, anaropoka ropoka tu mambo yasiyoeleweka!” Scoba akajibu.

“Namhisi ndiye *master plan* wa hii *movie*...”

“Sure?”

“Sure! Mpe jicho, usimwache, huku naona kikao kinakwisha sasa,” Chiba akamwambia Scoba kisha akafunga kile kidirisha.

Scoba akaangaza macho yake huku na kule, hasimwone yule kichaa.

Kaenda napi? Akajiuliza. Hapo, akateremka kwenye gari na kuvuta koti lake ambalo nyuma lina maandishi T.T.C. Akatupia kichwani kofia yake ya ‘Mungu usinione’ na kuingia barabarani kumtazama yule kichaa. Chiba tayari alikwishatuma taarifa ya tukio hilo kwa TSA 1 ambaye aikuwa katulia Ofisi Ndogo pamoja na Madam S.

* * *

Mkutano katika hoteli ile ulimalizika. Wajumbe wakatoka nje na kupiga picha ya pamoja kisha kila mmoja akachukua usafiri wake tayari kurudi mapumzikoni au katika sehemu zao za kazi. Mheshimiwa waziri, naye, alisindikizwa na mlinzi wake mpaka kwenye gari lake na kuondoka. Muda wote huo, Gina alikuwa katulia kimya kwenye chumba kilichokuwa na vinywaji na vitafunwa huku akiwa kavalia sare maalumu ya wahudumu wa hoteli hiyo. Alipohakikisha kuwa ukumbi upo tupu, akaingia na kuchomoa kile kinasa sauti pale katika pazia na kukitia mfukoni, kisha akaingia chooni na kuvua zile sare, akatoka akiwa mtu mwingine kabisa.

Kwa haraka akafika nje na kuangaza angaza kana kwamba kuna kitu alichokuwa akitafuta, lakini haikuwa hivyo. Dakika chache tu, gari moja, dogo, jeusi, likasimama mbele yake, akafungua mlango na kujitoma ndani. Lile gari likaondoka na kuiacha hoteli ile.

“*Evacuate area!*” sauti ya Madam S ikasikika katika vyombo vya kunasa mawasiliano. Scoba akaamua kuacha kumfuatilia yule kichaa akarudi garini. Tayari Chiba alikuwa keshakamilisha kazi yake. Scoba akaondoa gari kutoka pale na kupotelea mjini.

“*Ofisi Ndogo tafadhali,*” sauti ikasikika tena na uelekeo ukawa huo. Dakika kama ishirini baadae, Chiba na Scoba wikalicha lile gari katika maegesho ya Wizara ya Mambo ya Ndani kisha wakachukua gari dogo na kufika mara moja katika miadi yao na H.O.T yaani *Head Of TSA*.

Timu nzima ilikutana katika ofisi hiyo mchana wa siku hiyo, na kikao kifupi kikaendelea kati yao, tungeweza kukiita kikao cha siri.

“Haya, najua mlikuwa na kazi nyingi siku hizi na kila mmoja anaona nchi inavyokwenda, kwanza nataka kujua wazi nini mmepata katika tafutishi za leo? Maana nimesikia kuna mauaji yamefanyika huko

Golden Tulip na mfanya biashara mmoja ametekwa akiwa tayari kuingia hotelini... ni ujambazi? Nauliza kwa sababu tukio limetokea katika eneo ambalo tulikuwamo hivyo hatuna budi kujaribu kuona kama mambo haya yana uhusiano,” Madam S aliwaambia vijana wake.

“Bila shaka, kwanza naweza kuwaonesha jinsi tukio hili lilivyotokea kisha tukaanza kujadili...”

“Sawa!” wote wakaitikia kabla Chiba hajamaliza kusema. Akachukua kadi mmweko na kuipachika katika kompyuta yake kisha akaunganisha na luninga kubwa iliyofungwa ndani ya ofisi hiyo na kuiruhusu ile picha iendelee. Ijapokuwa haikuonekana vizuri sana kutokana na uwezo wa kamera, lakini iliweza kueleweka. Iliwachukuwa kama dakika tano hivi kuweza kuelewa tukio lile maana walikuwa wakirudisharudisha nyuma.

“Ilikuwa hivyo!” Chiba akawaambia na kuzima ile runinga.

“Huu siyo ujambazi! Kwanza hebu tuchunguze huyu mtu ni nani, tukishamjua tunaweza kujua kama ni ujambazi au la!” Amata akasema na wote wakaitikia isipokuwa Dkt. Jasmin.

“Kama wamesema ni mfanyabiashara, kwa nini isiwe ujambazi?” Jasmin akauliza.

“Una uhakika gani kama ni mfanyabiashara? Ili kujihakikishia ni lazima tumchunguze tujue huyu ni nani! Ngojeni niwaambie kitu, huyu mtu katekwa ee.. kwa nini katekwa? Labda alikuwa anakwenda kumdhuru waziri, kwa mfano. Na sisi si wageni katika swala la ulinzi wa viongozi, vipi kama *invisibles* waligundua njama hii na kutuma kikosi cha siri kumnasa? Kwenye *briefcase* yake kulikuwa na nini?” Amata akazungumza na Madam S akaonekana kutikisa kichwa kuwa ameelewa vema asemacho.

“Sawa kamanda! Tazama huyu mtu....” Chiba akasema tena na kuwasha ile runinga. Mara hii walimwona yule kichaa akiwa amekaa sehemu na mara baada ya tukio alisimama na kuelekea kule walikouawa wale polisi.

“Huyu ni kichaa, ameketi hapa, ng’ambo ya barabara kwa muda mrefu sana. Baada ya tukio anakwenda kutazama nini kimetokea... mtazame... Hakurudi pale, akatokea njia hii huku na hata nilipomtuma Scoba kumwalia hakumwona tena. Kapotelea wapi?” Chiba akaeleza na kuuliza.

“Yeah! Nimekutana na huyu kichaa pale kwenye tukio, alikuwa anaongea mambo ambayo sikuyaelewa, ‘Oooh, yes! Yes! Wamekufa hawa, eeeee wamekufa hawa, wamekufa kabisa ... Hakuna!! Hakuna! Aaaaa

hakuna kabisa ni hawa hawa tu, wamekufa hawa.... Bado bado mmmm hapana wamekufa,’ mi sikuelewa haswa maana ya maneno haya, lakini nilihisi kuwa anafanya *double talkin* yaani kuna anayeongea naye na pia kujifanya anaongea ovyo,” Scoba akaeleza.

Ukimya ukatawala, kila mtu akiwa anatafakari... “Kuna jambo, tunaweza kuchambua hili kwa maneno haya...” Amata akasema kisha akachukua karatasi na kuandika yale maneno ambayo Scoba aliyasema, akaiweka ile karatasi katikati. Madam S akaichukua na kuisoma kwa makini kisha akarudisha macho yake kwa vijana wake.

“Huyu hakuwa kichaa asee! Jinsi haya maneno yanavyokuja kichwani mwangu, alikuwa anawasiliana na watu au mtu fulani akimpa uhakika kuwa hao askari wamekufa, tazama haya maneno yake. ‘*Oooh, yes! Yes!* Wamekufa hawa, eeeee wamekufa hawa, wamekufa kabisa...’ Alikuwa anamhakikishia hilo, na haya ya hapa anasema, ‘Hakuna! Hakuna! Aaaaa hakuna kabisa ni hawa hawa tu’. Maana yake nini? Yaani, hakukuwa na mtu mwingine wa kuwaletea shida zaidi ya hawa hawa tu...” Madam akasema.

“Uko sawa Madam! Kuna simu niliinasa na nilipoifuatilia nimegundua kuwa mpigaji aliyepewa jina la ‘*Sir*’ alikuwa Mtwara na huyu mwingine alikuwa eneo la hoteli, je atakuwa ni huyu kichaa?” Chiba akamkata kauli Madam S na kufanya wote wamgeukie.

“Kazi imekwisha!” Amata akasema. Kisha akainuka na kuliendea jokofu, akatoa *Coke* baridi na kurudi mezani, huku wenzake wakibakia wamemtumbulia macho. Maana hawakujua nini anataka kufanya. Aliporudi, akaketi kitini pake. Baada ya kumeza fundu moja, akaendelea “...kutokana na maneno ya Madam, juu ya hayo aliyoyasema Scoba, na hii simu unayoisema Chiba, kazi imekwisha. ‘*Sir*’ yupo Mtwara, nami nilikuwa Mtwara kabla ya kurudishwa kibabe na Madam, nani huyo Sir? Ni Toress Alexis Kazumari? Au kuna mwingine? Na kama aliyekuwa anaongea naye alikuwa hapo hapo mitaa ya hotelini, hakika ni huyu kichaa,” Kamanda akasema kisha akapiga fundu jingine la maana na kuitua chupa mezani.

Madam S akaandika jina lile, Toress Alexis Kazumari, katika kijitabu chake. Kisha Chiba akaeleza nini simu ile ilikuwa ikieleza. Hapo Madam akachukua mambo muhimu na kuyaweka katika kitabu chake kilekile, kisha akakifunga na kuwatazama tena.

“Hatuwezi kuchezeza namna hii! Ina maana hapa kuna kundi la kigaidi, na kwa nini liendeshe misheni zake huku tunalitazama?

Leo wameuawa askari wawili, kesho je? Wanatujua kiasi gani hawa jamaa?” Madam alionekana kukunja sura kama kawaida yake mambo yakishaanza kumuumiza kichwa chake.

“Kama alivyosema Amata, nahitaji utambuzi wa kujua mtu huyu aliyetekwa ni nani?” Madam S akamaliza na kusimama. Kaeni mguu sawa nitawaita muda si mrefu ila kwa sasa, nahitaji mfanyie kazi mambo mawili makubwa; moja, mumtambue huyu mtu ni nani, yaani aliyetekwa, na pia nahitaji mtambue ile maiti kule Muhimbili ni ya nani? Kuna kitu nakinusa, tuonane baadae,” akachukua koti lake na kulivaa kisha akawaaga na kuondoka zake.

* * *

Ndani ya chumba cha maiti katika hospitali ya Muhimbili, Dkt. Jasmin alikuwa amesimama na ule mwili uliungua ukiwa umelala juu ya kitanda maalumu cha uchunguzi. Upande wa pili kulikuwa na Scoba aliyekuwa akimsaidia kwa hiki na kile huku kila wakati akikimbilia chooni maana alikuwa akihisi kitapitapi.

“Vipi?” Scoba akauliza baada ya kumwona Jasmine yupo kimya sana.

“Marehemu ni mwanamke!” akajibu.

“Sijauliza jinsi ya marehemu, nimekuuliza wewe ‘vipi?’” akarudia kwa msisitizo.

“Kuna kitu hapa nimekipata sikielewi nafikiri ni utambulisho wa huyu marehemu, ni kitambulisho inaonekana alikiweka mfukoni kwenye...”

“Kitu gani?” Scoba akauliza na kuzunguka upande wa pili, akashika kwa mikono yake kitu kama kibati kigumu chenye umbo lisiloweza kueleweka... “Kihifadhi!” akamwambia Jasmin.

“Yeah, nimechukua sampuli kadhaa kwa ajili ya kupima DNA kisha tutamtambua huyu ni nani!” akamwambia Scoba kisha akaandika kwenye faili lake mambo kadhaa aliyoyapata katika tafutishi hiyo akalifunga na kuukabidhi ule mwili kwa mhusika wa sehemu hiyo kisha wao wakaondoka zao.

* * *

Katika chumba maalumu cha utambuzi ndani ya ‘*Safe House*’ yaani Shamba, Chiba, Amata na Gina walikuwa wametingwa na kompyuta na vikorokoro vingine vingi wakijaribu kusikiliza maelezo kutoka kwa

Chiba. Mbele yao kwenye kioo kikubwa kulikuwa na picha kama kumi hivi zikionesha sura za watu tafauti ambao wanashahabiana kwa mengi.

“Kwa hiyo huyu sasa ni mmoja wa hawa!” Chiba akawaambia.

“Anhaa kwa hiyo inabidi tumchambue mmoja baada ya mwingine kati ya hawa?” Amata akatupa swali.

“Ndiyo! Tazama walivyofanana, na wote ni Waafrika! Huyu kumpata si shida kwanza ni kujua watu hawa wanatoka nchi zipi na kama kuna anayetokea Tanzania basi tunaanza na huyo kutafuta habari zake,” Chiba akaeleza.

“Na kama hayuko anayetokea Tanzania je?”

“Hapo ndo kazi itakuwa ngumu!”

Chiba akaendelea kupapasa zile picha kwa kompyuta yake na kuiweka moja baada ya nyingine kuweza kutafuta maelezo zaidi. Picha ya kwanza ikaonesha kuwa mtu huyo ni Mwafrika ya Kusini, tena mwandishi wa habari wa gazeti la *The Sun Shine*. Mtu wa pili ni raia wa Ghana na wengine wengi kutoka sehemu tafauti na watatu kati yao hakukuwa na maelezo hata kidogo achana na wale ambao tayari *status* zao zilisoma ‘*deceased*’ yaani wameshakufa. Kati yao mtu wa nane kumchunguza alionekana ni raia wa Marekani.

“Si nimekwambia!” Amata akasema.

“Kuwa anaweza kuwa si Mtanzania?”

“Ndiyo, si Mtanzania, hebu tazama jina lake” Amata akamwambia Chiba.

“Hakuna Mmarekani anyeitwa Kasalu!” Gina akadakia kutoka alipoketi, akasimama na kusogea jirani.

“We umeona wapi jina hilo?” Chiba akauliza.

“Wakati unazungusha kutafuta maelezo yamepita majina kama sita hivi yakimshabihi huyo mtu na mojawapo ni Kasalu Johnson. Sasa mi naona tulichukue hili la Kasalu Johnson na kulifanyia kazi hapa Tanzania kwa kuwa ni la Kisukuma hilo,” Gina akasema. Kamanda Amata akamkazia jicho mwanamke huyo kisha akatikisa kichwa.

“Umekomaa sasa, na umejifunza mengi huko ulikokuwa!” akamwambia.

“Kidogo tu, ila yanatosha sana katika utambuzi. Moja ya majaribio yangu ilikuwa ni kutambua maiti iliyoharibika miezi sita nyuma, asee hizi si kazi hizi!” Gina alilalama na kutoka nje ya chumba hicho.

“Kasalu Johnson!” Amata akajisemea.

“Vipi?” Chiba akauliza.

“Tuanze na hilo!” Amata akajibu. Chiba akaichukua ile picha na lile jina kisha akaingiza kwenye mtandao wa watu hatari Afrika, hakumuona, akahamisha na kuingiza kwenye mtandao wa kiulimwengu haukumtambua, lakini alipotafuta kwenye watu maarufu, haikumpa muda. Wakampata.

“Johnson Kasalu, Mtanzania aliyesoma na kukulia Marekani kabla hajachukua uraia wa huko...” Kamanda Amata akasoma akamaliza, akamtazama Chiba na wakati huo Gina tayari alikuwa amerudi.

“Ina maana alikuwa hapa nchini? Maana inaonekana ofisi zake ziko hapa Jijini ila ana matawi huko USA, Qatar na China. Basi na tutafute ofisi zake hapa ziko wapi, twende tukatembelee,” Amata akapendekeza.

“Wazo zuri!” Gina akadakia. Chiba akaendelea na kazi yake na baada ya dakika moja tu akaja na majibu ya wapi mtu huyo anaweza kupatikana.

“*J & K Group of Company, NIC building floor* ya sita,” Chiba akasema kisha akamgeukia Amata.

“Nimekupata, inabidi tuwe wageni wake siku ya leo,” Amata akasema mara baada ya kutikisa kichwa chake.

“Sawa, sasa wewe na Gina mwende, mimi nitabaki hapa kwa kuwa bado kuna kazi za kufanya za utambuzi,” Chiba akasema. Gina akatabasamu.

* * *

Majira kama ya saa kumi hivi, Amata akaegesha gari nje ya jengo la Kitega Uchumi. Akiwa anafuatwa nyuma na Gina. Akaweka koti lake vizuri na kuingia katika jengo hilo. Kidole chake cha kati kikabonyeza kitufe namba sita kisha ile lifti ikapanda juu. Gina hakuingia, badala yake akatumia ngazi kuifikia ghorofa ile.

‘J & K’, maandishi yaliyobandikwa kwenye mlango wa kioo yalimkaribisha Amata. Akasukuma mlango na kuingia ndani. Moja kwa moja akajikaribisha kiti kilichokuwa mbele tu ya mwanadada mrembo.

“Karibu sana nikusaidie nini?” sauti nyororo ya msichana huyo ikayatekenya masikio yake.

“Naitwa Mr. Spark! Mkurugenzi wa kampuni ya *AGI Investment*. Nina shida na Bwana Kasalu...” akasema huku akijiweka vema kitini.

Yule mwanadada akashusha pumzi na kuketi sawa kitini kabla ya kumjibu mgeni wake huyo.

“Bwana Kasalu ametoka tangu majira ya saa tano hivi, hajarejea hadi sasa,” akamjibu. Amata akatulia kimya kisha akatupa swali lingine.

“Kwa kuwa nina shida naye nyeti na ya kiofisi, unaweza kunielekeza nyumbani kwake?”

“Hapana, kwa kweli hata sijui ni wapi anaishi mtu huyu,” yule mwanadada akajibu. Amata akatulia kimya huku akili yake ikizunguka huku na kule.

Kuna umuhimu wa black bag job kufanyika katika ofisi hii ! Akawaza huku akinyanyuka, “Asante! Sijui unaitwa nani mrembo?”

“Ziada!” akajibu kisha wakaagana na mgeni wake. Amata akatoka nje ya ofisi ile. Gina aliyekuwa kajibanza kandoni tu mwa mlango alimwona ‘kaka’ yake huyo akitoka na kusimama. Kisha akarudi kuchukua ngazi za kushuka chini huku Gina mara hii akiingia kwenye lifti. Dakika tatu baadaye, wakawa pamoja ndani ya gari.

“Vipi?” Gina akauliza.

“Twende Golden Tulip, hapa hayupo tangu saa tano asubuhi na inaonekana hata katibu wake hajui bosi wake yuko wapi,” Amata akamwambia Gina huku akiingiza gari barabarani na kutimua mbio.

HOTELI YA GOLDEN TULIP

Muda huo wa saa kumi na moja, utulivu ulikuwa umerejea katika hoteli ile, biashara iliendelea kama kawaida kana kwamba saa kadhaa zilizopita hakukuwa na patashika iliyotokea eneo hilo. Amata akaegsha gari na wote wawili wakateremka.

“Gina!” akaita.

“Bee!” usiondoke hapa. Kaa garini, kwa lolote, nipe *signal*. Kisha yeye akaingia ndani ya hoteli ile, akapita mapokezi na kuingia kwenye ujia mrefu huku akikagua mlango baada ya mlango. ‘SECURITY’. Maandishi haya yalimfanya atulie kwa sekunde kadhaa. Kisha akakamata kitasa na kukinyonga. Mlango ukafunguka. Ndani hakuna mtu. Akaingia na kuurudishia nyuma yake huku akiizungusha funguo aliyokuta mlangoni, upande wa ndani. Chumba hakikuwa kikubwa, na kile alichokihitaji ndicho alichokikuta. Luninga moja kubwa yenye vichumba kama sita hivi ndani yake na kila kimoja kilikuwa kikionesha picha ya eneo fulani la nje ya hoteli hiyo.

Kamera namba sita ndiyo iliyokuwa ikionesha picha za nje ya mlango mkubwa na maegesho. Akabonya vitufe fulani kwenye chombo cha kuongoza kamera hiyo na kuirudisha nyuma mpaka saa tano na kufika wakati wa tukio lile la utekaji.

‘Lexus jeusi liliwekwa maegeshoni. Kijana mrefu mwenye tambo la kimazoezi aliteremka na kuelekea katika mlango mkubwa wa hoteli hiyo. Katikati ya barabara, gari jingine linakuja kasi na watu wanashuka kwa haraka na kuanza mshikemshike lakini wanamzidi nguvu na kufanikiwa kuondoka naye.’ Amata akameza mate.

Kwa nini hii kamera ilikuwa inafuata nyendo za mtu huyu tangu kushuka kwenye gari mpaka anatekwa? Akajiuliza. Alipotazama kwenye kompyuta ndogo iliyo pembeni tu akagundua kuwa bado ilikuwa ikirekodi matukio ya siku hiyo, hivyo hakupenda kuisumbua. Akatazama tena saa ya tukio lile. Saa 5:26 asubuhi. Akaweka kichwani saa hiyo kisha taratibu akafungua mlango na kutoka katika kile chumba. Mara simu yake ikaanza kufurukuta mfukoni, akaichomoa na kutazama kwenye kioo. Gina! akaikata. Kwa mwendo wa haraka akatoka na kupita mapokezi, akatoka nje. Simu yake ikatikisika tena mfukoni, akaitoa na kuiweka sikioni.

“Kushoto kwako!” Sauti ya Gina ikasikika. Kwa tahadhari, Amata akageuka akijua labda kuna hatari. Haikuwa hivyo, badala yake akamwona mtu mmoja mchafu, aliyebeba makorokoro mengi akikatisha barabara bila kujali usalama wake. Akafikiri mbinu ya kumkamata, akakuta ni ngumu kwa sababu watu bado walikuwepo eneo hilo. Akasukuti kwa jozi la sekunde huku akitembea na jicho lake likiwa kwa yule kichaa. Akapata wazo, akawahi gari lake na kuingia, akawasha na kurudi nyuma kwa kasi, akaingia barabarani kinyumenyume, hakusimama mpaka aliposikia kishindo.

“Amata umegonga!” Gina akapiga kelele.

“Makusudi!” akajibu huku akiteremka kutokea upande wake.

“Umeuwaaaa! Wewe usikimbie!” watu wakapiga kelele wakati Kamanda tayari keshampakia kichaa yule ndani ya buti na kufunga mlango wa nyuma, akaingia garini na kuondoka kwa kasi.

Mwendo ule wa kasi ukamfikisha katika kituo cha polisi cha Surrender, akakata kushoto na kuegesha gari mbele ya kituo hicho. Askari watatu waliokuwa wameketi chini ya mwarobaini wakainuka na kuliendea gari lile. Akawaonesha kitambulisho na kuwapa maagizo kumshusha huyo mtu haraka. Wale vijana wakafanya hivyo na muda mfupi tu yule kichaa akafikishwa kwa kuburuzwa katika chumba kidogo na kubwagwa chini huku damu zikimchuruzika katika maeneo ya kichwani ambayo aliumia mara alipoanguka.

“Wamenikamata! Wamenikamata! Wamenikamata! Mi si mwalifu jamani, nimeumia! Nimeumia!” Yule kichaa akawa akiongea maneno

mfululizo.

“Mvueni nguo!” akawaamuru wale askari, nao wakaanza kazi ile mara moja.

“Vipi? Mbona mmeleta kichaa, inakuwaje?” Mkuu wa kituo akaingia ghafla huku akifoka, Amata akamtazama tu kisha akamjibu.

“Niitie Inspekta Simbeye haraka, huyu ni mtu wake!” akamwambia. Yule mkuu akatulia kwanza na kumtazama Amata vizuri. Akaingiwa na hofu ya nani anayejiadini kumwita Simbeye. Askari, wakuu wa vituo, waliujua ukuu wa Inspekta huyo. Akatoka na kurudi ofisini. Yule kichaa, sasa alikuwa uchi wa mnyama, amejikunyata akiwa kimya.

“Endelea kuongea, nakusikiliza,” Amata akamwambia, “...Unajifanya kichaa, siyo? Utaniambia leo Johnson Kasalu yuko wapi!” akaongeza kisha akaziendea nguo zile chafu, ndipo aliposhangaa kukuta ndani ya nguo chafu kuna nyingine safi. Akapekuwa kila kona na kukutana na simu ndogo ambayo ilibanwa kwenye ukosi wa shati la ndani na mfuko wa suruali ulikuwa na kifaa kingine kinachonasa mawasiliano.

“Hivi ni vitu gani?” akamwuliza. Yule kichaa akabaki kimya, “...Hutaki kujibu ee? Sawa. Subiri muda wako, utaongea tu!” akawageukia wale vijana, “...Mpeni nguo zake avae kisha mtieni pingu, tupa selo, atapelekwa *central* muda si mrefu,” kisha yeye akatoka nje ya kituo kile na kurudi garini.

“Vipi?” Gina akauliza.

“Madam S alikuwa sawa kabisa, mshenzi yule si kichaa tazama hii,” akampa ile simu na kifaa chake cha kunasa mawasiliano.

“Aisee!” Gina akashangaa.

“Sasa huyu ndiyo ufunguo wa kila kitu, hata kama kazi hii tumetakiwa tusifanye, sasa itafanyika kwa mtindo mwingine,” Amata akamwambia Gina huku akiondoka mara tu baada ya kuwasiliana na Simbeye kuwa mtu huyo afikishwe *central* na mahojiano yatafanyika usiku wa siku hiyo.

“Gina! Hii vita ni kubwa...”

“Nimeona. Sasa tunafanyaje? Yetu hii!” Gina akajibu.

“Yeah, hawa jamaa wanatufanyia dharau sana, nilikuwa mahali pazuri tu kabla sakata hili halijasitishwa, mpaka sasa ningekuwa mbali sana katika uchunguzi. Tutawasikiliza wazungu mpaka lini? Wenyewe tu kuna vitu vinawashinda. Unajua ni dharau sana kwa mtu kukuchungulia ukiwa chumbani kwako na mkeo...”

“Unamaanisha nini?”

“Namaanisha wanachokifanya hawa wajinga,” Amata akajibu.

SURA YA 15

CABO DELGADO

LORD DIMENS alikuwa ndani ya ofisi yake ya siri ambayo ni watu wachache tu wanaojua. Ndani ya ofisi hii alikuwamo na mtu mwingine mmoja, huyu alikuwa ni kati ya wachache wanaojua mengi kuhusu huyu bwana na biashara zake pamoja na hila zote anazozifanya huko duniani. Chochote ambacho bwana huyu angetaka au angefikiri kukitenda, iwe dhidi ya ubinaadamu au vyovyote vile basi huyu angekuwa wa kwanza kumshirikisha na kumsaidia kuamua. Kwa ujumla uswahiba wao ulianza mbali sana tangu Dimens alipokuwa akitumiwa na shirika la kijasusi la Urusi, wakati ule, KGB, kabla halijasambaratika. Na liliposambaratika, yeye alijiondoa kabisa kwa sababu tayari alikuwa amejenga urafiki na watu hatari sana katika kila kona ya dunia akiwemo huyu aliyekaa naye ofisini.

“*Yes sir!*” akaitika wito yule jamaa. Dimens akasafisha koo na kujiweka sawa kitini.

“Kila kitu safi? Hakuwapa usumbufu kumkamata?” Dimens akauliza.

“Amekamatwa kama kuku mwenye mdondo!” yule jamaa akajibu.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Hah! *Very good indeed!* Unajua, hawa watu mi nawaona kama kunguni vile. Hawawezi kunisumbua kabisa, sasa nina uhakika katika Tanzania tumewamaliza. Vijana wamefanya kazi nzuri sana,” Dimens akasema huku mikono yake kaikusanya pamoja juu ya meza yake ambayo ukiitazama tu utajua kuwa thamani yake inaweza kujenga zahanati moja yenye gari la wagonjwa.

“Lakini...”

“Lakini nini?” akamkatiza kijana wake kwa swali.

“Tumepata pigo na nina wasiwasi linaweza kutuletea madhara kama halitashughulikiwa haraka,” yule kijana akajibu.

“Niambie!”

“Kule Tanzania, wakati wa kumsaka yule jamaa, kikosi kiliweka mtu ambaye haikuwa rahisi kutambulika. Wanasema aliweza kufanikisha kila kitu lakini alikamatwa jioni ya jana ileile!” akaeleza.

“Come on! Nani kamkamata na kamgunduaje?”

“Mpaka dakika hii taarifa kutoka Mtwara inasema kuwa huyu mtu kakamatwa na makachero wa Tanzania,”

“Ina maana hawa Watanzania waliujua huu mchezo mapema?”

“Aaaa....”

“Sikiliza Bonston!” akamkatisha. “Kuna mambo mawili tu, kwanza inawezekana ndani ya mtandao tulioujenga huko Tanzania kuna mamluki anayetoa mikakati yetu kwa adui. Nchi kama ile haina ulinzi wowote wa kusema utatutikisa sisi. Hao wenyewe FBI na kaka zao wametulia na kufunga *file*, itakuwa wao?” Dimens akaongea kwa ukali.

“Sir, usiseme hivyo, kumbuka Tanzania ndiyo imekuwa nchi hatari sana katika ukanda wa Afrika kwenye maswala ya kiusalama hasa upelelezi. Nina rekodi nyingi tu za hawa jamaa. Tangu wakati ule wa maisha ya kibeberu huku kusini mwa Afrika, ni nchi hii imeshiriki ukombozi wa nchi zote hizi mpaka hii tuliyopo...”

“Acha uoga Bonston! Zile zilikuwa enzi za Nyerere, hayupo sasa! Ni Falsafa yake unayoizungumzia, na si kitu kingine,” Dimens akafoka.

“Tuyatazame haya kiusalama zaidi, na si kihistoria...” Bonston akasema.

“Enhe!”

“Lazima tujue kuhusu hii nchi, mimi naitilia shaka. Tangu nikiwa jeshini kule Israeli nimesikia habari za hawa jamaa kuwa wana *invincible security* ya hatari sana. Wana majeshi ambayo hata mengine hayapo serikalini. Kwa muundo huu, hawa si wa kuchezea. Nimetumiwa picha moja ya mtu ambaye kanyanyasa sana pale Mtwara na inasemekana ni hatari kuliko hatari yenyewe,” Bonston akamwambia Dimens kisha akampa ile picha. Lord Dimens akaitupia jicho na kuiangalia kwa makini picha hiyo.

“Ni nani huyu *cocroach*?” Dimens akauliza kwa dharau huku akiondoa miwani yake usoni na kuikamata mkononi.

“Mr. Spark!”

“Aaaaaa hah! Hah! Hah! Hah! Jina tu linaonesha ana utoto mtupu, hah! Hah! Hah! Eti Spark. Spark!” alipomaliza kusema hayo akachukua ubamba wake mdogo na kubofya hapa na pale. Ukutani, ikawaka

luninga kubwa kisha akaifanyia *scanning* ile picha na kuiingiza katika mtandao wake wa watu hatari ambao mashirika mbalimbali ya kijasusi yanawatambua. Baada ya kuchakatachakata kwa sekunde kadhaa, sura ya kijana huyu ikaonekana kwa uzuri kabisa. Dimens na Bonston wakasoma maelezo yale kwa umakini mkubwa huku wakijadiliana hili na lile.

“Amata Ric, siyo?” akauliza.

“Ndiyo!”

“Agent wa ndani wa TISS katika kitengo maalum. Kitengo gani? Sijui! Wamesema tu kitengo maalum” Dimens akauliza na kujijibu mwenyewe.

“Nimejaribu kuwasiliana na watu wangu sehemu mbalimbali. Wapo watatu wanamjua vyema huyu bwana, wamenipa rekodi zake tofauti ambazo kwazo,” akatulia kidogo “...hatuna budi kujipanga kumkabili, hata kama tuna mtandao hatari kiasi gani, maana keshavuruga mitandao hatari mingi tu tunayojua, sikutegemea kama ni huyu!” Bonston akasema.

“Mitandao gani kavuruga? Zaidi sana labda vikundi vya ujambazi tu, Afrika haiwezi kuitetemeshwa Europe, itakuwa ni vijimtandao vya waaasi maporini kwao huko au majangiri labda...!”

“*Sir!* Najua unamaanisha nini, nisikilize... unamkumbuka Tracy Tasha?” Bonston akauliza.

“Tracy Tasha, Tracy Tasha, Tracy Tasha, aaaaaannnhhhh, *yes!* Namkumbuka huyu binti kutoka Kansas, alikuwa muuaji hatari sana, nilikuwa nashangaa jinsi anavyoweza kutekeleza mauaji na kuwachomoka wanausalama papo hapo...namhusudu sana!” Dimens akasema.

“*Yes!* Tracy Tasha alishakufa, na alifia Dar es salaam yaani Tanzania, kwa mkono wa huyu jamaa...” Bonston akaeleza.

“*Noooooo! not possible,*” akafoka huku akigonga ngumi mezani.

“Baada ya kumuua Tracy, huyu jamaa ndiye aliangusha mtandao wa kidhalimu wa Sir. Robinson Quebec ndani ya Canada... na kufanikiwa kumuua *Partiner* George Mc. Field...” kijana akaendelea kusema.

“Kwa hiyo, unamuogopa?” Dimens akamuuliza Bonston.

“Si kwamba namuogopa ila kabla hujapambana na adui lazima ujue uwezo wake na wa wale aliowashinda kisha utajua nini cha kufanya kwenye *battle field*,” Bonston akaeleza. Kauli hii ilimfanya Lord Dimens kutulia kwa jozi la sekunde. Kisha akabonyeza sehemu fulani, na mlango

mdogo pembeni mwa meza yake ukafunguka. Akatoa chupa kubwa ya pombe na bilauri mbili, akajimiminia na nyingine akammiminia kijana wake.

“*Cheers!*” akamwambia na kugonganisha bilauri zao, ‘nge!’ “*You have to stand and confront him!*” akamwambia kuwa asimame na kumkabili huyo mtu.

“*Yes, I wish so!*”

“*Good!* Sikia, sisi hatutishwi na mtu awaye yote; awe rais au waziri au mkuu wa majeshi wa taifa lolote duniani. Hatuogopi. Mtandao wetu ni imara na unajua nini unafanya. Sasa nataka uhakikishe huyu mtu anakuwa marehemu kabla hatujafanya ile biashara yetu pale Maputo mwezi ujao. *By the way*, nililokuwa nimekuitia hapa ni kuwa mwezi ujao tutafanya mnada wa hii chanjo baada ya kuiona kuwa inafaa na inafanya kazi vizuri sana. Tumeiboresha kidogo na kuibadilisha nembo. Miezi sita iliyokuwa ndani ya maabara hii imetosha kuifanya kuwa chanjo bora kabisa. La pili, Yule Daktari Edward ndiye atakayekuwa mzungumzaji wa *formula* hii siku hiyo. Hakikisha mnamfanyia mabadiliko ya kutosha ili asijulikane na mtu. Katika kusambaza mialiko ya wadau wachache, hakikisha ni mialiko miwili tu inayofika Tanzania na yote apatiwe Torres Kazumari yeye anajua nani mwingine wa kumpa. Hiyo itakuwa ni siku ya biashara kubwa ambayo haijawahi kutokea duniani. Dimens Lab-Tech inaidhihirishia dunia kuwa haishindwi kitu katika uwanja wa tiba... hah! Hah! Hah! Hah!”

Baada ya cheko hilo, ukimya ukatawala kati yao, kila mmoja akipiga funda kadhaa za kinywaji kile kikali.

“Na huyu kibaraka wa CIA tumfanye nini?” Bonston akauliza.

“Huyo awe kitoweo cha vijana wangu, yeyote anayemtaka aende akamalizie haja zake huko. Akigoma, sikufundishi cha kufanya,” Dimens akajibu na kisha kumtaka kijana yule kuondoka ofisini humo kwani muda wake ulikuwa umekwisha. Bonston akatoka na kuingia kwenye lifti kisha akapanda juu kwa kuwa ofisi hiyo ilijengwa chini ya ardhi sambamba na maabara ile ya siri.

* * *

Huko Mtwara, saa kadhaa baadaye, Torres Kazumari alikutana na vijana wake mahiri kabisa na kikao kifupi kikaendelea kati yao.

“Mkuu amepokea kwa masikitiko habari ya kukamatwa kwa Mpaya

Kichaa. Hii ni hatari kwetu kama watambana kumhoji, na hakika kama chombo chake cha mawasiliano kimegundulika, ndiyo shida zaidi,” akawaambia.

“Kiukweli mbinu iliyotumika kumkamata hata sisi hatukuitegemea...”

“Msicheze kabisa na yule jamaa. Ukikutana naye, usimpe nafasi ya kusema hata neno moja, wala asikukaribie mita kumi, muue. Hafai! Boss Mkuu amesema mtu yule auawe mara moja asije kuleta madhara, ila mi nimemwambia asiwaze juu ya hili kwani kazi yote itafungwa ndani ya saa chache zijazo na Tanzania itajuta kwa nini inafanya kazi hii ilhali imeambiwa iachane nayo,” Torres akawaambia vijana wake na wao wakapiga makofi.

“Anajulikana kama Kamanda Amata, na nyumbayake mmeshaipeleleza, mnaijua, hata mliweza kumwekea maiti kitandani kwake. Sasa nahitaji roho yake ndani ya saa chache,” akawaambia huku akiwapa picha nyingine ya Amata na mtu mwingine ambaye naye alitakiwa kuuawa kwani angekuwa ni tatizo. Na wao wakaweka ahadi kumletea roho hiyo hata kama ni kwenye mfuko wa Rambo. Baada ya dakika kadhaa za kikao hicho, wale vijana wakaondoka tayari kwa kazi. Mara tu walipoondoka na kumwacha Torres peke yake, akavuta laptop yake na kuiwasha kisha akapekuwa picha kadhaa na kuitazama ile ya Amata akiwa na mfanyakazi wa mapokezi wa kampuni yake ya *CdG Marine Tour*. Torres akatabasamu maana alijua wazi kuwa anaweza kumtumia mwanadada huyo kumnasa Amata na kumuua kama kuku tu.

“Tausiaa!” akaongea kwa sauti ya chini huku akiendelea kupakua picha nyingine nyingine, alipojiridhisha akampigia simu meneja wake katika hiyo kampuni na kuongea naye machache.

“Kama tulivyofanya mwaka jana, sasa andaa tena ile michezo ya kupiga mbizi na safari hii itafanyika hapa Mtwara. Hakikisha Tausi anakwenda Dar es salaam kuweka sawa mambo yote pamoja na kupata vibali,” akatoa maagizo.

“Kuhusu vibali mkuu mbona tunaweza kutumia barua pepe tu kwa mamlaka husika?” Yule meneja akauliza.

“Unakumbuka mwaka jana tulichelewa sana kupata vibali na tulitumia njia hiyo uisemayo. Mwaka huu sitaki hali ile ijirudie. Mtume Tausi, mwezeshe kwa kila kitu akiwa tayari kwa safari unipe taarifa tafadhali. Na anatakiwa asafiri haraka iwezekanavyo...” akamwambia na kukata simu.

“Ok Boss, nimekusoma,” akajibiwa.

Basi! Mchezo umekwisha, najua Tausi akifika Dar' ni asilimia kubwa atamtafuta huyu jamaa, na kwa kuwa anapenda totoz atajitokeza tu na hapo ndipo itakuwa nafasi yangu ya kunyofoa robo yake. Dawa ya mvanaume ni mwanamke mrembo, basi! Akawaza huku akiifunga ile laptop na kuisogeza pembeni.

DAR ES SALAAM...

Mvua kubwa iliendelea kunyesha katika jiji hilo. Kama kawaida, kero ya usafiri, barabara kujaa maji, umeme kukatika, vyote vilienda sambamba. Kama hukuwahi kuishi katika jiji hili hasa nyakati za mvua usingeweza kuijua adha hii kutokana na kupendeza kwa maeneo yake hasa katikati na baadhi ya viunga vyake.

Siku hii ilimkuta Madam S katika kikao kizito cha watu wawili, yaani yeye na Rais. Hii ni kwa sababu yeye alitakiwa kuwasilisha taarifa zake zote kwa mkuu wa nchi na si vinginevyo. Watu kama hawa ni sehemu ya walinzi wa karibu wa Rais. Huitwa *invisible* yaani 'wasioonekana'. Ni walinzi wa siri. Tofauti na wengine, yeye alikabidhiwa kitengo nyeti cha usalama wa nchi hususan maswala mazito yanayoigusa Ikulu moja kwa moja. Katika kutekeleza hayo, ndipo hutumia kikosi chake cha TSA ambacho nacho kilikuwa ni cha siri sana. Watu wake walijulikana kama wanausalama mbele ya macho ya wao wenyewe, waalimu mbele ya wanafunzi, wafanyabiashara mbele ya wateja, madaktari mbele ya wagonjwa, madereva mbele ya wasafiri. Kila mmoja alikuwa na kifuniko chake kilichomficha kazi yake halisi, '*secret* au *undecover agent*', walijulikana hivyo. Si kwamba walikuwa wakijificha wasioonekana, la, lakini walijificha mbele ya jamii kwa kazi wafanyazo na zinazowatambulisha. Kumiliki vitambulisho vya kila aina, pasipoti zaidi ya moja au kumi za nchi tafauti, ilikuwa ni kawaida kwao.

"Nalirudisha kabrasha hili kwako kutokana na kwamba yale uliyoniambia ni hatari kwa taifa letu! Selina, kila ambacho vijana wako wataigundua nyuma ya hili nahitaji taarifa hapa. Hilo moja. Lingine, kamati ya uchunguzi wa lile tukio imekamilisha taarifa zake lakini kuna utata mmoja, ambao, kwenye taarifa yako umenipa jibu moja lakini jingine limebaki linapelea... Nahitaji ufanyie kazi, maiti moja au mtu mmoja ambaye mpaka sasa hajulikani alipo. Katika mabaki ya ule moto zimepatikana maiti zilizoungua. Kwa idadi ya watu waliokuwa ndani ya maabara ile, mmoja hayupo na huyu inatiliwa shaka sana asije kuwa mamluki, naomba uchunguze, kama kafa, katoroka au ni moja

ya njama zake kufanya uhalifu huu!” aliposema hayo akampa nakala ya kabrashia lenye taarifa ile.

“Hili pia chukua, litakusaidia,” akamwambia na Madam S akasimama tayari kuondoka. Baada ya kuagana, akavuta hatua mpaka mlangoni kabla hajafungua akasikia sauti nyuma yake.

“Selina”!

Akageuka.

“Usimpe mtu kazi hiyo zaidi ya Kamanda Amata!” akasema huku akitabasamu.

“Isipokuwa...”

“Ikibidi.”

* * *

Mvua kubwa bado ilikuwa ikinyesha wakati Madam S akiliacha jengo la Ikulu. Barabara za mjini zilijaa maji na kumfanya apate tabu kidogo kuendesha gari lake. Alipotazama saa yake tayari ilikuwa saa saba usiku, akainua simu yake na kupiga namba fulani, kisha akasiliza.

Upande mwingine wa jiji hilo, maeneo ya Msasani, muziki laini ulikuwa ukisikika huku viumbe wawili wakiwa juu ya kitanda kikubwa wakifuarahia uumbaji wa Mwenyezi Mungu katika miili yao.

“Ulienda, ukaniacha peke yangu, nilikumisi sana na nilimisi huu utundu wako,” sauti ya kiume ikaunguruma.

“Mmmmh! Acha uongo, wewe ninavyokujua mimi, si ajabu ulikuwa na mwingine, wanavyokushobokea utafikiri sijui nini...”

“Umeanza maneno yako wewe...” Amata akamwambia Gina na mara hiyo saa yake ikaanza kumfina, akamwacha Gina kitandani na kuelekea bafuni.

“We vipi?” Gina akauliza wakati Amata akijichomoa mwilini mwake.

“Nakuja mpenzi, nimebanwa ghafla!” akamjibu na kuingia maliwato kisha akaufunga mlango. Akabofya kitufe cha kuruhusu ujumbe katika saa hiyo, na mlio hafifu kama ule wa *printer* ya *matrix* ukawa ukisikika na kijimkanda kirefu kikajitokeza upande wa kulia wa saa hiyo, akauvuta na kukaata, kisha akausoma.

‘Fika nyumbani kwangu haraka, usiku huu...’

Ujumbe ukaishia hapo. Amata akakifinyanga kile kijimkanda na kukitia chooni kisha akaflash maji kukiondoa. Akaamua kuoga moja kwa moja na alipotoka hakurudi kitandani tena.

“We mbona hueleweki? Umeniacha njiani halafu unachukua suruali unaenda wapi?” Gina akauliza huku akitupa shuka upande wa pili na kujiinua kuketi kitandani. Umbo lake zuri la kuvutia likamfanya Amata ashindwe kuendelea kuvaa suruali yake.

“Kuna sehemu natakiwa kwenda, nilishasahau!” Amata akajibu na dakika chache baadae akawa tayari kwenye muonekano wa kuondoka. Akapachika bastola yake vizuri kiunoni.

“Haya bwana wasalimie wanawake zako uwapendao,”

“Wivu huo umeanza lini?” Amata akamtupia swali.

“Nimeanza leo...” Gina akajibu huku akiinuka kitandani, “Haya ukimalizana nao urudi hapa, siondoki kitandani mpaka uje umalizie!” akamwambia.

Kamanda Amata akaiacha nyumba ya Gina usiku mnene, akaondoka na gari lake na kuikamata Barabara ya Old Bagamoyo kuelekea Morocco kisha akakunja ile ipitayo Ubalozi wa Marekani na kuibukia Namanga, akakunja kushoto na kuelekea Masaki.

Robo saa baadae tayari alikuwa akiegesha gari lake ndani ya jumba la Madam S.

“Karibu! Najua nimekung’oa kifuani na mvua hii,” Madam akaanza kumtania huku akiwa kamfungulia mlango wa kuingia sebuleni.

“Aaaah *no!* nilikuwa *disco...*”

“Hivi Amata unafikiri utanidanganya mimi wewe? Ulikuwa kwa Gina, haya kataa! Kila siku nakwambia muoe unajifanya oooh mara eeeh! Shauri yako, utanyang’anywa tonge mdomoni!” Madam akamwambia huku wakiketi mezani ambapo katikati yao kulikuwa na makabrasha mawili na pombe kali.

“Keti!” akamwambia na Amata akaketi akiwa mpole kabisa.

“Sikiliza Amata, kazi inaanza usiku huu, Ikulu imetoa oda ya kuanzisha tena uchunguzi huu wa upotevu wa chanjo, kwa siri. Sambamba na hilo kuna mtu mmoja, imeonekana kuwa maiti yake haikupatika katika mabaki ya ule moto, inatakiwa ijulikane, kafa, katoroka au yeye ndiye kahujumu swala hili!” akamwambia.

“Ina maana apatikane mfu au hai?”

“Ndiyo!”

“Hili swala tungekuwa mbali sana Madam, maana nilikuwa nimefika mahala pazuri... *by the way*, naweza kuanzia nilipoishia ila ujue kwamba adui yetu anatujua, si ajabu hata hapa tulipo anajua kuwa tupo,” Amata akaeleza huku akijimiminia kinywaji.

“Najua, lakini unafikiri kwa nini tumekupa *rank* ya TSA 1? Ngoja nikwambie, mheshimiwa Rais amenisisitizia kazi hii kukupa wewe tu, anakuamini na anajua uwezo wako kwani ulimkuna sana katika sakata lile lililopita,” Madam akasema na kutulia akisubiri kijana wake amalize kummiminia kishapo akainua bilauri yake na kugugumia mafunda kama matatu hivi, akaishusha na kuiweka mezani.

“Sasa kuna taarifa hapa ambazo nitazifanyia kazi mwenyewe, imegundulika ile maiti tuliyoikuta kwako, Jasmini ameikuta na *badge* ya utambulisho, mwanamke yule ni ya Mellanie...” Madam akasema.

“Mellanie?” Amata akauliza.

“Ndiyo, ni ndugu yetu kutoka Langley. Baada ya Chiba kupewa utambulisho huo na kuzama katika uchunguzi alibaini kuwa mwanamke huyu alikuwa akifanya kazi katika shirika binafsi la ndege, ni rubani,” Madam akaeleza.

“Aaaaa ok, itakuwa yeye aliileta ile ndege iliyolipuka! Hawa jamaa wanafanya kazi zao kwa kasi kiasi gani au si binadamu!” Amata akabaki katika mbutwao.

“Binadamu kama wewe tu... sasa Amata, hii kazi inahitaji utulivu sana, kama adui anakujua ujue atakuwa anajua udhaifu wako pia na hili ni jambo baya sana. Hakikisha unalileta lile sanduku hapa na majibu yote yanayotakiwa kufika yafike. Yeyote aliyehusika ukimtia hatiani haina haja ya huruma, kanuni yetu ni ile ile, *deffence* and *offence*. Kumbuka kwa jambo la juzi la kumkamata yule kichaa tayari watakuwa nao wanajiweka sawa. Nipe ramani!” Madam akamaliza.

“Yeah, katika mahojiano amekiri kuwa aliyekuwa anawasiliana naye ni mtu kutoka Mtwara ila hata yeye hamjui kwa jina wala sura. Kasema tu kuwa yupo Mtwara akili yangu inarudi kwa Torres Alexis Kazumari, na huyu ndiye nitakayeanza naye,” Amata akamwambia Madam S.

“Naaa... sasa kuhusu huyo Mellanie, umeijulisha Langley?” Amata akaongeza swali.

“Hapana, Dkt. Jasmine anaendelea na vipimo vya DNA, akikamilisha ndo tutafaya utaratibu huo,” Madam S akaeleza.

“DNA! Ya nini? Au utambulisho wenu mna mashaka nao?” Amata akauliza. Madam S akavuta kabrasha lingine na kulifungua, humo akatoa mkufu uliunganishwa na kipande cha bati gumu, akampatia Kamanda.

“Mellanie McDonald...” akasoma.

“Vyema, tuachane na hilo, kuna taarifa kidogo za siri ambazo nahitaji kukupa kwa msaada zaidi ili mimi na wewe tuweze kujenga picha ya tukio hili kabla hatujavuta hatua kwenda mbele. Taarifa hizi ni zile ambazo nilizipata kule Ngerengere,” Madam S akamweleza Amata juu ya kila alichokiona kwenye kumbukumbu za wanaanga kupitia rada yao. Amata akabaki kinywa wazi pasi na kusema neno, Madam akaendelea, “Najua swali unalotaka kuuliza, lile sanduku lililobeba chanjo halijaungua wala nini, lipo salama na lipo mahala fulani limefichwa. Ila sijui ni nani kalificha. Ile ndege imelipuliwa na baada ya kulipuliwa, waliolipua wameruka kwa *parachute* na kutoroka. Bila shaka, wametoroka na ile chanjo...” Amata akaendelea kusikiliza huku akili yake ikikimbiza kumbukumbu.

“Shut up, bitch, and you will die by fire, fuc you,”*

Kumbukumbu ya maneno hayo ikamjia kichwani. “Yes! Yes!” akasema kwa sauti ndogo ambayo Madam S aliisikia bila shida.

“What?” Madam akauliza baada ya kugundua kuwa Amata amepotelea kwenye kumbukumbu nzito.

“Endelea Madam, nakusikiliza...”

“Kwa hiyo sasa picha ya kwanza ninayokupa baada ya uchunguzi wangu mimi ni hiyo ila wewe unaweza kuangalia kutoka hapo,” akamweleza. Amata akajimiminia kinywaji na kupiga fundu jingine kisha akamtazama Madam S, “Upo sahihi, sasa naunganisha picha...” akatuliza kidogo na kupiga fundu lingine.

Time! Time! Time! Here we go! (sauti ya kiume)

I’m burningggggg! (sauti ya kike)

Maneno haya yalirudi kichwani mwa Amata mara kwa mara, na kutokana na taarifa ya Madam S aliyoipata kule Ngerengere, hakuwa na shaka kuwa hujuma imefanyika.

“Madam, nikiwa Mtwara nilifanikiwa kupata kadi sakima ndogo kutoka kwenye saa ya yule mhanga aliyetoroshwa ambayo ilikuwa na uwezo wa kuhifadhi sauti na picha. Baada ya kuifanyia utafiti na kusikiliza kilichopo na picha ambazo niliziona, na nini unaniambia, sasa nakupa jibu kamili kuwa ile ndege imeangushwa, na sasa naamini kuwa hilo sanduku lipo mahala,” Amata akasema.

“Ndiyo!” Madam akamuunga mkono.

...Noooo! Nooo! (sauti ya kike)

You can’t do that bast.... (sauti ya kiume)

'Paaah!! Paah! Paaah!' (mlio wa bastola)

'Kelviinnnnnn!' (Sauti ya kike)

'Shut up, bitch, and you will die by fire, fuc you,'* (sauti ya kiume)

Amata akatulia kwa nukta kadhaa kisha akamwewesa midomo yake na kutamka kwa sauti ya chini, "Kelvin, Kelvin..."

"Kelvin ndiyo nani?" Madam akamkatisha.

"No! Yatupasa kumjua Kelvin, nafikiri ndiye *masterplan* wa mchezo huu. Katika sauti ninazokumbuka kwenye ile kadi ni huyu mwanamke akilitaja hili jina kisha akafuatiwa na mlilo wa bunduki, risasi tatu," Amata akaeleza na Madam S akaandika jina hilo katika kijitabu chake.

"Kelvin ni nani?" Madam akauliza.

"Mtuhumiwa namba moja kuanzia sasa," Amata akajibu.

"Apatikane!"

"Atapatikana labda tu awe amekufa!"

"Kafukue kaburi lake umlete hapa!"

Tangu hapo, kichwa cha Kamanda Amata kikawa hakitulii, kikitoa picha hii na kuweka ile, kikikumbuka sauti hii na kuiacha ile, jina la Kelvin lilikuwa kichwani mwake.

Kelvin ni nani? Akajiuliza pasi na kupata jibu.

"Tuonane Shamba asubuhi tuweke mambo sawa!" Madam akamwambia Amata kisha wakaagana.

* * *

Asubuhi iliyofuata ilimkuta Kamanda Amata katika kituo cha polisi cha kati, katika ofisi aliyoketi alikuwa akitazama na mtu mwenye mwili wa wastani, mtu mzima ambaye tayari ngoziye ilishakuwa na kiasi cha makunyanzi. Leo hii, alikuwa ndani ya sare nadhifu ya kipolisi iliyosheheni nyota begani mwake zinazoweza kuhesabika kirahisi tu.

"Ndiyo kijana!" Inspekta Simbeye akaanzisha mazungumzo.

"Mtu wetu anasemaje, nahitaji tu kujua kuwa wamempeleka wapi Johnson!" Amata akamwambia Simbeye.

"Ameeleza. Baada ya kipigo kikali ameeleza mengi ambayo uliyataka..."

"Ndiyo!"

"Anasema Johnson amehifadhiwa kwa muda huko Mkuranga kwenye nyumba ya tajiri mmoja wa Kiyemen, ila kutoka hapo anasema hajui ni wapi kijana huyo atapelekwa," Simbeye akaeleza.

“Mkuranga?”

“Ndiyo!”

“Mkuranga siku hizi imekuwa chimbo la wahalifu wa kutumia silaha. Sijajua kama vyombo vya usalama havijui au vinapuuzia, ila ni hatari huko tunakoelekea,” Amata akazungumza.

“Achana na hayo kijana!” Simbeye akamkatiza.

“Sawa, asante, mengine nitumie kwa nukushi, wacha nishughulike na hili,” Kamanda akaagana na inspekta huyo na kurudi garini kisha akatia moto na kukamata Barabara ya Kenyatta akaiacha ile inayoelekea Magogoni akanyoosha moja kwa moja mpaka jengo la NIC au wengi huliita Kitega Uchumi. Akaegesha gari na kuvuta hatua kuingia ndani ya jengo hilo, moja kwa moja akafika katika ofisi ya J & K, akatikisa mlango, umefungwa.

Secretary mpaka sasa hajafika? Akajiuliza. Alipohakikisha hakuna nyendo ya kuhofia akachukua funguo zake na kupachika kitasani, akakinyanyasa kidogo tu na kitasa kikakubali, mlango ukafunguka. Akaingia ndani na kuufunga nyuma yake. Ofisi ile haikuwa kama alivyoikuta jana yake. Vitu vilikuwa shaghalabaghala. Kengele za hatari kichwani mwake, zikalia. Akatazama kila kitu na kutikisa kichwa, kwa maana alijua wazi kuwa hata aliyefanya upekuzi huo si mzoefu wa kazi hiyo. Mpekuzi alipekuwa kwa fujo.

Kuna kitu kinatafutwa, kitu gani? Akajiuliza. Hii ikampa shauku ya yeye kujua. Akauendea mlango wa pili na kuufungua. Bastola mkononi. Akaingia ndani. Hali ni ile ile. Hakugusa kitu, akatazama kwa macho ya kikachero, akagundua kuwa mpekuaji hakuwa mtaalamu kabisa wa kazi hiyo, hivyo ni rahisi sana kwa mtu kama huyo kukosa kile ambacho anakitaka. Akavuta hatua na kuiendea meza, akaketi juu ya kiti cha Johnson. Akavuta droo moja baada ya nyingine kutazama hapa na pale, hiki na kile. Pamoja na yote hayo, bado hakupata la maana zaidi ya kukutana na makabrasha ya kibiashara tu, na biashara zote hakuona hata moja haramu. Maswali lukuki yalijipanga kichwani mwake yakisubiri majibu.

Johnson ana ubusiano gani na bili sakata? Akajiuliza na kushusha pumzi ndefu. Akajiegemeza kitini akiwaza. Amata akajaribu kuweka matukio sawa katika kichwa chake. Akaondoa wazo kuwa kijana huyo anahusika katika hilo, lakini bado mawasiliano ya yule kichaa yalikuwa yakienda Mtwara kwa nani? Hapa akapata kidogo kajiuhusiano ka mambo haya

mawili.

*Ok, cha kufanya sasa ni kujua Johnson Kasalu ni nani. Kusema tu ni Mmarekani Mtanzania, mfanyabishara baitoshi. Wangempiga risasi na kuchukua pesa wakaenda zao, lakini wamemteka, ofisi yake wameipekua, kuna nini? Hapa kuna jambo, lazima lijulikane, na jambo lenyewe lipo humuhumu ndani ndiyo maana walikuja! Akawaza kwa kina huku bado macho yake yakipepesa huku na kule, na mara hii yakatua ukutani kwenye picha kubwa ya *Monalisa*. Picha ya kupendeza, yenya mchoro wa mwanamke mzuri wa kupendeza sura na umbo. Iliyochorwa na mchoraji maarufu ambaye mfanowe haujawahi tokea hata sasa, Leonardo Da Vinci. Mchoro huo ulichorwa kwa rangi za kuvutia.*

Hivi wanawake wazuri kama hawa wapo duniani kweli? Akajiuliza.

Hii picha inasiri kubwa! Akawaza na kujiweka tayari kunyanyuka kuiendea picha hiyo maana alijua kuwa wakati mwingine hawa matajiri huficha vitu vya thamani katika picha hizi. Kwa Amata hili halikuwa geni.

Alipotaka kunyanyuka, mwili wake ukaingiwa baridi ya ghafla. Hatari. Akatulia kitini na kuiweka bastola tayari. Hakukosea. Sekunde chache tu akahisi mlango ukifunguliwa na sauti za watu zikiingia ndani huku wakiongea Kireno. Hakuielewa sawasawa lugha hii lakini kwa hisia tu alijua kuwa kuna mmoja anayewalaumu wenzake. Amata kwa haraka akaingiza mkono katika mfuko wa ndani wa koti, akachukua kiwambo cha sauti na kukifunga haraka katika bastola hiyo. Akaishika sawia mkononi mwake huku akiwa bado kaketi kitini akisubiri na mlango wa pili ufunguliwe. Sekunde kama kumi hivi akaona kitasa kikinyongwa na mtu wa kwanza akaingia ndani, hakumchelewesha. Risasi ya kwanza ikaufikia moyo, jamaa akajibamiza ukutani na kisha akaangukia ndani.

Kishindo cha kuanguka kwake kikawashtua wale wawili upande ule.

“Hey! Pinto, o que aconteceu?” mmoja akauliza kuwa nini kimetokea huku naye akiingia mzima mzima. Wakati huo tayari Amata keshakiacha kiti na kuhamia upande mwingine. Akamshuhudia jamaa akiingia taratibu huku akimtazama huyo aliyemwita ‘Pinto’ akiwa chali huku macho yamemtoka. Huyu akawa mjanja lakini mwoga, hakugeuza sura yake kutazama popote pale, akarudi nyuma na kurudi kwenye ile ofisi ya kwanza huku akiufunga ule mlango. Amata akasikia wakizungumza tena kwa Kireno, na nukta hiyo hiyo, akasikia mlilo wa toni ya simu, akajua kwa vyovyote inaweza kuwa wanawasiliana na wengine.

Hakuruhusu hilo litokee. Akauendea mlango na kuufungua ghafla. Hakukosea. Walikuwa vijana wawili tu, risasi yake ilipoiacha bastola ikamfumua mmoja na kumbwaga kando kama mzigo. Yule aliyeshika simu akajikuta ikimondoka, maana alihisi kakutana na mzimu.

“Quieto!” Amata akamwamuru akimtaka kubaki kimya. Hili ni neno moja kati ya machache anayoyafahamu katika lugha hii ya Kireno. Yule jamaa akatii na kubaki katumbua macho. Kamanda Amata akasogea kwa miguu yake taratibu na kuifikia ile simu, akainama kuichukua. Kitendo hicho ilikuwa ni nafasi ya yule bwana kufanya yake na Amata alijua hilo hivyo alilitegemea.

Yule bwege akarusha teke na kuipiga bastola ya Amata, nayo ikamtoka mkononi na kuangukia upande mwingine. Nukta hiyohiyo, Amata kwa kutumia mguu wake akamchota mtama na jamaa akajibwaga chini kama mzigo huku kisogo kikipiga kwenye meza.

Akajitahidi kuinuka lakini ikawa ngumu, Amata akamwendea na kumkamata ukosi wa shati, akamtikisa na kumtandika kichwa kimoja cha kilo nyingi, yule mtu akazirai. Akamburuza mpaka ndani ya kile chumba na kurudi kumburuza mwingine mpaka mlelele walimo wengine.

Akaanza kuwapekua mmoja baada ya mwingine, akawakuta na fedha mchanganyiko; Dola za Kimarekani, Euro, Shilingi na kila mmoja alimkuta na hati za kusafiria. Hakuzipekua ndani, akazitia kwenye mfuko wa suruali yake, huyu wa mwisho akamkuta na kijitabu kidogo cha kumbukumbu, akakichukua na kukitia mfukoni kisha akawalundika pamoja. Ila harakaharaka alijua kuwa si Watanzania au la walitumia Kireno ili watu wasielewe nini wanazungumza.

“Bastardos!” akawatukana na kisha akarudi kuichukua bastola yake. Tayari akili yake ilikuwa ikisoma hatari tupu, akarudi ndani haraka na kuiendea ile picha. Akajaribu kuipapasa huku na huko hakuona kama kuna aina yoyote ya saraka katika eneo hilo. Akajaribu kuing’oa, akashangaa haing’oki. Akafanya kama anaizungusha, ikazunguka. Ndipo akasikia mlio hafifu wa muziki na mara nyuma ya ile picha kukaonekana kitu kama kitasa cha dijitali. Hakuumiza kichwa kwani alijua ni jinsi gani ya kuvidanganya vitasa kama hivyo. Akachukua moja ya funguo zake, akaivuta kwa nyuma na katikati ikabaki kitu kama msumari, akapachika kwenye tundu dogo katika hiyo loki kisha kwa mkono wake mwingine akabofya tarakimu 0001, kitasa kikafyatuka na

kijimlango kikafunguka.

Ndani ya saraka hii mlikuwamo na kabrasha mbili kubwa pamoja na funguo kadhaa, kibunda cha noti, bastola na kitambulisho kilichopachikwa nembo nzuri ya dhahabu yenye mfano wa ngao na juuye kuna kichwa cha ndege aliyetanua mbawa zake, ambayo kwa Amata haikuwa tabu kuitambua, lakini ilimwacha kinywa wazi.

“Ndiyo maana wamemteka! Shabash!” akajisemea. Kwa haraka akatia kile kitambulisho mfukoni na kuzishika zile kabrasha mkononi, hakuchukua pesa. Akatoka kwenye ile ofisi na kuufunga mlango kana kwamba hakuna kilichotokea, akateremka chini na kuingia kwenye gari lake. Akachukua simu yake na kupiga namba fulani, isha akaiweka sikioni.

“Ndiyo kijana!” sauti ya upande wa pili ikaitikia.

“Jengo la Kitega Uchumi, ghorofa ya sita, ofisi ya J & K Group of Company kuna mzigo wako wa kawaida,” Amata akamwambia Inspekta Simbeye.

“Mara hii kijana?” Simbeye akashangaa.

“Kama kawaida!” akakata simu na kuwasha gari kisha akaondoka kwa kasi kurudi Posta ya Zamani. Na mara hiyo hiyo simu yake ikaita, alipoitazama hakuwa mwingine ni Madam S. akatazama saa yake, tayari ilikuwa saa nne kasoro dakika chache asubuhi.

* * *

Nje ya jengo la Kitega Uchumi, gari moja aina ya Marcedec Benzi jeusi lilikuwa bado lipo maegeshoni. Ndaniye kulikuwa na mtu mmoja tu aliyeonekana kusingia na kushtuka.

Mh! Hava jamaa vipi? Mtu huyo akajiuliza, na baada ya sekunde kadhaa akaamua kuteremka kwenda kwenye jengo hilo ili ajue kulikoni. Akiwa hata hajavuka barabara, akasikia ving'ora vya magari ya polisi vikiwasili eneo hilo. Akasimama na kusubiri kuona kulikoni. Magari mawili, Landrover Defender, meupe yakaingia na kuegeshwa huku vijana wenye bunduki waliovalia kiraia wakiruka na kukimbilia ndani ya jengo hilo.

“Shit!” akajikuta akitamka huku akirudi nyuma na kuingia tena garini na kuwasiliana na wenzake ambao hawakuwa eneo hilo.

“Missão fracassada, missão fracassada!” akatoa taarifa kuwa mpango umeshindikana.

“O *que está acontecendo?*” sauti ya upande wa pili ikauliza kuwa nini kimetokea.

“*Não sei o que aconteceu, mas a polícia está aqui,*” akawapa taarifa kuwa hajui kimetokea nini ila polisi wamezingira eneo.

“*Oh meu Deus, fique lá e veja o que é o próximo,*” akamtaka kusubiri ajue nini kinaendelea kisha ile simu ikakatika.

Yule jamaa akatulia garini kimya kabisa huku akijikuta analowa jasho. Dakika kama ishirini baadae ikatolewa miili miwili kwenye machela na mtu mwingine akiwa kavishwa pingu mikononi na kusukumwa na askari hao kuingia garini. Sura yake tu ikatosha kumwambia kuwa wenzake hao tayari wako matatani. Akawasha gari na kuliacha likiunguruma. Baada ya yale magari ya polisi kuondoka naye taratibu akaingia barabarani na kutokomea.

* * *

Amata aliwasili katika ofisi hizo za siri kabisa ambazo wao huziita Shamba au kiofisi huitwa ‘*Safe House*’ saa moja baadae. Kwa kutumia milango anayoiua yeye, alifika moja kwa moja katika ofisi ya Madam S na kumkuta mama huyo tayari keshajaa.

“Mbona umechelewa miadi? Si unajua mi nina kazi nyingi,” Madam akasema.

“Najua!”

“Sasa?”

“Kuna kazi nilikuwa naifanya inayohusiana na hilihili, ndiyo imenichelewesha,” akajibu huku akijiweka sawa pale kitini.

“Ok, tuanzie tulipoishia,” Madam akasema na Amata moja kwa moja akachukua pochi yake na kutoa kadi sakima ndogo na kumpatia. Madam S akaipokea na kupachika kwenye kifaa chake ambacho hutumia kusikiliza au kutazama nini kipo ndani ya kadi za mtindo huo. Baada kama ya dakika mbili tatu hivi akakizima na kushusha pumzi.

“Nakubaliana na wewe, huyu Kelvin atakuwa ndiyo *master plan* wa hii kitu, sasa tunampataje maana inaonekana yupo hai na anajua sanduku lile lipo wapi,” Madam akamwambia Amata.

“Yeah! Sasa sijajua bado, je huyo ambaye sura yake imeonekana kwa kupita tu, ni nani au ndiyo Kelvin?” Amata akaongea kwa shaka.

“Usijali, hii kazi nitampa Chiba naye ataweza kutambua kila kitu

kwa kuwa ni kazi yake, akimaliza nitakujulisha. Mpaka sasa tunajua ndani ya ndege kulikuwa na watu watatu na tumepata maiti moja na mwingine ndiyo huyo katoroshwa hospitali na Kelvin ambaye inaonekana yuko hai, lakini katika ile picha ya rada inaonekana kama watu wawili waliruka kwa mwamvuli, tafuta ukweli wa hili Kamanda!” Madam akamwambia.

“Sawa mama! Lakini tuna maiti ya Mellanie, na tumetambua kuwa ni rubani, je yeye si mtu wa nne katika ndege ile?” Amata akatia shaka.

“Mmmm! *Yes*, hili lilinipita kabisa. *Anyway*, endelea na kazi mimi nitaliweka sawa hili!” Madam S akamwambia Amata.

“Sawa mama!” akaitikia.

“Kwa msaada wowote niambie nitakupatia,” Madam akamwambia huku akinyanyuka kitini. Amata hakumwambia lolote kuhusu tukio la pale jengo la Kitega Uchumi, akaiacha ofisi hiyo na kuondoka zake. Moyoni mwake alikuwa akiwaza tu apate mahala tulivu atulie na kuchambua zile tafutishi za wale aliowaua na zile za Johnson alizozichukua kwenye saraka ya ukutani.

Nyumbani kwangu si mahala salama! Akawaza, huku akibadili gia na kutokomea mitaani katika kitongoji cha Kigamboni.

* * *

Katika jumba moja kubwa la kifahari huko Mkuranga, Johnson Kasalu alikuwa hoi katika chumba kimojawapo, baada ya kupokea kipigo na mateso makali ili tu aseme mpango gani unafuata kutoka CIA baada ya ule wa kwanza kufungwa. Ijapokuwa aliteswa sana na kupoteza fahamu mara kadhaa, kijana huyo hakuweza kusema lolote na hata walipokuwa wanajipanga kwenda ofisini kwake kupekua, yeye alikuwa amejifanya kazimia huku akiwasikiliza yote ambayo walikuwa wakiyapanga. Moyoni mwake alikuwa akiomba wasije kugundua saraka yake ya siri ambayo huifadhi nyaraka zote nyeti kutoka makao makuu, Langley.

Zaidi yake yeye, kulikuwamo watu wengine wawili, Wazungu. Johnson aliwaona Waafrika pale alipokamatwa na kufikishwa hapa tu. Mara alipokabidhiwa kwa Wazungu hawa, wale vijana wakaondoka na yeye kutupiwa ndani ya ngome hiyo yenye mateso makali. Alipoingizwa tu kwenye moja ya chumba pweke, Johnson alihisi wazi harufu ya kifo,

lakini kwa kuwa mateso ni sehemu ya kazi yake, aliuandaa mwili wake kwa hilo, kisaikolojia na kiakili. Kipigo alichokipata kutoka kwa jamaa hawa wawili kama ingekuwa mwenzangu na mimi, tayari tumekusahau, lakini Johnson alivumilia na kuzirai zaidi ya mara moja na alipozinduka shughuli ikaendelea.

“Amekataa kabisa kusema!” mmoja akamwambia mwenzake kwa lugha ya Kireno, Johnson akiwa chini sakafuni kimya, alielewa vyema lugha hiyo. Mara simu ya mmoja wao ikaita na ndipo akapokea rasmi taarifa ya vifo vya watu wake wawili na mwingine kukamatwa.

“O *que?*” Yule mwingine akauliza kuna nini. Swali hili likamfanya Johnson pale chini kumakinisha akili yake ili ajue nini hasa kinaendelea.

“*Pinto e Petros foram mortos,*” akajibu kwa sauti ya chini kuwa Pinto na Petros, wawili kati ya wale aliowatuma wameuawa. Haikuwa habari nzuri hata kidogo kwa jamaa hawa, kila mmoja alitukana matusi yake huku akirusha mikono hewani. Katika mazungumzo na simu hiyo Johnson alielewa wazi kuwa vijana hao wameuawa ndani ya ofisi yake. Swali likambakia ni nani aliyefanya mauaji hayo ndani ya ofisi hiyo, na alikuwa anatafuta nini. Ndani ya moyo wake alifurahi sana kusikia kuwa jamaa wale wameuawa na mwingine kukamatwa, alitamani kupiga kelele za ushindi lakini akajizuia na kubakisha kelele hizo ndani yake.

Nani amefanya mauaji haya ofisi kwangu na anataka nini? Alijiuliza pasi na kupata majibu. Mara mlio wa gari likiingia getini ukasikika, Johnson akakumbuka gari hilo, akajua ni lile ambalo liliwapeleka mjini wale jamaa ambao sasa ni marehemu. Akasubiri kusikia nini kitazungumzwa, akaendelea kujilaza kimya.

“Enhe, nini kimetokea,” mmoja akamwuliza yule aliyesalia, tena kwa sababu alikuwa dereva la sivyo naye angekuwa tayari ‘*kang’ata gunia*’.

“Dah! Ni ngumu kueleza, tulienda kwenye ile ofisi lakini hatukupata zile *document*. Tuliporudi kwa Pinto akasema hatujui kutafuta, ikabidi twende sote lakini mara hii, Pinto akataka mimi nibaki garini wao watatu wakenda zao,” akaeleza.

“Kwa nini walitaka we ubaki garini?” akauliza kwa hasira.

“Pinto alisema kuwa nibaki garini ili kuangalia usalama na vile vile akanipa dakika tano tu kuwa wakiwa hawajashuka basi niende kujua nini kimetokea. Muda fulani Petros akanipigia simu lakini ikakatika. Nikajua tu kuwa amekosea, nikasubiri nikaona kimya, nilipoamua kwenda ndipo nikaona magari ya polisi yakifika eneo hilo,” Jose akajibu

na kuanzwa kububujikwa na machozi.

“Dah! Hii habari akiipata Dimens sijui itakuwaje. Unajua tumelipwa pesa nyingi sana kutekeleza hii kazi lakini sijui ni nini kinatokea,” akamgeukia tena Joze.

“Sasa, ni polisi au ni nani kafanya mauaji hayo?”

“Mi sijui!”

“Sawa, hatuna muda wa kupoteza, huyu apelekwe Mtwara kama tulivyoagizwa na huko ndo tutajua tunafanya nini...” aliyeonekana kama kiongozi akatoa amri na safari ile ikaandaliwa.

* * *

Mbwamaji Safari Lodge...

Kamanda Amata alitulia kimya katika moja ya vyumba ndani ya lodge hiyo. Akiwa kayabwaga kitandani makabrasha yale, ambayo aliyachukua ofisini kwa Johnson. Sasa ilikuwa tu ni wakati wa kuyasoma na kuyachambua kabla hajatoa taarifa hiyo kwa bosi wake. Kwa kukitazama tu kitambulisho kile cha Johnson tayari akamtambua kijana huyo kuwa ni agent wa siri wa CIA. Hii tu ilitosha kujua kwa nini katekwa na uhusiano uliopo kati yake na tukio hilo.

Kabrasha la kwanza lilikuwa limeeleza mengi sana kuhusiana na operesheni za siri ambazo bwana Johnson anazifanya ndani ya Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Kati ya operesheni hizi, Amata akajikuta akiijua moja tu, lakini hakuwa anajua kuwa ni CIA inahusika. Akasoma na operesheni nyingine hatari sana ambazo hata alitamani kufunga kabrasha hilo kwa jinsi mipango na utekelezaji vilivyosukwa kitaalamu.

Kuna vitu tunaviona vya kawaida sana kumbe loh, kuna maslahi ya watu! Akawaza huku akilifunga kabrasha lile na mwili ukimtetemeka. Akaliweka pembeni lile la kwanza ambalo katika sakata hili halikumsaidia sana kwani lilieleza juu ya oparesheni nyingine kabisa ambazo hata hivyo Kamanda Amata aliona si za kufumbia macho. Alifurahi kuzigundua kwani moja ya furaha ya mwanausalama ni hiyo, kujua kila kinachoendelea nchini kwake, iwe cha heri au cha shari. Hivyo katika hili akajiwekea nadhiri, kuwa akimaliza tu swala hili la kuisaka hiyo chanjo iliyoibwa atawasilisha yote haya kwa HOT kisha waanze kuyafanyia kazi moja baada ya jingine.

Kuna mambo ni hatari sana kwa usalama wa taifa lakini jamii na vyombo vya usalama vinachukulia kawaida! Akajiwazia huku akitikisa kichwa. Lile kabrasa juu yake liliandikwa 'Not for Unauthorized Eyes'.

Kabrasa la pili ndilo haswa lilikuwa likieleza juu ya swala la AIDIOSIS na mkataba wake ulioingiwa miaka kingi nyuma ikiwa ni moja ya sera ya kuboresha maisha. Kamanda akausoma mpango huo mchafu ambao haukupendeza hata kusomwa na binadamu. Mikataba iliyosainiwa ndani ya dokument hizo ilikuwa ni yakutisha kabisa, uhalifu wa mwanadamu dhidi ya mwanadamu mwenzake, anayejiona 'bora' dhidi ya yule anayemuona 'duni'.

Kitu gani hiki? Akajiuliza huku akifinya macho na kufinyua. Akaendelea kupekua mbele na kukuta viapo vilivyowekwa kwa yeyote ambaye atavunja mkataba huo. Hapa akakuta orodha ya majina ya watu waliokwishavunja mkataba na ndipo alipogundua kuwa hawa watu wengi wao walikufa katika vifo vya utata. Akayanakili majina hayo na kuyaweka pembeni kwenye kijitabu chake. Alipatwa hamu ya kujua watu hawa ni akina nani na wamekufaje ingawaje wachache alikuwa akijua. Kurasa mbili mbele akakutana na swala la Sir Drostdyhof Fenegan. Akamsoma mtaalamu huyo na ndipo alipokuja kujua muunganiko wa tukio hili.

Hata kama mi ni mvanausalama, haya sikuyajua. Dunia inaficha mengi! Akawaza huku akiendelea kusoma taarifa hiyo kama kitabu cha riwaya. Katika kurasa huu ndipo akapata kile ambacho kilikuwa kikimpa shida, Kelvin. Hapa akaona watu waliotumwa kuja kumshughulikia Sir Fenegan. Kelvin na Cindy. Akaendelea kusoma huko mbele na kugundua kuwa daktari huyo tayari alikwisha uawa na hawa watu.

Nini kikafuata? Akajiuliza, kisha akafunua kurasa nyingine za mbele na kugundua mpango mzima wa shirika la afya na lile la kijasusi la Marekani juu ya chanjo hiyo.

Huku walitumainisha kuwa wanaichukua kwa ajili ya kuendelea na vipimo zaidi kujua kama inafaa au haifai kutumiwa na binadamu lakini mpango wa nyuma ukawa ni kuzuia kabisa isiwepo duniani. Amata akagundua kuwa ugonjwa huu ni wa kutengenezwa na binadamu ndani ya maabara ilikuwa *'Biological Weapon'* yaani silaha ya kibaiolojia. Zaidi ya hapo akakutana na mengi ya kutisha, mkakati mzima wa jinsi gani ya kumtokomeza mtu mweusi ambaye wao wanamwita 'kizazi duni'. Zaidi ya hayo akakutana na kurasa nyingine mpya iliyoandikwa

'Section 2'. Katika kurasa za upande huu akakutana na mpangokazi wa pili, kikosi cha pili ambacho kilikuja kumaliza kazi na hapa ndipo palimtisha zaidi ya chochote. Kwa taarifa za vifo vya ajabu, uvamizi na kupotea kwa baadhi ya watu wa kikosi hiki kilichoitwa 'Team 2'. Katika watu waliorudi USA mmoja hakujulikana kabisa yuko wapi, jina lake la kificho likawekwa pale, 'Tetty'. Zaidi ya hilo, katika kurasa hizi ndipo akapata jibu la yule mwanamke aliyemkuta hospitalini akamjua kwa jina lake Cindy na kuwa alichukuliwa na wenyewe na kurudishwa Marekani ambako alifariki. Amata akashusha pumzi ndefu, alipojiangalia mwilini akakuta amelowa jasho na umeme umekatika kitambo yeye akiwa hana habari. Lakini akabaki na maswali mwishoni kuwa kesi hiyo imefungwa kwa agizo la rais wa Marekani.

Pamoja na yote aliyosoma, Amata hakujua mengi kuhusu nani hasa anapambana naye. Alijuwa kuwa hawa *CLA* si maadui wake, lakini nani yuko nyuma ya haya yote? Jina Dimens ambalo alikutana nalo kwenye kurasa ya 125 akalikeka pembeni. Akafunga lile kabrasha na kuliweka na lile lingine kisha akayatia kwenye mfuko wa plastiki, akachukua pamoja na kile kitambulisho cha Johson akakiweka kando. Akainuka na kuondoka zake. Kwa ujumla hakujua anaenda wapi. Wazo la wapi pa kwenda akalipata akiwa njiani.

B.O.T! Akawaza huku akikamata Barabara ya kurudi kivukoni kisha afike mjini. Ilimchukua saa moja na dakika kama ishirini hivi akawasili katika benki hiyo, akateremka na moja kwa moja akafika mapokezi.

"Nahitaji kuhifadhi nyaraka zangu!" akamwambia mhudumu.

"Nyaraka gani?"

"Mafaili kadhaa ya kibiashara," akamweleza kisha utaratibu ukafuatwa. Chini ya jengo hilo kulikuwa na sehemu kubwa ya kuhifadhi nyaraka zote za siri. Kamanda Amata akateremka pamoja na mtu mwingine mpaka huko shimoni. Akajaza fomu kadhaa kisha akahifadhiwa nyaraka hizo na kupewa funguo moja kwani katika sefu hizo huwa kunakuwa na funguo mbili; moja inabaki benki na nyingine hupewa mteja. Na ufunguaji wa sanduku hilo hutegemea funguo hizo mbili, huwezi kufungua kwa funguo moja, lazima zote mbili ziwepo.

Nje ya jengo hilo, Amata akainua simu yake na kupiga kwa Madam S, tayari mwanamama huyo alikuwa keshafika Ofisi Ndogo kama kawaida yake.

"Nakusubiri hapa, njoo haraka nataka kutoka!" Madam akamwambia

Amata kwa simu kisha kijana huyo akawasha gari na kuondoka. Lakini kabla hajafika akaingia kwanza kwenye ofisi nyingine ya wanasheria. Hapa, mmoja wa wanasheria hawa ni rafiki yake waliyesoma pamoja shule ya msingi, aliyejulikana kama, Mh. Namoto Godfrey. Hakuwa na mazungumzo mengi bali kusaini tu karatasi fulani fulani kisha akaondoka zake.

* * *

“Karibu, maana hatukupanga kuonana sasa!” Madam akamwambia Amata.

“Ndiyo ila nimekuja kwakuwa kuna mambo ya msingi sana inabidi tuyaweke sawa kabla sijaingia msambweni, maana hata sijui ni wapi tunaingilia,” Amata akamwambia Madam S.

“Mbona unanitisha?”

“Sikutishi, bali ndiyo ukweli uliopo!” akamjibu kisha akampa kile kitambulisho cha Johnson. Madam S akakipokea na kukitazama vizuri, akatikisa kichwa kisha akamtazama Amata.

“Huyu ni Johnson?” akauliza.

“Ndiyo! Anaitwa Regan McLean, Johnson ni kificho tu. Kwa maana nyingine mtu huyu ni *Resident Spy*,” Amata akaeleza kitaalam.

“*Legal* au *Illegal*?” Madam akaongeza swali kutaka kujua zaidi.

“Warusi wamekuharibu mama yangu! Ndiyo, ni *Illegal Resident Spy*,” Amata akajibu.

“Sawa, sasa nimejua kwa nini walimteka,” Madam akasema na baada ya hapo Amata akamweleza kila kitu alichokigundua juu ya sakata zima hilo. Madam S alibaki kinywa wazi, hakuamini anachokisikia kama ni cha kweli au cha kutunga. Pamoja na yote, hakumwambia kabisa juu ya yale makabrasha.

“Amata, unanisimulia hadithi za akina Mteko Vano au? Mbona kama riwaya fulani hivi,” Madam akauliza.

“Ni riwaya haswa na wachezaji wa riwaya hiyo ni TSA,” akamjibu. Madam S akakaa kimya kwa sekunde kadhaa, kisha akavuta droo yake na kuweka kile kitambulisho, akaifunga.

“Mauaji ya asubuhi leo umeyasikia?” Madam akauliza.

“Siyo tu kuyasikia, ndiyo ilikuwa stafutahi yangu kwa leo,” Amata akajibu na kumfanya mama huyo kujiegemeza kitini.

“Tayari?”

“Tayari! Kazi imeanza kunoga,” Amata akajibu. Kisha akaongeza na ombi.

“Madam nahitaji kuwajua watu hawa...” akampa ile orodha aliyoiandika likiwemo jina la Dimens. Madam akayatazama kisha akamtupia swali, “Mbona huyu Dimens umemweka peke yake?”

“Huyo ndiye adui mkuu katika sakata hili, na vibaraka wake ndiyo hawa waliokuwa ndegeni, Doddy na Kelvin kwa mujibu wa kile nilichokiona na kukiamini...”

“Umejuaje?”

“Kwenye ndege kulikuwa na watu wanne tu, Mellanie na Doddy marubani, Cindy na Kelvin ndiyo walikuwa wanaunda *Team 1*. Sasa mwili wa Mellanie tumeupata, tena ulilala kwenye kitanda change. Cindy tuna taarifa zake na wewe umenambia kwenye picha za rada kunaonekana watu wawili wameruka kwa mwamvuli, maana yake hawa ni Kelvin na Doddy kwa sababu taarifa niliyoisoma kwenye kompyuta ya Johnson ni hiyo kuwa ndani ya ndege walikuwa hao tu, ila bado *CIA* hawajagundua hujuma hii kinagaubaga..”

“Tuko mbele!” Madam akasema.

“Tena mbele sana!” Kamanda akamalizia.

* * *

Siku hii kwa Amata ilikuwa nzito sana, tangu tukio la asubuhi mpaka mchana na sasa tayari jua lilikuwa linatua.

“Vipi? Kula!” Gina alimwambia baada ya kuona chakula cha mpenzi wake kinapoa tu.

“Nakula mpenzi!” akajibu.

“Maana naona hauko hapa kabisa...”

“Ni kweli Gina, niko mbali sana, yaani pua zangu zanusa harufu ya kifo,”

“Kwa nini?”

“Hili sakata la sasa nahisi ni gumu sana, maana mpaka sasa sijui napambana na nani, yuko mbele yangu au nyuma yangu. Hawa jamaa wana mtandao mkubwa sana mpaka naogopa. Tazama walivyowaendesha hawa Wamarekani wanaojifanya majasusi wa dunia mpaka wamefunga faili, ndani ya miezi michache tu na si kawaida yao,” akasema.

“Wewe ni Amata Ric, Kamanda Amata, TSA 1, *Code 005*, hakuna kinachokushinda. Mimi ninaamini siku zote kuwa kwako kifo huletwa na Mungu na si mwanadamu, umesahahu haya? Ni nani aliyekata pumzi ya Tracy Tasha? Yuko wapi Kamanda aliyemfunga kinywa Bill Van Getgand? Ni Amata yupi aliyempasua George McField? Au si wewe uliyemaliza uovu wa Sir. Robinson Quebec na kumfutulia mbali muuaji Codec?... Amata, amka Amata! Usiniangushe mpenzi, nakuhakikishia ukirudi mara hii nakuzalia mtoto, tena wa kiume...” Gina akampa moyo na kumfanya kijana huyu kutabasamu. Kwa maneno hayo, Gina aliidhihirisha nguvu ya mwanamke.

“Sasa mtoto wa mimi na wewe atakuwa na talanta gani?”

“Ngumi tu, kama wazazi wake, atakua anakamata na kukomesha wizi wote wa kuku mtaani!” Gina akajibu kisha wote wakacheka kwa bashasha.

“Sikiliza Gina!” Amata akamwambia, kisha akatoa bahasha ya khaki na kumkabidhi.

“Kuna nini humu?” akauliza.

“Naingia katika kazi hatari na ngumu. Nikifa, mpe bahasha hii Madam S na si mtu mwingine, nikirudi unikabidhi mimi mwenyewe,” akamwambia. Gina akaisoma bahasha ile, juu ilikuwa imeandikwa ‘HARUFU YA KIFO’.

“Sawa mpenzi, ingekuwa heri kama unahisi unakufa basi tufunge ndoa kabisa,” Gina akasema akimaanisha.

“Utabaki mjane, halafu utanifanya nijisikie wivu nikiwa kaburini wakati midume mingine inapojibeeba na mi nikiendelea kuoza. *By the way*, umechelewa! Mi naanza kuwakabili watu hawa usiku huu,”

“Wapi?”

“Sijui! Naomba nipigie simu kesho saa mbili asubuhi,” Amata akamwambia Gina kisha akasimama tayari kuondoka.

“Amata, mbona leo sikuelewi? Umekuwa na mafumbo mengi sana kama mashairi ya Rangimoto...”

“*No time to waste dear!*” Amata akamwambia kisha akamkumbatia kwa nguvu na kila mmoja akaangusha machozi. Gina akamtoa Amata kifuni pake na kuvua mkufu wa dhahabu aliyovaa shingoni, wenye kidani chenye jina lake akamvika Amata.

“Na-ta-ka u-ru-di na mku-fu ... huu, hapa!” Gina akamwambia huku akilia kwa vikwifukwifu. Amata akamtazama msichana huyo, ambaye

ndani ya sura iliyopambwa kwa machozi, uzuri wake ulionekana wazi pasi na kificho. Wakabaki wakitazamana kwa jozi la sekunde, hakuna aliyemsemesha mwenziwe.

“Nakupenda Gina... na sina budi kukuaga,” akamwambia kisha akauweka mkono uliokunja ngumi kifufuni pake huku akimtizama mwanamke huyo. Gina naye akafanya vivyo hivyo, na wote wakatamka pamoja.

“For my people, for my nation!”

* * *

Dakika chache tu baada ya kuachana na Gina, Kamanda Amata alishika njia mpaka kituo cha polisi cha kati. Jioni hiyo alimkuta Inspekta Simbeye akiwa bado ofisini.

“Karibu kijana!” akamkaribisha, na Amata akavuta kiti na kuketi kimya.

“Mbona unaonekana una mawazo sana?” akamtupia swali.

“Ah! Kawaida tu. Vipi mtu wetu yupo?” Amata akauliza akitaka kujua habari za yule jamaa aliyemsulubu kule katika ofisi ya Johnson.

“Yupo nilikuwa nakungoja wewe tu...”

“Hamjamsemesha?” Amata akauliza.

“Tumemsemesha sana tu, hivi hapo alipo, yu nusu mfu,” Simbeye akamwambia Amata, kisha akampa karatasi ambayo ameandika mambo machache yaliyosemwa na mtu huyo. Zaidi akampatia na *cassette* ndogo ya sauti ya mahojiano. Akavichukua vyote na kuvitia mfukoni, kisha akaagana na Simbeye na kutokomea zake.

Breki zake zikamsimamisha katika hoteli moja ya kawaida sana maeneo ya Magomeni Mapipa. Akateremka na kuliacha gari nje. Ndani ya hoteli hiyo akachukua chumba kwa muda kwa kile alichokiita mapumziko, lakini haikuwa hivyo. Katika ghorofa ya tatu, akajifungia kimya na kuanza kuisoma ile karatasi na kujitahidi kuielewa. Mateka yule alieleza kwa mapana sana kuhusu misheni yao na nani aliyewatuma. Hapa alitajwa tena tajiri wa Kireno aliyechanganya vinasaba na Waswahili.

Torres Alexis Kazumari! Akajisemea na kuikunja ile karatasi, kisha akaitia mfukoni.

“Mapumziko yamekwisha! Kazi yangu inaanzia Mtwara. Nikimtia mkononi mshenzi huyu anayeitwa Torres nitajua nini cha kufanya. Kwa sasa yeye ndiye turufu yangu pekee... Nikiwa safarini kuelekea Mtwara lazima niache kazi kwa Gina kuifuatilia hii nyumba ya Mkuranga,

hakika ndipo palipo na kambi yao,” akajisemea kwa sauti ndogo.

Mara simu yake ikaita, pindi tu alipokuwa akisimama tayari kuondoka. Akaitazama na moja kwa moja haikumpa shaka. Akainua na kuiweka sikioni.

“TSA 4 nakusoma!” akapokea simu kwa mtindo huo, akimruhusu Scoba anayejulikana kiofisi kama TSA 4 azungumze.

“Fika Polisi Ufundi, katika ukumbi wa chakula haraka iwezekanavyo. Nikute pale!” ile simu ikakatika mara baada ya ujumbe huo. Amata akabaki kapigwa na bumbuwazi kwa kuwa hakutegemea kabisa simu ya mtu huyo kwa muda huo. Hakuchelewa. Akateremka chini haraka na kuuwacha ufunguo mapokezi huku akiahidi kurudi usiku huo.

Kutokana na foleni za Jiji la Dar’, hasa katika barabara hii itokayo Posta ya zamani kuelekea Kurasini, ilimchukua Amata dakika kama tisini kufika kituo cha Polisi Ufundi, Kilwa Road. Akaingiza gari ndani na kuliweka katika maegesho. Hatua za haraka haraka zikamfkisha katika bwalo ambako maafande wengi hupenda kukaa humo kuburudika na kinywaji au hata chakula. Haikumsumbua Amata kumwona Scoba kwani aliketi mahala pa wazi tu.

“Yes komredi,” Amata akamwambia Scoba, mara tu baada ya kuketi.

“Pole sana kwa mikikimikiki,” Scoba akamwambia nduguye.

“Nimepoa, lakini ndiyo kazi yetu,” Amata akajibu wakati huo mhudumu wa bwalo hilo upande wa vinywaji akawasili.

“Mmeshasikilizwa akina kaka?” akawauliza.

“Hapana,” Amata akajibu huku akimtazama, “Nipatie Safari Bia, sijui na mwenzangu...” akamwambia.

“No! hapana,” Scoba akakataa hoja ya Amata, “Yeye mpe maji, mimi nipe bia,” akamwambia na yule mhudumu akaondoka zake. Mazungumzo kati ya wawili hawa yakaendelea huku vinywaji navyo vikimiminwa matumboni mwao. Baada ya mazungumzo marefu, Scoba akamtazama Amata kisha akampa ishara ya kuinuka na kumfuata huku akiacha noti ya Shilingi 5000 mezani.

Wakatembea taratibu mpaka kwenye maegesho mengine ya upande wa pili.

“Kamanda huu ndiyo mzigo niliyokuitia,” Scoba akamwambia huku akimkabidhi funguo ya gari ikiwa ndani ya kijimfuko cha plastiki.

“Sijakuelewa Scoba...” Amata akasema huku akiutazama ule ufunguo.

“Najua una kazi kubwa na nzito, itakayokutaka kusafiri huku na kule. Ofisi imeniagiza nikuandalie gari hili ambalo si mara zote hutumika. Nimelifanyia majaribio na sasa liko sawa,” Scoba akasema. Amata

akabonyeza kibonyezo kimoja na taa za lile gari zikawaka na kuzima. Scoba akampa ishara waingie, akafanya hivyo huku yeye akiketi nyuma ya usukani.

“Kilimanjaro!” Amata akasema huku akiukamata usukani.

“Ndiyo, nakukabidhi gari hili, *Kilimanjaro XXXL new model*, , lina injini kubwa na yenye nguvu, silinda nane, lina uwezo wa kukimbia Kilomita mia nne kwa saa...”

“La haula!” Amata akahamaki.

“...*Linasense alcohol*, ndiyo maana nikakwambia usinywe. Ukinywa pombe haliwaki kwa sababu ili liondoke lazima utamke nywila yako kwa kinywa katika kioo hiki kidogo. Ukisoma kitabu chake cha maelekezo, basi utajua vyema linavyotenda kazi,” Scoba akaeleza.

“Chomeka funguo,” akamwambia, naye akafanya hivyo.

“Weka kiganja cha mkono wako wapa,” akamwambia na Amata akafanya hivyo.

“Tamka neno utakalo, na ndiyo itakuwa nywila ya kuwashia gari hili,” akamwambia. Amata akafuata maelekezo.

“Washa sasa!”

Amata akawasha gari, nalo likakubali bila hiyana.

“Thank you, your identification is acceptable and secure. Enjoy your Kilimanjaro super sonic speed car XXXL”

Sauti ya kike ikamkaribisha ikimwambia kuwa utambulisho umekubaliwa na kuhifadhiwa.

“Kuwa mwangalifu na wanawake,” Scoba akamwambia huku akiondoka taratibu kufuata lile gari alilokuja nalo Amata.

Kamanda akaliondoa taratibu na kutoka nje ya lango la kambi hiyo na kukamata barabara kurudi mjini. Hakika lilikuwa gari la kipekee sana kuanzia starehe ya ndani, muziki, na kila kitu kilikuwa cha kugusa tu.

“Torres Kazumari, kaa chonjo, usiku huu nitakuwa Mtwara,” akasema huku akibadilisha gia na kuongeza kasi.

* * *

Akiwa tayari katikati ya jiji, simu yake yenye majina ya marafiki ikaanza kuita. Namba hakuijua. Akawasha indiketa ya kushoto na kuegesha pembeni. Akachukua simu na kuiweka sikioni pasi na kusema

kitu

“Mimi Tausi naongea, wa *CdG Marine Tour*,” sauti ya upande wa pili ikamwambia. Amata akatulia sekunde mbili hivi akishusha pumzi, kisha akaamua kuijibu.

“Tumewahi kuonana?”

“Sasa ningejuaje namba yako? Si tulibadilishana kadikazi pale Msanga Mkuu Mtwara!”

“Anhaaaaa! Tausi! Nimekukumbuka sasa, niambie!” Amata akameza mate ya uchu. Maana jinsi tu alivyomuona mwanamke huyu wa Kimakonde siku ya kwanza, ucheshi wake na vishimo vya mashavuni, alibaki hoi. Kama isingekuwa simu ya Madam S siku hiyo mwanamke huyu asingepona.

“Nipo Dar! Nimekuja kikazi...” Tausi akasema.

“Umefikia wapi mrembo, kama upo radhi nije kukusalimia!” Amata akauliza.

“Nipo hapa, Green Valley Hotel, Room namba 126” Tausi akajibu.

“Sawa, nipe saa moja tu ijayo nitakuwa hapo,” Amata akajibu kisha. akajitazama kama jinsi alivyo anafaa kukutana na malaika huyo. Akaona hapana, hana budi kubadili nguo na kujiweka katika muonekano mwingine.

“Mbona sina sura ile anayojua?” akajiuliza kwa sauti kiasi kwamba kama kungekuwa na mtu kiti cha pili angesikia.

“Nifanyeje?” akajiuliza tena na hakukuwa na wakumjibu.

“*Any way*, naenda na sura yangu hii hii na nguo zangu hizi hizi,” akapitisha uamuzi na kurudisha gari barabarani kisha kuondoka.

SURA YA 16

MTWARA

USIKU HUO HUO katika mji wa mtwara, Toress alikata simu mara baada ya kusikiliza mazungumzo ya Tausi na Amata. Akatabasamu na kuinua simu yake nyingine.

“Hey Costa! Nimeshamnasa. Nilikwambia, huyu mwanamke atamtafuta tu. Sasa kaeni tayari, atakuwa hapo hotelini baada ya dakika arobaini na tano hivi. Hakikisheni mnaniletea hapa akiwa na pumzi. Tahadhari huyo jamaa ni hatari sana leo hii asubuhi kaua watu wetu wengine wawili. Sasa hakikisheni hamleti mchezo naye *unless otherwise* nitawakuta nanyi marehemu..”

“Usijali, sijawahi kukosea, na usiku huu ninakuletea huko Mtwara!”

“Sawa!”

Toress Alexis Kazumari akajiegemeza kitini na kufungua tabasamu pana huku akizungukazunguka katika kiti hicho.

Wakimleta hapa, ni moja kwa moja Cabo Delgado! Akawaza huku akiwasha luninga yake kubwa na kutazama habari ya saa mbili usiku ambayo ilitawaliwa na habari za mauaji yaliyotukia asubuhi ya siku ile katika Jiji la Dar es salaam. Haikumpendeza. Akazima na kuweka chaneli ya michezo kana kwamba ile taarifa ilikuwa ikimpa ukakasi wa moyo.

Si anajifanya mjanja! Atafika hapa leo hii niuone ujanja wake! Akawaza. Ijapokuwa Toress alijipa moyo lakini bado alihangaika moyoni kujua ni jinsi gani ataweza kuwa na huyo mtu akiwa hai mpaka amfikishe Cabo Delgado kama alivyoamriwa na bosu wake, Dimens. Mbali na hayo, aliendelea kupiga moyo konde huku akisubiri taarifa njema kutoka kwa vijana wake. Mara kwa mara aliingiwa na ubaridi kila alipoitazama picha ya Amata juu ya meza yake.

Piiip! Piiip! honi ya gari ikamfanya moyo wake upae kwa mshtuko,

akatazama kwenye runinga yake na kuona ni nani alikuwa akipiga honi hiyo.

“Oooh Jozé!” akatamka huku akibofya batani na lile lango likafunguka. Walinzi wa ndani ya wigo wakawapokea Wazungu hao watatu na kuwaelekeza wapi pa kuingilia huku wao wakimkusanya Johnson na kumwingiza katika chumba maalumu.

“*Bem-vindos Camaradas!*” Toress akawakaribisha jamaa hao katika sebule yake kubwa na mara tu mwanadada mrembo akawaletsa vinywaji vikali ili kuondoa uchovu wa safari.

“*Muito obrigado!*” wakaitikia kwa pamoja, kisha wakatazamana na kucheka.

“Sijafurahia taarifa niliyoipata kutoka Dar’ leo. Hivi huyu ni nani hata anatusumbua hivi?” Toress akaanzisha mazungumzo mara tu baada ya yule mwanadada kutoka mle ndani.

“Hata sisi mpaka sasa hatujajua, maana polisi walifika eneo lile na hatujui walipataje taarifa hizi,” mmoja akajibu.

“Ha! Mnafikiri aliyefanya kazi hiyo ni polisi?” akawauliza na kuwapa ile picha.

“*Quem é ele?*” yule aliyepokea picha hiyo akauliza kuwa huyo ni nani.

“*Ele é chamado Amata Ric,*” akawajibu kuwa anaitwa Amata Ric. Wale jamaa wakatazamana tena na kurudisha macho yao kwa Toress.

“Mnamjua?” akawatupia swali.

“Ndiyo, tuna taarifa zake tangu tukiwa Portugal, kuwa tuwe na hadhari sana na huyu mtu, hatukutegemea kama atakuwa pale...”

“Huyu ni shetani, si binadamu! Anaweza akaibuka hata hapa tulipo, mi sitaki kumwona kabisa huyu, na sasa nimetuma majini yakamkamate na usiku huu afike hapa. Mi nilitaka nimuue lakini Dimens anamtaka akiwa hai,” Torres akaongea kwa ukali.

“Tuliache hili, mmemleta Johnson?” akawauliza.

“*Yes!*”

Wakainuka pamoja na kuingia katika mlango fulani, kisha wakaibukia chumba cha chini na kufungua mlango mkubwa wa chuma. Kilikuwa chumba kama stoo kubwa yenye makorokoro mengi yaliyorundikwa huku na huko. Ningeweza kusema ilikuwa gereji au sijui ni karakana fulani. Johnson alikuwa katika moja ya minyororo mikubwa amening’inizwa na wale vijana huku miguu yake ikiwa nusu futi kutoka sakafuni.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Umekamatika, huna ujanja nyang’au wewe! Nyama yako itakuwa chakula cha nguruwe kwa Dimens. Tunasubiri

nyang'au lingine lifike hapa muda si mrefu muungane nalo," akamwambia kwa dharau na kummwagia pombe kali usoni. Toress na wageni wake wakatoka na kufunga lile lango.

"Ni kwa mara ya kwanza ngome ya Dimens inatikisika, na aliyeitikisa si hawa *CLA*, ni huyu kidudumtu anayejiita TSA. Nitaanza kumsurubu hapa kwa mkono wangu mwenyewe," akajigamba kisha akawataka wakapumzike lakini wao wakasema wanasubiri mpaka mateka huyo mwingine afikishwe hapo ili nao wamtie adabu.

* * *

Huko Dar es salaam, katika Hoteli ya Green Valley, chumba namba 126, Tausi aliendelea kujigeuzageuza kitandani huku akimsubiri yule aliyekuwa akimtaraji. Hakujuu lolote linaloendelea mpaka nukta hiyo. Kila aliposikia mchakacho wa viatu vya mtu atembeaye, moyo wake ulipaa kwa furaha, lakini bahati mbaya mtu huyo alipitiliza na kuingia mlango mwingine. Hata yeye mwenyewe hakujua kwa nini amempenda ghafla mwanaume huyo, ilhali ni mara moja tu wameonana, tena kwa sadfa. Aliitazama simu yake, hakukuwa na ujumbe wala *missed call*. Akaendelea kusubiri.

Nje ya hoteli hiyo, katika maegesho ya magari, vijana wawili walikuwa wamejificha kwenye mti wenye ukubwa wa wastani, wakimsubiri mtu huyo waliyetakiwa kumtia mkononi siku hiyo. Walichoambiwa na bosi wao katika mkakati huo ni kutoa taarifa tu kama amewasili. Ijapokuwa walikuwa wakipata tabu kupambana na mbu wenye njaa, waliendelea kusubiri hapo. Azma yao ilitimia dakika chache tu tangu wawe eneo lile. Mwanga wa wastani wa taa za gari ukawamulika na kisha ukaelekea upande mwingine. Lile gari likaingia maegeshoni na kuzima taa zake. Ilipita dakika tano, hakuna aliyeshuka kutoka katika gari lile. Baada ya kuzimwa injini, kijana mmoja mkakamavu kwa mwonekano, akateremka huku mkono wake wa kuume akiwa amebeba kasha la karatasi ngumu. Kwa wale wanaopenda kula, isingekuwa kazi kwao kujua kuwa ile ni *Pizza*. Hakuwa mwingine ni huyo aliyesubiriwa katika chumba namba 126. Kamanda Amata.

Kwa hatua zake za kawaida. Amata akatembea kuelekea mlango mkubwa wa hoteli hiyo na kupotelea ndani. Ghorofa ya kwanza akaifikia kwa kutumia ngazi, kisha akatafuta mlango aliyokuwa anautaka. Akaupata. Dakika moja na sekunde kadhaa ziliisha akiwa kasimama mlangoni huku hisia zake zikijaribu kuhisi chochote ama ndani ya chumba hicho

au nje. Alipojiridhisha na ukimya huo akakijaribu kitasa, umefungwa, akagonga mara tatu.

Kutoka chumbani, Tausi akakurupuka kitandani na kuuendea kwa shauku. Akaufungua mlango na kujikuta uso kwa uso na mtu asiyemjua.

“We ni nani?” Tausi akamuuliza huku akimtazama kuanzia juu hadi chini. Amata hakujibu ila akamsukumia ndani na yeye mwenyewe kuingia na kufunga mlango nyuma yake. Yule mwanamke akarudi nyuma haraka huku bado akiwa kwenye hamaki, akachukua chupa ya soda iliyokuwa juu ya meza.

“We ni nani? Usipojitaja nakupasua na hii chupa!” Tausi akasema kwa nguvu, Amata akabaki kumwalia mwanamke huyu mweusi mwenye umbo namba nane, miguu iliyojaa nyama na makalio yaliyobinuka kidogo. Ushoroba kati ya meno yake ya mbele katika kaakaa la juu la kinywa chake vilimwongezea urembo kila ulipoonekana.

“Tulia Tausi...”

“Umelijua jina langu?” yule mwanamke akauliza huku katoa macho.

“Pale Msanga Mkuu katika ofisi za *CdG Marine Tour* ulinipa kadikazi yako, nami nikakupa yangu. Nilikuwa na madevu hivi na sura ya kiutu uzima. Ile haikuwa sura yangu, nilifanya *make up* tu,” Amata akaongea kwa upole.

“Toka hapa! Sikujui, nyi’ ndiyo wabakaji nyie! Toka kabla sijapiga kelele!” Tausi akasema huku akizidi kurudi nyuma na mara hii akajikuta kafika ukutani.

“Sawa! Ninaondoka,” Amata akajibu na kuingiza mkono mfukoni, huku ule mwingine bado ukiwa na lile kasha, akatoa simu na ile kadikazi ya Tausi. Kwanza akampa lile kasha.

“Pokea, zawadi yako!” akamwambia.

Hakika hakuna mwanamke asiyependa zawadi, Tausi akavuta hatua na kuchukua lile kasha mkononi mwake. Hakulifungua. Akaliweka mezani huku bado machoye yakiwa yamejawa woga. Amata akatumia simu yake kuipiga namba ya Tausi kutoka kwenye ile kadi. Tausi akatupa jicho kwenye simu yake na kukuta jina lile lile ‘Spark’.

Katika hali isiyo ya kawaida, mwili wa Amata ukasisimka na vinyweleo vyake vikasimama kwa nusu sekunde, akaihisi hatari.

“Umekuja peke yako?” akamuuliza.

“Ndiyo, peke yangu” akajibu.

“Kwa nini umenifanya hivi?” Tausi akaongeza swali.

“Vip...” kabla Amata hajamaliza, taa ikazimika. Kwa akili ya haraka, akageuka mlango. Kachelewa. Ule mlango ukafunguliwa kwa

nguvu ukampiga usoni na kumchana sehemu ya mdomo wa juu. Akajikuta akipokea makonde mazito ya uso ambayo kwa uzito wake yalimchanganya kidogo. Alipokuja kukaa sawa, akamwona mtu hewani akija akielekea kifuaani mwake. Akamkwepa na kumtandika mapigo ya karate mgongoni na kuhakikisha amevunja pingili. Yule mtu akapiga yowe na kufika chini kama mzigo akijibamiza vibaya kwenye kona ya kitanda. Tausi akapiga kelele, na wakati huo huo Amata akasikia mlio hafifu wa bastola iliyofungwa kiwambo cha sauti. Ghafla mwanamke yule akawa kimya na kufuatiwa na kisindo cha kuanguka chini. Amata akajiweka tayari kwa mapambano. Mbele yake kulikuwa na mtu mmoja, na nyuma yake vilevile. Akawekwa kati. Ngumi ya kwanza ikamkosa, ya pili akaiepa kisha akarusha teke la nyuma na kumpata sawia tumboni yule aliyetaka kumshambulia kwa upande huo. Akamkamata wa mbele na kumtwanga vichwa vitatu vya maana. Jamaa akaguna kwa maumivu na kujikuta akienda chini. Kabla hajafika, akainuliwa na teke zito na kutupiwa upande wa pili.

"Tiiiiiyyyaaaaaa!" jamaa akatokea nyuma kwa nguvu zote. Amata, kwa haraka akachomoa kisu chake na kumdidimiza shingoni. Mjinga yule, akajibwaga chini akipigania maisha yake. Kabla hajajiweka sawa, Amata, akahisi kitu kizito kikimpiga kisogoni. Akajitahidi kugeuka na kukutana na mtu aliyeshika gongo kubwa. Hakuelewa kama alikuwa mmoja au wawili au wangapi maana macho yake yakaanza kupoteza nuru. Yule jamaa mwenye gongo hakuwa na huruma. Akadhamiria kumtandika la tumboni. Ijapokuwa alizidiwa lakini alijitahidi kutopoteza lengo. Alirudi nyuma kwa haraka na lile gongo likapita kando. Kutokana na nguvu aliyotumia jamaa yule, akapepesuka na kumpa nafasi Kamanda kumpelekea mapigo. Mapigo matatu ya karate ya hatari kabisa yakampata yule jamaa na kumsukumia mbali kidogo.

"Siku zako zimekwisha mbwa wewe!" Yule jamaa aliongea kwa ubabe. Amata akanyamaza kimya huku kichwa chake kikisumbuka kwa maumivu. Yule jamaa alipeleka pigo moja la nguvu likatua sawia kwenye paji la uso wa Amata. Akasukumwa nyuma na kujibamiza ukutani. Jamaa akaruka hewani kwa minajiri ya kumshindilia Kamanda ukutani kwa guu lake lakini akajikuta akitua peke yake wakati Amata keshahamia upande mwingine na mkononi mwake tayari alikuwa na stuli. Hakumpa nafasi adui yake. Akampiga na ile stuli ya mninga. Pigo lile likamchana vibaya ngozi ya uso. Yule mjinga akapepesuka na kusimama, akajishika kichwani, damu zimemtapakaa, akawa mbogo. Hatua tatu, akampiga kumbo Amata, wakasukumana mpaka kwenye dirisha kubwa la kioo na

kujibamiza kwa nguvu. Lile dirisha likatawanyika vibaya na kuwaacha wawili hao wakiagukia nje kutoka ghorofa hiyo.

Nje ya hoteli hiyo, Amata na adui yake walianguka vibaya kwenye bustani ya maua. Mpasuko wa kioo cha dirisha na kishindo cha mwanguko ule, kiliwavuta walinzi wa hoteli na watu kadhaa. Nukta hiyo hiyo, gari moja jeusi, subaru likasimama eneo hilo, watu wawili wakateremka haraka na kumchukua yule jamaa wakamtia kwenye gari na kuondoka naye. Amata akabaki pale chini akijigeuza huku na huko.

“Ginnnnnaaaaaaa!” akajitahidi kuita lakini sauti hiyo hakuna aliyeisikia zaidi yake. Akajihisi akitumbukia kwenye shimo kubwa sana na refu. Kamanda Amata akalala kimya juu ya zile nyasi huku damu zikimvuja maeneo ya kichwani, kisogoni pake.

* * *

“Pole sana jamaa!” kijana mmoja kati ya wale wawili alimpa pole huyo waliyemwoko huku akimpangusa damu na kumsafisha majeraha.

“Atakuwa amekufa yule!” yule jamaa akasema.

“Sidhani akaitikiwa...”

“Kichapo nilichompa ni cha mbwa mwizi,” akawaambia.

“Kufa? Sidhani, ila atakuwa ameumia sana kama ni hivyo...”

“No amekufa... siwezi kuliacha jiji hili mpaka nihakikishe hilo,” akawaambia wakati gari likiingizwa uani katika *godown* fulani huko Temeke Sokota. Wakateremka huku wakimkokota mtu wao mpaka ndani. Huko wakakutana na daktari wao maalumu ambaye alitumia *godown* hili kama kliniki kuwasaidia watu kama hawa.

* * *

Huko Mtwara, Toress alikuwa akizunguka huku na huko ndani ya jumba lake akisubiri habari njema kutoka kwa Joao na Costa, lakini kimya. Saa zikapita, mpaka akaanza kuingiwa na wasiwasi. Aliporudi katika sebule kubwa akawakuta wageni wake bado wako macho wakitazama mpira.

“Hakuna habari mpaka sasa, napiga simu ya Joao, haipatikani...” akawaambia.

Kila mmoja akatazama saa yake, naam, saa nne usiku ilikuwa ikiyoyoma kuelekea saa tano.

“Inawezekana kapata kikwazo huko!” Joze akajibu.

“Kwa Joao, si rahisi. Lakini, ngoja tumpe muda...” Toress akasema huku naye akijibwaga kitini. Wakati huo huo, simu yake ikapata uhai. Akatazama kwenye kioo na kuinyakua haraka, akaiweka sikioni.

“Joao!” Toress akaita, “Mbona unaongea kama unaumwa...?” akamuuliza kisha kikafuatia kimya akiwa anasikiliza upande wa pili.

“Unasema?” akauliza zaidi kana kwamba hajasikia alichoambiwa.

“Hakikisha unajua kama amekufa... na kama hajafa, fanya juu chini ujue wapi yupo, ikiwezekana tumteke akiwa hai ikishindikana tummalize,” akamwambia.

Ile simu ikakatika na uso wa Toress ulionekana wazi kukosa furaha, akajiegemeza kitini akiwa kimya kwa sekunde kadhaa.

“Vipi?” Joze akamuuliza.

“Watatu wamekufa, vijana na yule msichana niliyemtumia kama chambo naye ameuawa,” akawaambia.

“Oh come on!” Joze akapiga kite.

“Basi imeshatokea! Nimewapa kazi, ikiwashinda itabidi tutumie mbinu za kimafia,” Toress akasema.

“Atapatikana tu kwa nguvu yoyote...” Joze akasema kisha akainua bilauri yake na kujimiminia kinywani kinywaji chote.

Toress Kazumari akabaki kimya akijikuta hana la kusema. Kichwani mwake mawazo mengi yalipita na kupishana, alitamani apae mpaka alipo Amata na kumng’atang’ata mpaka ammalize. Hakuamini mara kadhaa alipoambiwa kuwa ‘fulani kauawa’. Akilini mwake, alijua tu kuwa kijana huyo anabahatisha lakini mara hii alijikuta akianza kumhofia adui yake.

“Huyu jamaa ananinyima raha sasa!” akasema.

“Kazi bado Toress!” Joze akamwambia chotara huyo. Akamtia moyo kwa maneno matamu ya kishujaa. Toress akawaacha wageni wake na kuingia kwenye chumba chake kidogo. Ndani ya chumba hiki aliketi kitini mbele ya kompyuta na kuandika taarifa fupi kwa Dimens ambaye kwa hali zote alikuwa anasubiri taarifa nzuri kuliko hiyo.

* * *

Usiku wa saa tatu na nusu hivi, Gina alishtuka usingizini mara baada ya kifaa chake maalumu kumpa taarifa. Mlio hafifu uliosikika ulimfanya akikamate kifaa hicho cha *XT2IT* na kutazama katika kioo. Hakujiuliza swali alikurupuka haraka na kuliwahi kabati lake. Akachukua jinzi na kuvaa kisha fulana yake pana kidogo, viatu vya

mpira na kofia. Akaiendea droo yake na kuchukua bastola, akaifutika kiunoni ikiwa imesheheni risasi, na *magazine* nyingine mbili akazibana na mkanda wa jinzi hiyo. Mwisho akachukuwa kifaa chake hicho na kukivaa mkononi, akatoka kama mwenda wazimu na kujitupia garini huku geti likifunguka taratibu.

Ndani ya gari hilo, akafyatua simu ya upepo na kubofya nobu moja, simu ile ikawaka na kuruhusu mtumiaji kuongea.

"TSA 1 in danger! Location, Green Valley Hotel!"

Gina akasema kisha akaingiza gari barabarani na kuikamata barabara ya Old Bagamoyo. Mbele kidogo akakunja kushoto na kuchukua barabara ya kutokea Rose Garden, na alipoikuta ile ya kuelekea Mwenge, akakunja kulia na kubadili gia huku akiongeza kasi. Kifua chake kilikuwa kikipanda na kushuka kwa hamu ya kufika mapema eneo la tukio. Wakati anakunja kona kuchukua Barabara ya Shekilango kuelekea barabara ya Morogoro, akapishana na gari la wagonjwa likiwa kasi sana huku likipiga king'ora, na nyuma yake likifuatwa na gari la polisi. Akajikuta akifunga breki ya ghafla na mara nyuma yake kikasikika kishindo kikubwa.

"Nini sasa hii?" akasema huku akigeuka nyuma kutazama na kukuta gari lililo nyuma yake likiwa limemgonga. Hakuumiza kichwa wala kufikiri, akawasha gari na kuondoka kwa kasi kuendelea na safari yake. Dakika kumi baadae, akawasili katika hoteli ile, aliposhuka tu, macho yake yakalakiwa na kundi la watu. Hakuuliza wala kujiuliza, kasi yake ilikuwa ikielekea ndani ya hoteli ile. Lakini akajikuta ghafla akidakwa mkonowe na kurudishwa nyuma. Gina akatoa tusi baya kumwelekea huyo aliyemshika.

"Acha matusi msichana!" sauti ya Scoba ikamwambia.

"Oh! Samahani!" Gina akawa mpole na kumtazama kijana huyo, mfanyakazi mwenzake katika idara moja, nyeti, ya serikali. Akamvuta pembeni na kumkumbatia.

"Usifanye vitu kama mtoto, Gina. Unaenda wapi?" Scoba akamuuliza.

"Mxiuuu!!!" akasonya na kutulia kwa sekunde kadhaa.

"Huyu hapa! Mshenzi sana!" sauti ya kijana mmoja ikasikika na kuyavuta masikio ya wengine waliokuwa hapo.

"Nani hawa?" Scoba akamuuliza Gina baada ya kuona vijana wale wakimfuata.

Gina alipowatazama akamkumbuka mmoja wao, akajua ni wale wenye gari lililomgonga nyuma pale kwenye kona ya kuingia barabara ya Shekilango kutoka ile ya Bagamoyo.

“Nimeharibu gari lao...” akamjibu Scoba.

“We msichana mshenzi sana! Yaani unanisababishia ajali, kisha unakimbia...” sauti ya kilevi ya yule kijana ilitiririka na matusi ya aiibu. Scoba alikuwa kimya akisikiliza huku bado akiwa amemkumbatia Gina.

“Kwa hiyo matusi ndiyo yananyoosha gari lako?” Scoba akamuuliza.

“Na we braza akili yako kama demu wako tu, ***** zako,” akatukana huku mwenzake akiwa tayari keshamfikia Gina na kutaka kumtoa mikononi mwa Scoba. Lakini kabla hata hajafanya hivyo akajikuta chini kwenye vumbi, mita kama mbili hivi. Hakujua nini kimempata mpaka kufikia hali hiyo. Scoba alikwishampa pigo la dharula.

“Ninyi si mnapajua polisi! Nendeni mkashtaki kuwa mmegongewa gari lenu...” Scoba akawaambia huku akimwondoa Gina kuelekea pale alipoegesha gari. Akalizunguka nyuma na kuona jinsi lilivyobonyea kisha akatazama la wale jamaa lilivyofumuka boneti na shoo ya mbele ikiwa inaning’inia. Alitamani kucheka kwa monekano huo lakini akatulia. Aliwatazama wale jamaa wakija upande ule, akawasubiri huku tayari Gina akiwa kwenye kiti cha abiria.

“Sasa braza, tuelewane, tumalizane, mi nikanyooshe gari langu..” yule jamaa akamwambia Scoba ambaye tayari alikuwa ameshafungua mlango kuingia ndani.

“Tuelewane? Kwani hapa nani kamgonga mwenziwe? We kama unataka ulipwe nenda polisi, wao ndo’ wanajua sheria za barabarani,” akamwambia huku akiingia ndani na kufunga mlango.

Ndani ya gari, Scoba akashusha pumzi ndefu, kisha akapiga usukani kwa mikono yake miwili na kutulia kimya akitazama nembo ya gari hiyo iliyo katikati ya usukani.

“Scoba!” Gina akaita.

“Yes Gina! Nambie...”

“Umemwona Amata?”

“Ndiyo, amechukuliwa na gari la wagonjwa kakimbizwa hospitali?” Scoba akajibu. Gina akavuta kumbukumbu na kukumbuka lile gari alilopishana nalo.

“Atakuwa mzima? Maana Kamanda mpaka atumie *EX* ujue hali ni tete,” Gina akaongea kwa upole huku machoye yakiwa yametona machozi yasiyotaka kuanguka.

“Tulia Gina. Jasmini atakuwa huko atatujulisha hali yake...”

“Ameenda?” Gina akauliza kwa shauku. Scoba kabla hajajibu, akabaki kimya akikodoa macho upande wa hoteli huku akimshtua Gina kwakumgusa paja. Gina naye akageuka kutazama. Machela tatu

zilikuwa zimebeba watu; mbili zilifunikwa kabisa ikiwa ni ishara kuwa waliobebwa hawakuwa na uhai na moja ilifunikwa nusu na muuguzi mmoja akiwa na dripu mkononi mwake. Zile machela zilizofunikwa zikapakiwa ndani ya Land Cruiser la polisi na dakika chache baadae, likaondoka. Ile machela nyingine ikapakiwa kwenye gari la wagonjwa la serikali lililosimamishwa hapo likiwa na safari zake. Simu ya Scoba ikaita, akaiinua na kuona namba ya Chiba. Akafyatua na kuiweka sikioni.

“Tukutane *AGI* haraka!” sauti ya Chiba ikamwambia na kisha simu ikakatika.

* * *

Ndani ya ofisi ya *AGI Investment* ambayo Kamanda Amata na Gina hufanyia kazi zao, watu watano walikuwa wameketi kimya. Jopo hili kuwa hapa kwa dharula, haikuwa kawaida. Ukimya ulijidai kati yao, kila mmoja alionekana kuwaza lake lakini hakuna aliyesema chochote. Simanzi. Madam S alikuwa akiwatazama vijana wake kwa zamu, aliyasoma mawazo kupitia macho ya kila mmoja wao. Dakika kumi za ukimya zikazimwa na kelele ya simu juu ya meza hiyo. Macho ya Madam S yakampa ishara Jasmine kuipokea kwani yeye ndiye anayeweza kuelewa misamiati ya kiganga. Hakuwa na shaka kwani alijua kwa vyovyote simu hiyo itakuwa ni kutoka hospitalini kwa kuwa ndiko alikoacha namba ya simu hiyo.

“*AGI Investment*, hello...” akaita na kutulia kusikiliza sauti ya upande wa pili.

“Hello! Hapa ni hospitali ya Agha Khan ...”

“Endelea...”

“Tumempokea mgonjwa wenu saa moja iliyopita. Huduma imeanza kufanyika, na taarifa ya awali ni kuwa mgonjwa amepata *Severe Traumatic Brain Injury... glas-gow coma scale* yake tatu chini ya kumi na tano,” mtu wa upande wa pili akaeleza.

“Oh *shit!*” Jasmine akajikuta kwenye bumbuwazi.

“Kuweni na subira, tutawajuza zaidi...” ile simu ikamwambia. Daktari Jasmine akaishusha na kuiweka kwenye kikatio chake. Kisha akainua uso na kuwatazama.

“Vipi?” Madam S akauliza, ikiwa ndilo neno lake la kwanza tangu waingie katika ofisi hiyo.

“Hali si nzuri. Daktari anasema, Amata amepatwa na *TBI*, yaani

ubongo wake umepata shida, labda alipigwa kichwani, lakini daktari anasema hana fahamu kabisa wanachokiona kwake ni kupumua tu na si kingine, hana hisia yoyote...” Jasmine akasema kwa kukata tamaa. Chozi likamdondoka mezani, na kila mtu akalishuhudia.

“Chozi lako linamaanisha nini? TSA 1 hawezi kupona?” Madam S akauliza. Na kwa swali hili, kila mmoja akatega sikio kusikia nini Jasmine atasema, kwa kuwa yeye alikuwa ni daktari mbobezi ndani ya kitengo cha TSA.

“Kuna mawili...” Jasmini akaanza kueleza.

“Yaani kufa au kupona. Si ndiyo?” Madam akamalizia.

“Ndiyo ...” Jasmine akajibu.

“Hayo ya kawaida kwa mwanadamu...” Madam S akajibu na kutulia kimya akitafakari jambo, kisha akafungua kinywa chake tena, “Akifa tutamzika kwa heshima zote, za kijeshi, kishujaa na kidini na za kiTSA...” akaeleza.

Wote wakatikisa kichwa kuashiria wameelewa maneno hayo. Hawakuwa na budi kujikaza kiume kwani kazi yao ilieleweka vyema, maisha yako unatembea nayo mkononi.

“Hilo, halina shaka Jasmine, usilie... sasa nieleze upande wa pili, anaweza kupona?” Madam S aliuliza tena.

“Ndiyo! Anaweza kupona kwa asilimia kubwa tu lakini tukae tukijua kwamba; kwa kile ambacho daktari amekieleza, ni binadamu wachache sana wanaopona na kuwa katika hali ya kawaida. Sasa hatujui katika hao wachache kama na yeye atakuwepo au la, hapo ni Mungu na Malaika wake,” Jasmini akasema. Kisha akatulua kwa sekunde kadhaa.

“Hilo ndilo tunalolihitaji, kwa gharama yoyote ile. Hata kama nchi itabidi ikope benki ya dunia, hilo ndilo tunalolihitaji...” Madam S akasema.

“Ni kweli, kwa sababu ili arudi kwenye hali ya kawaida tunahitaji timu kubwa ya madaktari wabobevu watakaofanya kazi usiku na mchana bila kuchoka. Na tunahitaji hospitali kubwa ya kisasa itakayoweza kufanikisha hilo, yenye mitambo tiba ya kisasa...” Jasmini akaeleza.

“Sawa! Kamanda lazima arudi kwenye hali yake ya kawaida, labda tushindwe kabisa au Mungu aamue vinginevyo. Sasa ipo hivi, mnisikilize ... Tunasitisha shughuli zote kwa sasa, na nguvu yetu itakuwa kwa afya ya Amata tu. Kwa hiyo kila mtu arudi kwenye shughuli zake za kawaida kuanzia sasa na atafanya lile tu ambalo ofisi itamtaka, sawa?”

“Sawa!” wote wakajibu.

SURA YA 17

ASUBUHI YA SIKU iliyofuata, Joao alikuwa akijisikia vyema kabisa. Mazoezi madogo madogo yalikuwa yakimpa ahuwani ya afya na maumivu yake ya usiku uliyopita. Pembani yake daktari aliyekuwa akimtibu alikuwa akifuatilia kila kitu. Wakati yote hayo yakiendelea simu ya mkononi ya kijana huyo ikaita. Akateremka kutoka katika mashine aliyokuwa akifanyia mazoezi na kuichukua.

“Boss!” akaita.

“Yule jamaa amelazwa Agha Khan. Taarifa zilizonifikia mapema asubuhi hii, lakini hana fahamu yoyote...” sauti ya Torres ikayafikia vyema masikio ya Joao. Kijana huyo akahisi moyo ukianza kumwenda mbio.

“Hajafa?” akauliza.

“Sasa angekuwa amekufa ningekwambia amelazwa? Fanya juu chini umalize kazi hiyo leo. Wewe unajua njia zote za kuingia sehemu kama hiyo. Hakikisha unamkata pumzi maana kumchukua mzima hatuwezi tena,” Torres akamwambia Joao.

“Sawa Boss, tegemea majibu mazuri... na vipi hawa wenzetu wa jana?”

“Achana nao, kama hawana ndugu basi watazika na halmashauri ya jiji...”

Joao, akatulia kwa sekunde chache kisha akaitikia na kukata simu. Hakuendela na zoezi tena; akaingia ndani na kuanza kupanga safari yake hiyo. Hakuona haja ya kuchelewa kwani Waswahili wanasema ‘biashara asubuhi’. Vifaa vichache ambavyo aliona vinafaa akaviweka kwenye mkoba wake. Akawataarifu vijana wake kuwa wawe tayari kwa safari hiyo ya kuelekea Agha Khan.

* * * *

HOSPITALI ya Agha Khan

Dkt. Prakesh alifunga kabrasha lake lenye taarifa zote za Mr. Spark na kulisogeza kando. Daktari huyu, Mtanzania, mwenye asili ya Kiasia, alijikuta katika wakati mgumu alipopewa oda ya kuuondoa uhai wa mgonjwa wake mara tu baada ya kukata simu iliyomuunganisha na jopo la TSA. Baada ya kuiweka simu ile chini, simu yake ya mkononi iliita kwa namba ngeni naye akaipokea na kuisikiliza. Si kwamba alikuwa hajui kuwa inatoka wapi, la, ila alishitushwa na ujumbe wa simu hiyo.

"You have to kill him! Kwa gharama yoyote..." aliambiwa.

Si kwamba angeshindwa lakini maadili ya kazi yake hayakumruhusu. Akakumbuka mara tu baada ya kupokea gari la wagonjwa hospitalini hapo katika kitengo cha dharula, ni yeye aliyekabidhiwa mgonjwa huyo.

"Mr. Prakesh!" sauti ilimwita nyuma yake alipokuwa kwenye haraka ya kuingia katika ofisi yake.

"Nina haraka tafadhali, tuongee baada ya kazi," akamjibu aliyemwita hata bila kumtazama.

"Najua, ila hakuna mazungumzo, ni karatasi hii tu basi, ichukue tafadhali" yule bwana akamwambia. Prakesh hakugeuka nyuma badala yake alinyoosha mkonowe kwa nyuma na kukabidhiwa karatasi hiyo.

Kabla ya yote haya, Prakesh baada ya kumuona mgonjwa mara kadhaa na kuanza taratibu za matibabu, alimweka katika chumba cha wagonjwa mahututi. Chumba cha peke yake na muuguzi tu. Hapo akaikumbuka ile karatasi na kuichukua. Haikuwa na mambo mengi; namba mbili za simu ndizo ziliandikwa hapo. Hakusita, akachukua simu yake na kuipiga.

"Mgonjwa wetu yu katika hali gani?" akaulizwa kutoka upande wa pili.

"Hali yake si nzuri, tumemlaza kwa kuwa hana fahamu kabisa..." akamueleza huyo aliyempigia.

"Asante daktari, tupo chini ya miguu yako, tunaomba kwa gharama yoyote apone..." mtu yule akasisitiza na simu ikakatika. Prakesh akashusha pumzi na kujiweka vyema kitini pake.

Huyu ni nani? Daima sipendi kuingiliwa kazi na mtu wa nje. Kupona au kutokupona kwa mgonjwa ni majaalwa ya Mwenyezi Mungu! Akawaza kisha akainuka na kuchukua stethoscope yake na kuiweka shingoni, na sphygmomanometer akaitia katika mfuko wa koti lake, akatoka na kufunga ofisi.

Baada ya dakika kama arobaini na tano hivi, alirudi akiwa na

kabrasha mkononi mwake, akaliweka mezani na kuanza kuandika vitu fulani fulani. Akiwa karibu kabisa na kumaliza kazi yake hiyo ndipo akagundua kadikazi iliyokuwa juu ya meza yake. Akapiga namba iliyopo na kutoa taarifa aliyotakiwa kutoa akakata simu na kutulia kimya.

Takribani dakika mbili baadae, mlango wa ofisi yake ukagongwa na kufunguliwa. Mtu mmoja, mwanaume mrefu aliyevalia suti nadhifu ya gharama kubwa akajikaribisha na kuketi kitini, akakunja nne, na kuondoa miwani usoni pake.

“Dkt. Prakesh!” akaita huku akiweka ule mkoba wake mezani na kumsogezea Mhindi huyo.

“Mkoba huu ni kwa ajili yako...” akamwambia. Baada ya hapo akainuka tayari kuondoka.

“Umetoka wapi, na wewe ni nani?” Prakesh akauliza.

“Kila kitu kipo ndani, maelekezo yote na kadhalika!” yule bwana akajibu na kuipachika miwani usoni pake, kisha akatoka na kuufunga mlango nyuma yake.

* * *

Dkt. Prakesh, akaufungua ule mkoba, alichokikuta ndani yake hakuamini macho yake. Moyo ukamwenda mbio, akapumua haraka haraka, na alipohisi utulivu, akachukua kijikaratasi kilichokuwa juu yake, akakifungua.

*Just kill the patient! We do not need him...
you have only ten minutes to do so.*

*Unless otherwise, we will stop your breath in any way,
we are after you!*

Ujumbe ule ulisomeka namna hiyo, ukimtaka amuue mgonjwa aliyempokea na akapewa dakika kumi tu. Kama asipotekeleza basi angeuawa yeye. Na ndani ya mkoba ule kulikuwa na bandali tano za noti za Kitanzania. Kwa haraka haraka kulikuwa na kama Shilingi Milioni tano hivi. Mhindi huyu akajikuta njia panda. Afanyeje? Atekeleze lipi, amuue mgonjwa achukue noti hizo na kuepuka kifo, au amuache abaki hai? Mtihani. Katika yote hayo aliujali zaidi uhai wake kuliko hizo pesa.

Ina maana wananunua pumzi ya mtu? Akajiuliza huku kijasho kikimtiririka kila kona ya mwili wake.

IKULU - Magogoni

Katika ofisi moja ya siri ndani ya Ikulu ya Magogoni, Madam S alikuwa ameketi mkabala na Rais wa nchi. Mazungumzo ya watu hawa wawili yalichukua nafasi. Hoja kuu ikiwa ni juu ya Amata. Mkuu wa nchi alishtushwa sana na taarifa aliyoipata kutoka kwa Sellina kuhusu hali ya TSA 1.

“Wamejua kuwa wakimmaliza huyu watakuwa wametuweza?” akamuuliza Madam S, naye akajibu kwa kutikisa kichwa. Rais akatikisa kichwa kupingana na hilo.

“Sasa wewe na ofisi yako mmejipangaje?” Rais akauliza.

“Tunataka tumhamishe haraka kuelekea kwenye hospitali kubwa nje ya nchi. Tayari daktari wetu anafanya mpango katika hospitali ya Apollo huko India, akipata nafasi tu tutamhamisha...”

“Oh! Safi sana, popote mtakapokwama, mnipe taarifa haraka sana, na hata hivyo nitatoa oda sasa hivi ndege ya Rais ikae tayari ili afike mapema zaidi. Na hili kundi lazima tulifutilie mbali...” Rais akasema kwa ghadhabu na wakati huo huo akainua simu na kupiga kwa mamlaka ya anga ili waanze kufanya utaratibu wa kupata kibali cha kuingia huko.

Wakiwa bado ndani ya ofisi hiyo, simu ya Madam S ikaita, akaichukua na kutazama. Dkt. Jasmin.

“Yes Jasmine!” akaipokea simu hiyo na kuchukua kama sekunde thelathini kuisikiliza.

“Mheshimiwa!” akamwambia Rais.

“Nakusikiliza...”

“Taarifa kutoka kwa daktari wetu zinasema kuwa nafasi imepatikana hivyo killichobaki ni mpango wa usafiri,”

“Hilo halina tabu kabisa...” Mkuu wa nchi akajibu, na wakati huohuo simu yake ikaita, akaipokea na kuzungumza na mtu aliyepiga.

“Sellina! Kila kitu tayari, mfikisheni mgonjwa uwanja wa jeshi, mtaondoka na ndege ya serikali, Private Jet ya Rais, yenye kasi, mtafika mapema tu. Nawatakia yote mema kabisa na unijulishe kila hatua ili nitoe msaada kama ukihitaajika. Nahitaji apone na arudi katika hali yake... *all the best*,” akamaliza na kuagana na Madam S.

HOSPITALI ya Agha Khan

Ukimya ulitamalaki katika chumba maalum alicholazwa Amata. Mitambo tiba iliyokuwa ikiendesha maisha ya mgonjwa huyo ilifanya

kazi kimyakimya. Zaidi ya mgonjwa huyo ni muuguzi mmoja tu wa kiume aliyekuwa kando ameketi kwenye kiti chake chenye meza ndogo ambayo juu yake kulikuwapo kabrasha na kikasha kidogo cha dawa. Kijana huyu macho yake hayakuwa mbali sana na mashine zile. Kila wakati alizitazama na kuandika kile kinachoonekana katika kioo chake.

Ilikuwa yapata saa tatu tangu Kamanda Amata kufikishwa juu ya kitanda hicho, muuguzi huyo alipoona kitasa cha kidijitali kikijifyatua. Akatazama mlangoni kutaka kujua ni nani anayeingia muda huo. Kijana mmoja mrefu, aliyevaa koti la kidaktari na kabrasha mkononi mwake alijitoma ndani na kuurudisha mlango ule nyuma yake.

“Habari kijana!” akasalimia.

“Nzuri, karibu...” yule muuguzi akamkaribisha huku akiinuka kitini.

“Mgonjwa anaendeleaje?” akahoji.

“Hali bado, tunategemea madaktari bingwa kufika hapa kwa ajili ya usaidizi...” yule muuguzi akajibu akiwa hajui kama kuna mpango wa siri wa kumwondoa hospitalini hapo.

“Oooh! Tumekwishafika, na wenzangu wataingia hapa muda si mrefu... labda aaaannh unaweza kunipisha kidogo kuna *procedure* nataka kufanya mara moja...” yule jamaa akamwambia muuguzi. Yule kijana akamshangaa daktari huyo, hakutegemea hilo kwani kiutaratibu lazima muuguzi awepo wakati daktari anafanya jambo lolote kwa mgonjwa.

“Samahan! Umesema?” akauliza tena kana kwamba hakisikia.

“Nimesema nipishe kidogo!”

“Utaratibu katika wodi hii, sitakiwi kumwacha mgonjwa na mtu mwingine yeyote hata kama ni daktari au mama yake. Kwani dokta hujui kuwa hii ni *ICU*?” yule kijana akasema.

“Unanifundisha kazi?” daktari yule akaongea kwa ukali.

“Sikufundishi, ila nakushangaa kwa sababu haijawahi kutokea, au la uwe na kibali maalumu kutoka kwa Mganga Mkuu kuwa ifanyike hivyo,” yule kijana akamwambia kwa kujiamini kabisa.

Nje ya Hospitali

Dakika kumi kabla

Gina na Daktari Jasimine waliwasili katika viwanja vya hospitali hiyo, wakiambatana na Madam S. Wakaegesha gari vizuri na kuteremka. Muda huo huo, gari jingine aina ya Volvo, saloon, jeusi, lenye vyoo vyeusi nalo likaegeshwa karibu sana na gari walilokuja nalo Madam S na mabinti zake. Lile Volvo likafunguliwa mlango wa mbele, akashuka

kijana mrefu aliyevalia suti nadhifu. Mkononi mwake alishika mkoba mweusi wa ngozi, akaupachika begani. Baada ya kuongea maneno machache na dereva wake, akaondoka kuelekea ndani ya jengo la hospitali hiyo. Yote hayo yalishuhudiwa na macho sita ya TSA hawa wa kike. Gina akachukua miwani yake maalumu na kuivaa, akaiweka sawa na kutazama kupitia vioo vya gari hilo. Kutokana na teknolojia ya miwani hiyo, Gina aliweza kuona ndani ya gari lile wote waliokuwamo.

“Wapo wanne, na aliyeshuka!” Gina akasema, na ghafla akamshika bega Madam S.

“Vipi?” Madam akauliza.

“No! hawa si watu wazuri, tumwokoe Amata, *please!*” Gina akapiga ukelele garini baada ya kuona wale waliobaki ndani wakiweka sawa silaha zao. Gina akateremka haraka, akifuatiwa na Jasmine. Madam S akabaki garini akiwaangalia mabinti hao wakiwa na haraka kuelekea ndani ya hospitali hiyo.

* * *

Gina alifika moja kwa moja katika dawati la mapokezi, pasi na simile, akawasukuma aliyowakuta huku akishika kitambulisho chake mkononi.

“Polisi, polisi, nioneshe chumba cha Daktari Prakeshi, haraka tafadhali,” akamwambia mhudumu.

“Korido ya pili, kushoto, chumba namba saba,” akajibiwa.

“Asantel!” Gina akajibu na kuanza safari hiyo kwa kukimbia huku akishuhudia Jasmine tayari keshakunja kona kuelekea upande huo. Hatua kama kumi na tano nyuma yao, walinzi wa kampuni binafsi walikuwa wakiwafuata kutaka kujua kulikoni.

Dkt. Jasmin alikuwa wa kwanza kuufikia mlango wa ofisi ya daktari Prakesh. Alipotaka kuufungua akagundua kuwa kitasa cha mlango huo kimevunjwa kwa nje.

“Shiit!” akang’aka na kurudi nyuma hatua tano kisha kwa kasi akakimbia na kuruka hewani akitanguliza miguu yake miwili. Jasmine alitua kwenye mlango kwa kishindo.

Kitasa kikafyatuka na kipande cha ubao kikamegeka. Mlango ukafunguka na kujibamiza upande wa nyuma. Wakati huo Gina alikuwa tayari na bastola mkononi, risasi moja tayari imeshaingia chemba ikisubiri amri tu ya kidole cha shahada cha mrembo huyo. Lakini ghafla wote wakapigwa na bumbuwazi, Gina akashusha bastola

yake chini akisonya kwa nguvu huku akigeuka huku na huko.

“Mwanaharamu!” akasema kwa gadhabu huku macho yake yakiutazama mwili usio na uhai wa Prakesh ukiwa kitini. Kifuani pake, upande wa moyo, kulionekana mchirizi mwembamba wa damu katika koti lake jeupe. Tayari tukio lile lilikwishavuta watu ndani ya hospitali hiyo, wauguzi, wafanyakazi wengine na waliokuja kutazama wagonjwa.

“Askari, toa watu nje, gari lolote lisitoke getini kuanzia sasa, wala mtu yeyote asitoke nje ya geti...” Gina akatoa amri kwa wale walinzi binafsi wa kampuni kongwe nchini. Nao mara moja wakajua nini wanapaswa kufanya. Baada ya hapo, kitendo cha haraka Jasmini tayari alikuwa akikwea ngazi kupanda ghorofa ya pili ambako alijua wapi Kamanda Amata amelazwa.

* * *

Chumba 117 ICU

Mabishano kati ya muuguzi na daktari aliyekuja bila utaratibu yalifikia pabaya. Yule jamaa alirusha ngumi iliyotua sawia kwenye shavu la muuguzi yule. Kutokana na kuwa mwili wake haukuwa katika hali ya kimapigano, yule kijana alishtuka mishipa ya shingo na kujikuta akianguka vibaya. Muanguko ule ukafikia kwenye nyaya zilizokuwa zikiendesha mitambo tiba kutoka mwilini mwa Amata, zikafyatuka na kuchomoka.

“Kufa tu, msh...!” yule daktari mvamizi kabla hajamaliza kutamka, mlango ulipigwa teke na kufungukia ndani, ukambamiza mgongoni. Akajivuta mbele na kuchomoa bastola ndogo yenye bomba upana wa kalamu. Alichokishuhudia ni mwanadada akitua sakafuni huku akijirusha sarakasi. Risasi mbili zikachimba sakafu. Gina alikuwa tayari kando ya eneo lile. Alipojaribu kujiweka sawa, yule jamaa akamchota ngwara, Gina akarudi chini mzima mzima. Wakati Jasmini anaingia ndani ya chumba hicho alimshuhudia yule bwana akiwa tayari kufyatua risasi kwa Amata.

Kwa ustadi wa aina yake, Jasmine aliruka sarakasi na kutua kwenye swichi moja ya kitanda na kuipiga kwa mkono. Wakati risasi ya yule jamaa ikifyatuka kile kitanda kikashuka chini, hivyo shabaha ikawa fyongo.

“Mhhhhhhh!” yule jamaa akapiga unyende wa hasira na kujikuta

katika wakati mgumu, amkabili nani. Gina aliinuka kwa haraka, lakini kabla hajafanya lolote, akajikuta akipokea konde zito, likamrudisha chini. Huyu bwana alikuwa na kasi na nguvu za ajabu. Kiwango chake cha upiganaji hakikulingana na cha wanawake hawa. Jasmine akachomoa bastola, lakini hakuweza hata kuitumia kwani yule bwana aliipiga kwa mguu kwa wepesi wa ajabu na kuitoa mikononi. Gina akajitahidi kuiwahi ili aidake, akajikuta akisindikizwa na guu la mgongoni lililomsukuma kwenye kitanda cha Amata, akadondokea juu yake. Tayari wakati huo yule bwana alikuwa keshaikamata bastola ya Jasmine iliyotua mikononi mwake. Gina akajua nini kitakachotukia, kwa nguvu zake zote, akajigeuza upande wa pili na kufanikiwa kupiduka na kitanda upande wa pili. Risasi nyingine ya yule bwana ikamkosa Amata na kupenya godoro, ikatua kwenye mkono wa Gina na kuchana nyama. Kamanda Amata akiwa hana fahamu akaaguka chini sakafuni huku kitanda kikirudi chini na Gina akijitupa upande wa pili.

“Mhhhhhhhhhh!” yule bwana akapiga unyende wa hasira kwa mara nyingine kwa kukoseshwa shabaha. Akilini mwake alijua kuwa sasa kakutana na wanawake hatari, maana walikuwa wakimzidi akili kwa kila namna.

“Ginaaaaaaaaaa!” Jasmine aliita kwa nguvu maana kwa damu aliyoiona ikitawanyika alijua swahiba wake keshakutana na risasi. Kelele zile zikamchanganya yule muuaji, akajikuta akipokea pigo la kiti kutoka nyuma yake. Likatua kisogoni na kumfanya apesuke, akajikwaa kwenye kitanda na kuanguka vibaya juu yake.

“Jasmiiiiinnn! Kubaton...” Gina akapiga ukelele.

Dkt. Jasmine akaelewa ni nini anachoambiwa, akazungusha mkono wake haraka na kuchomoa kifaa aichotumia kubania nywele zake ndefu. Kifaa hiki kinachojulikana kama Kubaton, huwa kinakuwa na ncha upande mmoja na urefu wake ni kama inchi tano na nusu hivi. Akakichomoa na kujirusha kumwendea yule jamaa. Na wakati huo huo yule mjinga naye akageuka kumdhibiti Jasmini maana alijua vyema hiyo silaha, alipoinua mkono wake akajikuta umeshikwa na nyaya, alipjitahidi kuutoa, akachelewa. Alimshuhudia Jasmini akimjia kwa hasira. Joao alijikuta uso kwa usona kifo. Alipotaka kumkwepa, akarudishwa na teke kali la Gina.

“Aaaaaaaaaa!” Jasmine alipiga kelele na kwa nguvu zote akashusha mkono uliotua upande wa kushoto wa kifua cha jamaa yule.

“Aaaaiiigghhhh!” yule bwana akapiga yowe la uchungu, ile Kubaton

ilizama moyoni. Jasmine alibaki kauma meno kwa hasira, mwili ukimtetemeka huku akihema kwa nguvu. Dakika hiyo hiyo, askari watatu wenye silaha wakaingia na kukuta hali tete ndani ya chumba hicho.

“Shoga umemmaliza?” Gina akauliza kwa sauti ya chini.

“Ta-ta-tayari...” Jasmine akajibu. Chiba na Scoba wakiwa na Madam S wakaingia katika chumba hicho, kila mmoja akamchukua wake.

“Wawekeneni chumba namba kumi na nne, huyu mmoja ana jeraha ahudumiwe!” daktari mwingine wa Kihindi aliyefika hapo akatoa agizo na jopo la wauguzi likafanya kazi hiyo huku Scoba akihakikisha hilo. Chiba akamwendea Amata na kumkuta kama mfu. Dakika hiyo hiyo, naye akaja kuondolewa na kupelekwa haraka kwenye chumba kingine. Chiba akamtazama Madam S, kisha macho yake yakatua kwa ule mwili wa daktari bandia aliyelala kimya huku amekodoa macho kama mtu aliyeshikwa ugoni, huku mkono wake ukiwa kifuni na damu ikitapakaa chini.

Chiba akausukuma mkono wa huyo jamaa na kuona kishina cha kubaton, huku *key ring* yake ikibaki nje. Kwa kidole chake akapachika kwenye ringi hiyo na kuichomoa.

“Chibaaaa!” Madam S akang’aka, na Chiba akamtazama, “Acha bwana!” Madam S akamwambia.

“Tangu lini umekuwa na huruma?” Chiba akamuuliza huku tayari akikisafisha kile kifaa kwenye sinki la maji.

* * *

Huko nje ya hospitali hiyo, tayari ulinzi mkali uliimarishwa. Si tu na kampuni ile ya ulinzi bali tayari, polisi, kikosi maalumu cha kupambana na uhalifu kiliwasili. Lile gari jeusi lililokuja na yule daktari bandia, lilikuwa limezungukwa na mitutu ya bunduki. Hakutakiwa mtu kutoka ndani ya gari hilo. Mchezo wote huu wa nje ulichezwa kwa kasi ya pekee na Madam S aliyekuwa amebaki garini baada ya mabinti zake kutoka na kwenda ndani ya jengo hilo.

Dakika kama thelathini baadae, askari walioingia ndani ya jengo la hospitali wakaanza kutoka huku wengine wakiwa na machela iliyobeba mwili wa muuaji aliyezidiwa kete na ‘kina Gina. Wakafika na kuuweka ndani ya Land Cruiser lao.

“Mmemuwahi?” mmoja wa askari aliyebaki nje aliuliza.

“Si bora ingekuwa sisi! Kuna maninja wa kike huko ndani, yaani si wa kuoa...”

“Kwa nini?”

“Wanawake wanapigana kama Cynthia Rothrock na Cynthia Khan...”

Wote wakaangua kicheko na kuuweka vyema ule mwili.

“Haya walete hao, ila umakini unahitajika, wana silaha hao!” kiongozi wao akatoa amri na wale askari wenye silaha waliozunguka lile gari, wakaweka sawia bunduki zao ikiwa ni pamoja na kuruhusu risasi ziingine kwenye chemba kusubiri amri.

“Tunaomba kwa usalama wenu, mtoke wenyewe bila silaha!” askari aliyekuwa juu ya lile Land Cruiser akasema kupitia *megaphone*. Dakika mbili zikapita, hakuna aliyeshuka garini, tangazo likarudiwa mara ya pili na safari hii likaongezwa kidogo, “... tukirudia mara ya tatu nguvu itatumika!” zikapita tena dakika mbili, hakuna aliyetoka. Tangazo likarudiwa mara ya tatu, na hapo mlango wa nyuma ukafunguliwa, akatoka kijana mmoja, mikono kichwani, akaamriwa kulala chini kifudifudi huku mikono ikiwa kisogoni. Mwingine akafuatia, kisha wa tatu ambaye ni dereva. Wakafungwa pingu na kupakiwa katika lile Land Cruiser, safari yakuelekea kituo kikuu cha kati ikaanza kwa mbwembwe.

* * *

Katika chumba kimoja wapo Gina alikuwa akishonwa jeraha lake na daktari wa hospitali hiyo.

“Bahati nzuri, risasi haikufika kwenye mfupa!” yule daktari akamwambia Gina huku akiwa tayari amekwishamaliza kazi yake. Mlango ukafunguliwa na yule muuguzi aliyepigwa kwenye kile chumba cha Amata akaingia.

“Asante afande umeokoa maisha yangu, yule mtu alikuwa ananiua...” akamshukuru Gina.

“Usijali, asante kwako, kwa kuwa ulipoamka, kama si kumpiga na kile kiti, angetuua sote,” Gina akasema huku keshasimama, tayari kwa kuondoka.

Baada ya mambo yote kuwekwa sawa, gari la wagonjwa lilikuwa tayari kwa safari ya uwanja wa ndege kumpelekea Kamanda Amata. Jasmine na Scoba wakateuliwa kumsindikiza TSA 1, pamoja nao, muuguzi mmoja pia alipata nafasi hiyo. Chiba na Gina wakatakiwa kubaki na Madam S kwa kazi maalumu ya kufanya.

MTWARA

Habari ya dharula kwenye luninga ndiyo iliyomshtua Toress katika ofisi yake. Hakuamini kile anachokiona, vijana wake wakiwa wamelazwa chini na kufungwa pingu kama kuku. Jasho likamtiririka, mwili ukamtetemeka. Akainuka na kutoka sebuleni, akaliendea jokofu na kutoa pombe kali, akanywa mafunda kadhaa.

“Vipi?” sauti ya Jozé ikamshtua.

Toress akageuka nyuma na kumtazama kijana huyo wa Kizungu, akiwa katika fulana nyepesi na suruari ya mazoezi.

“Aaaaaaggghhhh! Tumezidiwa kete tena, wote wamekamatwa ...” akamjibu.

“Na Joao...”

“Nahisi amekufa, kwa sababu kwenye habari wamesema jambazi mmoja ameuawa na polisi...” akamjibu na kujitupia kochini. Jozé akavuta hatua na kumwendea pale kitini.

“Nakwenda Dar es salaam!” akamwambia Toress kwa sauti ya kumnong’oneza.

Toress akamtazama Jozé, akatikisa kichwa chake na kutulia kwa sekunde kadhaa.

“No!” akamwambia.

“Kwa nini?”

“No, means no...” Toress akajibu na kujiinua pale kitini huku uso wake ukiwa umesawajika kwa hasira na gadhabu vikiambatana na kisasi cha wazi.

“Nitaandika taarifa gani kwa Dimens?” akapiga kelele na kuipiga ile chupa chini kwa hasira.

“Aaaaaaiiggghhhh!” akapiga kelele na kuelekea chumbani.

* * *

*Mtukufu Lord Dimens,
Misheni yetu inaelekea kushindwa kwa upande wa Tanganyika.
Vijana wetu wanakufa na wengine kadhaa wapo katika mikono ya dola.
Tufanye nini?
Mjoli wako
Toress*

Baada ya dakika 10...

Abort mission,

Return to zero... a.s.a.p

Ujumbe huu ulimkuta Toress akiwa kalewa chakari ndani ya chumba chake. Alielewa maana ya ujumbe huo kuwa anatakiwa kufika haraka sana Cabo Delgado. Akajiinua taratibu na kutoka tena sebuleni huku akipepesuka kwa kilevi.

“Jozé! Jozé! Safari ya Cabo Delgado sasa... Mtukufu anataka tufike haraka iwezekanavyo,” Toress akasema.

“*Ok Sir!*” Jozé akajibu na maandalizi ya safari, ikiwamo kumchukua Johnson yakaanza.

SURA YA 18

CABO DELGADO

LORD DIMENS aliketi ofisini kwake akipekuwa kabrasha hili na lile huku akipiga mruzi kuigiza melodia ya wimbo *Guantanamera*. Wapambe wake walikwishamzoea mtu huyu, aliyekuwa jasusi kwa zaidi ya nusu ya umri wake katika shirika la *KGB* miaka ya nyuma. Ilikuwa ukimsikia anapiga mruzi kufuatisha melodia hiyo ya *Guantanamera* basi ujue mambo si shwari kichwani mwake. Moyo wake ulikuwa na uchungu na hasira nyingi kabisa baada ya kupata taarifa ya kazi iliyokuwa ikifanyika huko Dar es Salaam mchana wa siku hiyo. Alipomaliza mambo yake pale ofisini akabinya kitufe kimoja na mara mlango ukafunguliwa, Bonston akaingia ndani.

“Kijana wangu! Mambo si mazuri, nashindwa kujua ni jinsi gani Bwana Toress anashindwa safari hii kunifurahisha...” akamwambia Bonston, mlinzi wake mtiifu katika kazi zake zote za siri. “K w a nini *Sir*?” Bonston akauliza.

“Vijana wameuawa, pamoja na Joao, ambae alikuwa tegemezi la Toress, ameuawa leo na wengine kutiwa mbaroni...” Dimens akaeleza kwa huzuni.

“Wameshindwaje kazi ndogo kama hiyo... kuua mtu mmoja tu!” Bonston akashangaa.

“Taarifa, tangu mwanzo, zinasema mtu huyo ni kiumbe hatari sana, na nina *code* zake za kiusalama... ila nashindwa kujua ni kweli Tanzania inaweza kuwa na kiumbe kama huyu?” Dimens akauliza kisha akawasha kompyuta yake ya ukutani na kuiweka picha ya Kamanda Amata. Chini ya picha hiyo kulikuwa na wasifu wa mtu huyo, lakini ni kwa mistari michache sana. Bonston akashusha pumzi.

“Utakumbuka maneno yangu mkuu!” Bonston akasema. Dimens akamtazama kijana huyo kwa jicho kali. Kisha akarudisha macho kwenye meza yake na kuongea kwa uchungu.

“Huyu anachafua hali ya hewa. Toress alikwishafika mbali sana, huyu Joao alishapambana naye na kumweka *unconscious*, lakini wameshindwa kumuua akiwa kitandani hana fahamu,” Dimens akasema, “Ni bora nitishe kwanza shughuli ya Maputo, ya kuinadi ile chanjo; nihakikishe huyu mshenzi yupo kaburini... nahisi kabisa, anaweza kuvuruga...” Dimens akasema huku akimtazama kijana wake mkakamavu.

“Unataka kunipa kazi?” Bonston akauliza.

“No! wewe huwezi kufanya kazi nyepesi kama hii. Toress anakuja leo hapa, pamoja na Jozé na mateka yule agent wa CIA,” Dimens akaeleza, “Umfunge kulekule *Hell 6*,” akamwambia.

“Lord, hakutakuwa na hatari yoyote tukimfunga pamoja na yule mwanamke?”

“Wala hakuna hatari, yule mwanamke si mmemfunga vyema? Na huyu mfungeni minyororo ya maana, ila nataka niue mmoja kwa mkono wangu huku mwingine akishuhudia, na nikifanya hivyo nataka mreodi video na kuituma Langley,” akamwambia.

“Ok!” Bonston akajibu na kutoka nje ya ofisi hiyo.

* * *

Saa nane mchana, chopi iliyotumwa kuwachukua Toress na wenzake pamoja na mateka ikawasili katikati ya msitu huo ambako Dimens alikuwa ameweka makazi yake. Na chini ya ardhi kukajengwa maabara kubwa sana ya kisasa ambayo hata serikali ya Msumbiji haikuwahi kugundua ujenzi huo zaidi ya nyumba na viwanja vya kuchezea vinavyoonekana katika uso wa nchi. Kwa ujumla walijua makazi yake tu hawakujua kitu kingine kinachoendelea.

Johnson Kasalu, akiwa amedhoofu, alikuwa kimya katika kiti maalum ambacho mikono yake ilifungwa kwa mikanda migumu.

Nchi hii haina usalama kabisa, mtu anaingia na chopi katika mipaka yako hata humgundui! Johnson akawaza, akifikiri jinsi chopi hiyo ilivyongia na kuwachukua huko kwenye mapori, Kusini mwa Tanzania, lakini ndani ya mpaka, isigunduliwe. Waliporuka, ndipo akagundua ujanja wa kepteni huyo, alikuwa akiirusha kwa kiwango ambacho rada isingeweza kuiona kiurahisi. Mara baada ya kuvuka mpaka tu na kuingia Msumbiji

akainyanyua juu zaidi.

Tupo juu! Wananipeleka napi? Akajiuliza. Hakukuwa na wa kumjibu, akafumbua jicho kwa chati na kutumia hisia zake kujua hali aliyonayo. Mikono na miguu ilifungwa kwa kamba madhubuti. Hakujitikisa, wala hakufanya makeke yoyote, akatulia kama kwanza na kufumba macho yake huku akijaribu kusikiliza kile wanachoongea lakini hakuambua vingi kutokana na kutokuijua lugha hiyo kwa ufasaha.

Mwendo wa saa mbili angani, ile chopa ikawasili panapotakiwa. Johnson aligundua kuwa wamefika baada ya kusikia kile ambacho nahodha alikuwa akiwasiliana na watu wa chini na pia jinsi pangaboi zilivyokuwa zikipunguza kasi ya mzunguko.

Tumefika! Akawaza na kimyakimya kumuomba Mungu wake. Moyoni alijua wazi kuwa sasa huku anakoletwa ndiko mwisho wa maisha yake. Akatulia mpaka kile chombo kilipokanyaga ardhi na yale mapangaboi yaliposimama na kutulia. Toress akawa wa kwanza kushuka, akakutana na Bonston, wakasalimiana. Akafuatia Jozé. Mara baada ya kushuka, vijana wawili waliovalia suti nadhifu nyeusi, wakaingia kwenye helikopta hiyo na kushuka na mateka huyo. Johnson Kasalu alikokotwa na kuingizwa katika mlango mmojawapo upande wa mbele wa himaya hiyo ya Dimens. Huko ndani akaingizwa kwenye lifti na kuteremshwa chini ya ardhi mpaka *Hell 6*.

Mara tu baada ya taa kuwashwa, macho ya Johnson yakakutana na mwanamke anayemfahamu vyema, Tetty.

“Hii ndiyo nyumba yako na huyo mwanamke, mkitaka *honeymoon* mtajuana wenyewe...” aliongea kijana mmoja kwa dharau mara baada ya kumfunga vyema mateka huyo. Kisha taa zikazimwa na giza nene likatawala.

* * *

Toress alitulia kimya katika chumba maalum chenye makochi mawili na meza ndogo katikati. Mpaka dakika hiyo alikuwa peke yake ndani ya chumba hicho akisubiri mwenyeji wake, Lord Dimens. Ukimya ulikuwa umetawala, ubaridi kutoka katika kiyoyozi na harufu nzuri ya manukato ndivyo pekee vilikuwa vikimfariji. Hakikuwa chumba kikubwa, bali kidogo lakini kiliwekwa katika hali ya kupendeza. Akiwa amemezwa na lindi la mawazo, akasikia sauti ya ala ya muziki ikipiga wimbo wa Guantanamo, na mara mlango ukafunguka, mwenyeji wake

akaingia na kuketi kitini kisha ule mlango ukajifunga huku ile sauti ya muziki nayo ikipotea hewani.

“Toress Kazumari, umeniangusha sana katika misheni hii...” Dimens alianza pasi na salamu.

“Si hivyo mkuu!”

“No! Unajua kuwa unaniweka hatarini sana? Kwa sababu katika historia yangu, sijawahi kutikiswa namna hii... tena Tanzania!” Dimens akalalama.

“Wametuzidi ujanja mkuu!” Toress akasema.

“Hapana! Wewe ni mzembe, tangu nikuruhusu kuanzisha biashara zako ili zifiche nini unafanya, umekuwa mzembe sana... tunafanya kazi ya hatari, inagharimu maisha, wewe unachukulia rahisi tu,” Dimens akalalama.

“Ni makosa ya wale waliokuwa uwanja wa vita...”

“Noooo! Sivyo. Ni makosa yako wewe kutafuta watu dhaifu dhaifu, kwenye vita lazima ujue unapambana na nani, Toress! Mh!” Dimens alikuwa mwekundu sura yote kwa hasira.

“Nilikodi wauaji wenye viwango tafauti, nikitegemea kwamba kazi haitakuwa ngumu hasa ninavyojua Tanzania...” Toress akasema.

“Ni kweli, lakini ulipoona hali ni tete kwa nini hukumtumia Jozé ambaye nilikuruhusu umkodi kwa gharama kubwa?” Dimens akauliza.

“Ndiyo nilikuwa nataka nimtume awamu hii, hivi leo ilikuwa aondoke kuelekea Dar es salaam...”

“Umechelewa Toress... Joao keshakufa, na hao manyang’au watatu wako mikononi mwa polisi, wakikutaja kuwa ni wewe umewatuma! Je? Utabaki hai?” Dimens akamuuliza.

Toress akatulia kimya, akahesabu wapi na wapi kakosea, akang’amua ukweli wa hilo.

“Yaani hivi ninavyokwambia, tayari nyumba yako ipo kwenye uchunguzi mkali... ndiyo maana nikakwambia mje wote, asibaki mtu pale, maana ingekuwa faida kwao,” Dimens akamwambia kwa msisitizo. Jambo hili la mwisho likamfanya Toress akodoe macho kwa mshituko.

“Umeniudhi, na yeyote anayemuudhi Lord Dimens, huuawa na nafasi yake atapewa mtu mwingine...” Dimens akasema huku akiinuka kitini.

“No! Sir, don’t do that...!” Toress akaomba msamaha asiawe, akapiga magoti akilia kama mtoto lakini hiyo haikusaidia. Mlango ukafunguliwa na Bonston akaingia na timu yake ya vijana wawili.

“Mchukueni, mkamuulie mbali, sitaki kumuona!” Dimens akatoa

amri, na wale vijana wawili wakamkamata Toress huku na huku na kuondoka naye.

“Bonston, kutoka kwenye mwili wa huyu mjinga toeni viungo vyote muhimu, kama moyo, figo, macho, kongosho... na kama damu yake ni safi, muinyonye yote na kuihifadhi kwa shughuli zetu... halafu ganda lake mkaliteketeze huko...” Dimens akamwambia kijana wake, naye akaitika na kutoka nje ya chumba kile.

“Siwezi kuvumilia wajinga! Ukileta mambo yanayohatarisha biashara yangu, nakuua kwa faida... *Im trusting in money and wealth not in God!*”

* * *

Huko Dar es Salaam Chiba na Gina walikuwa katika uchunguzi juu ya tukio lililomfika Kamanda Amata usiku uliotangulia. Akiwa na bandeji sehemu ya juu ya mkono wake, fulana yake ya mikono mirefu iliificha na hakuna mtu ambaye angeona jeraha hilo.

Waliwasili katika hoteli ile jioni ya siku hiyo. Baada ya kupata kibali cha meneja wa hoteli wakapanda mpaka katika chumba kile na kukuta bado damu zimetapakaa huku na kule kwa kuwa waliamuliwa wasikisafishe kwanza ili kutokupoteza ushahidi. Kutoka waliposimama, Chiba alitoa kamera ndogo na kupiga picha kadhaa, ikiwamo ya chumba kizima, na kila eneo ambalo walihisi lingewapa jawabu la tafutishi zao.

“Walikuwa wanne!” Gina akasema baada ya kuzunguka huku na huko ndani ya chumba kile. Akavuta hatua hadi karibu na kona ya chumba, akachutama na kuangalia vizuri. Kulikuwa na damu imeganda.

“Mmoja alijipiga hapa, naona nywele kadhaa zimebaki,” akamwambia Chiba. Kijana huyo akatoa kifaa maalumu na kuchukua zile nywele, akaziweka kwenye kijimfuko. Wakapekua hapa na pale mpaka kwenye lile dirisha. Gina akatikisa kichwa na kuangalia chini ya jengo hilo.

“Kuna mawili, ama Amata alipigwa na kitu kizito au aliangukia ile mita ya maji pale...” akasema. Chiba akasogea mpaka pale na kutazama kule chini akachukua picha kama mbili tatu hivi. Waliporidhika na uchunguzi wao, wakatoka mpaka kwenye chumba cha watu wa usalama. Huko walikuta vijana watatu wakiwa kazini, wakajitambulisha na kuomba kuona picha zilizorekodiwa na camera za usalama. Pasi na shaka, wakaruhusiwa, Chiba akarudisha nyuma mpaka siku iliyopita, saa moja usiku na kuanza kutazama huku akikimbiza kidogo ili kufikia apatakapo.

Haikumchukua muda, akapapata apatakapo, Gina akaandika kwenye simu yake, saa na dakika ambayo gari la Amata lilionekana kuingia katika maegesho na kisha akateremka na kuingia ndani ya hoteli hiyo.

“Chumba kilichofanyika mauaji kilipangishwa na nani?” Chiba akamuuliza mmoja wa wale vijana.

“Msichana tu, mkitaka maelezo mtayakuta kaunta...” yule kijana akajibu. Gina akameza mate kwa jibu hilo. Wivu. Baada ya kujiridhisha hapo, Chiba akaomba kupatiwa nakala ya *Compact Disc* yenye picha ya tukio zima. Akapatiwa kwa kibali cha meneja wa hoteli.

Katika meza kubwa ya kaunta, wakapatiwa jibu stahiki.

“Mwanadada, mwajiriwa wa *CdG Marine Tour*, alitokea Mtwara...”

“Mtwara?” Gina akadakiza swali.

“Ndiyo Mtwara...” akajibiwa.

Baada ya mazungumzo ya dakika chache, wakaondoka zao.

* * *

Katika hospitali ya Mwananyamala, Chiba na Gina waliwasili jioni hiyo, moja kwa moja wakaonana na utawala, baada ya kujitambulisha wakasikilizwa shida yao.

“Hapa tumepokea maiti mbili, yule mwanamke hakufa ila alikuwa kapoteza fahamu kutokana na kupoteza damu nyingi...” muuguzi wa zamu akaeleza.

“Tunaweza kumwona?” Chiba akauliza.

“Hayupo hapa, tumemrufaa kwenda Muhimbili jana ile ile,” wakajibiwa. Baada ya mazungumzo hayo, wakaongozana mpaka chumba cha kuhifadhi maiti.

Maiti mbili za wanaume zilikuwa bado juu ya vitanda vya chuma maana majokofu yalikuwa yamejaa, zikafunuliwa. Chiba akatumia kamera yake ndogo na kuzipiga picha tofauti tofauti kwa ajili ya kazi zao. Baada ya kumaliza zoezi hilo, safari ikawa kuelekea kituo cha polisi cha kati.

Iliwachukua takribani saa moja kufika hapo baada ya kupambana na foleni za jiji la Dar es salaam. Pindi walipowasili, wakakutana na Inspekta Simbeye aliyekuwa akiwasubiri kwa hamu.

“Poleni sana vijana!” akawasabahi.

“Asante ...”

“Lakini msijali, unapotetea taifa lako hata ikibidi kutoa uhai, fanya

hivyo,” akawaambia.

“Sawasawa!” Chiba akajibu.

“Najua mmekuja kuchukua majibu yenu...”

“Ndiyo,” wakajibu kwa pamoja.

“Nina habari ya masikitisho sana kwenu, wale vijana tumewakuta asubuhi wakiwa wamekufa, kila mmoja kwenye selo yake,” akawaambia.

“Yaani?” Chiba akang’aka huku Gina akikunja sura.

“Kilichosababisha kifo...”

“Sumu, vidonge vya sumu, sasa hatujui walikuwa navyo au kuna mtu kawapatia,” Simbeye akawaambia Chiba na Gina. Gina na Chiba wakatazamana, baada ya sekunde nne hivi kama si tano wakageuka na kumtazama tena Inspekta Simbeye.

“Kwa hiyo...”

“Hakuna walichosema,” akamalizia kwa kuwajibu namna hiyo. Akili za Chiba zikapanga na kupangua, kisha zikafikia uamuzi. Wakaagana na Simbeye, wakatoka na kuondoka zao.

* * *

HOSPITALI YA MUHIMBILI

Tausi Mpendamali alirudiwa na fahamu jioni ya saa moja, saa chache tu kabla ya kutimia saa ya ishirini na nne tangu akutwe na mzimio huo. Maumivu ya sehemu za mbavu ndiyo yaliyomrudisha tena duniani. Akatazama pande zote akishangaashangaa. Macho yake yalikuwa yakiona vitu kama vimulimuli na rangirangi zikipita huku na kule. Akajaribu kutikisa mkono, ukatikisika. Muuguzi ndani ya chumba kile aligundua kuwa msichana huyo amekwishaamka, akasubiri tu arudiwe na fahamu sawasawa.

“Tausi!” akamwita kwa sauti ya upole. Tausi akageuka kumtazama kisha akatabasamu, na yule nesi akatabasamu naye kwa pamoja.

“Yuko wapi Mr. Spark?” Tausi akauliza.

“Spark? Ni nani huyo?” yule muuguzi akauliza.

“Kwani hapa niko wapi?” akauliza tena, huku akigeukageuka kutazama mahala alipo, mashine zilizomzunguka.

“Hospitali... upo hospitali Tausi...” yule muuguzi akamwambia huku akimweka vizuri kitandani pale.

Saa moja baadae, Gina na Chiba wakaingia katika chumba hicho.

“Sasa mnaweza kuongea naye, hata yeye amekubali, japo ana kumbukumbu chache,” muuguzi akamwambia Chiba. Chiba na Gina wakasogelea kitanda kile na kumsabahi Tausi naye akajibu. Kwa kuwa wote walikuwa wamevalia makoti meupe yeye alijua kuwa hao ni madaktari kama wengine.

“Tausi, pole sana, lakini jambo kubwa tunapenda kusikia kutoka kwako mambo kadhaa... tunahitaji kukurudisha kwenu lakini hatupajui.. unaishi wapi?” Chiba akauliza.

“Mimi aaaaaanh ninaishi Mtwara...” akajibu kwa sauti ya taratibu.

“Na unafanya kazi wapi?” Chiba akauliza swali lingine.

“Kampuni ya Utalii wa majini, *CdG Marine Tour*... tupo Mtwara, Msanga Mkuu,” Tausi akajibu, Gina akatikisa kichwa kwa kuwa alikwishasikia habari ya ofisi hiyo katika vikao vyao.

“Bosi wako ni nani?” akamtupia swali jingine.

“Anaitwa Toress Kazumari, anaishi Mtwara...” Tausi akaeleza kila kitu.

“Unakumbuka nini kilitokea jana katika hoteli ya Green Valley?” Gina akauliza.

“Aaaaaiii kichwa changu!” Tausi akalalama maumivu.

“Pole Tausi, utapona tu!” Muuguzi akamwambia huku akimweka vizuri kitandani.

“Jana! Nilivamiwa chumbani kwangu,” akajibu.

“Ilikuwaje? Nieleze...”

“Nilikuwa namsubiri rafiki yangu, Mr. Spark...” kwa kauli hiyo, moyo wa Gina ukaruka samasoti. Akameza mate ya wivu na hasira.

“Ili mfanye nini?” Gina akajikuta karopoka swali.

“Aaa hata ha-hakuja yeye, akaja m-tu mwingine kabisa, tukiwa tuna-o-nge-a taa zikazimika, kukatokea ma-pi-gano, basi, sikumbuki zaidi...” Tausi akaeleza kwa tabu kidogo huku muuguzi akimpa pole na kumshika hapa na pale.

“Asante sasa utulie upate dawa, ukijisikia una nguvu tutakupeleka nyumbani kwako, isitoshe pia tungependa hata kujua kwa bosi wako,” Chiba akasema huku akifunga kabrasha alilokuwa akiandika yote hayo. Usiku wa saa tatu wakaondoka katika hospitali hiyo na kuelekea Ofisi Ndogo ambako walikuwa na miadi na Madam S saa nne usiku ya siku hiyo.

SURA YA 19

HOSPITALI YA APOLLO – INDIA

KAMANDA AMATA alifikishwa katika hospitali hii kubwa, iliyojengwa ndani ya Jiji la New Delhi, nchini India mara tu baada ya kuhamishwa kutoka Agha Khan ya Dar es Salaam.

Kutokana na unyeti wa hali yake na umuhimu wa mtu mwenyewe, jopo la madaktari bingwa lilipiga kambi kuhakikisha hakuna roho itakayouacha mwili. Madaktari hawa wapatao kumi na wawili, walishirikiana na wauguzi bingwa wa kada tofauti ukiachilia mbali wataalamu wa madawa. Jumla ya wote ilikuwa yapata thelathini na wawili, wakitokea nchi tofauti. Kila daktari alikuja na timu yake ya wauguzi na wasaidizi. Palikuwapo na mabingwa wa upasuaji. Mabingwa wa mifumo ya fahamu, ya upumuaji na wengine wengi. Wote hawa walikuwa wakifuatilia hatua kwa hatua maendeleo ya afya ya mgonjwa wao. Serikali ya Tanzania iliweka pesa nyingi katika afya ya mtu huyo ili kuhakikisha anapona na kurudi kwenye majukumu yake ya kawaida. Daktari Jasmini naye alikuwa miongoni mwao akihakikisha hakuna hujuma yoyote inayofanyika dhidi ya maisha ya TSA 1.

Ilimchukua majuma mawili kuamka kutoka katika mzimio. Usingizi uliomchukua katika safari ya mbali ambayo hata yeye mwenyewe hakuijua bado. Kwanza alianza kusikia sauti za watu wakiongea, lakini maneno yao hayakuwa sawa; alisikia kama mwangwi mzito ndani ya kichwa chake. Sauti ile iliusumbua ubongo wake kwa dakika kadhaa mpaka alipoanza kujitikisa.

“Anaamka!” Daktari Jasmine akamjulisha mmoja wa madaktari wale. Naye akawaita wengine. Sekunde tu wote walikuwa wamekusanyika na kuzunguka kitanda huku wengine wakisoma taarifa anuai zinazopita

kwenye vioo vya mashine tiba zilizomzunguka. Hii ilichukua kati ya dakika kumi hadi thelathini hivi kabla ya kope zake nazo kuanza kuchezeza.

“Amata! Amata!” Jasmine aliita taratibu baada ya kuambiwa kufanya hivyo. Saa moja baadae aliweza kufumbua macho lakini hakuwa anaona sawasawa.

“Mwacheni!” Dkt. Zera Hamsud, mtaalamu wa mifumo ya fahamu, raia wa Israel, ambaye alikuwa kiongozi wa jopo hilo akawaambia, nao wakatekeleza.

“Itamchukua muda sana kuamka kabisa... na kazi ngumu ya kuifanya ni pindi atakapoamka kabisa. Maana itatubidi kuhakikisha anarudi kama mwanadamu wa kawadia, akiwa na akili timamu,” akawaambia. Wote walibaki kimya wakimtazama Amata pale kitandani.

Baada ya kufumbua macho, alitulia kimya na kuwa kama mtu anayeshangaa kitu fulani asichokijua. Wauguzi walikuwa wametingwa kufuatilia mashine hizo zilizokuwa zikitoa taarifa mbalimbali kwenye mifumo ya moyo, ubongo, fahamu na kwingineko.

* * *

Ilichukua wiki mbili nyingine, Kamanda Amata kuamka kabisa na kuweza kukaa. Mazoezi mengi yalifanyika, kama kumwita kwa jina lake, kumtekenya, kumshtua kwa kupiga kelele na mengine mengi. Hii ilikuwa ni kupima kama hisia zake zimerudi sawasawa au bado.

“Mambo mengi anaweza kuhisi ila bado kumbukumbu haijarudi, na hilo ndilo jambo la msingi sana. Tukifanikisha hilo, itabaki kazi ndogo ya mazoezi ya viungo na umakini...” Dkt. Zera akamwambia Jasmine.

“Lakini sasa anaweza kutembea sivyo?” Jasmin akauliza.

“Yap! Wataalam wa viungo wataanza naye mazoezi ya kutembea,” akajibiwa.

Afyu ya Kamanda Amata ikaanza kutengemaa kwa msaada mkubwa wa wataalamu hao, mazoezi ya viungo na ya utambuzi yaliendelea kufanyika kila siku. Hakuwa na shida katika kuongea, ila wakati mwingine hakuwa anaongea vitu sawasawa.

* * *

CABO DELGADO

Kikao kifupi kilifanyika katika jumba la Lord Dimens huko katika msitu wa Cabo Delgado. Taarifa iliyoletwa na Jozé ambaye sasa alikabidhiwa kazi ya Toress na kukabidhiwa jumba la kule Mtwara ilimfurahisha Dimens.

“Uchunguzi wote umefanyika, hakuna dalili ya huyo binadamu katika ardhi ya Tanzania,” Jozé akaeleza.

“Mmmmmh! Bado najiuliza wapi huyu mtu kahifadhiwa? Kwa sababu hatujui hata nyumba zao za siri...” Dimens akasema.

“Ni kweli, lakini mwezi mmoja ambao nilitawanya watu wangu niliyowakodi, wenye taaluma ya juu ya kunusanusa mambo, wangetambua tu,” akaeleza.

“Enhee, niambie kutoka Maputo, tunaweza kufanya shughuli yetu mwezi ujao?” Dimens akamgeukia mtu mwingine mwenye asili ya Uzungu kama wao.

“Bila shaka, kila kitu kipo sawa, nimeshawapanga watu katika sehemu nyeti kujua kila kinachoendelea. Kwa ujumla kule ni shwari kabisa,” akajibu mtu huyo.

“Na yule mpumbavu bado mmemhifadhi?” Dimens akarusha swali.

“Aaaaa Lord! Tulitekeleza takwa lako, tulimchinja na kuuchoma moto mwili wake...”

“Oooh safi sana Rodriguez, umefanya vyema. Yule mjinga angetusumbua, na hilo ni pigo lingine kwa vibaraka wa CIA. Na hawa nao nitahitaji tuwatoe viungo tunavyohitaji kwa ajili ya biashara za kimaabara ...” Dimens akaeleza.

“Ok! Bonston, sasa anza kufanya maandalizi ya uzinduzi wa chanjo ya *AIDIOSIS*. Alika makampuni yote makubwa ya madawa duniani, wafike Maputo. Atakayekuwa na pesa ya kununua kanuni hiyo tutamuuzia kwa pesa iliyotakata. Kufikia jioni ya leo, nahitaji unipe taarifa ya wapi tunafanyia, nani na nani umewaalika ili nitoe maelekezo ya mwisho...” Lord Dimens akaongeza kusema kisha akafunga kikao hicho cha watu watatu. Kama kuna siku ambayo huyu bwana alifurahi ni hii, pamoja na taarifa aliyoipokea kutoka kwa Jozé, bado alitoa maagizo kuwa uchunguzi wa wapi Amata yupo uendele, na akipatikana au kujulikana amalizwe.

LANGLEY - Virginia

Kama ilivyo kwa Dimens, huku nako kulikuwa na kikao kikiendelea. Wakuu wa idara nyeti za ndani ya CIA walikutana. Kikao hiki kilikuwa ni baada ya mwezi mzima wa kufanya chunguzi za siri za upotevu wa chanjo walioichukua kutoka Tanzania.

“Dimens anataka kutufanya wajinga,” mjumbe mmoja akaeleza.

“Sasa hivi kaka kimya lakini naamini ataibuka muda si mrefu, na hapo atakapoibuka ndipo pa kummalizia kabisa,” mwingine akasema.

Mazungumzo juu ya oparesheni ambayo ingeundwa kumkabili ‘shetani’ huyo iliitawala meza hiyo ya pembetatu. Tafutishi za siri zilizopatikana ambazo zilifanywa kimya kimya, zilibaini kile ambacho TSA walikipata. Zaidi ya hapo, walijua kuwa Dimens anafanyia shughuli zake huko Afrika, kabla hawakujua ni nchi gani lakini baada ya kupokea taarifa ya kifo cha mtu wao huko Maputo, wakaanza kuelekeza macho na masikio yao katika nchi hiyo.

“Inawezekana akawa anafanyia shughuli zake Msumbiji?” mjumbe mmoja akauliza.

“Mbona bidhaa zake nyingi zimeandikwa Brazil?” mwingine akauliza.

“Dimens hayupo Brazil, kwa sababu vijana wangu wamefika huko, wamefanya uchunguzi mkubwa sana mpaka hiyo anwani ilipo... kuna duka tu la dawa na vifaa vya mahospitali na inasemekana si la Dimens wala hahusiki. Na ndiyo duka kubwa linalosambaza madawa karibu nusu ya nchi ukiacha serikali,” mjumbe mwingine akajibu.

“Hata ajifiche vipi, atapatikana tu. Kinachonishangaza, anawajuaje watu wetu kirahisi hivyo? Ndo maana nasema inawezekana kuna mamluki anayetoa habari zote kwake,” aliyekuwa kiongozi wa jopo akasema na wengine wakaunga mkono swala hilo.

“Sawa, sasa tutafanya operesheni kama nilivyosema katika maeneo makubwa matatu, Brazil, Msumbiji na Tanzania kwa awamu ya kwanza. Tutaingiza watu wetu kwa siri, watafanya uchunguzi wa siri na walete taarifa kwa siri vile vile. Popote atakaposadikiwa yupo, tutahakikisha tunamfutulia mbali, hata kama ni kwa kuangusha kombora tutafanya hivyo!” akawaambia. Mipango ikawekwa sawa na wakaazimia operesheni hiyo ianze bila kuchelewa. Kikosi kilichotumwa Brazil kilitakiwa kuanzia kazi katika duka hilo kubwa la dawa, kile kilichotumwa Tanzania kilitakiwa kuanza na uchunguzi wa kupotea kwa Johnson Kasalu na

Tetti, wakati kile cha Msumbiji kilitakiwa kuanzia kuchunguza mauaji ya wakala wao wa Maputo.

* * *

Maandalizi ya uzinduzi wa chanjo ya *AIDIOSIS* chini ya kampuni tanzu ya dawa na vifaa tiba huko Msumbiji yalipamba moto. Tayari jiji la Maputo lilikuwa kwenye hali ya kupokea wageni kwa ajili hiyo. Mahoteli makubwa yalikwishafanyiwa *booking* kwa ajili ya kulaza wageni kwa siku tatu wakati uzinduzi na uuzwaji wa formula utafanyika. Kwa kufuatia kilichotokea Tanzania, serikali ya Msumbiji ilimuahidi mwekezaji huyo kuweka ulinzi mkali katika maeneo nyeti ambayo wageni wanaingilia ili tu kumjua yeyote mwenye nia mbaya. Kwao ilikuwa jambo kubwa sana chanjo hii kugunduliwa nchini mwao, wasijue kuwa ni hiyo hiyo ndiyo iliyoibwa kule Tanzania.

Hoteli yenye hadhi ya nyota tano ya Radisson Blu ilichaguliwa kupokea wageni wanaokuja kwa shughuli hiyo. Hoteli hiyo iliyojengwa pembezoni mwa Marginal Avenue, katika Jiji la Maputo, ilionekana na kusifika kwa usalama. Lakini zaidi ya hapo, ni kutokana na wageni wenyewe watakaofika. Yalikuwa yamesalia majuma matatu tu shughuli ile ifanyike, kila kitu katika kila idara kilikuwa kimekamilika.

Huko Cabo Delgado, Lord Dimens alikuwa mwenye furaha sana baada ya kuona mafanikio ya maabara yake kwa kuweza kuibadili kidogo pasi na kuigusa *formula* ile, kisha kuiongeza vitu tofauti. Ukuaji wa kibiashara na makampuni mengi duniani kote ulimpa jeuri ya kujiona yeye ndiye mungu mdogo. Kipindi kilichobaki walikitumia kumuweka vizuri Dkt. Edward Minzi kwa kumfanyia mabadiliko ya sura, mwili na kadhalika.

* * *

SHAMBA – Safe House

Habari ya shughuli ya uzinduzi wa chanjo hiyo nchini Msumbiji haikua siri tena. Kila sehemu walisikia na kujua nini kinatendeka ndani ya majuma machache yajayo katika Jiji la Maputo. Madam S, Chiba na Gina walikuwa wameketi katika meza kubwa, ndani ya chumba cha mikutano. Agenda iliyowekwa mezani, ilikuwa ni hiyo hiyo.

“Wameibuka, wangepotea kuificha tu ndani?” Madam S akauliza.

“Tuna uhakika? Maana siku hizi kila wataalam wanachunguza jambo hili hili... vipi ikiwa si chanjo hii iliyopotea huku kwetu?” Chiba naye akaweka swali mezani.

“Nakuelewa vyema, tunachotakiwa kufanya kwa sasa ni kuchunguza mambo mengi lakini lazima tufike Maputo siku hiyo. Yatupasa kuwepo kwenye hiyo shughuli kwa njia yoyote ile, tukashuhudie nini kinatendeka. Ikiwezekana tujiingize kwenye moja ya kampuni kubwa za madawa ili tuweze kupata mengi zaidi...” Madam S akasema.

“Ok labda mimi niulize, nini hasa tunachotaka kufanya? Kuzuia mnada au kwenda tu kuchunguza? Na tutajuaje kama ni yetu ilhali hatujui hata ilikuwaje?” Gina akauliza.

Kwa ujumla, wote watatu walibaki njia panda, ombwe la Kamanda Amata likaonekana wazi.

“Kwani Madam, Amata hawezi kufika maana si tayari yupo sawa?” Gina akaongeza swali.

“TSA 1 bado, kadiri ya daktari anasema bado, kuna vitu havijakaa sawa japokuwa anatembea, anazungumza, kuna mambo anatambua na mengine bado... wamesisitiza inabidi akae kama miezi mitatu mingine,” Madam S akajibu.

“*Oooh no!* hapana Madam, basi aje amalizie tiba zake hapa Shamba, we huoni inaweza kuwa ni moja ya kampeni yeye kubaki huku mambo yanaharibikia Msumbiji?” Gina akalalama.

“Unayosema yana uzito wake... *any way*, mi nitasafiri kesho kuelekea India, nitaona hali yake na kuzungumza na daktari kama atamruhusu basi tutafanya hivyo, kama hatomruhusu basi. Ni lazima tufuate masharti ya daktari maana yeye ndiye ajuaye afya ya mgonjwa wake,” akawaeleza.

“Hata hivyo hawezi kuingia kazini mara moja kwa sababu inampasa kupita kwenye majaribio mbalimbali ili kuona *fitness* yake pamoja na mambo mengine ya kiintelijensia kama yapo sawa kichwani mwake,” Chiba akasema na Madam S akatikisa kichwa kukubaliana naye.

* * *

INDIA – New Delhi

Siku mbili baadae...

Madam S alifika moja kwa moja kwenye chumba maalumu ambacho Kamanda Amata alikuwamo. Ilikuwa ni safari ya ghafla au tungeweza kuita ziara ya kushtukiza. Si Jasmin wala Scoba aliyekuwa na taarifa ya ujio huo. Wakati madaktari wamekwenda kwenye chumba cha mapumziko ambamo wangekaa kama saa mbili hivi pamoja na kupata chakula, ni Jasmine na Scoba tu waliobaki katika chumba hicho wakiongea hili na lile na mgonjwa wao. Mlango wa kioo kizito ukafunguliwa kwa swichi maalumu na mwanamama huyo akaingia ndani kama mzimu. Jasmini akasimama na kuafuatiwa na Scoba, wakasalimiana na kumkaribisha.

“Wala msishtuke, nilikuwa nasubiri muda huu ambamo mtabaki peke yenu ili nifike...” akawaambia na kuwatoa hofu.

“Karibu sana HOT,” Jasmine akamkaribisha kwa kumtaja cheo chake.

“Nimekwishakaribia,” akawajibu. Kitu pekee ambacho walikishangaa ni kuwa Madam S hakuwa na ucheshi ule waliouzoea. Hii ikawafanya wajue wazi kuwa ujio wake haukuwa wa matembezi tu bali kuna jambo nyuma yake.

“Mnaweza kunipisha kidogo? Nina mazungumzo na kaka yenu,” akawaambia nao wakatoka nje na kuwaacha wawili hao peke yao. Madam S akamtazama Amata kisha akazitazama zile mashine ambazo sasa zilikuwa zimezimwa isipokuwa moja tu iliyobanwa katika kidole chake.

“Unajisikiaje?” ndilo lilikuwa swali la kwanza.

“Najisikia vyema, na ninahitaji kurudi kazini mara moja,” Kamanda Amata akasema huku akikaa vyema kitandani, akiwa ndani ya pajama la hospitali.

“Huwezi, huwezi kurudi tena kwenye *field* yako. Kitanda kitakuwa ndiyo starehe yako kwa maana unaendekeza mapenzi kuliko kazi,” Madam S akamwambia.

“Hayo si maneno ya kunambia!” Amata akajibu.

“Huna msaada tena kwetu! Yule mwanamke wako utamkuta tumekuwekea, ukifika mkamalizie uzinzi wenu,” Madam akamwambia kwa sauti ya ukali lakini isiyofika mbali.

“Mwanamke! Mwanamke gani?” Amata akauliza.

“Humjui? Aliyekufanya ufike huku nani. Wanawake watakuua,” akamwambia na kumrushia picha ya Tausi, “Unamjua huyo?” akamtupia

na swali. Kamanda Amata akaichukua ile picha na kuitazama kwa makini, hakuna kumbukumbu iliyokuwa ikija juu ya Tausi.

“Sikiliza Amata, ulikuwa mzuri sana kwenye kazi, na mara nyingi nimekuusia juu ya wanawake! Epukana nao, hutaki kunisikia. Mara hii umeinusa harufu ya kifo, mara ijayo utakufa kabisa...” akamwambia.

“Madam S, sikuelewi, nini kilitokea?”

“Nini kilitokea?” Madam akarudia swali lile lile kisha akatulia kidogo baada ya kukumbuka Jasmine alimwambia kuwa mtu anayepata tatizo hili, akipona anaweza kuwa anapoteza kumbukumbu za matukio ya nyuma.

“Shiit!” akanga’ka na kuinyakua ile picha mkononi mwa Amata.

“Nahitaji kurudi kazini!” Amata akasema kwa ukali.

“Huwezi. Mpaka ufaulu majaribio kadhaa ndipo naweza kukusainisha kuwa *field agent* kwa mara nyingine,” Madam S akajibu. Ukimya ukachukua nafasi kati yao, wakatazamana kwa nukta kadhaa, kila mmoja akamsoma mwenzake.

“Huna faida Amata, beji yako inachukuliwa na mtu mwingine! Kwaheri ya kuonana,” Madam S akageuka na kubonya kitufe kuruhusu mlango kufunguka, hakugeuka nyuma.

“We mamaaaaa!” Amata akapiga kelele na kujiinua pale alipoketi akajikuta akijigonga vibaya kwenye ule mlango ambao sasa ulikwishajifunga, akajitupa tena kitandani. Mashine iliyofungwa kidoleni mwake ikapeleka ishara kwenye mashine nyingine na kuanza kupiga alarm. Jasmine na Scoba walikuwa wa kwanza kufika kwa sababu wao hawakuwa mbali sana. Ndani ya chumba hicho walimkuta Amata akiwa katika hali mbaya, jasho likimwagika. Kimya! Akiwa katulia kitandani.

Mara moja Jasmine akaanza kutoa huduma ya kwanza huku akimwacha Scoba akifanya jitihada za kuomba msaada kwa vifaa maalumu ndani ya chumba kile. Haikuchukua muda, madaktari na wauguzi wote wakawasili kila mmoja kwa kasi yake na kuanza kuhakikisha mgonjwa wao anarudi katika hali ya kawaida.

“Nini kimetokea?” Dkt. Zera akauliza wakati wote wakiwa wametingwa kumshughulikia mgonjwa, hakuna aliyejibu. Dakika tano baadae, akashtuka baada ya kushtuliwa kwa shoku ya umeme.

“Yuko wapi? Yuko wapiiiii?” Amata akauliza huku akiinuka pale kitandani kwa fujo. Scoba na Jasmini wakamdhibiti na kumrudisha

kitandani huku muuguzi mmoja akiwa tayari keshamdunga sindano ya usingizi isiyo na madhara. Haikumchukua muda akapitiwa na usingizi huku mashine ya *Vital Signs Monitoring* ikiunganishwa tena na mwili wake na kuanza kazi upya.

* * *

Kamanda Amata alibebwa na usingizi mzito baada ya ile sindano aliyodungwa na yule muuguzi kufanya kazi yake. Dakika chache baadae, alijikuta yupo katika ardhi nyeupe sana kana kwamba imefunikwa na theruji lakini cha kushangaza hakukuwa na theruji hiyo isipokuwa mchanga wa kawaida tu. Miti michache ilizunguka eneo hilo. Majani yake yalikuwa ya njano tupu. Upepo mkali kiasi ukaanza kuvuma na kupukutisha majani yale lakini cha kushangaza hayakwisha mitini.

“Niiikkoooo wwwaappiii?” akauliza kwa sauti ya kukoroma ndani ya huo usingizi. Mara kutoka katika vumbi la ardhi ile ng’avu lililochanganyika na majani ya ile miti, katikati ya upepo wa kisulisuli, Amata alimwona mwanaume. Mtu mzima. Aliyevalia jambakoti jeusi tupu lakini lilishonwa kwa kitambaa chepesi. Kichwani mwake akiwa na kofia aina ya pama, nyeusi yenye nyoya jekundu katika kingo ya upande wa kushoto. Mtu yule alikuwa kasimama umbali mfupi sana kutoka pale alipo, kila alipojaribu kuinua mkono amsike, hakumfikia. Ule upepo mara hii ukawa unavuma kwa utulivu na kufanya vazi la yule mtu kupepea taratibu.

“Upo kwenye mpaka wa uhai na mauti,” yule mtu akamjibu. Amata ndipo akagundua kuwa huyo mtu hakuwa na jino hata moja, kibogoyo. Kinywa chake kilikuwa chekundu sana.

“Uuuhhhaaiiii nnnaaa mmmuuuuutttiii?” akauliza.

“Ndiyo... upo kwenye hatari kubwa, kubwa sana... Nani aliyekuleta huku?” akajibiwa na kuulizwa swali.

“Nnnnniiisssaaaaaiiiddiiiiiee!” akasema.

“Huwezi kupata msaada kutoka kwangu, kwani hapa tuliposimama, nipo mbali sana na wewe. Lakini...”

Katika usingizi ule aliona kama yule mtu anamrushia picha, akaidaka na kuishika kwa mikono yake miwili.

“Geuza nyuma ... ukipewa picha uwe na tabia ya kugeuza nyuma, inawezekana anayekupa kakuwekea ujumbe au kumbukumbu fulani inayohusiana na picha hiyo...” mara yule mtu akatoweka kwa mfano

usioelezeka. Amata akaigeuza ile picha, kweli, nyumaye kulikuwa na anwani.

*Shiv Temple,
C-96, Canal Colony, Okhla,
New Delhi,
Delhi 110025, India.
Zainabiya Al-Bakbir*

Akiwa bado katika usingizi mzito aliushuhudia upepo ule ukivuma tena. Yale majani yakaanza kurudi kwenye miti kama mwanzo. Na hali ile ilipotulia akajikuta akitazamana na mwanga mkali wa kitu kama jua uliyokuwa ukihakisiwa vyema na mchanga ule na kumfikia usoni moja kwa moja. Akaatabika sana na mwanga huo kisha akafumbua macho katika uhalisia, akajikuta juu ya kitanda, watu kama kumi hivi wamemzunguka wakiwa katika mavazi ya kiganga yenye rangi tofauti.

“*Wellcome back Spark!*” Sauti ya Dokta Zera ikamwambia, huku taa kubwa yenye mwanga mkali iliyokuwa juu ya kitanda hicho ikizimwa.

“*Thank you Sir!*” Amata akajibu kwa ufasaha kabisa. Akatazama huku na huko. Zaidi ya Zera, daktari bingwa kutoka Israel alimtambua Jasmini kirahisi sana akamsalimu kwa kumpungia mkono huku akitabasamu. Dakika thelathini baadae, aliamishwa na kurudishwa kwenye chumba chake cha kawaida. Safari hii walishangaa kwani alikuwa amerudiwa na fahamu kwa asilimia karibu tisini.

SIKU ILIYOFUATA

Asubuhi na mapema siku iliyofuata, Kamanda Amata alitoka na kupelekwa chumba cha mazoezi ili kuanza kuupa mwili mazoezi madogo madogo. Ndani ya chumba hiki alikutana na watu mbalimbali ambao nao walikuwa katika tiba ya mazoezi. Tofauti na wao, yeye aliletwa kwa mazoezi ya kawaida tu ili kutazamwa ukakamavu wake upo kwa kiwango gani. Mwilini wake, zikaunganishwa mashine ambazo zingeweza kuonesha uwezo utendaji kazi wa mwili wake kuanzia ubongo, misuli na vitu vingine.

Baada ya saa mbili za mazoezi, Amata alirudishwa chumbani na kukirejea kitanda chake tena mara baada ya kuoga na kuuweka mwili katika hali ya usafi. Ndani ya chumba hiki, mara hii kulikuwa na wauguzi wawili wa kike; mmoja Mfaransa na mwingine Muisrael.

Akiwa ameketi kitandani, na mavazi yake ya wadini akachukua nukta kadhaa za utulivu akiwa kainama chini na kufumba macho kwa nguvu. Akaikumbuka ndoto aliyoota siku iliyotangulia. Maneno ya yule mtu na picha aliyompatia. Hapa akajikuta kwenye utata na kutokuelewa, akakumbuka kuwa picha ile hakuitazama upande wa juu kuona kilichopo badala yake aliikumbuka tu ile anwani. Akakumbuka zaidi kuwa hata Madam S alipomtembelea hospitalini hapo, alimpatia picha, akaitazama upande wa juu tu na ule wa chini hakuutilia maanani.

*Shiv Temple,
Zainabiya Al Bakbir*

Ni mambo hayo mawili tu aliyakumbuka kwenye anwani ile kwa uhakika zaidi, mengine hakuyakumbuka sawasawa.

“*Shiv Temple!*” akajisemea kwa sauti ndogo. Yule muuguzi Mfaransa ndiye aliyesikia neno hilo, akamtazama Amata.

“Unasemaje?” akamuuliza.

“Nahitaji kwenda nje?” akamwambia.

“*No! please*, muda wako wa kwenda nje bado haujafika, afya yako bado haijatengemaa...”

“Kadiri ya maelezo yenu, nimekaa humu zaidi ya mwezi mmoja na nusu...” Amata akalalamika.

“Ndiyo, upo sahihi kabisa, na kwa maelekezo ya daktari unatakiwa ukae hapa miezi mitatu...”

“*Impossible ...*” Amata akajibu kisha akapanda kitandani akiwa anamtazama mwanadada huyo Mfaransa, mwenye nywele ndefu, miwani iliyomkaa vizuri na kuyaficha machoye yaliyojaa kila chembe ya uzungu ndani yake. Macho ya paka.

“Hellen Duponchel...” Kamanda akatamka jina la mwanadada huyo baada ya kusoma katika kitambulisho kidogo kilichopachikwa upande wa kulia wa kifua chake, juu ya titi dogo linaloweza mtoa udenda rijali yoyote kama ataliona likiwa wazi. Hellen akamkazia macho mgonjwa wake.

“Wewe ni mzuri sana! Mrembo haswa ambaye ungefaa kuwa *Miss World...*” Amata akamwambia huyo muuguzi.

“Naona umepona eti? Maana ushaanza kujua virembo na vibaya...” Hellen akasema.

“Dunia inaamini kuwa wanawake warembo hutoka Ufaransa, pasi na shaka hata wewe umetokea huko, maana jina tu limedhihirisha

hilo kwangu... asante kwa huduma yako nzuri...” Kamanda Amata akamwambia muuguzi huyo.

“Unatakiwa ulale sasa,” yule muuguzi akasema huku akiandaa dawa ya kumpatia.

“Sawa, ila nategemea kupata huduma nyingine nzuri sana kutoka kwako...” akazidi kumwambia huku akijiweka vyema kitandani.

Kamanda Amata hakulala usingizi kama ambavyo wao walifikiri, alikuwa akiwasikiliza yote waliyokuwa wakiongea. Aidha alikuwa akiona nani anaingia na anazungumza nini na nani anatoka. Mazungumzo ya madaktari tofauti waliokuwa wakiingia na kuzungumza na wauguzi aliyasikia vyema hasa yale ambayo yalikuwa katika lugha ya Kiingereza. Aliendelea kubaki kwenye hali ile bila wengine kujua. Jioni ya siku hiyo, wale wauguzi wakabadilishana na kuingia wengine. Muda wote aliokuwa kajifanya kulala, Amata alikuwa akirudisha fikra zake katika matukio ya mwisho kuyakumbuka. Fikra zake zote zikahitmishwa na taswira ya Tausi Mpendamali, binti wa Kimakonde ambaye kwaye ndiyo hali hii ikamkuta. Zaidi ya hapo ni giza na kutokujua nini kiliendelea. Alijua tu baadae kuwa yupo India kutokana na maandishi aliyokuwa akiyasoma ukutani ndani ya hospitali hiyo. Kibaya zaidi akajaribu kufikiri nini kinaendelea katika kuitafuta chanjo iliyopotea, na nini hatima ya wale adui zake waliyotaka kuyagharimu maisha yake. Akaanza kupumua kwa nguvu, jasho likaanza kumtiririka, vifaa vilivyomzunguka vikaanza kupiga kelele vikiashiria kuna hatari. Muuguzi aliyekuwa zamu akawahi kumpa huduma ya kwanza kabla hali haijawa mbaya huku tayari akiwa keshabonya kengele ya hatari ambayo huwashtua madaktari maalumu wanaomtibu. Kamanda Amata akainuka ghafla na kumpiga kichwa kisicho na madhara yule muuguzi. Kwa pigo lile akajikuta anakosa muelekeo na kuanguka upande wa pili. Azma ya Amata ilikuwa sahihi, yule muuguzi alipoteza fahamu.

Kamanda Amata akainuka haraka, akaiwahi nobu ndogo ya kufunga mlango, akaibonya na milango ya kuingia katika chumba hicho ikajifunga. Akachomoa kila kilicho mwilini mwake, akaliendea dirisha kubwa na kusogeza kioo kando. Akajikuta akitazama ardhi kutoka ghorofa tatu juu. Akajitokeza nusu na kutazama huku na kule, akaona bomba la chuma la inchi nne linalotumika kushusha maji taka katika tanki maalumu. Akashukuru moyoni na kulitumia hilo kufika chini bila kujulikana.

Mara baada ya kufanikiwa kufungua mlango, madaktari kama sita hivi

wakaingia wakiwa na askari wa ulinzi katika hospitali hiyo na kukuta hola. Zaidi ya muuguzi aliekuwa sakafuni, ndani ya mzimio, hakukuwa na mtu mwingine yoyote wadini. Upepo mwanana ulikuwa ukiingia kupitia dirisha lililoachwa wazi. Dokta Zera akaliendea na kutazama nje, zaidi ya miti na maua mazuri aliyokuwa akiyaona kule chini kwa msaada wa mwanga wa taa, hakuona kingine.

“Ametekwa?” sauti ya askari ikamuuliza daktari yule.

“Labda! Inabidi hii kesi ifike panapohusika...” Daktari Zera akamwambia yule askari huku moyoni akijua kwa vyovyote, Spark kama anavyomwita, atakuwa ametoroka.

Mungu akubariki na akulinde popote uendapo! Zera akajisemea kimoyomoyo na kutoka taratibu kuelekea kule ambako yule muuguzi amepolekwa kwa huduma ya dharula.

* * *

Nje ya hospitali hiyo, Kamanda Amata alifikia kwenye bustani nzuri ya maua, hakupoteza muda, akazunguka upande wa pili ambapo kuna barabara na maegesho ya magari. Hakuuliza. Upande ule kulikuwa na magari ya kukodisha yamejipanga tayari kwa kutoa huduma. Akaingia katika mojawapo na kuketi siti ya nyuma.

Dereva wa gari hilo alikuwa amesinzia kwenye kiegamo cha kiti, alipohisi mtikisiko, akashtuka na kutazama nyuma. Macho yake yakagongana na yale ya Amata, akabaki kinywa wazi huku midomo ikimtetema.

“Shiv Temple, haraka sana...” akamwambia kwa Kiingereza. Yule dereva bado alibaki kwenye mbung’ao.

“Ipi?” akamuuliza Amata.

“Kwani we unaijua ipi?” akamjibu kwa swali.

“Zipo nyingi, sasa inabidi uniambie Shiv Temple ipi au ipo uelekeo gani?” yule dereva alimsaili Amata huku akimtaazama kwa woga.

“Aaaaannhh Okhla...”

“Sawasawa!” yule dereva akamjibu na kuwasha gari huku bado akiwa na wasiwasi. Akainua kifaa cha kuongelea na kuanza kuongea Kihindi na mtu upande wa pili. Haraka sana Amata akakinyakuwa kile kifaa kutoka mikononi mwa yule dereva na kumwamuru aendeshe gari.

“Hapa njia fupi ni kupitia Vishwasji Sadak na Barabara ya Kalinji Kunj, hiyo ndiyo fupi na ni kilomita tano tu, dakika zetu kumi na

mbili tutatakuwa pale. Au unataka ya kupitia Barabara ya Mohammad Ali Jauhar Marg?” yule dereva akamwambia Amata.

“Endesha gari...” akamwambia kwa ukali, na yule jamaa akaingiza gari barabarani, akazunguka upande wa pili wa maegesho na kuingia Barabara ya Vishwasji Sadak na kuendesha kwa mwendo wa wastani huku ndani ya gari hilo muziki wa Lata Mangeshkar ulikuwa ukiburudisha. Kamanda Amata hakuwa na amani kwani hakujua ni nini yule bwana aliongea kwa lugha ile ya Kihindi. Mara kwa mara alikuwa akigeuka nyuma kutazama kupitia kioo, kama kuna gari linalowafuata. Mwendo kama wa dakika tano hivi, yule dereva akaiacha barabara ile na kukunja kona kushoto na kuchukua ile ya Kalinji Kunj. Hapo akaongeza mwendo na dakika sita baadae alifika katika hekalu hilo na kuweka gari katika maegesho.

“Unapita hapa kwenye hiyo njia, utavuka daraja dogo hapo na hekalu utalionga mbele huko...” yule dereva akamwelekeza. Kamanda Amata akafungua mlango tayari kuteremka.

“Hey *Sir!* Ni rupia 150 tafadhali,” dereva akaomba ujira wake kwa kazi aliyofanya. Kamanda Amata akajifanya kama anajipapasa hivi, lakini ghafla, akafyatua pigo moja la karate lililotua maeneo ya juu kidogo ya shingo ya yule dereva. Akajibwaga katika kiti cha upande wa pili na kupoteza fahamu.

“Utaamka baadae!” Amata akamwambia na kuteremka haraka, kisha akafuata ule ujia alioambiwa na yule dereva mpaka akavuka huo mto na kukuta geti dogo. Upande wa pili wa geti, kulikuwa na hekalu kubwa la Kihindu, lililopendezeshwa kwa taa zenye mng’aro wa rangi ya dhahabu. Akavuta hatua bila kujali watu wachache aliokuwa akipishana nao huku wakimtazama kwa mshangao. Yeye hakujali, na moja kwa moja akafika kwenye kingo kabisa za hekalu hilo. Vijana walioonekana kama walinzi walimsimamisha kwa maneno ya lugha ya Kihindi, akatii na kusimama hata kama hakuelewa.

“Zainabiya Al Bakhir ,” Amata akatamka jina hilo na kuwatazama wale vijana. Na wao pia wakatazamana, kisha wakamgeukia mgeni wao kana kwamba hawajamuelewa anazungumza nini. Kabla hawajaongeza swali, kijana mwingine akatokea nyuma yao na kuzungumza kwa Kihindi, kisha Amata akatakiwa kufuatana na kijana huyo kwenda huko alikotokea.

Safari yao iliishia katika jumba kubwa nyuma ya hekalu hilo. Jumba hilo pia, kama lilivyo hekalu lile, lilipambwa kwa nakshi nzuri za

kuvutia za Kiajemi. Zuria safi lenye michoro ya kupendeza likamlaki Kamanda, akatikisa miguu kuvua viatu, ndipo akagundua kuwa hakuwa navyo mguuni.

“Usiwe na wasiwasi, keti kwenye takia, na mwenyeji wako ataungana nawe punde tu,” yule kijana akamwambia kwa Kiingereza. Amata akaketi juu ya mto mkubwa ulio chini, katika zuria hilo. Haikupita hata dakika, mwanamke wa makamo, mrefu aliyejivika nguo nzuri za kumetameta akaingia mahali hapo huku akifuatwa na wasichana wengine takribani sita hivi, wenye utuli na ubani mikononi mwao.

“Amata Ric!” yule mwanamke akaita na Amata akanyosha mkono kumsabahi lakini yeye akatikisa kichwa kukataa na kuifutika mikono yake ndani ya vazi lake.

“Zainabiya Al Bakhir?” Amata akauliza.

“Ndiyo! Karibu sana,” yule mwanamke aliyejulikana kuwa ni Zainabiya akamjibu na kumkaribisha Amata. Wale wasichana wakachoma udi na kuweka chini zile chupa za utuli. Harufu nzuri ikatapakaa mahali pote, huku wao wakiondoka na kuwaacha wawili tu.

“Pole sana!” akamwambia.

“Asante!” Amata naye akajibu.

“Nimefuata maelekezo niliyoyapata ndotoni, anwani imenifikisha hapa...” akasema.

“Nilikuwa nakusubiri, nilijua utafika,” Zainabiya akamwambia.

“Mpaka wa uhai na mauti... maana yake ni...”

“Kifupi ni kuwa, roho yako inatafutwa kwa udi na uvumba,” Zainabiya akamwambia Amata. Amata akatega sikio kusikiliza.

“Kitu ulichotumwa ukitafulute kinaifanya roho yako iwe rehani na maisha yako kuwa hatarini. Kama si wenzi wako ... ungekwisha kufa, kwani kifo chako kilikufata ukiwa usingizini...” Amata akasikiliza tu pasi na kusema lolote.

“Sasa sikiliza, una siku nne tu kukamilisha kazi yako, biashara inafanyika Msumbiji katika Jiji la Maputo...” Zainabiya akamweleza Amata.

“Biashara?”

“Ndiyo. Kwani hujui, Lord Dimens yuko tayari kuuza *formula* ya *Anti-Aidiosis* kwa matajiri wa ulimwengu...”

“Shiiit!” Amata akajikuta anaingiwa na hasira, “Umejuaje yote haya? Nawe u hapa siku zote?” akamtupia swali.

“Mimi ni dada yako kutoka Lubyanka!” Zainabiya akajibu huku

akifungua vazi lake upande wa kushoto. Juu kidogo ya titi lake jeupe la mviringo kulikuwa na kitu kama muhuri mweusi au kwa sasa tungeita tattoo yenye mchoro wa nembo ya shirika la umoja wa kisovieti la maswala ya ulinzi wa ndani (*People's Commissariat for Internal Affairs*), NKVD.

“Unafanya nini hapa?” Amata akamuuliza wakati mwanamke huyo akifunika titi lake.

“Mafichoni... lakini nafanya kazi binafsi. Nilipewa taarifa yako na mtu asiyejulikana anayependa kuvaa mavazi meusi naye ni mweusi kama wewe, ameshafanya kazi kama yako...” akatoa bahasha nyeusi juu yake ina picha ya nyoya jekundu, “Chukua hii,” akamwambia. Amata akaipokea na kujaribu kuiminyaminyana.

“Unatakiwa kuondoka India saa chache zijazo...” Zainabiya akamwambia Amata. Ukimya ukatawala kati yao, akiwa bado kwenye mshangao, akawasili msichana mwingine mrembo na kusimama kando yao. Zainabiya, akainuka na Amata akafanya vivyo hivyo.

“Go! Mfuate huyu binti...” akamwambia.

“Zainabiya! Nina mambo ya kuzungumza nawe...”

“Hakuna nafasi kwa sasa, wakati ni kama tishu, go!”

* * *

Hakikuwa chumba kikubwa, lakini kilichosheheni kila kitu ndani yake. Ni ndani ya kasri lile lile, Amata aliingizwa na yule binti.

“Kila kitu kipo hapo!” yule binti akamwambia.

“Unaitwa nani?” Amata akamuuliza. Lakini badala ya kujibu yule binti akaondoka. Kamanda Amata akashusha pumzi na kuona kila kitu ni miujiza kwake. Akatazama kitanda cha wastani kilicho mbele yake, akavuta hatua na kusimama kando. Akakibonyeza bonyeza. Akakiacha na kulielekea kabati, akafungua na ndani yake akakuta kumening'inizwa suti safi, nyeusi. Palikuwa na saa ya mkononi pamoja na bastola juu ya kijidroo kidogo kilichokuwa wazi. Bastola aina ya *Glock 23* ilikuwa imelala kwa utulivu. Hii ni bastola inayopendwa sana na polisi huko ughaibuni na mawakala wa siri wa serikali. Uwezo wake wa kubeba risasi kumi na tano ndiyo unaowavutia wengi. Akageuka na kukirudia kitanda, akaketi. Katika mfuko wa pajama lake la hospitali akaichomoa ile bahasha na kuichana. Ndani yake kulikuwa na pesa za Kimarekani. Vibunda vitatu vya noti za dola mia mia, akatikisa kichwa juu chini

kukubaliana na alichokiona. Akazitoa na kuweka kitandani, ndani ya bahasha kukabakiwa na tiketi ya ndege, akaichomoa na kuitazama. Ilikuwa tiketi ya ndege inayoondoka saa nne kutoka muda huo. Akainua uso na kutazama saa ya ukutani, ikamwonesha kuwa ni saa tano usiku kwa saa za India. Tiketi hiyo ilionesha mwanzo wa safari ni jiji la New Delhi na mwisho ni Maputo, Msumbiji na ilikuwa ya mruko mmoja tu. Ndani ya bahasha hiyo hiyo akakutana na karatasi nyingine ndogo, akaichukua na kuisoma.

Montebelo Girassol Hotel
Room 412

Baada ya kusoma akakitia kinywani na kukitafuna, kisha akaingia maliwato kuuswafi mwili wake.

SURA YA 20

DAR ES SALAAM

JNIA – saa 8 usiku.

MVUA YA RASHARASHA ilikuwa ikiendelea kunyesha katika jiji hilo. Usiku huu tayari watu wengi walikuwa majumbani mwao baada ya mikiki mikiki ya kila siku. Hali katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es salaam (JNIA) ilikuwa shwari. Katika maegesho ya magari, Madam S na Chiba walikuwa wametulia ndani ya gari lililokuwa likiunguruma tangu limeingia maegeshoni hapo. GMC, gari la Kimarekani, jeusi, imara na lenye nguvu ndilo lililokuwa limewabeba wawili hao.

“Hizi taarifa za TSA1 zinanichanganya kidogo,” Madam S akamwambia Chiba.

“Zisikuchanganye kwani si mara ya kwanza,” Chiba, aliyekuwa nyuma ya usukani akamwambia bosi wake.

“Kinachonichanganya ni kuwa ametoroka au ametekwa?” maana hatuna taarifa kamili hapa.

“Kwa swala la kutekwa sidhani... labda kutoroka,” Chiba akamwambia.

“Kuna wakati TSA 1 huwa ananiudhi sana hata hufikiria kumnyang’anya beji yake, arudi zizini,” Madam akaongea akionesha wazi kuwa kuna mambo hayamfurahishi kabisa.

“Hulka tu mama...”

“Hapana, kuna wakati wa kazi na wakati wa mambo hayo anayoyapenda, hajifunzi... mara ngapi anaingia matatani kwa sababu ya wanawake? Na hii ashukuru Mungu wake tu...” Madam akalalama.

“Dah! Ni kweli lakini huwezi kujua kwa nini anapenda kufanya hivyo, isije kuwa ni mbinu yake ya kikazi,” Chiba akaongea na mara kioo

cha upande wa abiria, ambako Madam S alikuwa ameketi, kikagongwa. Hakushuka; akabonya batani moja na loki za milango zikafunguka. Daktari Jasmine na Scoba wakajitoma ndani na kufunga milango.

“Karibuni nyumbani! Baada ya miezi miwili ya kula kachori na kababu huko India,” Madam S akawaambia huku macho yake yakiwa mbele kana kwamba anayeongea naye yu huko.

“Asante!” wakaitika kwa pamoja.

“Kaka yenu...” akahoji.

“Yuko sawa, anaendelea vyema na hata kumbukumbu zake zimerudi kwa karibu asilimia themanini, ila shida ilobaki ni utendaji... hapo bado hajawa sawa,” Jasmine akasema.

“Nafikiri hauko sawa Jasmini...” Madam S akamwambia binti huyo huku akigeuka nyuma kuwatazama.

“Kwa nini unasema hivyo?” Jasmine akauliza.

“Inawezekana anatenda zaidi ya asilimia mia moja... hivi tunavyozungumza Amata hayupo Apollo...”

“Kha! Mmemwamisha au?” Jasmini akashangaa.

“Si bora tungemwamisha! Ametoroka,” akawaambia na kila mmoja akabaki kinywa wazi. Chiba akaondoa gari taratibu na kuliingiza barabarani

“Huyo ndiye TSA 1, sasa sijui yuko wapi, mtakaa mpange kisha mtanambia,” Madam S akawaeleza, “Ila kuna tetesi kuwa huko Msumbiji kuna uzinduzi wa chanjo ya *AIDIOSIS*, siku nne zijazo. TSA 2 na TSA 5 mtakuwa safarini kesho kufanya uchunguzi kama huo mzigo ni wa kwetu au nao wamevumbua wa kwao...”

“*Yes Sir!*” Chiba akajibu wakati akikaribia kabisa taa za TAZARA.

“Unaona sasa! Kaka yako keisha kuharibu,” Madam S akamwambia Chiba kisha wote wakacheka.

“Sitaki kuamini kama Kamanda ametekwa, ninachokiamini atakuwa ametoroka. Ni vipi kama atakuwa amesikia habari hiyo ya Msumbiji? Unafikiri hawezi kunuia kwenda huko?” Jasmini akauliza.

“Atawezaje ilhali hana dokumenti yoyote, hana pesa wala nini... tumempeleka yeye tu kule...” Madam S akasema.

“Mh! Madam S, samahani! Hivi umesahau *code* ya TSA1... *Code 005?* Hata kama hana pasipoti, hawezi kushindwa kuipata akiamua, lakini anao uwezo wa kusafiri anakotaka kwa njia usiyoitegemea. Nina uhakika hajatekwa, na wala hajatoroka...” Chiba akasema na wote wakamuunga mkono.

"Ila..." Madam akataka kujua.

"...TSA 1 yupo kazini," Chiba akajibu.

"Sijampa kibali, kwenda kule ni sawa na kufanya uhalifu, na akiua atakuwa matatizoni, akikamatwa hakuna wa kumtetea..." Madam S alizungumza akionekana kuwa na hasira za wazi.

"Sijawahi kusikia ukizungumza namna hii juu ya TSA1..." Scoba akaongea, "Umemchukia kiasi hiki?" akauliza.

"Hapana sijamchukia hata kidogo! Nampenda kuliko unavyofikiri, ila kuna wakati ananiudhi, huwa natamani nimchape fimbo kama mwanangu wa kuzaa..." Madam S akasema.

"Mpe nafasi..."

"Akiniridhisha nitamfikiria..." Madam akajibu. Daktari Jasmini na Scoba wakatazamana na kukonyezana.

* * *

CABO DELGADO

Katika uwanja mkubwa wa mchezo wa *Golf* uliojengwa nje ya kasri la Lord Dimens kulikuwa na watu wasiozidi wanne. Lord Dimens mwenyewe, na mwingine mtu mzima aliyevalia *track suit* nadhifu. Wote wawili walikuwa na fimbo mahususi kwa kuchezea mchezo huo. Umbali wa mita kama kumi hivi alikuwapo Bonston, mlinzi na msiri wa Lord Dimens, kijana shababi wa Kizungu aliyejaliwa mwili wenye jumbo la kiume haswa lililjengwa kwa misuli yenye afya iliyotokana na mazoezi. Pia kijana mwingine wa Kiafrika aliyekuwa na fuko kubwa lililosheheni vifaa mbalimbali vya mchezo huo. Kijana huyu kazi yake ilikuwa ni kubeba fuko hilo na kuwapatia vifaa hivyo pindi wanapohitaji.

Lord Dimens na mgeni wake, walikuwa wakicheza kidogo na kusimama kwa mazungumzo kisha wanaendelea tena.

"Unaonaje hali ya Maputo kwa shughuli ya kesho kutwa?" yule mgeni akamuuliza Dimens.

"Kila kitu kipo sawa, serikali imeweka ulinzi wa kutosha kuepuka yale yaliyotokea Tanzania..." Dimens akajibu.

"Serikali?" yule bwana akauliza, huku akipandisha vizuri *tracksuit* yake.

"Ndiyo, hatuna tabu na serikali, yenyewe inajua kile kidogo inachokiona..." akamsogelea mgeni wake na kumnong'oneza, "Hawajui kitu!"

Dimens akaendelea kucheza mchezo ule mara hii akapiga kwa nguvu na ule mpira ukaenda mbali na yule kijana wa Kiafrika alipaswa kwenda kuufuata na kuwaambia mabwana wake mahali ulipo nao huja baadae taratibu.

“Hii ndiyo kazi ya Waafrika siku zote... sisi tukipiga mpira wao wanaufuata, kwa mtindo huu hawataweza kujitawala... kupiga mpira ni maamuzi yetu, na wao kuufuata ni wajibu wao,” Lord Dimens akamwambia mgeni wake, naye akatikisa kichwa huku Bonston akitabasamu.

“Kila kitu kipo sawa... Radisson Blu Hotel ndiyo itayobeba wageni wote... na ukumbi wa mikutano wa Joachim Chissano utatumika kwa hafla yenyewe. Kuna walinzi wa siri wengi ambao hawaonekani kwa macho, hakuna hujuma itakayotokea...” Dimens akamwambia mgeni wake kwa kujiamini.

“Na vibaraka wa Langley, umewatazama?” yule mgeni akamuuliza wakiwa wanatembea taratibu kufuata kule mpira ulipo na Bonston akiwa nyuma yao kama mita kumi hivi.

“Wapo chini ya nyayo zangu, wa Tanzania ninaye, wa Maputo keshatolewa roho, na mwingine aliyetumwa ninaye... hawaniwezi, wasifikiri nilikaa pale kwa ujinga. Duniani ishi kwa malengo maadam umezaliwa, asiye na malengo ni marehemu pekee. Hivyo hata wewe unayepumua kila siku kama huna malengo, ni sawa na marehemu...” Dimens akajibu.

“Nimekuelewa!”

“Tuna saa arobaini na nane tu...” Dimens akamwambia huku akivua gloves zake ikiwa ni ishara kuwa mchezo umeishia hapo.

* * *

MAPUTO – MSUMBIJI

Habari za uzinduzi na mnada wa chanjo ya *AIDIOSIS* zilivuma na kusambaa kama pepo za Kusi. Mashirika ya habari ya Kimataifa yakavutika kujua nini kinajiri. Makampuni makubwa ya madawa yakasogea kufanya *betting* katika mnada huo. Wakazi wa jiji hilo walishuhudia wageni wa aina mbalimbali katika mitaa yao. Watu wa Lord Dimens waliweka macho yao katika kila hoteli kubwa, wakiwa na

wazo moja tu ‘wabaya wetu wasituharibie’.

Katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Maputo, unaojulikana kama Lourenço Marques au Mavalane, idadi ya wapokea wageni iliongezeka lakini kwa malengo tofauti. Wale waliohisiwa vibaya walipata tabu kidogo kutoka kwa vijana wa Dimens.

Ndege ya shirika la Air India ilitua salama salimini alasiri ya siku hiyo, baada ya kupitia miji kadhaa katika safari yake. Katika siti ya mwisho ndani ya behewa ya *Business Class*, aliketi Kamanda Amata akiwa katika suti ya gharama sana. Aliendelea kutulia kitini wakati abiria wengine wakishuka. Akageuka na kutazama nje kupitia dirisha la kando yake na kushuhudia majengo kadhaa ya uwanja huo na wafanya kazi wakipita huku na kule.

“Maputo *once again!*” akajisemea kwa sauti ndogo. Amata alikuwa bado analikumbuka sana jiji hili kwa mikikimikiki iliyomkuta miaka kadhaa nyuma. Akatabasamu na kusimama, akaweka vizuri koti na tai yake, akaipachika miwani yake ya jua usoni tayari kulikabili jiji hilo. Mara hii alijiweka kuwa abiria kama wa kumi hivi kutoka mwisho hivyo mbele na nyuma yake kulikuwa na watu. Hakuwa na mkoba wowote mkononi mwake wala sanduku katika buti la ndege hiyo. Alikuwa yeye kama yeye tu. Akiwa tayari katika mlango wa ndege hiyo na hatua chache kuifikia ngazi ya kwanza kuteremka, sauti ya kike ikamshtua kutoka kushoto.

“*Your card sir!*” akageuka na kumwona mrembo huyo wa Kihindi aliyependeza na vazi lake, mwenye midomo myekundu iliyopakwa rangi kiufundi haswa. Kamanda Amata akasita kwa sekunde chache na kumtazama. Zaidi ya kuhudumiwa naye kule ndegeni hakukuwa na mahusiano mengine kabla. Mkono wa mwanamke huyu ulikuwa na kadi ndogo. Akatabasamu na kuinyakua, kisha akaitia katika mfuko wa shati lake.

“*Thank you!*” akashukuru. Kamanda Amata akateremka ngazi za ndege hiyo na kuvuta hatua mpaka katika jengo la wasafiri ambamo humo alitakiwa kukamilisha maswala ya uhamiaji.

Katika dawati kubwa, aliweka pasipoti yake mbele ya mwanadada aliyevalia sare nadhifu ya Idara ya uhamiaji ya nchi hiyo. Akaichukua na kuifungua kurasa alizokuwa akihitaji. Ilikuwa mpya kabisa.

“Mr. Kelvin Sebuza!” yule mwanadada akaita huku akimwalia Amata usoni.

“Yes, ni mimi!” Amata akajibu.

“Ni mara yako ya kwanza kusafiri? Maana pasi yako haina muhuri hata wa dawa...” akamtania, naye akatoa tabasamu adimu kwa mrembo yule pasi na kujibu chochote.

“Unatakiwa kulipia Dola za Kimarekani hamsini kwa ajili ya *Visa*,” yule mwanadada akamwambia Amata huku tayari akiwa amekwishaweka muhuri wake mezani. Kamanda Amata akachukua kiasi hicho cha fedha na kumpatia, naye akaandika taarifa kadhaa na kugonga mhuri. Alipompatia pasipoti yake akaambatanisha na risiti ya malipo hayo.

“Asante sana!” akashukuru na kuliacha dawati lile huku akisindikizwa na macho ya mrembo huyo. Nje ya uwanja huo aliendea taksi iliyokuwa hatua chache kutoka kwake, mara baada ya kuvuka barabara mbili zinazotenganisha jengo la uwanja huo na maegesho.

“Karibu sana!” dereva kijana wa taksi ile alimkaribisha na kumfungulia mlango wa nyuma, akaingia na dereva naye akaketi nyuma ya usukani.

“Hotel Montebelo Girassol,” Amata akamwambia.

Yule kijana akawasha gari na kuliondoa taratibu kisha akachukua barabara ambayo inampeleka barabara kuu.

“Utanilipa kwa dola au?” dereva akauliza.

“Kwa dola ni nzuri zaidi,” Amata akajibu huku akigeuka nyuma kutazama kama kuna yeyote anayewafuata.

“Sawa! Dola tano mpaka hotelini,” akamwambia.

“Sawa!” akamjibu huku akiendelea kutazama nyuma mara kwa mara kujihakikishia usalama. Yule dereva akaendesha huku akipiga mruzi kufuatisha wimbo fulani ambao Amata hakuujua sawasawa. Akachukua barabara ya Accordos De Lusaka, akaendesha mwendo wa dakika chache tu na kuiacha barabara hiyo, akakunja kushoto na kuchukua ile ya Joachim Chisano na kuiacha ile ya Kenneth Kaunda kwa minajiri ya kupunguza urefu wa safari. Mara baada ya kupita mnara wa kumbukumbu wa *The Smiling Lion*, akanyoosha mpaka katika hoteli ile.

“Karibu sana, hii ndiyo Maputo, utainjoi sana kwa kukaa kwako hapa,” yule dereva akamwambia Amata huku akimpatia kadi yake ya kibiashara, “Ukihitaji kwenda popote iwe kustarehe au vyovyote vile, waweza kunipigia,” akamwambia. Kamanda Amata akaipokea na kumpa noti moja ya Dola tano za Kimarekani. Akamshukuru na kuiacha taksi hiyo.

Hatua zake zikamfikisha katika dawati la mapokezi, akapokelewa na kijana mtanashati, aliyevalia vazi la kupendeza lililonakshiwa kwa

kitenge kisichochosha macho.

“Kelvin Sebuza,” akataja jina lake mara baada ya kumsalimia kijana huyo.

“Karibu sana Mr. Kelvin, hapa ndiyo Montebelo Girassoul. Huduma yoyote unayohitaji utaipata...” yule kijana akamkaribisha kwa bashasha, “Una mzigo wowote?” akamuuliza.

“Hapana, sina. Nafikiri mzigo wangu tayari umeshafika niendako...” Amata akamwambia.

“Hah! Hah! Hah! Haya bwana karibu sana, *room* namba 412,” yule kijana akamwambia huku akimkabidhi funguo. Kisha akamwita mhudumu wa kike kutoka ofisi ya pili ili ampeleke Amata katika chumba chake.

* * *

Hoteli ya kimataifa ya Radissou Blue, iliyojengwa kando tu ya Barabara ya Nyerere ndani ya Jiji la Maputo, ilipokea ugeni wa kila aina, tayari kwa siku maalumu ya uzinduzi na mnada wa chanjo ya *AIDIOSIS*. Wapo wafanyabiashara wakubwa wa madawa waliofika katika hoteli hiyo. Makampuni na taasisi mbalimbali yalituma wawakilishi. Kwa ujumla, tukio hilo liliandaliwa kwa kiwango cha juu kuliko lile lililofanyika huko Lindi, Tanzania.

Ndani ya hoteli hiyo, katika chumba kimoja wapo, kulikuwa na watu wanne walioketi katika meza ya mzunguko. Katikati ya meza hiyo, kulikuwa na kompyuta kubwa zipatazo nne, yaani kila mmoja alikuwa na kompyuta yake, akifuatilia watu wake sehemu mbalimbali za jiji la Maputo. Taarifa zote, mawasiliano, picha za mnato na jongefu, zilikuwa zikifika katika meza hii. Na kutoka hapa ndipo amri ilitoka; kama afuatiliwe au aachwe. Kwa ujumla, kulikuwa na ubize wa hali ya juu kiasi kwamba ingepita hata robo saa watu hao wasiongee.

Ukimya wao ulikatishwa na mfurukuto ambao ulitokea katika simu mojawapo kati ya nne zilizokuwa mezani hapo.

“Endelea!” mtu mmoja kati yao aliipokea simu hiyo na kuweka sauti kubwa.

“Kuna mzigo umeingia tuna wasiwasi nao,” sauti ya upande wa pili ikasema.

“Mmeufungua kuutazama ndani kuna nini?” yule mtu akauliza huku

akionekana kuwa makini zaidi kuliko mwanzo.

“Bado, ila tunajua ghala gani umehifadhiwa...” sauti ile ikasema.

“Nipe jina la ghala hilo niwasiliane na wahusika,”

“Montebello Girassoul!” akajibiwa.

“*Copy!*” yule bwana akakata simu na kuanza kupiga namba nyingine, kisha akaiweka sikioni.

* * *

Nje ya hoteli hiyo ya Montebello, vijana watatu walikuwa kimya katika gari, kazi yao kubwa ilikuwa ni kusubiri amri tu ya nini wafanye. Ndani ya gari hilo, kulisheheni silaha nzito ikiwamo mabomu ya kurusha kwa mkono, bastola za kisasa na bunduki kubwa zenye nguvu. Vijana hao waliopewa mafunzo ya mapambano ya kila aina waliwekwa katika kila hoteli kubwa, tayari kumkabili yeyote atakayeonekana kuwa na hatari kwa upande wao.

Sauti hafifu ikasikika katika simu iliyo katikati ya kiti cha dereva na abiria. Haraka, akainyakuwa na kuiweka sikioni.

“*Squad 1 reading...*” yule bwana akaitikia na kutulia. Baada ya maneno kadhaa kutoka upande wa pili, akakata simu na kuwatazama vijana wake.

“Vipi?” mmoja akauliza.

“Kuna mtu kaingia hapo sasa hivi, inapaswa ajulikane ni nani na amekuja kwa lipi. Fununu zinaonesha ni mtu hatari kwetu,” yule bwana akajibu. Wale vijana wakajiweka tayari, wakipachika vyema bastola zao viunoni. Walipohakikisha wapo sawa, wakampa mkono kiongozi wao na kuteremka garini. Hatua fupifupi zikawafikisha mapokezi, hapo wakapata ushirikiano kwa asilimia mia, ikiwamo na namba ya chumba alichofikia mgeni huyo. Vijana hao, wakafika mpaka katika mlango wenye namba 412, wakapeana ishara za kuwa wawe tayari kwa lolote. Mmoja akasimama mkabala na mlango huo huku mwingine akiwa kando tayari kutoa msaada kama kuna upinzani wowote.

* * *

Ndani ya chumba kile, Kamanda Amata, pindi tu alipoingia alijihakikishia usalama wote, ikiwa ni pamoja na kutambua kama kuna vinasauti au kamera za siri. Kwa kuwa hakuwa na kifaa maalumu kwa kazi hiyo, alitumia mbinu za kawaida kuweza kuvitambua.

Alipojihakikishia usalama upo akakiendea kitanda na kukibonyeza bonyeza, kisha akafunua mto wa kulalia, na hapo ndipo akakutana na kitu asichokitarajia. Mashine ndogo ya sauti, akaiinua na kuigeuzageuza, ndiyo, kilikuwa kifaa maalumu cha kurekodia sauti. Kila alipojaribu kukiwasha hakikuwaka.

"Insert audio card!" sauti ya kike ilisikika kutoka katika kifaa hicho ikijirudiarudia. Kamanda Amata akakumbuka kadi aliyopewa na yule mhudumu wa ndege. Akaichomoa kutoka mfuko wa koti lake, akaitazama kwa kuigeuzageuza kana kwamba ndiyo mara ya kwanza kuiona. Akabonya kitufe kimoja na mlango mdogo ukafunguka katika kifaa hicho. Hapo palikuwa na sehemu wazi ya kupachika kadi hiyo, akafanya hivyo na kufunga. Kishapo akachukua vifaa vya kusikilizia na kupachika masikioni.

Ina maana hawa watu wana mtandao mkubwa namna hii? Akajiuliza kwa kuwa alijaribu kuunganisha matukio, kuanzia lile la ndoto, kukutana na Zainabiya mpaka huyu mhudumu wa ndege aliyempatia kadi hii. Akatahayari. Mara tu baada ya kupachika masikioni mwake, ikasikika sauti ya toni kama kengele ya mlango ya *'ding dong'*.

"Una jambo moja tu la kufanya, kumfuta duniani Lord Dimens. Mtu hatari, aliyeshindikana, anayetafutwa kila kona duniani. Haonekani kirahisi, zaidi ni jina lake tu kwenye chupa za madawa. Ni mwenye akili zinazotangulia saa nyingi mbele ya mawazo yako. Anaishi kama kivuli, haonekani kama bewa. Ni mtu hatari, mwenye ndoto zinazohatarisha ubinadamu.

Kesbo, atakuwapo kwenye hafla aliyoiandaa katika ukumbi wa mikutano wa Kimataifa wa Joachim Chissano, jijini Maputo. Ukiveza kumgundua, mfute duniani. Kwa nini tunakutaka umfute duniani? Hudburia hafla hiyo na mengi utayagundua... all the best!"

Mara baada ya ujumbe huo kumalizika, sauti ile ya toni ikasikika tena kisha kukabaki kimya. Kamanda Amata akiwa bado kasimama, akaondoa masikioni mwake kile kifaa cha kusikilizia, na alipobonyeza kitufe cha *off*, mfumo wa mashine ile ukaharibika kabisa, kwamba haiwezi kutumika tena.

Amata hakujua kama kapewa kadi yenye ujumbe mzito namna hiyo. Akiwa katika hali ya kutafakari, akajikuta mapigo ya moyo wake yakipiga kwa nguvu, akahisi hali si shwari eneo hilo. Akakitupia kitandani kile

kifaa, akaichomoa bastola yake kutoka kwenye mkanda maalumu mwilini mwake, akavuta hatua ndefu ndefu mpaka bafuni na kufungua maji katika bomba la mvua, kisha akarudi na kujificha sambamba na ubavu wa kabati la mbao.

Mlango ukafunguliwa kwa nguvu, na mtu mmoja akaingia akiwa ameficha sura yake kwa soksi kwa minajiri ya kutojulikana. Moja kwa moja mtu yule akaingia bafuni na kufyatua risasi ovyo, kisha akatulia.

“Vipi umemmaliza?” mwingine akauliza na kujitoma ndani ya chumba hicho. Amata akashukuru hisia yake ya kutokumshambulia yule mtu. Sauti hafifu ya kilinda usalama cha bastola ya *Glock 23* kikawafanya wageuke nyuma kutazama. TSA 1 hakufanya ajizi katika hilo, kidole cha shahada kikafanya kazi yake, risasi moja ikazama kifua mwa yule mtu wa kwanza, ikambwaga chini kama mzigo. Yule wa pili alipotaka kukimbia akachelewa kwani risasi nyingine ya Amata akamvunja goti na kumpeleka sakafuni huku akipiga yowe. Kamanda Amata akawahi na kuufunga mlango. Akazipiga bastola zao zilizokuwa sakafuni kwa miguu yake. “Nani kawatuma kwangu?” akamuuliza yule bwege pale chini.

“Si-si-si-ju-i,” akajibu huku akimwaga machozi na kugugumia kwa uchungu.

“Hutaki kunambia?”

“Kwe-li si-ju-i,” akajibu tena kwa namna ile ile. Kamanda Amata akamkanyaga kwenye goti lenye jeraha, akamnyoshea bastola usoni.

“Nakuua!” akamwambia.

“Hata ukiniua, sijui...”

“Mko wangapi?” akamuuliza na kukanyaga kwa nguvu.

“Aaaaaiiiiiiyyaaaa! Watatu, watatu, watatu...” akajibu.

“Mwingine yupo wapi?” akamtupia swali huku akimkanyaga zaidi.

“Kwenye gari, yupo kwenye gari...”

“Wapi?”

“Nje ya hoteli, nje tu...” akajibu huku akitetemeka kwa maumivu.

“Asante kwa majibu yako!” Amata akamwambia huku akiweka tayari bastola yake kwa kuachia risasi nyingine.

“Usiniue, tafadhali ...” yule jamaa akalalama.

Namba za gari... nitajie...”

“MP 203 D” akajibu.

Alipomaliza kujibu tu risasi nyingine ikatua kwenye goti la pili na

kulichakaza vibaya. Amata akawapekua haraka haraka, hakukuta cha maana. Akafungua mlango na kutoka, akaufunga kwa ufunguo kwa nje na kutoka kupitia mlango wa dharula.

Nje ya hoteli hiyo, Amata alitembea taratibu upande wa nyuma wa maegesho. Haikumchukua muda mrefu kuliona gari lile alilotajiwa namba. Kutokea upande wa nyuma akazunguka mpaka katika kiti cha abiria, pembeni mwa dereva. Akiwa na bastola mkononi, akafungua mlango na kuketi kitini.

“Tulia!” akamwambia huku tayari domo la *Glock 23* likiwa limegusa sikio.

“Si unaisikia harufu ya baruti?” akamuuliza, “Basi ujue ni muda mfupi uliopita nimewamaliza wenzio,” akamwambia. Yule jamaa, nyuma ya usukani, alishindwa ajibu nini, akabaki midomo ikimchezacheza.

“Nani amewatuma kwangu?” akamuuliza. Yule bwana akabaki kimya kabisa, “Nakuuliza...”

“Mi napigiwa simu tu, sijawahi kumuona bosi wangu,” akajibu.

“Ukinidanganya, hii bastola haitakudanganya,” Amata akamwambia.

“Kwe-kwe-li,” akajibu kwa kigugumizi cha woga. Mara simu, juu ya *dashboard* ya gari lile ikaita, Amata akaitazama. Kwa kitendo hicho akampa mwanya yule jamaa wa kufanya mambo. Kwa kono lake lenye nguvu, akaipiga bastola ya Amata, ikatoka mkononi na kuangukia kiti cha nyuma. Kono lake likaukamata vyema mkono wa Amata. Akaunyonga kwa nguvu lakini kabla hajatimiza azma yake akapokea pigo la kichwa, akaachia mkono. Kamanda akampa pigo jingine lililotua nyuma ya shingo, akajipiga kwenye usukani na honi kali zikasikika nje kwa sababu kichwa chake kilijipiga kwenye swichi. Yule jamaa akanyakua bastola yake kutoka kwenye pochi kiunoni mwake, Amata akauwahi mkono na kuukamata kiganja, akaugeuza kwa nguvu na kuifyatua risasi ambayo tayari ilikuwa kwenye chemba. Ikadidimia shingoni mwa yule jamaa, akatulia huku akimtazama Amata kwa huruma. Akafumba macho taratibu na kuegemea usukani, roho ikamwacha.

“Shabash!” Amata akanong’ona na kuanza kulipekua gari lile. Ndani ya *dashboard* akapata kijitabu kidogo cha kumbukumbu, akakitia mfukoni. Zaidi ya hicho kulikuwa na mabomu mawili ya kurusha kwa mkono *‘grenade’*, akachukua moja.

“Mlibeba mpaka mabomu kwa ajili ya mtu mmoja?” akasema kwa sauti ndogo. Akampekuwa marehemu na kuchukua simu yake. Alipomaliza,

akashuka na kuufunga mlango, akazunguka kwa dereva na kuufungua mlango wa upande huo. Akatazama mazingira ya humo.

“Ok!” akajisemea. Akachukua lile bomu na kuchomoa pini ya usalama, akalibana kiufundi kati ya mlango na kiti cha dereva kwa chini. Hivyo mlango ulilibana na kuendelea kulizuia lisilipuke. Ni mchezo wa hatari uliochukua dakika tatu hivi na kumwacha Amata akiwa kaloa jasho. Alipohakikisha mtego wake umekaa sawa, akaliacha eneo hilo na kusogea kando. Akaichukua ile simu na kuipekuapekua majina katika orodha ya wasiliani. Kabla hata hajafanikisha anachokitafuta, simu ile ikaita. *NASA* ikajiandika juu ya kioo, hakusita, akabonyeza kitufe cha kijani juu ya kioo hicho na kusikiliza.

“Hello!”

“We are dead!” Amata akajibu na kukata simu.

* * *

Jibu la simu ile likawashtua wale jamaa wanne pale katika meza ya mzunguko, walikuwa wakifuatilia kila kitu kinachoendelea katika jiji la Maputo.

“Huyu mshenzi lazima asakwe,” Felix akawaambia wengine.

“Ina maana aliyeongea ni yeye?” mwingine akauliza.

“Ndiyo, ana maana gani kusema *‘We are dead’*...” Felix akauliza. Mara moja, akainua tena ile simu na kubonyeza tarakimu kadhaa akaiweka sikioni.

“Squad 2, fika Montebello haraka, Squad 1 wanahitaji msaada...” akakata simu na kushusha pumzi kwa nguvu.

“Ni nani huyu?” Felix akauliza. Ukimya ukachukua nafasi yake kwa jozi la sekunde. Hakuna aliyekuwa na jibu sahihi la kumpatia bwana huyo. Akasimama, akaitazama saa yake na kuwaaga wenzake kuwa anataka kufika hapo Montebello na angerudi kwa dakika chache tu.

Nje ya hoteli ya Montebello, gari jeusi aina ya Toyota Land Cruiser likaegeshwa jirani kabisa na lile jingine ambalo lilikuwa likitumiwa na *Squad 1*. Vijana watano wakashuka, mmoja wao alikuwa akiongea kwa simu muda wote huku akilijongelea lile gari la *Squad 1*. Walipochungulia ndani wakashuhudia dereva akiwa kalalia usukani huku damu ya kutosha imetapakaa.

“Shiit! Wamemuua!” yule jamaa akaacha kuongea na simu na

kuzunguka upande wa dereva, kabla hajafungua mlango, gari jingine likaegeshwa upande huo. Felix alikuwa tayari amewasili eneo hilo.

“Victorino!” Felix akaita.

“*Yes Boss!*” akaitikia yule kijana.

“Vipi?”

“Ah! Jamaa ameuawa!”

“Ameuawa?” Felix akahamaki na kuwahi kwenye ule mlango wa dereva, akatazama ndani na kumwona dereva akiwa mautini. Akakamata kitasa na kuufungua mlango. Laiti angelijua kitakachotokea sekunde chache zijazo asingethubutu kuufungua mlango huo.

Sekunde mbili tu, mlipuko mkubwa ukatokea, lile gari likainuliwa na kutupwa kando. Moto ukadaka gari walilokuja nalo *Squad 2* na lile la Felix. Yote yakatetea kwa moto na kuwaacha vijana wale pamoja na Felix wakiungua vibaya. Tukio lile likavuta watu na magari ya zimamoto ambayo hayakuwa mbali yakasogea kutoa msaada.

* * *

Dakika chache baadaye, taarifa ya tukio hilo ikafika huko Cabo Delgado. Bonston hakuamini anachoambiwa, alihisi akili yake inataka kuhama, alizunguka zunguka hapa na pale. Akaingia ndani ya kasri lile na kuifuata lifti iliyomteremsha mpaka sakafu ya pili chini ya ardhi. Huko moja kwa moja akaingia katika ofisi ya Lord Dimens na kumkuta akiwa anaangalia matangazo ya dharula kupitia kituo cha televisheni cha taifa cha nchi hiyo *‘Televisao de Moçambique’*.

“Bonston!” Dimens akaita pindi alipomwona kijana huyo akiingia.

“*Yes sir!*” Bonston akaitikia huku akismama kwa heshima.

“Nani huyu anayeleta tabu hii?” akauliza.

“Lengo la kuja hapa ni kukwambia hilo, nimepata taarifa kuwa huyu mtu kaingia kutoka India, na jina lake ni Kelvin Sebuza...”

“Hilo si tatizo... kinachonisumbua ni kuwa, ndani ya masaa mawili keshafuta *Squad 1* na *2* na Felix... *no! you have to do something!*” Dimens akamwambia Bonston huku akionekana wazi kuwa uzee umemfika.

“*Ok, Sir!*” Bonston akajibu.

“Kesho tuna shughuli nyeti pale katika ukumbi wa mikutano wa Joachim Chissano, hivyo nataka umtumie ujumbe Jozé, afike Maputo leo, ahakikishe anamdhibiti huyu mtu kabla jua halijachomoza... *who is*

this bastard?” Dimens akatoa amri ambayo ilitakiwa kutekelezwa mara moja. Wakati Bonston anaondoka akamwita tena na kumpa ujumbe mwingine, “Mpigie *Chief* wa SISE, muulize kama ana habari yoyote kuhusu huyu mtu kisha nijulishe,” akamwambia.

Baada ya kufanya hayo yote, dakika kumi na tano baadaye Bonston akarudi mule ndani na kumkuta Dimens bado akitazama luninga.

“Enhe, najua utakuwa umekuja na habari za kufurahisha...” akamwambia Bonston.

“Yes! José ataingia Maputo muda si mrefu kutoka sasa, na *Chief* wa SISE anasema wao hawajui lolote kuhusu huyo mtu, hivyo nao wanamchukulia kama mhalifu tena gaidi na wapo kwenye msako mkali dhidi yake,” Bonston akafikisha taarifa.

“Sawa, naamini watamkamata, lakini tuwahi sisi kumpata kabla yao, asante Bonston! Na akipatikana, afikishwe *Hell 6*,” Dimens akamaliza.

SURA YA 21

SIKU ILIYOFUATA

PAMBAZUKO la siku hii lilimkuta Amata katika moja ya nyumba za kanisa kuu la Kikatoliki, Maputo. Kanisa la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, lililojengwa katikati kabisa ya jiji hilo, jirani na Mzunguko wa Independence. Akiwa katika lindi la usingizi, mlango wa chumba chake ukagongwa. Akainuka kivivuvivu na kwenda kuufungua.

“Umelala salama?” akaulizwa kwa sauti nzito ya kizee. Mzee huyu, Mtaliano, mwenye umri mkubwa aliyekuwa amevalia kanzu ya kitawa ya rangi ya udongo na mshipi mweupe kiunoni mwake alikuwa amesimama mlangoni mwa chumba hicho.

“Ndiyo baba!” Amata akajibu huku akitazama saa yake ya mkononi.

“*Vabene!* Basi dakika kumi kifungua kinywa kitakuwa tayari,” akamwambia Amata.

“Asante sana!” akaitikia na kuagana na mzee huyo huku akimtaazama akitembea kwa mwendo wa taratibu kwa msaada wa fimbo.

Amezeekea sasa! Akawaza, na kisha akaufunga mlango bila kufanya kelele yoyote.

Brother Antonio Ciampini, mtawa wa shirika la Wafransiskani alimpokea Kamanda Amata usiku wa siku iliyopita. Mzee huyu aliyeamua kujikatalia maisha ya anasa na kuingia katika utawa alihudumu katika shirika la kijasusi la Italia, SID, miaka mingi nyuma. Shirika hilo lilipogawanyika na kuzaliwa mengine mawili; yaani lile la SISDE lililo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi hiyo na SISMI lililo chini ya Wizara ya Ulinzi, yeye akaamua kuachana na kazi hiyo kwa kile alichodai kuwa ‘niliajiriwa na SID, na si vinginevyo’. Kamanda Amata

hakupata taabu kujieleza kwani wawili hawa wanafahamiana muda mrefu tangu huko Kilimanjaro ambako Amata amelitumikia taifa kwa miaka kadhaa huku mzee huyo akiwa mtawa kijana katika Seminari ndogo ya Maua ambapo kuna nyumba ya watu hao.

Nyumba hii ndogo ilijengwa pembezoni tu mwa Kanisa Kuu la Maputo. Alijua kuwa hapo ni sehemu pekee salama kwake kupumzika na kusubiri siku inayofuata, hakukosea.

Dakika kumi baadae, Amata akaungana na mzee huyo kwa stafutahi nzito. Wakiwa mezani waliongea mengi sana, maana ni muda mrefu hawajaonana.

“Amata Ric, mmmmmh, ni muda mrefu sana ... umekuja kufanya nini Maputo?” Antonio akauliza. Kwa kuwa Amata alimfahamu vizuri mzee huyo, wala hakuwa na la kumficha.

“Lord Dimens! Nimemfuata yeye...” akamwambia huku akiendelea kunywa kahawa yake taratibu.

“Lord Dimens, shetani wa ulimwenguni,” akamwambia.

“Kwa nini unasema hivyo...” Amata akauliza.

“Unajua! Ujinga wa kazi hizi hata ukiacha au kustaafu, akili yako haitastaafu, itaendelea kufanya kazi na kunusa hapa na pale. Nimemsikia sana huyo bwana, na ndiyo ilinipelekea kumfuatilia ili kujua vizuri ni mtu wa namna gani... Amata, CIA wanamsaka huyu jamaa kwa udi na uvumba. Na tayari wapo hapa Maputo kwa tukio la leo,” Antonio akamwambia Amata kwa sauti ya taratibu iliyosheheni uzee.

“Ni nani haswa?” akamtupia swali.

“Ina maana unamtafuta mtu usiyemjua?” Antonio akauliza.

“Yeah, simjui... zaidi ya kulijua jina lake tu”

“Nini kimekufanya umtafute?”

“*Brother!* Unajua tukio lililotokea Lindi mwaka jana?” Amata akamtupia swali.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Nilikuwa nangoja kuona idara za usalama Tanzania zitakuwa jinga kiasi gani kutolishughulikia hili... mlihujumiwa Amata. Na huyu jamaa leo anaipiga mnada ile chanjo akijigamba ni maabara yake imefanya ugunduzi huo. Uongo mtupu!” Antonio akasema. Amata akatikisa kichwa kwa maneno ya mzee huyo. Alimuelewa na yalimwingia.

“Ana maabara?” Amata akauliza.

“Ndiyo, ana maabara kubwa sana. Nimelijua hili kwa utafiti

niliyofanya, lakini mpaka sasa sijajua ni wapi ilipo,” akaeleza. “Bila shaka utaenda pale Joachim Chisano International Conference Centre kwenye ile hafla,” akaongeza kusema.

“Nimefika hapa lakini ukweli ni kwamba sijajua hasa naanzia wapi na nikamalizie wapi. Kama kuna hiyo hafla, nahitaji kwenda. Ninataka nilipate lile sanduku lenye sampuli ambalo ndani yake pia kuna *formula* nzima ya utengenezaji wa ile chanjo, kama haijaondolewa...” Amata akamwambia mzee huyo, “Nahitaji kuirudisha nyumbani, nahitaji kumfutulia mbali huyo Dimens,” akamaliza kwa kusema hayo.

“*Aspeta!*” akamwambia kwa Kiitaliano akimaanisha amsubiri. Akainuka na kwenda kwenye chumba fulani. Baada ya dakika tano akarudi na bahasha mkononi na kuketi.

“Chukua hii! Kadi ya mwaliko, itakayokuwezesha kufika mpaka ndani kabisa ya hafla hiyo. Ukishavaa suti yako, pachika hii sindano kwa upande wa ndani wa mfuko wa koti. Kazi ya hii sindano ni kuwasiliana na mashine yao ambayo itafungua mlango kwa wewe kuingia ndani. Aaaanh, jana sijakupokea na begi wala mkoba...”

“Sina suti ya kuvaa!” Amata akadakiza kusema.

“Usijali, nitakupatia. Ila ujue kwamba kuna ulinzi mkubwa na wa hali ya juu sana. Na kwa kitendo ulichowafanyia jana, umewachokoza. Amin nakwambia, unasakwa jiji zima. So, uwe makini na nyendo zako, epuka wanawake, hakikisha unakuwa *spy* kweli kweli. Nakuamini kijana wangu... nifuate!” akamwambia huku akisimama na Amata akamfuata.

Chumba cha tano kutoka sehemu ya kulia chakula, Amata aliingizwa ndani. Hakikuwa chumba kikubwa sana, ila kilikuwa na makabati matano yaliyosheheni suti za gharama na vifaa mbalimbali ambavyo angevihitaji kwa kazi yake.

“Chagua utakacho kijana, ila kuna hii zawadi yako,” akampatia mkanda wa kuvaa kiunoni, “Nataka utoke huko ukiwa *spy* na si vinginevyo,” akamwambia na kisha yeye akaondoka.

Dakika kama ishirini zilizofuata, Amata akarejea pale kwenye meza ya chakula akiwa kwenye suti nadhifu iliyomfanya aonekane kama tajiri fulani hivi. Mkononi mwake alipachika mwamvuli mweusi, miwani yenye kioo cheupe ilitulia vyema usoni pake. Kiatu chenye ncha kali kiliificha miguu yake.

“Naaam sasa umekuwa *spy*! Chukua na hii...” *Brother Antonio* akamsogezea kimkoba. Amata akakifungua na kubaki kinywa wazi.

Bastola mujarabu aina ya *Walther PPK* ilikuwa imelala kwa utulivu ndani ya mfuko wa plastiki kama mtototumboni mwa mama yake. Akaichukua na kuipakia risasi, akaibana vyema ndani ya koti lake. Na ile sindano akaipachika katika mfuko wa koti kama alivyotakiwa kufanya, akachukua ile kadi ya mwaliko na kuiweka katika mfuko wa shati lake.

“Hiyo sindano ina uwezo wa kuficha kila ulichonacho ndani ya mwili wako dhidi ya mitambo ya usalama. Hiyo miwani ina mawasiliano na ubamba huu hapa,” akamwambia na kumpatia ubamba mpya kabisa, kisha akaendelea kumwambia, “Na miwani hiyo hiyo unaweza kuitumia kutazama kila mmoja kabeba silaha gani mwilini mwake”.

“Waoh!” Amata hakuamini vifaa anavyokabidhiwa, vilikuwa vya hali ya juu sana.

“Na hii ndiyo funguo ya gari utakalotumia,” akamkabidhi. Amata akaipokea na kumshukuru mzee huyo.

“Uende na amani, kama tutaonana tena tumshukuru Mungu, kama lah basi si mapenzi yake... lakini najua utafanya *wonders*. Yaani utafanya ajabu la nane la dunia,” Antonio akamwambia huku akimwongoza mpaka kwenye maegesho. Hapo akakuta magari manne, moja kati ya hayo lilikuwa limefunikwa kwa kitambaa kizito. Akavuta na kufunua, likabaki wazi. *Kilimanjaro XXXL* likamlaki. Amata akatabasamu na kumtazama Antonio.

“Ndugu zako walishatangulia, wakaacha huu mzigo hapa, maadam umekuja, najua wewe ndiye wa kuutumia, haya, kazi kwako mwanaume,” akamwambia. Amata akamkumbatia mzee huyo, wakaagana, akaingia garini na kuweka *switch on*, kisha akatumia kiganja chake kuhakiki utambulisho wake, likamtambua na injini ikawaka.

“Naanzia nilipoishia...” akasema kwa sauti ndogo na kulitoa gari lile katika wigo wa kanisa na kuliingiza barabarani. Akaikamata Marginal Avenue na kukanyaga mafuta, gari lile lilikuwa likienda kasi ya kutosha. Dakika kumi tu zilimtosha kufika katika ukumbi huo wa mikutano. Askari wa usalama barabarani wakamwongoza wapi pa kuliweka. Akaliweka katika mtindo ambao isingemuwia vigumu kuondoka. Baada ya kuangalia nje na kujiridhisha na usalama uliopo, akafungua mlango na kuteremka. Katika uwanja huo kulikuwa na watu wengi, ukiwatazama tu utajua ni wenye pesa kwani magari ya kifahari yalimiminika. Maafisa balozi mbalimbali walikuwa wakiingia katika viwanja hivyo huku

vikundi vya burudani vikiendelea kuburudisha nje ya ukumbi.

Tangazo la watu kutakiwa ndani ya ukumbi likasikika, kamanda Amata akavuta hatua za kadiri kuelekea ulipo mlango wa kuingilia ndani. Kabla hajaufikia, akaona busati kubwa limetandikwa chini na katikati lina herufi H. moja kwa moja akajua kuwa hapo kutatua helikopta, akabadili mawazo. Akarudi kwenye gari lake na kufungua mlango, akafungua kijidroo, akatoa miwani nyingine kama ile ile akaivaa. Kisha ile aliyopewa na Antonio akaiweka juu ya *dashboard* ya gari hilo ikitazama upande ule ambapo helikopta ingetua. Kutoka palepale akachukua ule ubamba na kuufanya uweze kupata mawasiliano ya picha kupitia miwani hiyo. Alipohakikisha kila kitu tayari na tangazo la kuingia ndani likisisitizwa, akaufunga mlango na kuondoka zake.

Wakati wageni wakiingia ndani, huku nje kulibakiwa na wanajeshi na askari polisi wenye mbwa na wengine wakiwa juu ya farasi. Ulinzi uliimarishwa. Akaufikia mlango maalumu wa kungia ndani, ambapo lazima upite hapo ndiyo ufike ndani. Macho ya walinzi waliovalia suti nadhifu na vifaa vya mawasiliano, yaliyofichwa nyuma ya vioo vyeusi vya miwani yalikuwa yakimtazama yeye kwa husuda. Akaiweka miwani yake vizuri na kuwatazama mmoja mmoja. Kwa kutumia miwani hiyo yenye madini maalumu ambayo yanaweza kuona inavyoona *exray*, aliweza kujua kila mmoja ana silaha gani na ngapi mwilini mwake.

"*Sir!*" akasikia sauti ikimwita, akageuka na kukuta kijana mmoja akimwongoza kupita kwenye mashine hiyo ambayo lazima uvue mkanda, saa, na kila kitu cha chuma. Amata akapita bila kuvua chochote na hakuna kilicholeta shida. Wale jamaa wakazidi kumkazia macho. Hali hiyo ikavuta hisia za vijana wale. Akavuta hatua na kufika mlango wa pili, hapa akakutana na mwanadada mrembo anayegawa kikasha kwa kila anayeingia ndani. Akachukua na alipoufikia mlango wa mwisho, ukafunguka wenyewe na kumruhusu kuingia ndani. Akafanya hivyo kisha ukajifunga nyuma yake.

Ndani ya ukumbi huo kulikuwa na watu wengi wenye mchanganyiko wa mataifa na makabila. Kamanda Amata aliweza kuona wawakilishi wa mashirika makubwa na makampuni ya madawa. Watu wa Shirika la Afya duniani nao walikuwa na meza yao na wengine wengi.

"*Your complimentary card sir!*" sauti ya kike ikamshtua ikimtaka kuonesha kadi yake, akaitoa na kumpatia. Yule mwanadada akaitazama na kisha akamtazama Amata.

“*This way please...*” akamwambia kumuonesha njia. Amata akamfuata mpaka kwenye meza moja iliyofuatana na nyingine ambazo tayari zilikuwa na watu. Akawasalimu kwa ishara na kuketi huku akiweka kila kitu juu ya meza na kuisogeza kando *microphone* iliyokuwa hapo.

* * *

Katika chumba cha usalama, ndani ya jengo hilo, kulikuwa na vijana sita makini kwenye luninga, wakitazama kila anayeingia. Wakajikuta wote wakivutiwa na Kamanda Amata.

“Huyu ni nani?” mmoja akauliza. Kijana mwingine akaingia kwenye kompyuta yake na kupekua majina ya waalikwa, akasoma namba maalumu ambayo inaonekana tu endapo kamera za siri zitaimulika kadi hiyo. Na sehemu ambapo yule msichana alikuwa akikagua kadi zile kulikuwa na kamera hiyo. Hivyo kila akitazama kadi, ile kamera iliinasa ile namba ya siri na kuipeleka moja kwa moja katika chumba hicho. Huko wao wangejua mara moja mgeni huyo ni nani, na ametoka wapi. Na mwanadada huyo miwani aliyovaa ilimwezesha kusoma namba hiyo kwa urahisi.

“*Snake and Lion Medical Company USA!*” yule jamaa akawaambia wenzake.

“Jina lake!” yule wa kwanza akaomba na jina kabisa.

“Anamwakilisha Mkurugenzi ambaye ni Mr. Johnson Vibek,” akajibu.

“Ninauliza kwa sababu, huyu jamaa kuna mambo sijaelewa...”

“Yepi?”

“Amepita kwenye mashine za usalama na hajavua mkanda wala saa wala chochote, na hakuna *detection* yoyote, hamuoni kuwa ni tatizo?” baada ya hayo kila mmoja akaongeza umakini kumtazama Amata.

“Seth!” yule bwana aliyeonekana kuwa ndiye kiongozi wa kitengo hicho akamwita kijana mwingine aliyekuwa katika kompyuta namba sita.

“*Yes!*” Seth akaitika.

“Hakikisha umakini wako wote unaweka kwa mtu huyo, akiinuka tu toa taarifa afuatiliwe, huyu si mtu wa kawaida...”

“*Ok!*”

Ndani ya ukumbi ule matangazo yalikwisha, na ratiba ikaanza rasmi ikiwa ni kueleza juu ya Dimens Lab -Tech, ilipotoka, mafanikio na mambo mengine.

* * *

Mara ubamba wa Amata ukatikisika na kumshtua, akatazama kwenye kioo na kuona kuwa tayari unapokea mawasiliano kutoka nje. Katika kioo cha ubamba huo, aliweza kuona video yenye kiwango cha *HD* ikionesha kuwasili kwa helikopta moja kubwa na ya kisasa. Mara baada ya kuzima pangaboi lake mlango ukafunguliwa. Wakashuka vijana wawili waliovalia nadhifu sana, suti za gharama na vifaa vya mawasiliano masikioni mwao. Wakafuatiwa na kijana mwingine wa Kizungu mwenye miraba minne, mrefu kiasi, nywele nyeupe, ukimwangelia tu usoni utajua kuwa hakuwa wa kawaida, mpiganaji mwenye ujuzi. Nyuma yake akafuata mtu mwingine wa makamo, Mwafrika, aliyekuwa kavalia suti nyeusi, sambamba na wale wengine, ilikuwa na chapa ‘Dimens Lab – Tech’. Kifuani mwake kulining’inizwa beji maalumu yenye utambulisho wa jina lake kamili. Kamanda Amata akaikuza haraka na kuweza kupata jina lake, Prof. Hammon Masekela, *Lab Technologist*. Nyuma yake likashushwa sanduku jeusi ambalo lilibebwa na mtu mmoja. Nyuma ya huyo akashuka Mzungu mwingine wa makamo, mtu mzima, akasalimiana na watu kadhaa lakini si kwa kupeana mikono. Kisha wakachukuliwa na kupitishwa mlango mwingine kuingia nyuma ya ukumbi huo wa kisasa.

Kamanda Amata akashusha pumzi. Mapigo ya moyo yakaanza kwenda hobela hobela. Alilitambua haraka sana lile sanduku. Kama kuna kosa walilofanya Dimens Lab – Tech, lilikuwa ni hilo; walibadili na kufanyia marekebisho mambo mengi kwenye chanjo hiyo, pamoja na kumbadili mwonekano Dkt. Edward na kumpa jina Hammon Masekela lakini walisahau kubadili sanduku la kubebea chanjo zile pamoja na kompyuta yenye kanuni ambayo hukaa ndani yake.

Ni bili bili nililiona Londo! Akawaza na kujikuta akili yake ikitoka nje ya hafla hiyo. Hapo akaanza kuvuta picha ya jinsi tukio lile lilivyofanyika kule Lindi, akajikuta anashikwa na hasira.

Tuliibina! Akawaza.

* * *

Ndani ya chumba maalumu – ukumbini

Dkt. Edward alifikishwa katika chumba cha siri, pamoja naye alikuwapo Bonston, na kijana mwingine.

“Sikiliza dokta... mara baada ya kuzungumza Lord Dimens, itakuwa

zamu yako. Unatakiwa kuelezea kadiri ya unavyojua wewe na utaalamu wako. Tutaunganisha hiyo kompyuta na kila kitu kitaonekana kwenye luninga...” Bonston akamwambia. Daktari Edward hakuwa na cha kujibu zaidi ya kutikisa kichwa juu chini. Moyoni mwake alijikuta akishikwa na donge kwa kuona nchi yake inaibiwa kitu muhimu sana huku yeye akisimama kama msaliti ingawa si kwa matakwa yake.

“Unaona hiki?” Bonston akamwonesha Dkt. Edward kitu kama sabuni kilichofungwa kwenye nailoni huku baadhi ya nyaya zikitokea upande huu na kuingia upande mwingine.

“Hili ni bomu. Tunakuvalisha, ukipindisha maneno pale mimbarini mimi kazi yangu ni kubonyeza tu, na litakuua wewe peke yako...” Bonston akamwambia na kisha akamfunga bomu lile sehemu ya chembe ya kifua na kumvika koti lake.

“Kila kitu tayari, *all the best Doc!*” Bonston akamwambia.

Kule ukumbini, wageni walikuwa wakisikiliza hotuba ya Lord Dimens iliyojawa maneno matamu ya kumtoa nyoka pangoni. Makofi yasiyokwisha yalikuwa yakisikika. Kamanda Amata alikuwa katulia tuli akisikiliza kila lisemwalo, majigambo, mapendekezo, kejeli, dharau, vyote vilitoka kinywani mwa Mzungu huyo mzee.

“Dimens Lab – Tech, ndiyo maabara isiyo na kifano ulimwenguni, inayohakikisha thamani ya uhai inabaki kuwa Somoe kwa mwanadamu. Tunalaani tukio lililotokea Tanzania mwaka uliopita, na kwa sababu hiyo likatusukuma kurudisha heshima hii kwa Mwafrika. Tumegundua chanjo iliyo bora kabisa dhidi ya *virus* wa *AIDIOSIS*. Dimens Lab – Tech tunasema ‘sasa basi, *no more AIDIOSIS, no more crying, no more death*’”. Sauti ya Dimens ilipasua anga. Baada ya kuzungumza kwa dakika kumi na tano, hatimaye akamaliza hotuba yake. Akaiacha mimbari na kuingia kwenye mlango mmoja kati ya mingi nyuma ya jukwaa hilo huku akisindikizwa na makofi yasiyo na mwisho. Mwendesha sherehe akatoa taarifa kuwa wageni wakae tayari kuona nini kimepatikana huko maabara.

Dokta Edward Minzi au Hammon Masekela wa bandia, akasimama na kuelezea chanjo hiyo kwa undani huku akitumia maneno magumu ya kikemia. Nyuma yake skrini kubwa ikateremka na kuanza kuonesha jinsi chanjo ile inavyofanya kazi katika mwili wa mwanadamu. Zilikuwa ni dakika kumi na tano nyingine zenye mguso mkuu. Ukumbi ulikuwa kimya kabisa ukifuatilia dokumentari hiyo. Kamanda Amata alimtazama kwa makini daktari yule aliyekuwa akielezea na kuanza kumtilia shaka.

Nafikiri huyu ni maiti mojawapo kati ya zilizokosekana kule Londo! Akawaza. Wakati kila mtu ametulia akifuatilia makalapicha ile, yeye akili yake yote ilikuwa kwa Dkt. Hammon Masekela. Kwa siri akawa anarekodi mazungumzo yake huku akijaribu uwezekano wa kupata picha yake.

Ndani ya chumba cha usalama, kijana Seth alikuwa akimtaazama Amata kwa makini sana kwa kutumia kamera aliyokuwa akiiongoza. Akifananiwa na washiriki wengine, aligundua kuwa Amata hana umakini wowote katika makalapicha ile isipokuwa kuna yake anayoyafikiri. Akamtazama kiongozi wao na kumpa ishara kuwa asogee karibu na pale alipo. Alipofika, akamnong'oneza kitu. Yule bwana akatoka pale na kuchukua simu yake ya upepo, akazungumza maneno machache kwa lugha ya Kireno kisha akaitua mezani.

“Asante Seth!” akamshukuru.

* * *

Mara tu baada ya makala picha ile kumalizika, vijana wawili wenye miili mipana wakaingia ukumbini huku wakionekana kuwasiliana na mtu fulani. Moja kwa moja walielekea pale alipoketi Amata. Hayupo! Yaani hawakumkuta.

Wakapepesa macho huku na kule, na kushuhudia mlango wa kuingia vyooni ukimalizikia kufungwa. Mmoja wao akauelekea huku akifuatwa na mwingine, wakaufungua na kuingia ndani. Huko walikuta korido ndefu yenye milango kadhaa, lakini hawakumwona wanayemtafuta.

“Ametupotea!” yule jamaa akatoa taarifa chumba cha usalama, nako wakaanza kutafuta kamera ipi inamwona kwa wakati ule. Sekunde kumi, wakapewa taarifa ni mlango gani kaingia, nao wakafuata.

“Chumba cha mawasiliano,” wakaambiwa na wote wakasikia kwa wakati mmoja. Haraka wakaongeza mwendo na kuingia ndani ya chumba hicho. Kamanda Amata tayari alikwishazima mitambo yote ya mawasiliano, na kufanya jengo zima kuwa kimya. Simu, *microphone* na kila kifaa cha kielektroniki vilikuwa havifanyi kazi na kusababisha mtafaruku kidogo. Kilichofuata hapo ilikuwa ni kuzima swichi kubwa ya umeme ya jengo hilo iliyopo katika chumba kinachofuata. Tayari vijana waliokuwa wakifanya kazi katika chumba hicho walikuwa chini wakiwa hawana fahamu. Kamanda Amata akahisi mlango unafunguliwa. Akajua kumekucha. Alipogeuka tu akakutana na jamaa akimfuata mzima mzima. Akarusha konde likatua sawia puani pake, jamaa akaguna kwa maumivu huku damu zaikimmwagika. Amata akainua kiti cha chuma

na kumrushia yule wa pili ambaye alikuwa amekwishashika bastola, ikamtoka mkononi.

Huyu wa kwanza akainuka, kabla hajasimama sawa akapokea ngwala moja maridadi na kurudi chini mzima mzima. Yule wa pili akiwa bado anaugulia maumivu ya mkono, akamvaa Amata, wakayumba naye mpaka kwenye meza iliyosheheni kompyuta na vifaa vingine. Akambana uso kwa kono lake na kumweka kwenye wakati mgumu. Kwa akili ya haraka, akaikamata tai ya mjinga huyo na kuivuta, ikamkaba, akamwachia huku macho yakimtoka. Akatumia nguvu zake zote na kumsukuma kwa yule mwingine ambaye alikuwa akija eneo hilo, wakavaana na kuanguka chini. Amata akachomoa bastola yake ya PPK, akaondoa usalama na kufyatua risasi nne, kila mmoja akapata zake mbili na kutulia.

Haraka, akafungua mlango wa chumba cha pili, na kuingia. Huko ndani akakutana na swichi nyingi za kusambaza umeme jengo zima. Akatuliza akili kidogo, akaiendea kubwa kuliko zote yenye kupokea umeme wa jenereta na ule wa kawaida unaotoka *Electricidade de Moçambique*. Akaipeleka kwenye OFF, na umeme jengo zima ukazimika. Akafungua ndani na kuchomoa fyuzi zote, kisha akatoka haraka kwenye kile chumba, huku akivunja kitasa cha mlango kwa nje ili kuwafanya wachukue muda kuingia ndani.

* * *

Katika chumba cha usalama kila kitu kilizimika, kazi ikawa ngumu kujua adui yuko wapi. Walijaribu huku na huko hawakufanikiwa. Kilichobaki hai ni *radio call* na simu za mkononi pekee. Hali ikawa tete. Wajumbe katika ukumbi wa mkutano wakajikuta wanashindwa kujua wafanye nini, kama wabaki ukumbini au watoke nje. Tayari kikosi cha jeshi nje ya ukumbi huo kilizingira kuhakikisha mtu huyo hatoki huku askari wenye mbwa wakiingia ndani kuendesha msako.

Daktari Minzi (*Hammon Masekela*) akaondolewa haraka mara tu taa zilipozimika. Bonston na vijana wake wakamchukua haraka na lile sanduku na kuingia naye kwenye chumba maalumu ambacho kwacho Lord Dimens alikuwa ameketi akifuatilia tukio zima kupitia luninga kubwa ya kisasa.

“Mwambie Jozé, ahakikishe huyo mpumbavu kapatikana...” Dimens akamwagiza Bonston. Kijana huyo aliyeaminiwa sana na Dimens, akampa taarifa Jozé kwa simu naye akajibiwa kuwa tayari msako unaendelea.

Simu nyingine aliyoipiga ilikuwa ni kwa rubani wa helikopta, kuwa akae tayari kwa safari. Bonston, na timu nzima aliyokuja nayo wakajiandaa kutoka katika ukumbi huo, maana tayari hali ilikuwa si shwari.

Kamanda Amata mara baada ya kuhakikisha kuwa kila kitu hakifanyi kazi, alitokea mlango mwingine na kukimbia kupitia korido ile. Alipoziona ngazi za kuelekea chini, hakusita, aliteremka huku bastola ikiwa mkononi mwake.

“Hey!” akasikia sauti ya kike ikimwita, akageuka na hakuamini macho yake. Gina, alikuwa amesimama katika mlango wa chumba kidogo, akili yake ikacheza mara kadhaa na kujiuliza kama ni kweli anayemwona ni Gina au mtu kachukua sura ili amtie mkononi kirahisi.

“Hakuna muda wa kupoteza! Kamanda...” Gina akasema. Mara wakasikia watu wakija upande huo wakikimbia na sauti za mbwa kubweka. Amata hakujiuliza tena, akakimbilia katika kile chumba na kuingia, wakajifungia mlango. Gina akamdaka Amata, akamkumbatia na kumpiga mabusu kadhaa, wakanyonyana ndimi kwa sekunde tatu kama si nne.

“Twende juu,” Gina akamwambia. Amata akatazama na kukuta kuna vyuma vimechomekwa ambavyo vinaweza kumfikisha mtu juu kabisa ya jengo hilo.

“Juu kufanya nini? Wapenzi daima huenda chini,” Amata akajibu huku akimwangukia Gina usoni.

“Twende bwana, acha ujinga...” Gina akampigia kelele Amata kisha wakaanza kupanda kufuata vile vyuma. Wakaingia kwenye kitu kama dohani, baada ya umbali wa mita kama kumi hivi kwenda juu, ile njia ikaonekana kukunja na kumwezesha mtu kutambaa kwa magoti, wakafanya hivyo.

Huko nje, tayari Dimens, Bonston na timu yake walikwishaingia kwenye helikopta na injini ilikwishakuwaka. Lord Dimens alikuwa na hasira isiyo kifani, alitamani ashuke na kumsaka yeye mwenyewe huyo mtu aliyeharibu hafla yake lakini hakuweza. Ile helikopta ikanyanyuka taratibu na kuiacha ardhi ya eneo hilo.

Kutoka kwenye lile dohani walisikia kelele za mbwa na wakati huo huo mvumo wa helikopta ukafuatia.

“Aaaaaa *come on!*” Amata akapiga kite baada ya kujua kwa vyovyote amtakaye amekwishaondoka. Akaendelea na safari na kujikuta nje kwenye bustani kubwa ya maua, wakiwa wameliacha jengo kama mita mia hivi. Gina akabonya saa yake na dakika hiyo hiyo, Amata

akashuhudia gari lake likifika pale huku nyuma likifukuzwa na askari mwenye farasi. Kabla hawajaingia, Amata akafyatua risasi na kumtungua askari aliyekuwa juu ya farasi. Milango ikafunguka Gina akajitoma ndani na Amata akafuatia. Milango ikajifunga na gari lile likandoka kwa kasi huku nyuma likirushiwa risasi ambazo zote zilitua juu ya bati la gari hilo bila kuleta madhara.

Nyuma ya usukani, Scoba alikuwa ametulia tuli. Mara baada ya kuhakikisha watu wake wameingia, akatia gia na kuliendesha kwa kasi mpaka getini na kukuta tayari limeshafungwa. Hakuwa na muda wa kujiuliza, huku nyuma akiwa anafuatwa na askari wa farasi, akagonga walinzi watatu waliokuwa wakitaka kulizuia. Akavunja geti na kutoka nje kwa kasi ya ajabu huku askari zaidi wakiinga barabarani na kurusha risasi.

“Tumemwoko Kamanda kama tulivyoagizwa...” Scoba akasema huku akibadili gia na kuingiza nyingine. Gari nalo likaongeza kasi kama lilivyoamriwa. Barabara ya Nyerere ilikuwa na foleni kiasi, hii ikamlazimu Scoba kuingia barabara nyingine ili aweze kufanikisha azma yake. Akaiacha barabara hiyo kubwa na kukunja kulia ili atokezee barabara nyingine ya Marginal. Akakanyaga mafuta na kuifikia barabara hiyo. Alipoipita tu hoteli ndogo ya Kaya Kwanga akakutana na kizuizi mbele. Wanajeshi wawili, mmoja akiwa na silaha kubwa ya kivita RPG begani mwake. Alipogeuka nyuma akaona kuna kuna Land Rover la kijani na juu kuna watu watatu waliovalia sare ya jeshi.

Akapewa ishara ya kusimama. Scoba hakutaka kutii, badala yake akaongeza mwendo. Risasi zikaanza kumiminwa kwenye gari lile lakini hakuna hata iliyoweza kupenya. Yule mwenye RPG akaiweka tayari na kufinya jicho moja. Kisha dole lake la shahada likavuta kifyatulio nyuma na kuruhusu kombola lile kutema mzigo.

“*Attention!*” Scoba akawaambia wenzake, kisha akabonya nobu fulani iliyoandikwa *eject*. Lile gari likafunuka juu na viti vitatu vikatolewa nje kwa kurushwa hewani. Ni sekunde ileile gari lile likapigwa kwa RPG na kutupwa upande wa pili. Katika kuruka kule kiti cha Amata kikanasa kwenye miti kando kando ya barabara hiyo. Haraka wale jamaa kwenye Land Rover wakashuka na kumkuta Amata akiwa anamalizia kujinasua kwenye kiti kile. Alipotua chini akajikuta mikononi mwa askari wenye hasira, wakamuwahi na kumpa kipigo kikali mpaka akapoteza fahamu.

Jozé akawasili na vijana wake wengine wakiwa na gari aina ya Range Rover. Akawaamuru vijana wake kuteremka na kumchukua Amata,

wakafanya hivyo huku wakionesha vitambulisho bandia vya idara ya SISE. Wakamchukua Amata wakisaidiana na wale vijana wa jeshi na kumpakia kwenye Range Rover hilo. José, akaingiza gari barabarani na kuikamata barabara ya Marginal kama anarudi ueleke wa Montebelo lakini si huko. Mara baada ya kuupita mgahawa wa Dhow Maputo, akaufikia mzunguko ndogo ambao unakutanisha barabara ya Marginal na ile ya Setembro. Akazunguka na kuiacha hiyo ya Setembro, akachukua barabara ndogo ya Novembre ambayo ilimpeleka mpaka bandari ndogo ya Cetembe.

Katika bandari hiyo, kulikuwa na mashua ndogo ya kisasa imeegeshwa, akapakiwa humo na safari ikaanza. Baada ya kupigwa na upepo mkali wa baharini Kamanda Amata akarudiwa na fahamu. Alipofumbua macho akajikuta akitazamana na bunduki ya kivita ya AK 47. Mikono yake ilikuwa imefungwa kwa kamba imara na miguu yake pia. Akatulia. Wakiwa katikati ya bahari, chopa inayofanana kabisa na ya jeshi ikawakuta, ikateremshwa jirani kabisa na mashua ile, Amata akapakiwa, kisha José na vijana wake wawili nao wakaingia na kuondoka huku wakiiacha ile mashua na nahodha wake wakiendelea na safari.

“Umetusumbua sana mshenzi wewe!” José akamwambia Amata kwa Kiingereza. Amata hakujibu badala yake alimtazama tu na kutabasamu. Dakika arobaini na tano zikapita wakiwa hewani, Amata alikuwa amelazwa chali kati ya viti vilivyokuwa vikitazamana na miguu ya watu hao ikiwa kifuani mingine tumboni ilimradi tu kwao wamestarehe. Baada ya muda, Amata akasikia mabadiliko ya muungurumo wa chopa hiyo, akajua kwa vyovyote watakuwa wamefika na sasa wanatua. Hakukosea, chopa ile ilikanyaga ardhi mbele ya kasri la Lord Dimens huko Cabo Delgado. Akashushwa kama kiroba na kuanza kuburuzwa kuelekea ndani ya jengo hilo. Bonston alijitokeza nje ya kasri hilo na kumshuhudia yule aliyekuwa akiwafanya wasilale akiwa mikononi mwao.

“Mpelekeni *Hell*6, na mumfunge barabara kama wale punda wenzake,” Bonston akatoa maagizo na kisha yeye akarudi ndani katika kasri lile. Huko alikwenda kumpa taarifa Lord Dimens kuwa huyo mjinga anayesumbua vichwa vya watu, amepatikana. Naye hakujibu kwa sauti bali kwa kutikisa kichwa huku chupa kubwa ya pombe kali ikiteketea. Kamanda Amata akaingizwa ndani ya jengo hilo, akateremshwa kwa lifti mpaka sakafu ya chini. Akatolewa kwenye lifti na kutembeza harakaharaka huku mikono yake ikiwa imefungwa mpaka kwenye

chumba kimoja chenye mlango wa chuma. ‘*Hell 6*’, kiliandikwa namna hiyo kwenye mlango huo.

“Haya ndiyo makao yako unaposubiri kifo,” wakamwambia. Mlango ukafunguliwa kwa kadi maalumu. Kwa mwanga hafifu aliweza kuona kuwa kuna mtu mwingine humo ndani ila hakuweza kumtambua. Amata akafungwa kwa mnyororo na kuachwa humo. Chumba kilikuwa na giza la kutisha lenye ukimya usiopimika.

* * *

Gina na Scoba mara walipotoka kwenye lile gari, walijikuta wakiangukia nyuma ya hoteli ndogo ya Kaya Kwanga. Haraka haraka, wakatoka eneo hilo. Lakini pindi walipokuja barabarani kumsaidia mwenzi wao wakakuta tayari akiondoshwa na lile gari alilokuja nalo Jozé na kundi lake.

“Tumefeli!” Gina akasema huku machozi yakimlenga.

“Hatuna ujanja, turudi hotelini kisha tutajua nini cha kufanya,” Scoba akamwambia Gina. Wakatoka hapo na kuingia katika taksi moja iliyokuwa nje ya hoteli ya Kaya Kwanga. Hakuna aliyewagundua kama wawili hao walikuwa katika tukio hilo. Gina na Scoba walikuwa wamefikia katika lodge ya kawaida tu huko kwenye kitongoji cha Malghalene B. Walifanya hivyo makusudi ili kuepukana na usumbufu wa askari walioweka ulinzi hasa katika mahoteli makubwa.

SURA YA 22

CABO DELGADO

BAADA YA SIKU TATU, Lord Dimens aliwatuma vijana wake wasio na chembe ya huruma kwenda kuwatoa mateka wao kwa kuwa siku ya hukumu kama alivyoiita bwana wao huyo ilikuwa tayari.

Taa zikawashwa, Kamanda Amata, kwa shida akainua uso kutazama. Lango likafunguka, watu watatu wakaingia, wanaume walioshiba wakasimama huku wameweka mikono yao mbele na kuishikamanisha vifuani mwao.

“Muda wenu umefika!” mmoja akasema kisha akasogea karibu na Johnson na mwingine karibu na Amata.

“Aha! Ha! Hah! Hah! Watu wenyewe wote wachumba tu!” mwingine akadakia.

“Subirini mzee anakuja atawaonesha kazi, hamwezi kuitetemesha ngome ya Lord Dimens,” mmoja wao akaongea kwa dharau.

Amata akageuka kwa tabu na kutazama mbali kama mita kumi na tano hivi na kumwona Johnson akining’inia kama yeye, akatikisa kichwa na kurudisha uso wake chini. Haikupita dakika tano, wakaingia watu wengine kama wanne hivi. Dimens akaanza kupiga makofi ya dhuhaka na wengine wakafuatia, sekunde chache baadae akawapa ishara ya kutulia.

“Karibuni katika himaya ya Lord Dimens, kila anayejifanya mjanja hapa huwa ni mwisho wa kila kitu. Watazameni hawa, wote hawa ndiyo wajanja, si ninyi, ninyi ni mafala tu. Mmoja atakuwa chakula cha mbwa na mwingine cha nguruwe. Nani kawahi kuwaambieni kuwa Dimens hutetemeshwa na *FBI*, *CLA* au nani sijui, na nyie Tanzania

ni kambwa gani kale, *TISS*. Nani kawaambia ninyi? Mnajidanganya, nipo hapa miaka zaidi ya ishirini nafanya biashara zangu na hakuna wa kunizuia. Mimi ndiyo Dimens kama hamjui ni *Demons*. Chanjo yenu na *formula* yake niliichukua mimi, semeni kingine na ninatarajia kupata faida kubwa kwani nimeshainadi kwa matajiri. Wewe...” akamwendea Amata na kumnasa kofi, “Ulifikiri ungeweza kufanya nini majuzi kwa akili yako? Mbona umekamatika? Wewe na nchi yako wapumbavu tu,” akamwambia.

“Ninakwambia wewe kwa sababu huwezi kutoka humu ndani, na mtaalamu wenu ninae, Dkt. Edward atakuja kuwasalimu *soon*,” akatulia na kutembeatembea hapa na pale. Wale wengine wakiwa kimya kabisa. Akasimama katikati akamtazama Amata, “Wewe! Wewe! Wewe! Umeniulia watu wangu wengi sana. Nakwambia, kama ulikuwa unamtafuta nyoka miguu! Sasa umeipata”. Akawatazama vijana wake kwa zamu.

“Mpeni disprin! Kisha utawafungua uwaleta kule aliko yule mwanamke, nataka watolewe viungo muhimu kwa kazi zetu kisha miili yao ikatwekatwe kwa chakula cha wanyama wangu,” Dimens akaagiza.

Wakati Dimens na timu yake wakiondoka, huku nyuma kipigo kikali kikaanza. Amata akatandikwa kwa nguvu zote, makonde mazito ya tumboni na sehemu nyingine hatarishi za mwili. Akapigwa kwa vipande vya mbao ngumu na mbichi, mikanda na kila kilichokuwa karibu. Dakika kumi zilimuacha hoi bin taaban katika minyororo ile. Mifereji ya damu ilikuwa zikichuruzika hapa na pale katika mwili wake. Simu ya Bonston ikaita, akasogea kando na kuisikiliza, dakika moja kama si mbili akarudi.

“Wafungue! Madaktari wapo tayari wanasubiri,” akawaambia. Amata na Johnson wakafunguliwa wakiwa hoi. Amata akiwa na maumivu ya kipigo na Johnson akiwa hoi kwa uchovu. Wakaburuzwa mpaka kwenye lifti na kupandishwa mpaka katika chumba maalumu chenye mitambo ya kutosha. Haya yote yalifanyika katika sehemu ya chini ya jumba hilo ambayo ilikuwa ardhini.

Ndani ya chumba hiki, kulikuwa na vitanda vitatu na mitambo ambayo daima huonekana kwenye chumba cha upasuaji hospitalini. Madaktari kadhaa walikuwa tayari kwenye mavazi yao wakisubiri kila kitu kiwe sawa ili waanze kazi. Kitanda kimoja cha katikati tayari kulikuwa na mwanamke aliyefungwa hapo akiwa hata hajielewi, mwili wake ulikuwa dhoofu sana, mwanamke wa Kizungu.

Johnson alimtazama mwanamke huyu akamtambua.

“Tetty!” akajaribu kuita lakini sauti yake ilikuwa ya kinyonge sana. Yeye akapelekwa kitanda kingine na hiki huku akaletwa Amata tayari kwa kufungwa hapo.

Kufa kipumbavu si hulka yangu, bata kama nitakufa, na najua nitakufa, lakini sivezi kufa namna hii! Amata akawaza. Punde si punde, mbele yake akaletwa mtu mwingine akilindwa kwa mitutu ya bunduki. Mtu huyu, alikuwa mtu wa makamo, aliyeonekana wazi kuwa na sura ya kukata tamaa. Sura iliyoficha uchungu na hasira. Wakakutana na kutazamana. Yule mtu aliyekuwa kwenye vazi la kidaktari, alifichwa uso kwa barakoa. Akaishusha na kubaki uso wazi, akamtazama Amata.

“Naitwa Dokta Edward Minzi! Hawa jamaa wameiba chanjo yetu kule L...” akajitambulisha, na alipoongeza sentensi hiyo, akawauzi wale vijana. Wakaanza kumsulubu kwa kumpiga kwa vitako vya bunduki.

“STOP!” Bonston akawazuia, na wale vijana wakamwacha daktari yule akiwa hoi sakafuni huku akigugumia maumivu.

* * *

Katika chumba kingine, Dimens na wageni wake wachache walikuwa wameketi wakiangalia zoezi lile kupitia luninga kubwa iliyofungwa ukutani. Akainuka na kuwatazama wageni wake wachache kati ya wengi waliokuja kwenye hafla ile iliyovurugika.

“Msiwe na wasiwasi, haya ni maambatano tu, jaribio lenyewe litatukia muda si mrefu, ninachotaka muone ni jinsi gani mwanadamu anayahisi maumivu. Vijana wangu watawatoa hawa watu viungo kama moyo, figo, maini na vingine bila kutumia dawa ya usingizi. Katika mitambo yetu hapa tutaona ni wakati gani mwanadamu anapata maumivu makali sana, na tutaweza kujua nini siri ya kifo katika hatua kama hii. Kwamba, mtu hufa kwa maumivu au kwa kupoteza damu au kwa kitu gani hasa... karibuni kwenye *show*,” aliposema hayo akaketi na kukunja miguu yake mtindo wa nne, na mwanadada mrembo akasambaza vinywaji kwa wageni hao.

Wote hawakuwa na presha kwani walifurahia onesho hilo, hivyo walitulia kusubiri kuona.

* * *

Tetty na Johnson walikwishafungwa juu ya vitanda vile kwa mikanda imara. Zamu ya Amata ilipowadia, kijana mmoja aliyekuwa amemshika, akamsukumia kitandani huku yule aliyekuwa anawalinda akampiga kwa kitako cha bunduki mgongoni. Amata akahisi maumivu makali ya uti wa mgongo. Kwa hasira, akageuka ghafla na kumpiga kichwa kizito yule aliyemsukuma. Yule bwege akasukumwa nyuma kwa nguvu ya pigo lile. Nukta hiyohiyo Amata akamshindilia konde yule mwenye bunduki, kisha kwa nguvu zote, akaivuta ile SMG na kuigeuza, akamtandika nayo kichwani jamaa akaenda chini.

“*Ambushhhhh!*” sauti ya askari mwingine ikasikika, Bonston akaona hapa si penyewe, na kwa sababu jukumu lake lilikuwa kuhakikisha uzima wa Lord Dimens na himaya yake, akatoka haraka kwenda kumhifadhi mzee huyo jeuri.

Amata akajikuta na nguvu za ziada, akajua tayari ameharibu hali ya hewa. Akajitupa chini na kujiviringa huku akiachia risasi za kutosha kutoka kwenye SMG ile na kuhesabu watu takribani sita wakienda chini akiwamo yule aliyepiga kelele. Alipoinuka alikuwa na bunduki nyingine mkononi. akachomoa kisu kutoka kwa moja ya maiti ya wale walinzi na kukata mikanda imara kabisa iliyomfunga Johnson na ile ya Tetty, wakawa huru.

“Okoa maisha yako kaka!” Amata akamwambia Johnson na kumpa ile bunduki.

* * *

King’ora cha hatari kikalia jengo zima, hali ikabadilika. Lord Dimens akabaki katumbua macho, hakuwa anaelewa kinachoendelea. Akajikuta anashikwa mkono na Bonston ambaye tayari mkononi mwake alikuwa na bastola kubwa yenye nguvu, *Smith and Wesson*.

“*Whats happening?*” Dimens akataka kujua nini kimetokea huku akionekana kuchoka ghafla.

“*Nothing happened Sir!*” Bonston akamwambia bosi wake kuwa hakuna kilichotokea wakati tayari luninga ile ilikuwa ikionesha kulivyovurugika upande wa pili.

“*How?*” akang’aka

“Mzee twende nikakuhifadhi sehemu salama, mengine nitayashughulikia...” Bonston akamwambia huku akiondoka naye mpaka kwenye lifti maalumu na kumwingiza, kisha wakapanda juu

ghorofa mbili na kuingia kwenye chumba kingine.

“Kaa hapa!” Bonston akamwambia mzee wake na kumweka katika kiti, ndani ya *‘Escaping Chamber’*.

“Sikiliza Bonston, ukikutana na huyo mtu, muue! Yaani, muue papo hapo. Ila hakikisha umelichukua lile sanduku na kulileta hapa...”

“Yes Sir!”

Bonston akamwacha bosi wake ndani ya chumba hicho kidogo yeye akarudi kwa kazi mbili kubwa; kwanza kumshughulikia Amata pili kulichukua lile sanduku lenye chanjo.

* * *

Kamanda Amata akatoka ndani ya kile chumba, hatua chache mbele akakumbuka kawaacha wenzake, alipogeuka akakuta milango ikijifunga.

“Tulia papo hapo!” Kelele za walinzi zikasikika, hakujali, akajitupa chini na kujiviringa huku akiachia risasi mfululizo kuwapoteza malengo. Akajikuta kawapeleka chini wote. Bunduki aliyokuwa akiitumia, ikaishiwa risasi. Akaitupa na kuiendea AK47 iliyokuwa chini huku mwenye nayo akiwa ulimi nje. Kati ya wale walioanguka pale chini, mmoja wao bado alikuwa akihema, risasi ilimjeruhi begani tu.

“Simama, haraka!” akamwamuru. Yule askari akasimama huku akivuja damu.

“Nioneshe swichi za milango!”

“No, hata mi-mi si-zi-ju-i,” akajibu kwa shida kidogo. Amata akahisi kuna mlango unafunguliwa, akamkamata jamaa yule na kumweka mbele yake kama ngao. Akawatazama walioingia, akawahesabu kwa hesabu ya jumla, walikuwa wanne tu. Hakuumiza kichwa. Akawasukumia mtu wao nao wakamdaka. Kwa kitendo hicho wakampa mwanya Kamanda ya kuwatungua. Naye hakusita, akafanya hivyo, na kuwaacha bila pumzi. Akawaruka na kuufikia mlango wa lifti, akaingia na kuufunga kisha akabofya ghorofa ya kwanza. Chombo hicho kikamsogeza hapo alipopataka. Mlango ukafunguka. Akatoka, mtutu mbele. Ukutani akaona kibao kikubwa kimebandikwa na maelekezo, kwamba huku ni maabara, na huku ni *power room* pamoja na chumba cha mawasiliano. Akasukuti kwa sekunde kadhaa na kuamua kwenda *power room*. Chumba kikubwa, chenye mitambo mingi ya umeme ndani yake. Hakufikiria mara mbili, akaingia na kuangaza macho akaona boksi kubwa ukutani lililobandikwa stika ya fuvu ikiwa ni ishara ya hatari. Pembeni yake

kulikuwa na mengine madogo madogo yanayofanana kabisa na lile.

Safi sana, nikiondoa umeme, na mawasiliano mtakosa kama kule, hakika leo mmeingia choo cha kike tena cha kilabuni! Akawaza huku akipachua kijikufuli cha boksi hilo na kukutana na fyuzi kubwa tatu, akakamata mbili na kuzivuta, zikang'oka, kisha akamalizia ya mwisho. Kiza kinene kikatanda ndani ya jengo hilo. Taa za dharula zikawaka na kutengeneza nuru ya wastani. Kwa jinsi walivyokuwa wametengeneza jumba hili ni kuwa ikitokea tatizo la umeme na kuruhusu umeme mdogo wa dharula, basi milango yote hujifungua na kubaki wazi.

* * *

Bonston akiwa kwenye lifti akajikuta akikwama ghafla, umeme umezimika.

"Mshenzi huyu!" akajisemea. Kwa kuwa yeye anajua nini kitatukia, akasubiri sekunde kadhaa, mlango ukafunguka, akatoka na kuruka nje; akatumia ngazi za kawaida akashuka mpaka maabara na kuingia ndani.

"Kiongozi nini kimetokea, kazi inaharibika huku!" mmoja wa wafanyakazi wa maabara akamuuliza.

"Kuna hitilafu ya umeme, naombeni lile sanduku haraka!" akawaamuru.

"Aaaaa lakini!"

"Nini? Hakuna lakini hapa fanya haraka...!" akapiga kelele na wale jamaa wakapakia zile chupa ndogo za chanjo kwenye lile sanduku, likafungwa kwa vifungo vyake, akakabidhiwa Bonston, naye akaondoka nalo. Kichwani mwake alikuwa na mambo mawili tu, kwanza kuzifikisha kwa bosi wake, pili arudi kwenye mapambano.

Ni muda huo huo, yeye anatokea upande huu, na Amata anaingia upande mwingine ndani ya maabara hiyo hiyo na kuwakuta wale jamaa wakiwa kwenye hekaheka.

"*Stop*, weka mikono juu!" akawaamuru huku bunduki yake ikiwa tayari kwa kazi.

"Nipeni lile sanduku," akawaambia. Wale jamaa wakatazamana tu. Dakika hiyo hiyo, Johnson, Tetty na Dkt. Edward wakaingia. Yule daktari akapitiliza mpaka kwenye hifadhi maalumu iliyotumika kuhifadhi sanduku lile, hakulikuta.

"Lipo wapi?" akawauliza wale wafanyakazi.

"Limechukuliwa!" wakamjibu

“Aaaaaaaa nnnnnnnoooo! My work! my work!” akapiga kelele huku akirukaruka.

Kamanda Amata akajua tayari wameshachukua mzigo huo, hakukubali, akamtazama Dkt. Edward.

“Unajua wapi twaweza mpata Dimens?” akamuliza.

“Yes! Nifuate,” akamjibu na kuanza kutoka.

“Nataka niilipue hii maabara kama kisasi,” Amata akamwambia Edward.

“No, usiilipue, hapa tupo chini kama futi ishirini hivi, ukiilipua hatuwezi kutoka hata mmoja,” Edward akamjibu huku wakiendelea kupanda ngazi. Wakiwa juu wakaanza kusikia milio ya majibishano ya risasi huko chini.

* * *

“Oooh thank you very much!” Dimens akashukuru huku akipokea lile sanduku, akalibusu na kuliweka kando.

“Sasa kamalize kazi, naona na vijana wengine nao wameshaanza kazi yao, hakikisha hatoki hata sisimizi, ila tahadhari, maabara isiguswe kabisa,” akamwambia.

“Yes Sir!”

Bonston alipogeuka tu kutoka eneo lile, akakutana uso kwa uso na Kamanda Amata. Amata na Dkt. Edward hawakutegemea kuwakuta watu hawa mahali hapa kwa sababu hata Edward hakupajua. Safari yao ilikuwa ni ghorofa ya juu kabisa ambako ndiko makazi ya Dimens.

“Maabara! Maabara gani unayozungumzia?” Amata akauliza, “Hapa halitasalia jiwe juu ya jiwe!” akasema huku akiwa katuna misuli kwa hasira.

“Hah! Bonston, hebu mwoneshe kwanza sisi ni nani?” Dimens akamwambia kijana wake.

“Umekuja mwenyewe kwenye mikono ya shetani!” Bonston akamwambia Amata, “Na huyo daktari unampeleka wapi?”

Amata hakujibu kitu isipokuwa macho yake tu ndiyo yaliyoonesha uchungu wa kisasi, akainua bunduki yake na kuifyatua *magazine*, akamwaga risasi zote sakafuni, “Nitakuuwa kwa mkono!” Amata akamwambia. Sasa wote wakatunishiana misuli katika mitindo tofauti ya upiganaji. Makonde kama saba yakavumishwa na Bonston, manne kati ya hayo yakamtandika Amata, akaenda chini, na kujiinua haraka. Teke

la nguvu lililokuja usawa wa mbavu likamtandika na kumrudisha chini. Kamanda Amata bado alikuwa na uchovu kiasi fulani uliompelekea kushindwa mapambano ya mikono.

Akajifuta damu kinywani, mara hii akabadilisha, badala ya ngumi za kawaida akasimama katika mtindo wa *kung-fu*. Mapigo yaliyofuata kutoka kwa Bonston yakakingwa kiufundi na Amata akapeleka mapigo makali na kuzitandika vyema nyama za mikono yake juu ya viwiko na kumlegeza nguvu. Bonston hakujielewa, akajikuta kakamatwa kichwa na kuzungushwa kisha akapigizwa chini na kujikuta sakafuni. Amata akaruka hatua moja nyuma na kusimama wima akimwacha jamaa akigalagala.

“Inuka mwanaume, inuka! Kabahatisha tu huyo!” Dimens akapiga kelele na kijana wake akainuka na kuja mbogo, Amata akaruka juu kidogo na kumtandika teke moja zito. Bonston akaudaka mguu wa kamanda na kutumia kiwiko chake akadhamilia kuuvunja, lakini kabla hajafanya hivyo akajikuta akipata makofi mawili ya masikio, akamwacha.

Dkt. Edward hakujua kupigana, alichokifanya ni kuchukua ile bunduki isiyo na risasi na kumpiga nayo kichwani, Bonston aligeuka na kumtandika konde moja na kumwacha hoi chini akitema damu.

“Sasa nakumaliza!” Bonston akamwambia Amata.

“Wewe kwanza, babu yako baadae,” Amata akajibu.

Dakika mbili za mapigano makali zikaendelea na kuwaacha wanaume hao kila mmoja akiwa anatokwa damu hapa na pale. Pigo moja la mjinga yule likampeleka Amata ukutani, la pili akaliepa na yeye akaachia ngumi nzito ikatua mbavuni kwa adui yake. Bonston akaguna na kurudi nyuma, akampa nafasi kamanda ambaye alikanyaga ukuta na kuruka hewani kimo cha ng’ombe akamchakaza mateke mawili ya kichwani, njemba likayumba na kutulia tena. Pigo la kifo ambalo Amata hutumia kumaliza mchezo kwa watu jeuri kama hawa, likatua tumboni na jamaa akarushwa mpaka ndani ya kile kijichumba akajibamiza kwa nguvu, ndipo Amata akagundua kuwa Dimens hayupo, katoka saa ngapi hajamwona.

Bonston alikuwa hoi pale chini, tayari mbavu kadhaa zimeshavunjwa kwa pigo la Kamanda, “Una jingine? Bosi wako yuko wapi?” akamwuliza.

“*Out! Out!*” akaongea huku akikoroma.

“Wewe ulichoma maabara kule Tanzania, ulifikiri hatutakukamata? Hamwezi kulifanya Bara la Afrika kuwa la kuchezea, wehu ninyi! Kisasi

cha ndugu zangu, mliowaua ndicho hichi, nakuua, na huyo mzee wako hata aende sayari gani nitamuua, na hiki kimaabara chenu, nakitia moto usiku huu,” Amata akamwambia.

“*Never!*” Bonston akajibu.

“*Never say never again!*” akakanyaga kwa nguvu kiatu chake chini, kisu kikafyatuka kutoka mbele ya kiatu na kudidimia kifuani. Bonston akakamata mpini mdogo wa kisu hicho na kukichomoa kisha akakirusha kwa ufundi kabisa. Amata akakiepa na wakati huo huo akamwona kijana huyo akimjia huku katoa macho kama mjiusi aliyebanwa na mlango. Konde la Bonston, likaepwa na kuishia ukutani. La pili nalo likaepwa. Kwa nguvu ya pigo lile bwege yule akavutwa mbele na kujikuta kanasa kwenye mikono imara ya TSA 1. Amata akainasa shingo ya Bonston na kumzungusha kwa ustadi kisha akamvuta kwa chini na kumpa pigo moja la kiwiko, akampasua koromeo. Akamwinua sawa na kumshushia kipigo cha mbwa mwizi. Dakika moja ilitosha kumsambaratisha vibaya bedui huyo.

“*Goodbye Sir!*” Amata akamwambia na kumpigia saluti wakati adui wake akiipigania roho yake.

Kamanda Amata akiwa na maumivu hapa na pale, akaiokota ile bunduki na kuijaza tena risasi nne tu. Akamsaidia Dkt. Edward kumwinua pale chini.

“Pole dokta!” akamwambia.

“Sanduku kaka! Kapita huku!” Edward akamwambia Amata, kisha wote wakatoka na kupanda ghorofa ya juu.

* * *

Huko chini Johnson na Tetty walifanya kazi kubwa, walihakikisha hakuna anayelitwa askari wala mshika bunduki aliyebaki na uhai wake. Walipohakikisha kazi imetimilika, wakaanza kutafuta njia ya kutoka nje ya jengo hilo. Ijapokuwa hawakuwa na nguvu za kutosha hasa Tetty, walijitahidi kujiokoa. Mwanamke huyu hali yake ilionekana kudhoofu sana, mara kwa mara Johnson alimsaidia kumvusha hapa na pale mpaka wakaibukia nje ya jengo ila hawakujua wako upande gani. Kila walikopita walikuta maiti tu. Giza lilichachamaa huku mwanga hafifu ukijitahidi kumulika eneo hilo.

“Tunaenda wapi?” Tetty akauliza.

“Hapa ni kutafuta pa kujificha tu!” Johnson akajibu.

Mara wakasikia mlilo wa helikopta likiibuka vichakani na kuanza kunyanyuka kwenda angani.

* * *

Kamanda Amata alifanikiwa kumwona Dimens akipotelea vichakani. Hakumwacha. Akaenda naye sambamba na kujitahidi kumfikia, lakini kabla hata hajamgusa tayari helikopta ilikuwa imetiwa moto. Wakati Dimens anairukia na kudakwa na vijana wake, lile sanduku likamtoka mikononi.

"Nooooo!" akapiga kelele.

Kabla Amata hajaliwahi, akajikuta anakula mweleka na kuanguka vibaya huku ile helikopta ikianza kuinuka. Afanye nini; achukue lile sanduku au amwendee Dimens, utata! Akaukumbuka mkanda wake wa kiunoni. Akautazama, ni wenyewe. Akauvua haraka na kuunganisha upande huu na huu. Halafu kachomoa pini ya kufungia na kuipachika kati. Kitendo cha haraka, akaminyia batani fulani na kuurusha kwenye ile helikopta. Shabaha yake haikuongopa, Dimens akiwa mlangoni kapiga magoti anatazama lile sanduku aliona vyema kitendo alichofanya Amata. Akaudaka ule mkanda kwa mkono wake huku Amata akijitupa kifudifudi kwenye nyasi.

Kilichofuata ni mlipuko mkubwa sana, huku macho ya Amata yakimwona Lord Dimens akipasuka, kuchanika na kukatika vipande vipande. Ile helikopta ikawaka moto ikizunguka huku na huko na kujibamiza kwenye miti kisha ikaanguka na kutulia chini.

Kamanda Amata akasimama taratibu na kutazama chombo kile kinavyoteketea. Akapiga hatua chache na kulichukua lile sanduku. Hakuamini. Akalitazama na kulibusu.

"Kwa watu wangu, kwa taifa langu," akatamka maneno ya kiapo chake cha kazi. Kisha akaanza kujivuta kwa taabu kutoka eneo lile. Baada ya hatua kama ishirini hivi akakutana na Johson na Tetty nao wakiibuka vichakani.

"Comrade!" Johnson akaita. Amata akageuka na kumtazama, wakakumbatiana kwa nguvu.

"Thank you very much Comrade!" Johnson akashukuru na Tetty naye akajitahidi kumkumbatia japo alionekana kuwa mchovu sana.

"Siwezi kuliacha jengo hili namna hii! Hawa washenzi wamelipua maabara yetu Tanzania lazima nami nifanye sawasawa," Amata akasema

huku akijivuta kuelekea jengoni.

Johnson akamzuia, “Subiri, nimeacha kiatu changu kule na nilikiacha makusudi”. Amata akamwangalia kijana huyo miguuni, kweli hakuwa na kiatu kimoja. Johnson akavua kile kingine na kukikunja kwa namna fulani mpaka kisigino na ncha ya mbele vikakutana. Hamad! Mlipuko mkubwa ukatokea na kufumua ardhi, ukalitawanya jengo lote. Moto uliotengeneza mwanga mkubwa ukaonekana wazi hewani, ukiwaka kwa hasira. Amata akawageukia Tetty na Johnson. Wawili wale wakapiga saluti ya heshima kwa TSA 1 naye akaijibu.

SURA YA 23

DAR ES SALAAM

NDANI YA 'SAFE HOUSE', Chiba alishtuka kusikia *beep* kali kutoka kwenye vifaa vyake, akageuka na kukuta kwenye kioo chake cha kompyuta kukijiandika namba fulani.

"Shiiit! Eeeeeeh!" akajikuta akishangilia huku akiruka juu.

"We nini?" Jasmine akauliza.

"*This is* Kamanda Amata!" akajibu huku akiwasha luninga kubwa na kuingiza zile namba na mara akajikuta mbele ya ramani kubwa ya Afrika, ikamtembeza na kumsogeza *Mozambique*, Cabo del Gado. Hapo pakawa panaonekana *dot* nyekundu ikiwaka na kuzima.

Akageuka kumwambia Jasmine amwite Madam S. lakini mwenzake tayari alikwishafika ndani ya kile chumba.

"Madam S, ni kitu pekee ambacho nilikuwa naomba Mungu kiwe na sasa kimekuwa. Niliwapa Scoba na Gina mkanda wa kiunoni ambao una mlipuko mbaya ndani yake, na nikawaelekeza kuutumia. Mkanda huo nilikuwa nimeuunganisha na mitambo hii kwamba siku ukilipuka basi unioneshe kwa kutumia satelaiti ni wapi umelipuka...." Chiba akaeleza. Madam S na Jasmine wakabaki wanamshangaa.

"*Chiba are you serious?* Sasa ina maana Scoba na Gina ndo wamefanya hicho?" Madam akauliza na kusogelea ile luninga akaitazama na kutikisa kichwa, "*So?*" akauliza. Chiba akatikisa kichwa kukataa.

"Sasa?" Madam S akamuuliza Chiba ambaye daima alikuwa akitabasamu tu.

"TSA 1 yupo hapo awe hai au mzima. Yupo hapo, na n'najua yupo hai, yapasa twende sasa," Chiba akasema. Madam S akatazama saa yake, tayari ilikuwa saa sita usiku na dakika zake.

“Sawa. Haya, haraka fiken *Airwing* Majumbasita mtamkuta Kepteni Mwanachia pale,” akawaambia. Dkt. Jasmine alionekana wazi kuwa na furaha isiyo kifani. Akachukua bastola zake mbili akazijaza risasi, akavaa saa yake tayari kwa safari. Chiba naye akapachika bastola zake sawasawa, akachukua kompyuta yake ndogo yenye *GPS* na vifaa vichache. Pamoja nao wakachukua shubaka la huduma ya kwanza na kuingia garini.

“Huyu ndiye Kamanda Amata TSA 1” Madam S akasema huku akichukua kinywaji kwenye jokofu, “Sijui kama huko aliko kuna usalama, ramani sijaitazama vizuri. Ni wapi?” akauliza.

“Msitu wa Cabo Delgado!” Chiba akajibu.

“Aaaaa hapo tu?”

“Yes!”

“Oh, siyo Maputo?” Madam akauliza.

“No! huu mlipuko ni Cabo del gado,” Chiba akajibu huku akimalizia kuweka sawa vitu vyake. Wakaagana na Madam S na kuchukua gari lao tayari kuelekea uwanja wa ndege wa jeshi.

* * *

Ndani ya msitu mnene wa Cabo Delgado, Kamanda Amata, Johnson, Dkt. Edward na Tetty walikuwa wanaendelea kutembea pasi na kujua wapi wanaelekea. Lakini lengo lao ilikuwa ni kufika mbali na eneo la mlipuko. Kila walipogeuka nyuma walishuhudia bado anga lote liking’azwa kwa miale mikali ya moto. Tetty alionekana kuchoka sana na mwendo ule uliowachukua kadiri ya saa mbili porini.

Wakiwa katikati ya msitu huo, Amata akawataka wapumzike, nao wakafanya hivyo. Ndani ya msitu huo kulikuwa na ukimya wa kutisha. Sauti pekee zilizokuwa zikisikika ni za wadudu mwitu. Mara mlilo wa chopa ukasikika kwa mbali, Amata akawataka wenzake kutulia ili asikilize vizuri. Akaichukua bunduki aliyoichukua kutoka kwa vijana wa Dimens na kuiweka tayari kwa lolote.

* * *

“Unafikiri atakuwa katika msitu huu?” Jasmine akamuuliza Chiba kwa sauti kali kutoka na mvumo wa injini ya chombo hicho.

“Yeah, hawezi kukaa kule kwenye eneo hatarishi. Kwa vyovyote vile atakuwa kajificha msituni au awe amekufa!” Chiba akajibu.

“Chunga kauli yako, aliyekwambia Kamanda huwa anakufa ni nani?” Jasmine akauliza kisha wote wakaangua kicheko. Kepteni Mwanachia aliendelea kuongoza chombo kile huku moyoni mwake akiwa haamini hilo jina analolisikia kwa maana daima amekuwa akilisoma kwenye vitabu tu. Baada ya mwendo wa kama dakika arobaini na tano hivi ndani ya msitu ule mnene, kompyuta ya Chiba ilianza kutoa ishara kuwa wamekaribia eneo la tukio.

“Jasmine, toa ishara, kisha Kepteni atazunguka eneo lote,” Chiba akamwambia Jasmine aliyekuwa mlangoni. Mwanamke huyo akavuta kurunzi kubwa na kuliwasha kumulika msituni. Mtindo aliyokuwa akitumia kuwasha na kuzima kurunzi hiyo ulikuwa ni moja ya ishara za siri za TSA wawapo kwenye misheni kama hizo.

* * *

Kamanda Amata akaiweka bunduki yake tayari na kuruhusu risasi kuingia chemba kusubiri amri ya nini cha kufanya. Dkt. Edward, Johnson na Tetty walikuwa kimya wakiwa wamejificha nyuma ya mti na kumwacha kijana huyo pekee upande wa mbele. Mara akaona taa kubwa ikiwashwa. Akainua bunduki yake tayari kwa shabaha maana alijua kwa vyovyote mlengwa ni yeye. Lakini mara akaona ikizimwa na kuwashwa tena harakaharaka kama mara tano hivi ikazimwa na kuwashwa moja kwa moja, akajua kuwa ni chopa ya nyumbani, akatabasamu.

“*My Brothers!*” akawaambia wenzake. Nao wakatoka nyuma ya mti na kuja upande wa mbele. Amata akafikiri ni jinsi gani anaweza kuwapa ishara. Katika kuulizana, kumbe Dokta Edward alikuwa na tochi kiunoni mwake, wakatumia hiyo, kuwasha na kuzima, kuwasha na kuzima, kwa mtindo ule ule. Johnson alipotazama saa yake, ilikuwa imetimu saa tisa usiku. Kamanda Amata akaendelea kutumia kurunzi ya Edward kuwasha na kuzima huku akitafuta mahala pazuri ambapo mwanga wa kurunzi ile ungeweza kuonekana.

* * *

Mizunguko miwili usiku huo juu ya msitu wa Cabodelgado, bado Chiba na Jasmine ndani ya chopa ile hawakuweza kumwona Amata. Jasmine alikata tamaa na kuzima taa ile.

“Hakuna mtu bwana, sioni hata ishara yoyote kutoka chini,” akasema.

Mwanachia akashusha chini zaidi chopa lile. Sasa lilikuwa karibu zaidi, kama mita kumi juu ya msitu.

“Jaribu tena Jasmine, usikate tamaa!” Chiba akamhimiza, naye akaanza tena kuwasha na kuzima kwa mtindo ule ule. Ni wakati huo akiwa anaangaza taa yake na kutazama kwa makini akaona kitu kiking’aa ghafla kisha mng’ao ukapotea, kikang’aa tena lakini tayari wakawa wamepita.

“Chibaaa!” akaita na kuwapa ishara kuwa wageuze chopa na kusimama eneo hilo. Mwanachia akafanya hivyo, Jasmine akaona tena kile alichokuwa akikiona. Ile chopa ikasimama juu, mita kadhaa kutoka miti hiyo mirefu, Jasmine akamulika na taa ile kubwa katika lile eneo.

“Yeaaaaahhhh! Yuko hapa!” akapiga kelele na Chiba akawahi pale mlangoni.

Kutokana na miti mikubwa iliyoota hapa na pale chombo hicho hakikuweza kushuka chini kabisa hivyo wakashusha kamba mpaka chini kabisa.

Kule chini Kamanda Amata akamwambia Tetty aanze kuivaa kamba hiyo, naye akafanya hivyo. Akaichukua na kupachika chuma chake katikati ya maungio ya miguu yake, akawa kama amekalia bembea.

“Up!” Amata akapia kelele. Ile kamba ikaanza kupanda juu taratibu mpaka kwenye chombo hicho, kisha ikashuswa tena na tena mpaka wote walipomalizika, Amata akawa wa mwisho na sanduku lile mkononi mwake.

Ndani ya chopa hiyo kulitawaliwa na furaha ya aina yake. Kamanda akawatambulisha watu aliokuwa nao na wao wakafanya vivyo hivyo. Mara hii mlango ukafungwa na Jasmine akaanza kutoa huduma ya kwanza pamoja na kuwapatia maji, keki na vinywaji vingine baridi walau warudiwe na nguvu zao. Bila kuuliza, akamwekea Tetty dripu ya kumwongezea nguvu na kuganga majeraha ya Amata na Jonhson. Kamanda Amata akalibusu tena lile sanduku na kuliweka mahala salama.

“Asanteni kwa kutuokoa!” Amata akamwambia Chiba huku wakipeana mikono na kugongana vifua vyao mara tatu kama ishara yao ya ushindi.

“Usijali Kamanda, tumefurahi kukuona tena,” Chiba akasema wakati huo Jasmine alikuwa bize na Tetty kumpatia huduma hii na ile ikiwamo dripu zaidi na madawa mengine.

Wakiwa wamejisahau mara chopa ile ikayumba ghafla na kitu kama donge kubwa la moto likakatiza mita chache kutoka kwenye chombo

kile. Wote mle ndani wakaangukia upande mwingine.

“Vipi Kepteni?” Chiba akauliza.

“Tunashambuliwa!” Kepteni Mwanachia akajibu.

Kamanda Amata akarudi na kuketi kitini huku akitupa jicho upande wa chini, “Nifungulie niwatie adabu!” akamwambia Kepteni.

“Usihangaika kaka, dawa yao ndogo,” Kepteni akajibu na kuizungusha tena ile chopa, mara hii ikaanza kufyatua risasi mfululizo pande zote nne kuelekea chini. Amata akawahi kiti cha pembeni ya Kepteni, akaketi na kupachua kifuniko fulani kilichoandikwa ‘*Grenade*’, akabofya kitufe chekundu. Chini ya chopa ile kukafunguka kama vikasha na kuangusha mabomu kadhaa ambayo yalifanya milipuko ya hatari na kusambaratisha kila aliyekuwako huko.

* * *

SIKU NNE BAADAE

Uwanja wa Ndege wa Jeshi – Dar es salaam

Johnson Kasalu na Tetty walikuwa katika suti safi za Jeshi la Marekani. Wote wawili wakiwa wamebana kofia zao kwapani walikuwa wametazamana na kamanda Amata aliyekuwa mbele yao.

“Sikuwahi kukujua kabla, lakini hakika, sakata hili, limenikutanisha na mtu hatari. Jina nimelisikia mara kadhaa ila sikuwahi kuamini kama kweli ni mtu anayeishi. Sasa nimeamini, nimekuona kwa macho yangu. Asante sana kwa kazi bora hii, umeoko maisha yangu,” Johnson akamwambia Amata wakati tayari ndege iliyotumwa kutoka Marekani ilikuwa imewasili kuwachukuwa yeye na Tetty pamoja na mwili wa Mellanie na Kelvin uliookotwa baadae, ambayo ilikuwa ndani ya majeneza yaliyofungwa kwa bendera ya nchi yao.

“Tuko pamoja kaka, *CLA* na *TSA*,” Amata akajibu, kisha akavua saa yake, akampa Johnson, naye akavua yake akampa Amata.

“Mwambie bosi wako, hakuna Dimens wala *demons* katika uso wa dunia! Ila kuna Kamanda Amata *TSA 1, code 005*” Amata akamaliza. Johnson na Tetty wakapiga saluti naye akawajibu kwa kusimama kikamamavu. Wakageuka na kila mmoja akakamata machela yenye magurudumu iliyobeba jenze la Mellanie na mwingine la Kelvin na kutembea nayo taratibu kuelekea ndegeni. Katika mlango wa ndege ile walisimama wanajeshi wengine wawili wa Marekani wakiwa katika sare

nadhifu. Wakapiga saluti na kupokea majeneza yale na kwa utaratibu maalumu wakayapakia ndegeni. Safari ya kurudi Marekani ikaanza.

Kamanda Amata akasimama hima mpaka ndege ile ilipoacha ardhi, akageuka na kukutana uso kwa uso na Gina. Akavua mkufu na kumpatia. Gina akauvaa shingoni mwake akitabasamu.

“Nakudai!” akamwambia.

“Nitakulipa!” Gina akajibu na kumrukia, akamkumbatia huku miguu yake akiwa kaikunja kwa juu, akambusu mashavuni.

* * *

Saa mbili baadae, vijana wa TSA waliwasili Ikulu kwa mkutano na Rais. Wote wakiwa nadhifu kabisa. Madam S akamtazama Amata wake kisha akatikisa kichwa.

“Pole sana Kamanda! Umefanya kazi ngumu pasi na msaada,” akamwambia.

“Usiwe na wasiwasi, hii ni kazi niliyoichagua. Kwa watu wangu, kwa taifa langu...” Amata akajibu. Katika viwanja hivyo, Madam S na kundi lake walikuwa tayari kuonana na Mheshimiwa Rais jioni ya siku hiyo. Kutokana na kazi yao wote watano walikuwa katika mwonekano tafauti na siku nyingine wawapo uraiani, ama kajiweka hiki au kile ilimradi kuwapoteza wale wanaowatazama.

Dakika kama kumi hivi Rais alikuwa tayari kuonana nao, wakaelekezwa mahala maalumu pa kukutana naye, wao pekee.

“Tumefanikiwa kurudisha sanduku hili nyeti!” Madam S akasema huku wote wakiwa wamesimama wima kwa ukakamavu. Beji zao za kazi zikiwa zimebanwa vyema kifuani upande wa moyo. Akamkabidhi Rais naye akalipokea na kwa kusaidiwa na *Aide De Camp* wake, likawekwa mezani.

“Ninawaamini na nitawaamini daima. Usalama unaotakiwa kupotezwa kwa siri, utakomeshwa kwa siri vilevile. Endeeleni kulitumikia taifa, nakuambieni tena, mkiwa na tatizo lolote la kimaisha tafadhali, mna uwezo wa kuchukua pesa muda wowote kwenye akaunti zetu za siri, msisite! Asanteni kwa mara nyingine, nitakuja kuwatembelea ofisini kwenu kuona mfanyavyo kazi na kwa mazungumzo machache,” Rais akawaambia kisha wakaketi vitini. Kutoka mlango mwingine akaingia Dkt. Edward na kukaribishwa kiti kilichobaki wazi.

Madam S akasimama tena, “Mheshimiwa Rais, huyu hapa ni Daktari

Edward Minzi aliyepigania kugunduliwa kwa chanjo hii. Baada ya kuteketea kwa moto ile maabara yetu yeye alitekwa na wale majahili ili kumtumia katika kuitangaza chanjo hii kuwa ni yao...”

“Karibu sana Edward, taifa linautambua mchango wako. Kazi uliyoifanya ni kubwa sana huna budi kupata unachostahili. Basi, sasa naomba uhakikishe kama kila kilichopo humu ndani ni sahihi, maana binadamu sisi ni wajanja” Rais akamwambia. Dkt. Edward akasimama, tayari kufungua lile sanduku kubwa lililotengenezwa kwa plastiki ngumu, iliyofungwa kwa vifungo maalumu vya dijitali. Lenye uwezo wa kuhifadhi barafu kavu kwa siku saba kama halijaunganishwa na umeme.

“Subiri!” Chiba akasema na kunyanyuka, akavua saa yake na kubofya vitu flani kisha akaiweka juu ya sanduku hilo.

“Sawa, waweza fungua!” akamruhusu. Daktari huyo akaingiza namba za siri na kujaribu kufungua, likagoma, akajaribu tena, likagoma.

“Wamebadili nywila!” akasema.

“Tunafanyaje sasa!” Rais akauliza huku akimtaazama Madam S huku akishusha pumzi ndefu.

Chiba akainuka, akalitazama sanduku hilo kwenye pedi ya namba ili kujua mpangilio, kisha akachukua skana yake ndogo na kuipachika juu yake, akaiwasha. Mwanga wa kijani ukapita kutoka juu na kuja chini kisha kukabaki doti za kijani mule tu mwa kubonyeza.

“2804-1502,” Chiba akataja na kuiondoa ile skana. Daktari Edward akabonya tarakimu hizo na vifungo vyake vikafunguka. Akainua mfuniko taratibu na mvuke wa baridi ukatoka nje kwa sababu ndani yake kulihifadhiwa barafu kavu isiyopoteza baridi haraka endapo imefungwa barabara. Akatazama na kuhesabu.

“Ziko sawa, na hawakuwahi kuzichakachua! Zaidi ni kuzitoa humu na kuweka kwenye friza,” akasema Edward.

“Safi, naomba zifungwe, na zitakuwa mikononi mwa TSA kwa sasa, wao watajua wapi wanahifadhi. Kisha tutaona nini cha kufanya baadae,” akasema Rais. Dkt. Edward akafunga lile sanduku.

* * *

Nyumbani kwa Madam S

Usiku wa siku hiyo, nyumbani kwa Madam S kuliangushwa mbuzi mzima, vinywaji vikali viliteketea huku Amata akiwasimulia yaliyojiri

katika kutekwa kwake na mchezo mzima wa kule India. Furaha ya kukutana tena kama familia ikatamalaki.

“Ila ukome kutoroka hospitali...” Madam akamtania na wote wakacheka.

“Na sasa ni *cheers* kwa afya!” Gina akapiga kelele

Na wote wakagonga bilauri zao, “Cheeeeeerrrrrrssssss!”

Baada ya kumaliza shughuli, kila mtu alipewa chumba cha kulala. Gina akamshika shati Amata kabla hajakotelea chumbani.

“Unieleze, mi sikutoshi hata umfate huyo mwanamke wako? Mpaka ukapigwa nusu kufa! Mwanaume wewe!” Gina akamwambia.

“Huu si uzinzi... hii ni moja ya silaha za kumfikia adui, nilijua kuwa nimetegwa kule ndiyo maana nikaenda na ndiyo maana sikukwambia kwa sababu nilijua kuwa sasa kazi inawiva. Yule mwanamke aliuawa na wao wenyewe...” akamjibu.

Gina akatabasamu kwa jibu hilo, “Tausi hajafa,” akamwambia. Amata akashtuka na kumtazama Gina.

“Hajafa?”

“Ndiyo, hajafa ila alijeruhiwa vibaya sana...” Gina akaeleza.

“Oh masikini msichana wa watu,” Amata akasikitika.

“Pole mpenzi!”

“Asante!” akamjibu, “Uliniahidi nikirudi salama utanipa zawadi ya mtoto, nategemea zawadi hiyo!” akaongeza kusema.

“Twende chumbani! Ukikosa shabaha leo ndio basi tena!” Gina akajibu, wakajifungia mlango.

MWISHO

Wasiliana na Mwandishi:

JAMVI LA SIMULIZI ZA KUSISIMUA

Facebook:	Kamanda Amata
Facebook fun Page:	Jamvi la Simulizi za Kulisimua
Twitter:	Richard Ric Mwambe
Instagram:	Jamvi La Simulizi
Simu ya Mkononi:	+255 766 974865 / +255 672 160016
Whatsapp:	+255 766 974865
Barua pepe:	jamvilasimulizi@gmail.com info@richardmwambe.com
Tovuti:	www.richardmwambe.com

Wasiliana nami, mwandishi, pindi upatapo kitabu hiki. Niandikie jina lako na jinsi gani umekipata. Bila kusahau mahali ulipo. Usisite kutoa maoni yako. Nimetega sikio, nakusikiliza...

